**24 APRILI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 24 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. JULIANA D. MASABURI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo Mbunge wa Singida Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 163

### Kujenga Masoko kwa Wajasiriamali wa Mafuta ya Alizeti

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwajengea masoko wajasiriamali wanaouza mafuta ya alizeti pembezoni mwa barabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa wajasiriamali ambao wamekuwa wakiuza mafuta ya alizeti katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Biashara hii imekuwa ikifanyika pembezoni mwa barabara hali inayosababisha kupungua kwa ubora wa mafuta na kupoteza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya tathmini ili kuona njia bora zaidi ya kuwawezesha wafanyabiashara hao kufanya biashara katika maeneo bora na salama zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu haya ya Serikali, naomba kuuliza; kwa kuwa, Serikali imekiri uwepo wa tatizo hili ambalo linasababisha pia kupotea kwa ubora wa mafuta haya ya alizeti na tathmini siyo mkakati, Serikali sasa ina mkakati gani mahususi ikiwa ni pamoja na kuzielekeza halmashauri kujenga vibanda vya kutunza ubora wa bidhaa hii ambayo ni chakula ili pia kutunza afya za walaji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kumekuwa na changamoto ya kushuka kwa bei ya mafuta ya alizeti pamoja na alizeti yenyewe panapokuwa na uzalishaji mkubwa. Ni upi mkakati wa Serikali ili kutoa bei elekezi isiyoyumba panapokuwa na uzalishaji mkubwa wa alizeti ili kumnufaisha mwananchi wa chini kabisa ambaye kazi yake kila siku ni kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza tunatambua changamoto hiyo na tunafanya tathmini ili sasa tuandae mkakati wa kurekebisha changamoto hiyo kutokana na *evidence* ambayo tutaipata baada ya kufanya tathmini ya kimazingira.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni jumuishi, kwanza linahusisha wafanyabiashara wenyewe, na pia linahusisha halmashauri na viongozi wa halmashauri hizo, wilaya, mkoa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalifahamu hilo na inalichukulia *very serious,* ili tuweze kulifanyia tathmini na kuweka mkakati ambao unakubalika kwa pande zote za wafanyabiashara, wateja, pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusiana na changamoto ya bei ya mafuta ya alizeti, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu mafuta ya alizeti yanauzwa kwa soko huria,

lakini Serikali imeendelea kutengeneza mazingira na kuweka mazingira bora zaidi kwa ajili ya bei nzuri zaidi ya alizeti na pia ya mafuta. Kwa hiyo, Serikali imepokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge na tutayafanyia kazi pale inapowezekana ili tuweze kuboresha zaidi bei ya mafuta ya alizeti, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 164

**Kanuni za Uchaguzi wa Makamu Wenyeviti wa Halmashauri**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itabadili Kanuni ili Makamu Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya watumikie kwa miaka mitano badala ya mwaka mmoja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Halmashauri za Wilaya zinazoelezea Uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti zimetungwa chini ya Kifungu cha 70(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na Kanuni za Kudumu za Halmashauri za Miji zinazoelezea Uchaguzi wa Naibu Meya zimetungwa chini ya kifungu cha 42(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 288.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa mabadiliko ya sheria, kanuni na taratibu ni sehemu muhimu ya utawala bora na maendeleo endelevu ya jamii. Hata hivyo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikipokea hoja kutoka kwa wadau walio wengi kuhusu hitaji la mabadiliko ya kanuni hizi itafanyia kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Bunge lako hili ni mdau muhimu sana na hoja hii imetokea Bungeni kwako hapa; na kwa kuwa, pia utaratibu huu unaziingiza halmashauri katika gharama kubwa kila mwaka kuandaa Uchaguzi wa Makamu Wenyeviti; na pia, kwa kuzingatia R4 za Mheshimiwa Rais: Je, Serikali, haioni kwamba kuna haja ya kuchukua hoja hii na kuifanyia kazi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuchukua hoja hii ya Mheshimiwa Mbunge Ndaki na kuifanyia kazi. Ndiyo maana tumesema tutafanya tathmini kujiridhisha na kushirikisha wadau mbalimbali kwa sababu Uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti na Naibu Meya kila mwaka unasaidia kuwapa *exposure* Waheshimiwa Madiwani walio wengi kuwa tayari kuwa Wenyeviti au Makamu Wenyeviti kwa kipindi kingine. Kwa hiyo, tunaichukua hoja hii kwa ajili ya kuifanyia kazi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hili jambo la Makamu Mwenyekiti kuchaguliwa kila mwaka limeleta matatizo makubwa sana kwenye halmashauri. Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri anashindwa kufanya kazi kwa kutumia uwezo wake badala yake anakuwa masaa yote ni kujipendekeza kwa Mwenyekiti na Madiwani ili aendelee kuwepo. Kwa hiyo, tunaomba hili jambo lichukuliwe *serious,* ni jambo baya sana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naona huo ulikuwa ni ushauri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 165

**Ukarabati wa Kituo cha Afya Mkongo Gulioni – Songea**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati Kituo cha Afya cha Mkongo Gulioni pamoja na ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto na la Upasuaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Mkongo ni moja ya vituo vya afya 202 vilivyofanyiwa tathmini kwa ajili ya ukarabati mkubwa ili viendane na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kutafuta na kutenga bajeti kwa awamu ili kuwezesha uboreshaji wa miundombinu kwenye Kituo cha Afya Mkongo Gulioni, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, swali la nyongeza.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alisimama mbele ya Mheshimiwa Mariam M. Nyoka)*

**SPIKA:** Mheshimiwa uliyesimama mbele ya Mheshimiwa Mbunge anayeuliza swali, tafuta kiti ukae.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam subiri. Mheshimiwa Mbunge, tafuta kiti uketi.

Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, endelea.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nataka pia, niende kwenye kituo kingine cha afya kilichopo Manispaa ya Songea. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Kituo cha Afya cha Mji Mwema ikiwa ni pamoja na wodi ya akina mama, wanaume, pamoja na *OPD,* kwani majengo yake ni chakavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mariam Nyoka kwa namna ambavyo anaendelea kuwasemea wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mariam kwamba, tunafahamu Kituo cha Afya cha Mji Mwema katika Manispaa ya Songea ni moja ya vituo vikongwe na chakavu, lakini pia kina upungufu wa majengo ya huduma. Namhakikishia kwamba, tayari tumekiingiza kwenye orodha ya vituo 202 vya kuvikarabati kwa awamu ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu Kituo cha Afya cha Rutamba kwa sababu, nimekiulizia mara kadhaa? Kituo kile hakijapangwa kwenye eneo lolote na ukizingatia kule idadi ya watu ni kubwa sana, tarafa ile haina kituo cha afya na kituo kile ni kichakavu sana, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mama Salma Kikwete kwamba, Kituo cha Afya cha Rutamba ni kituo kikongwe, lakini kinahudumia

wananchi wengi, hakina miundombinu ya kutosha na tayari ameshalifuatilia sana.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina dhamira na inatafuta fedha. Wakati wowote fedha ikipatikana tutakwenda kukikarabati na kukipanua Kituo cha Afya cha Rutamba, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2023 Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walitupatia fomu za kujaza kuchagua vituo vya afya vya kimkakati na tukaenda majimboni tukatoa taarifa kwa wananchi wote kwamba tutapewa fedha. Je, ni lini fedha hii itaingia ili kuendana na zile taarifa ambazo tumepeleka majimboni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhakikisha wananchi wote nchini wanapata huduma za afya karibu zaidi na makazi yao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tulileta fomu hapa Bungeni, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, tulishaainisha kata za kimkakati kwa ajili ya kwenda kujenga vituo vya afya. Nawahakikishia kwamba Serikali bado ina mpango huo na tunaendelea kutafuta fedha. Mara fedha ikipatikana, maeneo yote ambayo yaliainishwa yatakwenda kujengewa vituo vya afya. Kwa hiyo, ahadi hiyo bado inafanya kazi, ni suala la muda tu, tutatekeleza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Bukene ambacho kinahudumia Tarafa nzima ya Bukene yenye kata

nane ni kikongwe, kimechakaa na kina upungufu wa majengo. Ni lini Serikali itatoa kipaumbele ili nacho kiweze kukarabatiwa, kiwe sawa na vituo vipya vinavyojengwa sasa hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Zedi kwa sababu ameleta orodha ya vituo vyake chakavu, kikiwemo Kituo cha Afya cha Bukene. Pia, nampongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega, ameleta orodha hiyo na pia, ameleta tathmini ya gharama inayohitajika kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa kituo hicho. Kwa hiyo, ni suala tu la muda tutatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kutekeleza mpango huo, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi. Wabunge wawili mliosimama nimewaona, Mbunge mmoja una swali leo, kwa hiyo, sitakupa nafasi. Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kituo cha Afya cha Changuge kimechoka na kimechakaa na Mheshimiwa Waziri alipita akakiona na akaahidi kukifanyia maboresho. Ni lini sasa kitatengewa fedha kwa ajili ya kufanyiwa maboresho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Chagunge kipo kwenye orodha ya vituo 202. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kitakarabatiwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 166

**Hitaji la Kituo cha Afya Tarafa ya Kimbe**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Tarafa ya Kimbe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa Kituo cha Afya katika Tarafa ya Kimbe. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi ilitenga shilingi milioni 136, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* ambapo jengo hilo limefikia 92%.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo hicho cha Afya cha Kimbe katika miaka ijayo ya fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nasikitika sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu, msingi wa swali langu ni kwamba tarafa hii ina kata mbili; Kata ya Negero na Kimbe ambapo wananchi wa kata hizi wanapata huduma Wilaya ya Handeni na Wilaya ya Mvomero na kwa kipindi hiki cha mvua ni kwamba wananchi hawapati huduma hiyo. Swali langu ni kwamba, je, Serikali iko tayari kujenga kituo cha afya cha kimkakati katika Kata ya Kimbe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atume timu yake ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenda kuangalia adha wanayopata wananchi kwenye huduma hii ya afya katika maeneo hayo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimtoe hofu na mashaka Mheshimiwa Omari Kigua kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Kimbe kwa sababu, wananchi wengi wanahitaji huduma za afya na kituo cha afya kilicho jirani kiko umbali mrefu sana. Kwa hiyo, ndiyo maana tumemwelekeza Mkurugenzi, ameshatenga fedha shilingi milioni 136 na tayari jengo la *OPD* liko 92%. Kwa hiyo, utaona tayari tumeanza utekelezaji na ni suala tu la kutafuta fedha, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunajenga kituo hicho na kinakamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na kutuma wataalamu, tunafahamu, lakini nitamwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa pia Mganga Mkuu wa Halmashauri waweze kuleta taarifa rasmi ili tuweze kuongeza kasi ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya kwenye Kata ya Mkomba katika Tarafa ya Kamsamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Juliana Shonza, amefuatilia sana kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo kuhusiana na kituo hiki cha afya. Tumemwahidi na tumekiingiza kwenye orodha ya vituo vya afya vya kimkakati. Kwa hiyo, naomba tu nimhakikishie kwamba tayari Serikali inatambua na inaweka mipango yake kwa ajili ya kwenda kutekeleza ujenzi wa kituo hicho cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, nataka kujua, ni lini Serikali itapeleka fedha kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kimkakati cha Igamba katika Tarafa ya Igamba, Wilaya ya Mbozi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani, kwa ajili ya kuanza kujenga Kituo cha Afya cha Kata ya Igamba wakati Serikali pia inatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kuwaunga mkono wananchi wa Kata hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, Kata za Mpendo, Jangalo na Lahoda ni kata za mpakani na hakuna kabisa huduma ya vituo vya afya. Naomba kujua, ni lini Serikali itatenga fedha ili kujenga vituo vya afya kwenye kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nirejee maelekezo ya Serikali na msisitizo wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba Wakurugenzi wote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa watambue maeneo ya kimkakati na maeneo ambayo wananchi wako mbali zaidi na vituo vya huduma za afya, waanze kutenga fedha za mapato ya ndani ili kuanza ujenzi wa maeneo hayo. Wakati huo walete tathmini na gharama zinazohitajika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi, kukamilisha vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Chemba kwamba waandae na watenge fedha kwenye bajeti, pia waanze ujenzi. Sisi Ofisi ya Rais,

TAMISEMI tutahakikisha tunakamilisha ujenzi wa kituo hicho, ikiwa eneo hilo linakidhi vigezo vya kuwa na kituo cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kituo cha Afya cha Msae, Mwika pale, toka niingie hapa Bungeni nauliza jamani, lini mtakarabati kituo hicho? Tunaambiwa pesa, pesa. Kwa nini vituo vingine vinajengwa, lakini kile cha kwangu hakijengwi? Mnataka mimi nisijisikie vizuri Bungeni hapa! *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kimei, kwenye Jimbo la Vunjo hamna kituo cha afya kipya hata kimoja kilichojengwa!

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Ngoja, anza kuongea baada ya kuwasha kisemeo. Hakuna hata kimoja kilichojengwa! Washa kisemeo.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, tumejengewa vituo vipya viwili, lakini kituo hiki kikongwe, mimi nilizaliwa kwenye kituo hiki…

**SPIKA:** Nilitaka tu kujua kama hakuna kituo cha afya chochote kilichojengwa. Kwa hiyo, vimejengwa viwili, unataka ukarabati. Haya, ahsante sana.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, mimi ninacholia nacho ni hicho cha Mwika.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeendelea kuliona sana Jimbo la Vunjo kwa kupeleka fedha kwa ajili ya huduma za afya, ujenzi wa vituo, zahanati, vifaatiba na magari ya wagonjwa. Tutaendelea kufanya hivyo Mheshimiwa

Mbunge. Tunatambua kwamba, kituo hiki cha afya ni chakavu na kwa hakika Serikali imeweka mpango wa kukarabati vituo vya afya chakavu baada ya kukamilisha ukarabati wa hospitali za halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inawezekana Mheshimiwa Mbunge umeona muda mrefu umesema hatujatekeleza kwa sababu tumeweka vipaumbele. Tukarabati kwanza hospitali kongwe za halmashauri ambazo tayari tumeshakarabati kati ya zile 50, tumeshakarabati 31, bado 19 na tunakamilisha mwaka huu wa fedha. Baada ya hapo, tutakuja kwenye vituo vya afya kikiwemo kituo hiki cha afya cha kwako Mheshimiwa Kimei. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni upi mkakati wa Serikali wa kujenga kituo cha afya katika Tarafa ya Vwawa, Eneo la Ihanda ambacho kitatumika pamoja na Ipunga na Ukwile? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ya kimkakati ambayo yanakidhi vigezo vya kuwa na vituo cha afya, yanajengewa vituo hivyo vya afya kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, ikiwa vigezo vinatimia, tutahakikisha tunatenga fedha, tunajenga kituo cha afya ili wananchi wapate huduma bora za afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Mtaa wa King'azi na Mtaa wa Saranga, wananchi hawana kabisa huduma ya afya na wanahudumiwa chini ya miti katika Ofisi za Serikali za Mitaa. Pamekuwa na ahadi ya Serikali za miaka miwili kukamilisha maboma katika mitaa hii miwili. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha tukamilishe maboma yale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge, amefuatilia lakini nilishamshauri pia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa sababu ya uwezo wa mapato yao ya ndani, wana uwezo wa kukarabati na kuwezesha zahanati ile ianze kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, fedha za mapato ya ndani ni fedha za Serikali, kwa sababu kumekuwa na kasumba ya baadhi ya watendaji kuamini kwamba fedha ya Serikali ni fedha inayotoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI au Serikali Kuu. Fedha ya mapato ya ndani ni fedha ya Serikali kama ambavyo fedha nyingine zinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii nimwelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo kwamba tunampa kipindi cha miezi sita waanze ukarabati na ukamilishaji wa majengo hayo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaambatana mimi na yeye kwenda kukagua pale na kazi ile itakuwa imeanza kupitia mapato ya ndani ya Manispaa ya Ubungo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, sasa aulize swali lake.

Na. 167

**Upanuzi wa Kituo cha Afya Mtanila – Chunya**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya Mtanila ili kiendane na vituo vinavyojengwa sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Mtanila ni miongoni mwa vituo vya afya 202 vilivyofanyiwa tathmini kwa ajili ya ukarabati mkubwa na kuongeza miundombinu ili kuendana na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga na itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa Kituo cha Afya Mtanila ili kiweze kutoa huduma bora za afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na tuna imani pesa hizo zitafika kwa wakati. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya tuna kata za kimkakati: Kata ya Ifumbo, Kata ya Matwiga pamoja Mafyeko, ambazo zimeanza kujenga vituo vya afya kwa nguvu za wananchi na ni muda mrefu. Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha za kutosha kukamilisha vituo hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Wilaya ya Chunya tuna changamoto kubwa sana ya watumishi hasa kwenye upande wa Idara ya Afya. Je, ni lini sasa Serikali itatupatia watumishi wa kutosha hasa madaktari ili kuweza kukabiliana na changamoto za uhaba wa watumishi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, hivi vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja, cha Kata ya Matwiga, Mafyeko na kata nyingine, ni vituo ambavyo kimsingi hata tulipofanya ziara kule na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alivisema na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulishavichukua. Pia Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza Mkurugenzi aanze kutenga fedha. Napongeza kwamba ameanza utekelezaji huo. Nimhakikishie tu kwamba Ofisi ya Rais,

TAMISEMI tunatambua na tutatenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo hivyo vya afya.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusiana na upungufu wa watumishi, ni kweli Halmashauri ya Chunya ni moja ya halmashauri ambazo zina upungufu mkubwa wa watumishi wa sekta ya afya. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tumeainisha kwa vipaumbele halmashauri zenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi. Kila kibali cha ajira kinapojitokeza watapewa watumishi wengi zaidi kuliko wa halmashauri zile ambazo zina nafuu ya upungufu wa watumishi. Kwa hiyo Halmashauri ya Chunya pia itapewa kipaumbele katika ajira zinazofuata. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujua mkakati wa kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Ulowa, ahadi ambayo Mheshimiwa Waziri na wewe mlikuja kuwaahidi wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kata ya Ulowa ni kata yenye wananchi wengi sana katika Jimbo la Ushetu. Tulishafanya ziara pale na kwa kweli mahitaji ya wananchi pale ni kituo cha afya. Nikuhakikishie tu kwamba, tumeshakiingiza kwenye Mpango wa Vituo vya Afya vya Benki ya Dunia na tunaamini fedha ikitoka mapema iwezekanavyo tutakwenda kuanza ujenzi katika Kata ya Ulowa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Amar, naomba swali lake lipate majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la Mheshimiwa Amar ni Na. 168. Simama uzungumze tena.

Na. 168

**Kusambaza Maji kwenye Shule za Msingi na Sekondari Nyang'hwale**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza maji kwenye Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Nyang'hwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Nyang'hwale yenye jumla ya vijiji 62. Kati ya vijiji hivyo, jumla ya shule za msingi na sekondari 34 zimefikiwa na huduma hiyo. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi tisa katika vijiji vya Iseni, Kabiga, Nyangalamila, Nwiga, Kasubuya, Nyamikonze, Nyijundu, Bululu na Ifugandi ambapo kukamilika kwake kutanufaisha wananchi wa vijiji hivyo ikiwa ni pamoja na shule za msingi na sekondari 10 zinazopatikana kwenye vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu katika vijiji vilivyobakia ili kuhakikisha vinafikiwa na huduma ya maji ikiwa ni pamoja na shule za msingi na sekondari zilizopo katika vijiji hivyo. Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji itaanza kufanyika

katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuimarisha huduma ya maji katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa limekuwa ni tatizo kwenye maeneo mengi inapotekelezwa miradi ya maji, taasisi hizi za shule na taasisi nyingine zinakuwa hazipelekewi mifumo ya maji, ni kwa nini sasa Serikali isiweke kama takwa la lazima kwamba, mradi wa maji unapotekelezwa, basi taasisi hizi hasa shule ziwe zinapelekewa maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa miradi mingi ya maji bado inasuasua kwa sababu wakandarasi wengi hawajalipwa, akiwemo mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Maji wa Ukala Jimboni Ukerewe, nini sasa mkakati wa Serikali ili mkandarasi huyo aweze kulipwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge, pia nimhakikishie kwamba moja ya takwa la lazima panapojegwa mradi wa maji ni taasisi lazima zipelekewe maji, aidha shule, zahanati ama vituo vya afya kuhakikisha kwamba wanapata hii huduma muhimu sana ya maji. Hayo ndiyo maelekezo na takwa la lazima katika Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nikiri na nishukuru Wizara ya Fedha kwamba hivi karibuni Wizara ya Maji tumepokea shilingi bilioni 60 katika kuhakikisha kwamba tunalipa wakandarasi hasa wale walio-*rise certificate* kwenye madai mbalimbali katika miradi ambayo wanatekeleza. Kwa hiyo, tutalipa kwa haraka kuhakikisha kwamba kazi zinaendelea katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la maji linaathiri shule za *boarding* na hasa watoto wa kike ndiyo waathirika wakubwa, je, Serikali ina mapango gani wa haraka wa kutatua tatizo hili hasa Mkoa wa Mara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge na ninatambua kabisa eneo la Mkoa wa Mara ni eneo ambalo kama Serikali tumewekeza hasa juu ya ujenzi wa miradi mikubwa, na sasa hivi tumekamilisha Mradi ule wa Mugango - Kiabakari - Butiama. Pia, kama Wizara ya Maji, tuna mitambo ya uchimbaji visima. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, maeneo ambayo yana changamoto, Wizara ya Maji tupo tayari kuchimba visima kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hizo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali hili; je, ni lini Mradi wa Maji wa kutoka Ziwa Victoria mpaka Mkoa wa Simiyu utakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi Wizara ya Maji mkakati wake ni kutumia rasilimali toshelevu ikiwemo maziwa na hivi ninavyozungumza mkandarasi yupo *site*. Nataka nimhakikishie, kwa sababu mkandarasi tumeshamkabidhi, tutakamilisha kazi ile kwa mujibu wa mkataba kama tulivyopanga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nataka kujua, kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa sana katika Wilaya ya Mbozi na Wilaya ya Momba ya upatikanaji wa maji, je, ule mradi mkubwa kutoka Momba ambao utahudumia Tunduma na Wilaya ya Mbozi

umefikia hatua gani hasa ukizingatia ni miezi miwili tu tumalize mwaka wa fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba eneo la Momba ni moja ya maeneo yenye changamoto ya maji, na Mheshimiwa Mbunge amekuwa akipigania kwa kiwango kikubwa, lakini *solution* ya Momba ni kutumia Mto Momba. Hivi karibuni tupo hatua za mwisho kabisa kumpata mkandarasi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Momba, tutakwenda kukabidhi mradi huo *site* kuhakikisha kwamba mkandarasi anapatikana kipindi hiki cha muda mfupi kama tulivyopanga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Igando – Kijombe ndani ya Jimbo la Wanging'ombe mkandarasi amepewa kazi tangu Septemba, 2023 wenye thamani ya shilingi bilioni 10.8. Tunataka kujua, ni lini mradi huu utaanza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge. Nataka nimhakikishie kwamba, kwa kuwa mradi huo upo katika utaratibu, utaanza mara moja. Nami nipo tayari kwenda kufuatilia na kusimamia juu ya uanzaji wa mradi huo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atatembelea Jimbo la Hanang kujionea miradi inayotekelezwa ili kuongeza kasi ya miradi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza na ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Hanang kwa ushirikiano mkubwa ambao ametupa hasa katika kipindi ambacho alipitia magumu. Namwahidi kwamba baada ya bajeti yangu nitafika katika eneo lake, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 169

**Mkakati wa Kunusuru Vyanzo vya Maji**

**MHE. ASYA SHARIF OMAR** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kunusuru vyanzo vya maji dhidi ya shughuli za kibinadamu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji inaendelea na Programu Maalum ya Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji iliyoanza mwaka 2021 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2035. Utekelezaji wa programu hiyo unashirikisha sekta zinazohusiana na maji pamoja na taasisi zake ambapo utekelezaji wake unafanyika kupitia Timu ya Kisekta ya Kitaifa iliyoundwa kwa kujumuisha sekta za maji, kilimo, mifugo, maliasili na mazingira.

Mheshimiwa Spika, kupitia programu hiyo, kazi mbalimbali za uhifadhi wa vyanzo vya maji zinatekelezwa ikiwemo kutambua vyanzo vya maji, kuweka mipaka na kuvitangaza vyanzo hivyo kwenye Gazeti la Serikali, kupanda miti rafiki wa maji kwenye vyanzo vya maji na kufanya kilimo na ufugaji rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa jumla ya vyanzo 3,285 vimetambuliwa ambapo kati ya hivyo, 317 vimewekewa mipaka na vyanzo 61 vimetangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu. Aidha, jumla ya miti rafiki 5,381,548 imepandwa katika vyanzo vya maji mbalimbali nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Sharif Omar, swali la nyongeza.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nitakuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyanzo vya maji ni jambo muhimu sana kwa maisha yetu, lakini pamoja na juhudi kubwa za Serikali ambazo wanazifanya, je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu inayohusiana na uharibifu wa vyanzo vya maji kwa kutumia mikutano ya kijamii na pia vyombo vya habari ikiwemo *TV* na redio? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kwenye hili kwa sababu wananchi wengi ambao wanatumia vyanzo vya maji inawezekana hawana ufahamu wa kuona athari za kutumia vyanzo vya maji na kufanya shughuli za kibinadamu, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli niungane na Mheshimiwa Mbunge kusema kwamba, tunapozungumzia vyanzo vya maji, maana yake ni kwamba pasipokuwepo vyanzo vya maji, hata hiyo Wizara ya Maji haipo.

Mheshimiwa Spika, nilishukuru Bunge lako Tukufu na wewe mwenyewe, kwani sisi kama Wizara tulikuja na kufanya mabadiliko ya sheria ili kuongeza umakini hasa juu ya suala zima la utoaji wa elimu na ushirikishwaji wa jamii. Nalishukuru Bunge lako Tukufu na sisi kama Wizara tumefanya mabadiliko makubwa hasa juu ya mabonde yetu ya maji.

Mheshimiwa Spika, kaulimbiu ambayo tumeisema, jamii ipo, viongozi wapo, wakishirikishwa tutafanikiwa, wasiposhirikishwa tutakwama. Huo ndiyo msingi katika kuhakikisha kwamba tunatoa elimu na kulinda na kutunza rasilimali zetu za maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 170

**Utekelezaji wa Miradi ya Maji Bukoba Vijijini**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza: -

Je, lini Miradi ya Maji katika Maeneo ya Ombweya, Rugaze, Nsheshe, Amani na Rukoma - Bukoba Vijijini itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika Wilaya ya Bukoba. Utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Vijiji vya Ombweya, Rugaze, Nsheshe, Amani na Rukoma umepangwa kufanyika kwa awamu ambapo awamu ya kwanza inahusisha uchimbaji wa visima virefu vinne katika Vijiji vya Nsheshe, Rukoma, Ombweya na Rugaze. Uchimbaji wa kisima kirefu katika Kijiji cha Nsheshe umekamilika ambapo kina uwezo wa kuzalisha maji lita 7,600 kwa saa. Aidha, utafiti wa maji chini ya ardhi unaendelea katika Vijiji vya Rukoma, Ombweya na Rugaze.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itahusisha usanifu na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika Vijiji vya Nsheshe, Rukoma,

Ombweya na Rugaze pamoja na upanuzi wa Mradi wa Maji Kibirizi kwenda Kitongoji cha Amani ambapo umepangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba kwa majibu haya niliyopata kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa hana uelewa wa kutosha kuhusu hali ya maji kule maeneo niliyotaja haya ya Ombweya, Rugaze, Rukoma, Amani na maeneo mengine. Je, nikimwomba kwamba baada ya Bunge au haraka iwezekanavyo twende aone mwenyewe hali ilivyo kule, watu wanakunywa maji yanayofanana na chai ya maziwa, atakuwa tayari? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hilo limekuja kama ombi, lakini sasa kwa maelezo aliyotoa Mheshimiwa Mbunge ni kama haya majibu siyo la swali alilouliza. Nimekuelewa vizuri Mheshimiwa Rweikiza!

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka ni kwamba, Mheshimiwa Waziri kwa majibu haya, hali ya maji kule ni mbaya sana, sasa kama hajafika na kuona mwenyewe anaweza akaendelea kunijibu hivyo, maana haya majibu siyo mara ya kwanza kujibiwa hivi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ngoja. Nataka kuelewa kwa sababu, kama swali lako halijajibiwa, haliwezi kuwa na swali la nyongeza. Maana yake jibu lije jipya, haya majibu yaliyotolewa kama unaona siyo majibu ya swali lako, ndicho ninachotaka kushughulika nacho sasa hivi. Ama ni majibu, ila wewe hujaridhika nayo, ama siyo majibu. Vijiji vilivyotajwa na miradi iliyotajwa haipo!

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, swali hili nimeliuliza leo siyo mara ya kwanza, wala siyo mara ya pili, najibiwa hivi hivi. Mwaka kesho, mwaka kesho, mwaka kesho, lakini hakuna kinachofanyika. Atakuja aone hali ilivyo kule ili aelewe vizuri zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, sawa. Sasa ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri, Mheshimiwa Mbunge ameleta ombi kwako Mheshimiwa Waziri ambalo unaweza kumjibu kwa ombi lake, lakini sasa hili jibu lililotolewa kwa hili swali, nafikiri jibu mtalileta baada ya wewe kuwa umeshaenda kule ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri kwa swali alilouliza Bunge na majibu yake. Ila kwa ombi lake wewe mjibu, lakini siyo kama swali la nyongeza kwa sababu majibu ya hili swali itabidi yaje upya. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ipo kwa minajimu ya kutatua matatizo. Mimi nipo tayari, lakini baada ya saa saba nikutane na Mheshimiwa Mbunge ili kinachohitajika kufanyika kwa haraka, tupo tayari kukifanya kuhakikisha tunanusuru wananchi katika maeneo yale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona. Hayawezi kuwepo maswali ya nyongeza kwenye majibu ambayo yamekataliwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 171

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Kata ya Karansi – Siha**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga kituo cha Polisi Kijiji cha Ashengai Kata ya Karansi – Siha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kata ya Karansi imeshatenga eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 2,023 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kata ambacho kitajengwa kwenye Kijiji cha Ashengai. Ujenzi wa kituo hicho umeshaingizwa kwenye mpango wa ujenzi wa vituo vya Polisi vya Kata vitakavyojengwa kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025 na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Katika Kata ya Karansi kumekuwa na matukio ya mauaji ya mara kwa mara. Mnamo mwaka 2016 aliuawa baba mmoja katika Kata hiyo na mnamo mwaka 2022 mwanamke mmoja alichinjwa. Je, Serikali inaongea nini au inawaambia nini wananchi wa Karansi, katika kuwasaidia ili kuepukana na matukio mazito kama hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, katika Kata hiyo hiyo kumekuwa na matukio ya uhalifu yakiongezeka sana kutokana na idadi ya wananchi waliopo. Hivi karibuni katika mwezi wa Tatu mwaka huu 2024, na mwezi huu wa Nne yamevunjwa maduka manne ya wafanyabiashara na mali za thamani ya zaidi ya shilingi milioni 48 zimepotea. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kujenga kituo kidogo cha Polisi ili kuwasaidia wananchi katika eneo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Zuena Bushiri, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii taarifa nimeipokea sasa kwamba kuna mauaji yalifanyika katika Kata hiyo, nitafuatilia kujua ni watu gani waliohusika, lakini pia ni hatua gani zilichukuliwa na Serikali kwa mauaji yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili; Jeshi la Polisi limesambaza Askari Kata ili kushirikiana na wananchi na kuboresha

ulinzi shirikishi katika maeneo yote na kuboresha doria ili kudhibiti masuala yote ya uhalifu katika Kata zetu na vijiji vyetu. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Mbunge awasihi wananchi wa Kata ya Karansi kushirikiana na Askari ili kuboresha doria katika maeneo yote ili Kata hiyo na Kata nyingine ziendelee kuwa salama, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itakamilisha jengo la Kituo cha Polisi Kata ya Mgoma Wilaya ya Ngara ambapo Kata hiyo iko mpakani mwa Burundi na Tanzania kwa ajili ya usalama zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itakamilisha vituo vya Polisi Kata 77 ambavyo tayari viko katika hatua za boma. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo chake alichokitaja pia ni moja katika vituo ambavyo vitakamilishwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kituo cha Polisi kilichopo Kengeja ni chakavu sana. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kadri ya upatikanaji wa fedha, Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa sasa hivi tunajenga vituo vya afya katika ngazi ya Kata na Jimbo la Mbulu Mjini hatuna vituo vya Polisi na katika Jimbo la Mbulu Mjini ... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, anza upya.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa sasa hivi tunajenga vituo vya Polisi katika ngazi za Kata na Jimbo la Mbulu Mjini tuna Kata 10 vijijini, lakini hatuna hata kituo kimoja cha Afya cha Kata, je… *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa umeeleweka.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Afya? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Umeeleweka Mheshimiwa, umeeleweka ni Kituo cha Polisi, ahsante sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini kwamba, ujenzi wa vituo vya Polisi vya Kata unaenda sambamba na ujenzi wa vituo vya Polisi vya Wilaya. Nimhakikishie pia kwamba, kadiri tunavyopata fedha basi tutazingatia pia ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Mbulu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hali ya kituo cha afya kule Siha, Kituo cha Polisi... *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya uhitaji wa kituo cha Polisi kule Siha inafanana kabisa na uhitaji wa Kituo cha Polisi katika Kata ya Lukozi Wilaya ya Lushoto. Ni upi mpango wa Serikali kwenda kujenga kituo cha Polisi katika Kata ya Lukozi? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ina mpango wa kujenga vituo vya afya 647 katika awamu ya kwanza na kadri fedha zitakavyopatikana... *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ni kwa sababu ninyi wenyewe mnauliza vituo vya afya, kwa hiyo, naye Mheshimiwa Naibu Waziri anawajibu vituo vya afya mlivyouliza. *(Kicheko/Makofi)*

Haya tusikilizane. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sekiboko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga kujenga Vituo vya Polisi 647 na itaendelea kujenga kadiri ya upatikanaji wa fedha kwa awamu kwa kadiri fedha zinavyopatikana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 172

**Hitaji la Gari la Zimamoto Korogwe Mjini**

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza: -

Je, lini Jeshi la Zimamoto Halmashauri ya Mji Korogwe litapatiwa Gari la Zimamoto?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Serikali imeshakamilisha taratibu zote za mkopo wenye masharti nafuu wa thamani ya Dola za Marekani milioni 100 kutoka Taasisi ya *ADEX* iliyopo Umoja wa Nchi za Kiarabu, kwa ajili ya kupata vitendea kazi mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa magari 150 ya Zimamoto na Uokoaji pamoja na vifaa kwa nchi nzima ikiwemo pia Wilaya ya Korogwe, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimea, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika swali la kwanza, imekuwa miaka mitatu sasa tangu nafuatilia gari la Zimamoto kwenye Halmashauri yangu na hadi leo sijapata majibu sahihi. Mji wa Korogwe ni kati ya Miji inayokua kwa kasi sana, majanga ya moto yanatokea na hakuna msaada wowote kwa kuwa hatuna gari la zimamoto.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni basi kubwa la abiria limeungua lote na kuteketea na nyumba ya mwananchi wangu katika Kata ya Majengo imeungua na kuteketea, hatuna msaada. Kwa hiyo, nahitaji *commitment* ya Serikali ya kweli, ni lini mtatupatia gari la Zimamoto?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tuna gari letu la Zimamoto ambalo ni chakavu sana, linahitaji matengenezo. Je, Serikali haioni haja ya kulikarabati hili gari la Zimamoto ambalo liko ili tukiwa tunasubiri hayo magari ambayo yanakuja, wakati huo tukiwa tunaokolewa kwa kutumia hili? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Kimea, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pole sana kwa wananchi wa Korogwe waliopatwa na changamoto hii ya moto, lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba, Wilaya ya Korogwe ni moja kati ya Wilaya zitakazopata gari la Zimamoto katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, kati ya magari 150 ambayo nimeyasema.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu utengenezaji wa gari ambalo liko kwenye matengenezo, nikitoka hapa nitalifuatilia kuhakikisha gari hili linapatikana ili liendelee kutoa huduma katika Wilaya ya Korogwe, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali italeta gari la Zimamoto katika Mkoa wa Manyara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tunanunua magari 150 ambayo tutayapeleka kwenye mikoa yote ambayo haina magari hayo ikiwemo Mkoa wa Manyara, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inanunua magari 150 kupeleka kwenye Halmashauri zote, je, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama itapata?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, katika magari 150, zitapata Halmashauri zote ambazo ni Wilaya zote 139 na Mikoa ambayo pia haina, ikiwemo Halmashauri ya Kahama katika Mkoa wa Shinyanga, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili iweze kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Maswa ni Wilaya kongwe, lakini haina Kituo cha Polisi. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo itabidi umletee majibu ya msingi kwa sababu swali la nyongeza hilo lilikuwa linahusu swali ambalo tayari limeshapita. Kwa hiyo, Mheshimiwa Esther Midimu swali lako ulilete kama swali la msingi.

Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mbeya kuna baadhi ya Wilaya zina changamoto za gari la Zimamoto, hasa Wilaya ya Chunya, kuna shida sana ya gari la Zimamoto. Je, ni lini mtapeleka gari la Zimamoto katika Wilaya ya Chunya? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suma Fyandomo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimesema katika mwaka wa fedha 2024/2025, tunatarajia kununua magari 150 na Wilaya ambazo ziko 139. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya

aliyoitaja itapata pia gari la Zimamoto na Uokoaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 173

**Msongamano wa Abiria na Mizigo Bandari ya Dar es Salaam**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kutatua changamoto ya msongamano wa abiria na mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwenda Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TPA* inafanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya kufanya maboresho ya ujenzi wa miundombinu ya kuhudumia abiria na shehena za mwambao pamoja na meli za utalii zikiwemo zile ziendazo Zanzibar. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali inategemea kukamilika mwezi Mei, 2024. Kazi hizi zinafanyika ili kuboresha Bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto ya msongamano wa abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuendeleza miundombinu hiyo kwa ubia na sekta binafsi ili kuikamilisha kwa wakati na viwango vyenye ubora wa usalama ambapo kutapunguza gharama kwa Serikali. Kukamilika kwa miundombinu ya kuhudumia meli na mizigo na abiria kutakuwa ni suluhisho la kudumu ambapo kutavutia meli nyingi za utalii kutumia Bandari ya Dar es Salaam.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Waziri wangu wa Miundombinu kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa sasa hivi, yana kina ndani yake. Kama ingelikuwa sitaki kumwuliza swali lingine, basi ilikuwa mimi niseme basi, maana nimeridhika nalo, lakini nina swali moja dogo la nyongeza nimpe Waziri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga meli Maziwa Makuu, je, ni lini itajenga meli ya baharini kwa ajili ya abiria na mizigo ikiwemo kwenda Zanzibar? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inamiliki meli pamoja na Serikali ya China kwa hisa ya 50% kwa 50%, ambayo ilijengwa mwaka 1967. Kwa sasa kutokana na umuhimu mkubwa wa usafiri kwenye Mwambao wa Pwani, kwa maana ya Malindi, Comoro, Tanga, Pwani, Zanzibar na maeneo mengine, Serikali ipo kwenye hatua ya upembuzi yakinifu katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 ili kufahamu gharama, wahitaji na fursa zilizopo katika bahari yetu, hatimaye kuweza kuanza kununua meli hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha marekebisho katika Uwanja wa Ndege wa Arusha, kwa kuwa Arusha ni sehemu kubwa kwa ajili ya watalii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo inabidi liletwe kama swali la msingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Catherine Magige utajibiwa kama swali la msingi.

Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wananchi wa Mkoa wa Geita wanategemea Bandari ya Mwanza na Bukoba. Sasa Mkoa wa Geita unakua na unajitegemea; tunalo eneo zuri kabisa la bandari ambayo haijaboreshwa ya Nkome ambayo ingetumika kushusha mizigo kutoka Kenya na Uganda. Je, Serikali ina mpango gani wa kuiboresha Bandari ya Nkome ili wananchi wa Mkoa wa Geita tuweze kuitumia kushusha mizigo yetu kutoka nje? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, tayari Serikali inafanya maboresho makubwa kwenye Ziwa Victoria kwa namna mbili; moja, tunajenga Bandari ya *North* Mwanza, Bandari ya Kemondo na Bandari ya Bukoba pamoja na kununua meli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha hatua hiyo, tutakwenda kwenye hatua ya pili ya kutazama maeneo mengine kulingana na uhitaji wake ambayo ni pamoja na eneo la Nkome ambalo Mheshimiwa Mbunge ameulizia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 174

**Taasisi Zinazotoa Mkopo kwa Riba Kubwa**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani kufuatilia na kuchukua hatua kwa Taasisi za Fedha zinatoa mikopo yenye riba kubwa kinyume na mwongozo wa *BOT*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisera, kiutawala na kisheria ili kudhibiti tabia ya baadhi ya taasisi za fedha kutoa mikopo kinyume na miongozo iliyopo. Hatua hizo ni pamoja na:

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Fedha inayolenga kusimamia ukwasi katika mfumo wa kibenki ili kuendana na mahitaji halisi ya kiuchumi na kuweka mazingira rafiki ya utoaji mikopo.

(ii) Kuendelea kuhimiza benki kuwasilisha taarifa za wakopaji pamoja na kutumia kanzidata ya taarifa za wakopaji wakati wa uchambuzi wa maombi ya mikopo ili kupunguza vihatarishi vya ongezeko la mikopo chechefu.

(iii) Kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya fedha ili kumsaidia mwananchi kufanya maamuzi sahihi kuhusu fursa za mikopo zilizopo, viwango vya riba na athari zake, vigezo vya kuzingatia na umuhimu wa kurejesha mikopo.

(iv) Kuitisha vikao mbalimbali vya majadiliano na wadau katika sekta ya fedha ili kutambua changamoto zilizopo na kushirikishana mikakati ya kukabiliana nayo; na

(v) Kufanya kaguzi, ufuatiliaji na tathmini ya uzingatiaji wa sera, sheria na miongozo iliyopo ili kuboresha na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wale wanaobainika kukiuka taratibu hizo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kumekuwa na hii mikopo kila mahali na ina athari kubwa kwa wanawake na vijana. Mikopo hii imesababisha wengi kupata tatizo la afya ya akili na ndoa nyingi kuvunjika. Mheshimiwa Waziri, haoni ni wakati mwafaka sasa hivi kukomesha mikopo hii ili kunusuru wananchi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na kuwepo kwa Sheria ya Mwongozo wa Benki Kuu wa Mwaka 2018 na Kanuni ya Mwaka 2019, bado mikopo hii imeendelea kuwepo hasa Kausha Damu katika mikoa zaidi ya 17 na hasa Mkoa wa Kilimanjaro, Jimbo la Moshi Vijijini. Nini kauli ya Serikali kulingana na hawa wanaokiuka sheria hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Njau kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana kwa kufuatilia jambo hili. Serikali inatoa maelekezo kwa taasisi hizo kuacha mara moja mwenendo huu na Serikali itafuatilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili, naagiza na kuelekeza *BOT* wafuatilie kwa karibu sana, kama kuna taasisi yoyote ambayo inaenda kinyume na sheria, Serikali haitakuwa na muhali kwa yeyote yule ambaye anaenda kinyume na sheria na taratibu ikiwemo kufuta leseni ya taasisi hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa makampuni ya simu sasa ndiyo yanaongoza kwa kutoa hiyo mikopo ya haraka haraka bila kujaza fomu wala chochote; vijana wetu ni

wengi ambao inakuwa kivutio na pia akina mama wajasiriamali wakiwepo akina mama wa Mkoa wa Kilimanjaro, lakini mikopo hiyo ni Kausha Damu. Ni lini makampuni haya yatalazimishwa kutoa elimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally, mama yangu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu siku hadi siku kupitia vyombo vya habari tofauti, lakini hasa na taasisi zetu za kifedha ikiwemo Benki Kuu.

**SPIKA:** Sasa hapo unajua yametajwa makampuni yanayotoa huduma za simu na nadhani hayo yanajulikana. Kama na yenyewe yanaingia kwenye huu mfuko wa kuitwa na yenyewe yanatoa Kausha Damu, nadhani mnaweza kuanza nayo. Kama sivyo hatutakuwa pia tumetenda haki hapa Bungeni kuwataja wao kama na wenyewe ni Kausha Damu wakati wale mnawafahamu na nafikiri wanafuata taratibu zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo mimi nadhani nikupe muda katika hiki kipindi kifupi ujaribu kufuatilia hapo nje, kwa sababu hatutataka tujikute tunayajadili makampuni humu ndani, wakati yanafuata taratibu zenu na najua yamesajiliwa. Hawa wanaosemwa huku ni wale wanafanya mambo ya kienyeji hivi ambayo hayafai.

Sasa makampuni ya simu napata wasiwasi kidogo, kwa hiyo, nitakupa nafasi hapa tukishamaliza haya maswali ukalifuatilie jambo hilo kwa sababu sitataka nianze kupokea barua za malalamiko kwamba na sisi tumeambiwa tunatoa mikopo ya Kausha Damu.

Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Je, Serikali ina mkakati gani kuelekeza Benki za *NMB*, *NBC* na *CRDB* kufungua matawi eneo la Kikatiti ambao ni mji unaokua

kwa kasi na pia umezungukwa na watu wengi sana wa Kata za Mararoni, King'ori na Maji ya Chai? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuwa naangalia swali la msingi linasemaje, na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Hilo nalo litajibiwa kama swali la msingi badala ya kuwa swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Utusaidie sasa kwenda kufuatilia hilo la makampuni ya simu yanayotoa mikopo. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 175

**Muswada wa Kuwalinda Watumiaji wa Bidhaa na Huduma Nchini**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawasilisha Bungeni Muswada wa kutunga Sheria ya kuwalinda watumiaji huduma na bidhaa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sheria ya kuwalinda watumiaji wa bidhaa na huduma ipo, ambayo ni Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003. Utekelezaji wake unasimamiwa na Tume ya Ushindani *(FCC)*. Kimsingi, sheria hiyo inabeba masuala makuu mawili, ambayo ni ushindani na kumlinda mtumiaji wa huduma na bidhaa katika soko la Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa sheria hiyo, vilevile kuna sheria nyingine za kisekta ambazo zinasaidia kuwalinda watumiaji katika sekta husika. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003 ili iweze kuendana na wakati wa sasa, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali lililotangulia lilikuwa linahusu masuala ya watumiaji na mikopo. Sasa ni lini Serikali kutokana na umuhimu wa watumiaji itatenganisha masuala ya ushindani na masuala ya watumiaji ili tuweze kuwalinda watumiaji wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Tanzania tunazalisha bidhaa. Ili kuuza ile bidhaa, watumiaji inabidi wanunue. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha watumiaji wa Tanzania wanunue na kutumia bidhaa na huduma zilizozalishwa hapa nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sheria hii tuliyoitaja inasimamia ushindani wa haki pamoja na kuwalinda walaji. Uzoefu unaonesha kwamba nchi nyingi duniani zinatumia sheria hii moja ambayo inachukua maeneo mawili kwa maana ya ushindani wa haki katika soko, lakini pia kupitia humo kumlinda mlaji, kwa sababu tunapitia sheria hii, pale ambapo tunaona kuna haja ya kutenganisha kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri, basi Serikali haitasita kufanya hivyo na tunachukua ushauri wake, lakini pia na wadau wengine ambao watatoa maoni wakati tunaihuisha au tunarekebisha Sheria hii Na. 8 ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli sisi kama Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, tayari tuna mikakati mbalimbali. Moja ya kaulimbiu yetu katika kuhakikisha tunakuza Sekta ya Viwanda na Uzalishaji nchini ni, *"Nunua Tanzania, Jenga Tanzania,"*

kwa maana ya nunua bidhaa zilizozalishwa Tanzania ili uweze kuijenga nchi yako Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kufanya hivyo, lakini kwa kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zina ubora unaotakiwa ili ziweze kushindana na bidhaa zinazotoka nje, kwa sababu ili kuhakikisha Watanzania wanapenda bidhaa zao za ndani, lazima ziwe na ubora ule ambao unalingana na bidhaa nyingine kutoka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kuhakikisha tunatangaza hilo, lakini kuhakikisha bidhaa zetu zinazalishwa katika ubora unaotakiwa, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 176

**Kuweka Vizimba Ziwa Tanganyika**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka vizimba Ziwa Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika ziwa huanza kwa kuainisha maeneo yanayofaa kwa kuzingatia vigezo vya kitaalamu na kisheria kwa lengo la kulinda ikolojia ya ziwa. Mpaka

sasa Serikali kwa kushirikiana na taasisi ya *The Nature Conservancy* imeainisha maeneo matano yanayofaa kwa ufugaji wa samaki kwa vizimba katika Ziwa Tanganyika. Maeneo hayo ni Katabe, Kalalangabo, Kirando, Kimbwela na Kigalye. Aidha, katika mwaka 2023/2024, Wizara imetenga kiasi cha jumla ya shilingi 233,500,000 kwa ajili ya kuendelea kuainisha maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* itatoa mkopo wa masharti nafuu kwa vizimba 29 kwa vikundi na watu binafsi walioomba na kukidhi vigezo. Mgawanyo wa vizimba hivyo ni kama ifuatavyo: Kigoma vizimba 25, Rukwa vizimba viwili na Katavi vizimba viwili.

Mheshimiwa Spika, aidha, zoezi hili ni endelevu ambapo katika mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Kilimo itaendelea kutoa mikopo kwa vikundi na wananchi ambao wataomba na kukidhi vigezo vya mkopo wa vizimba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, tunaishukuru Serikali kwa kutenga hiyo pesa kwa ajili ya kuwakopesha wavuvi, lakini bado wavuvi wetu hawana elimu ya mikopo. Je, Serikali ipo tayari kwenda kutoa elimu ya mikopo kabla haijatoa mikopo hiyo ili wavuvi wafahamu vigezo na masharti ili waweze kupatiwa hivyo vizimba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mwaka jana hapa tulizuia, Wabunge walitusaidia kuzuia kufungwa kwa Ziwa Tanganyika. Leo kuna sintofahamu kwa wavuvi wa ukanda wa Ziwa Tanganyika; Kigoma, Rukwa na Katavi. Wananchi na wavuvi wana taharuki kwamba ziwa linakwenda kufungwa. Je, ni ipi kauli ya Serikali ya

kuwaondoa hofu wananchi wa ukanda wa Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nianze na hili la kwanza la kutoa elimu kwa wavuvi. Ni kweli elimu ni muhimu sana, lakini nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge, miezi sita iliyopita mimi na Mheshimiwa Waziri na wataalamu wa Wizara ya Mifugo, tulifanya zoezi la kuzunguka katika maeneo yote ya pembezoni mwa Ziwa Tanganyika, lengo likiwa ni pamoja kuhamasisha wavuvi wetu kuwapa elimu juu ya namna gani wanaweza wakakopa vizimba na boti.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo tuliacha wataalamu wetu kwenye maeneo ya vijiji vyote vya wafugaji wakaendelea kutoa elimu inayohusiana na mikopo na namna ya uendeshaji wa vizimba. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama kuna eneo ambalo anafikiri bado hawajapata elimu ya kutosha, Wizara ya Mifugo kupitia Serikali tupo tayari kuendelea kutoa elimu hiyo ya mikopo na namna ya kuendesha vizimba hivyo na boti pia. Kwa hiyo, naomba katika hilo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tupo tayari kushirikiana naye katika kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, hili la pili, kuhusiana na kufunga Ziwa Tanganyika, kwanza ni kweli lazima tukubaliane mazao ya samaki katika Ziwa Tanganyika yanapotea na namna pekee ya kuyalinda ni pamoja na kuzuia shughuli za uvuvi katika maziwa yetu. Sasa tukiruhusu wavuvi waendelee kuvua na hali inazidi kuwa mbaya, samaki wanazidi kupotea, kwa kweli hatutakuwa tunaitendea haki Sekta hii ya Uvuvi. Kwa hiyo, tukafikiri kwamba pengine ni lazima tusimamishe shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika ili kuruhusu mazalia ya Samaki yaweze kuchukua nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, awe balozi mzuri katika hili. Hili lina lengo jema kwa sababu hata baada ya kufungua watakaonufaika katika zoezi hili ni hao hao wavuvi wanaoishi katika maeneo hayo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hiyo sehemu ya pili ya kufunga Ziwa labda kama mmekubaliana na nchi jirani. Kama hawafungi, sina hakika kama kuna mpaka wa samaki kwenda upande mwingine, wao wakaendelea wakati ninyi huku mmefunga. Yaani wavuvi wetu huku wawe wanalinda samaki kwa ajili ya wale wengine, ama mmekubaliana na nchi jirani kwamba wote uvuvi utasimama kwa muda halafu uvuvi utaanza baadaye? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Ziwa Tanganyika kama tunavyofahamu, linamilikiwa na nchi tatu: Zambia, Kongo na Tanzania. Hii ya kufunga, tarehe 15 Mei ni Mkataba wa Kimataifa dhidi ya nchi hizi zinazozunguka Ziwa Tanganyika kwamba ifikapo tarehe 15 mwezi Mei, lazima ziwa lote lifungwe katika nchi zote zinazozunguka katika ziwa hili.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, sisi Tanzania pamoja na kwamba mkataba huu tulisaini, tulikuwa hatujawahi kuutekeleza, lakini wenzetu wamekuwa wakifunga ziwa na sisi tukasema, basi kwa mwaka huu tuanze kutekeleza mkataba huu ambao tumeshausaini siku nyingi na hatujawahi kuutekeleza. Kwa hiyo, kwa mwaka huu tunaanza kuutekeleza kuanzia tarehe 15 Mei na kuendelea kwa muda wa miezi mitatu, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa ufafanuzi huo. Mheshimiwa Joseph Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Je, ...

*(Hapa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi alianza kuondoka kwenye podium)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali lako hili. Mheshimiwa Joseph Tadayo, swali la nyongeza. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali italeta mradi huo wa ufugaji wa samaki kwa vizimba katika

Jimbo langu la Mwanga katika Bwawa la Nyumba ya Mungu na Ziwa Jipe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba vizimba vinaambatana kwanza na hatua mbalimbali; hatua ya kwanza ni kufanya uchunguzi kama eneo hilo linaruhusu kuweka vizimba halafu baadaye ndiyo inakuja hatua hiyo ya pili.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatuma timu ya wataalamu kwenda kufanya uchunguzi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu na baada ya uchunguzi huo tutakuja na majibu kama je, eneo hilo linafaa kwa ajili ya vizimba ama la, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi sasa aulize swali lake.

Na. 177

**Mchango wa Lugha ya Kiswahili kwenye Kukuza Diplomasia ya Uchumi**

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR** aliuliza: -

Je, upi mchango wa Lugha ya Kiswahili kwenye kukuza Diplomasia ya Uchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili kwa sasa ni lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Umoja wa Afrika. Aidha, kwa sasa kila tarehe 7 ya mwezi Julai ya kila mwaka inaadhimishwa kama siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Lugha ya Kiswahili ni nyenzo muhimu katika kuwezesha mawasiliano duniani hususani katika shughuli za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, kitafiti na kisayansi. Hali hii inachangia moja kwa moja katika Diplomasia ya Uchumi kupitia ajira za wataalamu wa ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili, lakini pia huduma za ukalimani na tafsiri katika mataifa na mikutano mbalimbali na pia kutumika kama vyenzo wezeshi katika biashara.

Mheshimiwa Spika, aidha, lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika katika maelezo ya bidhaa mbalimbali na ushawishi wa Tanzania katika majukwaa ya kimataifa, machapisho ya vitabu na tafiti mbalimbali za kisayansi ambayo yamekuwa yakiuzwa na kuongeza pato la mtu mmoja mmoja na kuchangia pato la Taifa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, swali la nyongeza.

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa ridhaa yako naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa licha ya kwamba mtandao huu wa *Google* umekuwa ukitusaidia sana kutoa tafsiri ya lugha mbali mbali duniani kuja katika Lugha ya Kiswahili, lakini bado tafsiri ile haikidhi viwango na vigezo vya tafsiri sanifu ya Lugha sanifu ya Kiswahili. Sasa je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kufanya jitihada zozote ili kukiwezesha Kiswahili chetu sasa kuwa na sura ile ya kimataifa kwenye kuki-*brand?*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, kuna ithibati yoyote ya uwepo wa vituo vya utamaduni *(cultural centers)* katika hizi balozi zetu

mbalimbali duniani; na zinatoa mchango gani hizi *cultural centers* katika kuukuza na kuutangaza utalii wetu hususani katika kuueleza utamaduni wa Mswahili, Waswahili, Uswahilini na hata asili ya neno "Mswahili"? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa jinsi anavyoipambania Lugha ya Kiswahili hasa katika kuibidhaisha kimataifa na mara nyingi amekuwa akitoa michango na kuuliza sana masuala yanayohusu Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Google translation* au kuhusu tafsiri ya *Google* ni kweli kwamba Serikali inatambua mchango mkubwa wa tafsiri ya *Google* katika kukuza na kuiendeleza Lugha ya Kiswahili, lakini ni kweli kwamba baadhi ya wakati hii *Google translation* inakuwa haitoi lugha fasaha na sanifu. Hivyo basi, Serikali inafanya kila jitihada ili kuhakikisha kwamba tafsiri ambayo inakuwepo katika *Google translation* inakuwa fasaha na sanifu zaidi kuliko hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusiana na ithibati ya hivi vituo vya utamaduni katika Balozi zetu mbalimbali huko nje, kwanza naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara yetu imekuwa mdau mkubwa katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kubidhaaisha Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Kupitia mkakati huo sasa hivi tayari kuna Balozi 16 za Tanzania ambazo zimefungua vituo vya utamaduni na kufundisha lugha ya Kiswahili nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kukufahamisha kwamba hivi vituo vyote tayari vina ithibati kutoka Baraza la Kiswahili la Tanzania (BAKITA) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA).

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nitaleta matangazo kwenu kabla hatujaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni tangazo la wageni na tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika na tutaanza na wageni wa Spika kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Yupo Mheshimiwa Mwanaisha Khamis Juma ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mheshimiwa Abdallah Hussein Kombo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Namwona pale Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ameenda kuwa mwenyeji mzuri, amekaa nao kule juu, ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wameongozana na Ndugu Fatma Omar Ali ambaye ni Katibu Mezani na yupo pia Ndugu Said Khamis Ramadhan, Katibu Mezani, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na tutaanza na Ndugu Felchesmi Mramba ambaye ni Katibu Mkuu; yuko Dkt. James Mataragio - Naibu Katibu Mkuu; yupo Dkt. Rhimo Nyansaho - Mwenyekiti wa Bodi *TANESCO,* yupo Mheshimiwa Balozi Ombeni Sefue, Mwenyekiti wa Bodi ya *TPDC;* yupo Mheshimiwa Balozi Meja Jenerali Jacob G. Kingu, Mwenyekiti wa Bodi *REA;* na yupo Profesa Mark Mwandosya, Mwenyekiti wa Bodi, *EWURA,* ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Profesa Shupi Kaijage ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi, *TGDC;* yupo Ndugu Fadhili Manongi ambaye ni Mjumbe wa Bodi - *EWURA CCC;* yupo Dkt. Lutengano

Undule Mwakahesya ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi - *PBPA;* yupo Ndugu Francis Mwakapalila ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi - *TANOIL;* yupo Ndugu Emmanuel Gilbert, Mwenyekiti wa Bodi *GASCO;* na yupo Dkt. James Andilile, Mkurugenzi Mkuu - *EWURA*. Haya, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni Ndugu Gerald Maganga - Mkurugenzi wa Petroli, *EWURA;* Mhandisi Gissima Nyamuhanga, Mkurugenzi Mkuu *TANESCO;* Bwana Mussa Makame, Mkurungezi Mkuu *TPDC*; Mhandisi Hassan Said, Mkurugenzi Mkuu *REA;* Mhandisi Charles Sangweni, Mkurugenzi Mkuu *PURA;* Bwana Erasto Simon, Mtendaji Mkuu *PBPA;* Mhandisi Mathew Mwang'ombe, Meneja Mkuu *TGDC*; Mhandisi Sadock Mugendi, Meneja Mkuu *ETDCO,* Mhandisi Yusuph Kitivo, Meneja Mkuu *TCPM* na Mhandisi Baltazar Mrosso, Meneja Mkuu *GASCO,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ambaye ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, na hawa ni viongozi wa chama na Serikali kutoka Wilaya ya Bukombe, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya, Mhandisi Pascas Muragila, karibu ni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali ambao ni wageni wenu Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na wageni 16 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambaye ni Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, na hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoa Wilaya ya Butiama, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ambaye ni ndugu yake kutoka Unguja Kusini, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa ambaye ni rafiki yake, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni wanafunzi kutoa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni wafanyakazi wa *TANESCO* kutoka Mbozi, Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi) (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ighondo Ramadhani ambao ni familia yake kutoka Singida Kaskazini. Hapa pameandikwa familia yake, sasa sijajua kama mke yupo hapo ama vipi? Kwa hiyo, kwa kuwa hajasema hapa, basi ni familia yake, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wanane wa Mheshimiwa Cecilia Paresso ambacho ni kikundi cha Wajasiriamali wa *Royal Queen* kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 65 wa Mheshimiwa Juliana Shonza ambao ni Wenyeviti wa Umoja wa Wanawake Tanzania Kata kutoka Wilaya ya Momba na Tunduma, Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Kikundi cha Mtetezi wa Mama kutoka Mkoa wa Katavi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo na tutaanza na wanafunzi 149 na walimu tisa wa Shule ya Msingi *Fransalian Primary school* kutoka Morogoro, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi kumi wa itifaki kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika hawa wanafunzi wa *Fransalian* kutoka Morogoro, yupo binti wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, anaitwa Joan Joseph Mhagama. Sijui ndio yupi? Karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania *(TWPG)* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanawake kwamba

leo tutakuwa na kikao saa 7.00 mchana na kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti anawatangazia kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wanawake tukutane hapo ikiwa ni pamoja nami. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, aje awasilishe hoja ya Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2024/2025. Kabla sijaendelea naomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2024/2025. Aidha, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kama Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati katika Serikali ya Awamu ya Sita kuwasilisha hotuba hii, kipekee napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, uteuzi huu ni dhamana na heshima kubwa kwangu katika kuhakikisha kuwa sekta ya nishati inakidhi matarajio ya Watanzania ya kupata umeme wa uhakika pamoja na kuendeleza rasilimali za mafuta na gesi kwa maendeleo na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuahidi kuwa kwa kadiri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha, nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi na uaminifu mkubwa ili ndoto ya Mheshimiwa Rais, pamoja na Bunge lako Tukufu iweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 Februari, 2024 Taifa letu lilimpoteza aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi. Aidha, kabla ya hapo, tarehe 10 Februari, 2024 Taifa lilimpoteza aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, naungana na Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia, ndugu, jamaa, marafiki wote kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi wetu hawa, tuliwapenda.

Mheshimiwa Spika, Julai Mosi, 2023, Bunge lako Tukufu lilimpoteza Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali. Aidha, tarehe 8 Aprili, 2024, Bunge lako lilimpoteza Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani, Zanzibar. Naungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia ya Marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wote walioguswa na misiba hiyo. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wote mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, vilevile naungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kuwapa pole Watanzania wenzetu waliopatwa na majanga mbalimbali katika mwaka 2023/2024,

ikiwemo mafuriko na maporomoko ya mawe na matope katika maeneo ya Hanang Mkoani Manyara, Kibiti na Rufiji Mkoani Pwani pamoja na Malinyi, Ulanga, Ifakara na Mlimba Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango; na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa uongozi na juhudi zao katika kuleta maendeleo ya Taifa letu na kwa ushirikiano na miongozo wanayonipa katika kusimamia na kutekeleza majukumu yangu katika Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nikiri kuwa maelekezo na miongozo yao vimekuwa ni msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya sekta ya nishati. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*. Hii ni heshima kubwa na Tunu kwa Watanzania wote kwa ujumla kwa kuthaminiwa na kutambuliwa katika medani za Kimataifa. Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu ili azidi kukupa nguvu na hekima zaidi katika kutekeleza majukumu yako kama walivyokuchagua na wanavyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii vilevile kuwapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge lako chini yako. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* Katibu wa Bunge kwa usimamizi wa shughuli za Bunge. Ni dhahiri chini ya uongozi wenu, Bunge letu limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ipasavyo katika kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza wajibu wa kuwaletea maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Jerry William Silaa aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo; na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawapongeza Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Wote hawa nawatakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao haya mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo na watu wa Mbarali ili aweze kuwa mwakilishi wa jimbo hilo. Hakika ni heshima kubwa aliyopewa na wananchi wa Mbarali, na kwa kweli tunamtakia kila la heri katika kutekeleza jukumu lake na uwakilishi wake uliotukuka kwenye Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza sana Mheshimiwa. Dkt. David Mathayo David, Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao, ushauri na maoni yao katika kuisimamia kwa dhati sekta ya nishati kwa manufaa ya uchumi na kijamii kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge na Naibu Waziri wa Nishati kwa kuendelea kunisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. Napenda kumshukuru kwa dhati Katibu Mkuu Mhandisi, Felchesmi Mramba kwa utendaji kazi wake mahiri na ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Dkt. James Peter Mataragio kwa kuteuliwa na Rais kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati. Nawashukuru pia Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zilizo chini ya Wizara ya Nishati, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara kwa ujumla kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Wizara hii ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana watu wema wa Jimbo la Bukombe kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge wao. Kutokana na majukumu mbalimbali ya kitaifa, kuna wakati wananikosa jimboni, lakini wema wao, uvumilivu wao na kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa. Nawaahidi kuendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu katika kutekeleza majukumu ya Jimbo letu la Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana tena kwa dhati mke wangu mpenzi Benadetha Clement Mathayo pamoja na watoto wetu kwa upendo wa dhati walio nao kwangu. Wamekuwa wavumilivu katika kipindi chote ninapokuwa natekeleza majukumu, na wao kukubali kubeba sehemu ya majukumu yetu ya kifamilia ambayo ningepaswa kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kuvishukuru na kuvipongeza vyombo vya habari vikiwemo redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa kama Wizara kwa mwaka unaoishia 2023/2024. Vyombo hivyo vimekuwa mstari wa mbele katika kufuatilia kwa karibu miradi na shughuli zinazotekelezwa na Wizara, pia kuelimisha pamoja na kuhabarisha umma kuhusu mafanikio yaliyopatikana. Ni matumaini

yangu kuwa ushirikiano huu ambao umekuwepo utazidi kuimarika kwa mwaka wa fedha unaokuja kwa manufaa ya Taifa letu na wananchi kwa ujumla ili upatikanaji wa taarifa zilizo sahihi ziweze kuwafikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2023/2024 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka unaokuja 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha; kwanza, Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara, na pili, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka unaokuja 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2023/2024 uliongozwa na vipaumbele mbalimbali. Vipaumbele hivyo vilijikita katika kukamilisha miradi mbalimbali ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme na kuendelea kuchukua hatua nyingine za kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara inaendelea kupeleka umeme vijijini, katika vitongoji, na katika visiwa na maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa; ama kupeleka pia umeme kwenye vituo vya afya, pampu za maji, maeneo ya wachimbaji wadogo wa madini, maeneo ya kilimo, viwanda na shule, Mahakama za Mwanzo Vijijini, pamoja na kutekeleza mikakati na programu mbalimbali ili kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking)* nchini.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vingine vilikuwa ni kuanza maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia ya Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG);* kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda Hadi Tanga – Tanzania, mradi ule unaoitwa *(EACOP),* shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati, usambazaji wa gesi asilia viwandani, majumbani na nchi jirani, kuimarisha matumizi ya gesi asilia iliyoshindiliwa katika magari pamoja

na kunadi vitalu vilivyo wazi katika maeneo ya nchi kavu na bahari ili viweze kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ilielekeza pia kwa nguvu katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa ya mafuta na petroli, kutokana na umuhimu wake katika ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja kuimarisha ufanisi wa shughuli za bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, sehemu B ya Hotuba yangu ukurasa wa 8 - 119 inaeleza kwa kina utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na mafanikio yaliyopatikana ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme pamoja na shughuli za utafutaji, uendelezaji, usambazaji na matumizi ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya matumizi ya Wizara na mtiririko wa fedha kwa mwaka 2023/2024, Wizara ya Nishati iliidhinishiwa kiasi cha jumla ya shilingi 3,048,632,519,000 ambapo shilingi 2,609,156,128,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi 87,929,698,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2024, Wizara ilipokea jumla ya shilingi 1,813,026,147,000 ambazo zilikuwa zimeshapokelewa, ambapo shilingi 27,079,026,716 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,787,947,120,440 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spka, naomba nielezee kidogo sekta ndogo ya umeme na nishati jadidifu, uzalishaji wa umeme, kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji. Mafanikio yafuatayo yalipatikana katika mwaka wa fedha 2023/2024;

(i) Uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa kwenye mfumo wa gridi ya Taifa umeongezeka na kufika *Megawatt* 2,138 Machi, 2024 kutoka megawati 1,872.1 zilizokuwa zinazalishwa mwaka 2022/2023, hili likiwa ni ongezeko la 14.2%;

(ii) Kuanza uzalishaji wa umeme kupitia Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 ambapo tayari uzalishaji umeanza na megawati 235 kupitia mtambo Na. 9 tayari umekamilika. Aidha, matarajio ni kuwa mradi huu utakamilika Desemba, 2024 ambapo mitambo yote nane yenye uwezo wa kuzalisha *Megawatt* 235 kila mmoja itakuwa tayari kuzalisha umeme;

(iii) Kukamilika kwa ujenzi wa mitambo ya kufua umeme ya Kinyerezi I *Extension* ya *Megawatt* 185 ambapo kwa sasa mitambo yote minne inafua umeme kiasi cha megawati 40 kila mmoja na hivyo kuwezesha uzalishaji wa umeme kuingizwa kwenye gridi ya Taifa;

(iv) Kukamilika kwa mradi wa uzalishaji umeme wa kutumia maji wa Rusumo wa megawati 80 unaliojengwa kwa ushirikiano wa nchi tatu za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa wa umeme wa kila nchi, ambapo kukamilika kwa mradi huu kumeiwezesha nchi yetu kupata megawati 27 kutoka kwenye mradi huo;

(v) Ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa jua Mkoani Shinyanga wa megawati 150 unaendelea na matarajio ni kuwa mradi huo utaweza kuzalisha ifikapo Januari, 2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliendelea na utekelezaji wa miradi mingine ya uzalishaji umeme ikiwa ni pamoja na Mradi wa Malagarasi (megawati 49.5), Ruhudji (megawati 358), Rumakali (megawati 222), Kakono (megawati 87.8) na Kikonge (megawati 321) ambapo hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake ni kama ilivyofafanuliwa kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, umeme ukishazalishwa, hauna budi kusafirishwa na kusambazwa ili uweze kuwafikia watumiaji. Hivyo ni muhimu kuchukua hatua madhubuti za kukamilisha miundombinu mbalimbali ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Kutokana na hatua hizo zilizochukuliwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 za kuimarisha miundombinu hii, yafuatayo ni mafanikio yaliyopatikana:-

(i) Miundombinu ya kusafirisha umeme imeongezeka na kufikia jumla ya kilometa 7,745.4 ikiwa ni ongezeko la 21.7% ikilinganishwa na kilometa 6,363.3 za mwaka 2022/2023;

(ii) Kuanza kutumika kwa njia ya kusafirisha umeme wa kilovoti 400 kutoka Julius Nyerere hadi Chalinze pamoja na kituo kipya cha kupoza umeme cha Chalinze cha Kilovoti 400/210/132 kinachotumika kupoza na kusafirisha umeme unaotoka kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere;

(iii) Kukamilika kwa 99% kwa njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya *SGR*;

(iv) Kukamilika kwa 99.4% kwa Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga. Aidha, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Arusha hadi Namanga yenye urefu wa kilometa 114.3 umefikia 97.5% na kituo cha kupoza umeme cha Lemugur kimekamilika kwa 100% na kuwashwa;

(v) Miundombinu ya kusambaza umeme imeongezeka na kufikia kilometa 176,750.9, ikiwa ni ongezeko la 4.9% ikilinganishwa na kilometa 168,548.5 ya mwezi Mei, 2023;

(vi) Jumla ya wateja 4,784,297 wameunganishwa na umeme hadi kufikia Machi, 2024 ikiwa ni ongezeko la 9.4% ikilinganishwa na wateja 4,319,258 waliokuwa wameunganishwa na umeme Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya kusafirisha umeme iliyoendelea kutekelezwa ni pamoja na mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi; ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma *(TAZA);* ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma na Mradi wa Kuimarisha gridi ya Taifa

*(National Grid Stabilization Projects),* Gridi Imara, ambao na wenyewe umeendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma ya umeme kwa wananchi kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanua kituo cha huduma kwa wateja *(Call Center)* kwa kuongeza vifaa vya kupokea simu kutoka wakala 63 hadi 100; kuanzisha mfumo unaomwezesha mteja kuhudumiwa kwa haraka zaidi bila kupiga simu kwa njia ya ujumbe wa simu *(CHATBOT);* na kuanzisha mfumo utakaowawezesha wateja kupata taarifa maalumu ya hali ya upatikanaji wa umeme kwa haraka kwa njia ya ujumbe wa simu ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

Mheshimiwa Spika, nieleze kidogo upelekaji wa nishati vijijini. Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha upatikanaji wa nishati vijijini ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 jumla ya vijiji 11,837 sawa na 96.37% ya vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara tayari vimeunganishwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, aidha, ikiwa ni hatua ya kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi, jumla ya taasisi 63,509 zinazotoa huduma mbalimbali za kijamii ikiwemo elimu, biashara, pampu za maji, vituo vya afya na nyumba za ibada zilikuwa zimeunganishwa na umeme ikilinganishwa na taasisi 43,925 za Aprili, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kupeleka umeme vitongojini, katika visiwa na maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa *(Off grid),* vituo vya pampu za maji, wachimbaji wadogo wa madini, viwanda na kilimo na katika shule na Mahakama za Mwanzo ambapo mafanikio yaliyopatikana ni kama yalivyofafanuliwa kwenye hotuba yangu kuu.

Mheshimiwa Spika, nieleze kidogo kuhusu nishati safi ya kupikia. Kutokana na athari ya matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia ikiwa ni pamoja na athari za kiafya kwa wananchi wetu, uharibifu wa mazingira pamoja na athari nyingine za kiuchumi na kijamii, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mahususi ya kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliidhinisha Mpango Mkakati wa Matumizi ya Nishati Kupikia ya Mwaka 2024 – 2034, unaolenga kuhakikisha kuwa angalau 80% ya Watanzania wanaweza kutumia nishati safi ya kupikia itakapofika mwaka 2030. Malengo ya Mkakati huu ambao unabainisha majukumu ya wadau mbalimbali ni pamoja na kupunguza gharama za nishati safi ya kupikia, vifaa na majiko sanifu ya kupikia, kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu na uhakika ya nishati ya kupikia iweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuhamasisha uwekezaji katika nishati hiyo ya kupikia, pamoja na kuimarisha uelewa wa jamii kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wadau, Wizara iliratibu ushiriki wa kongamano ama Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliofanyika Dubai mwezi Novemba hadi Desemba, 2023. Kupitia Mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Programu ya Nishati Safi ya Kupikia itakayowawezesha Wanawake Barani Afrika waweze kutumia nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, mwezi Mei, 2024 kutafanyika Mkutano wa Mkuu wa Wakuu wa Nchi kuhusu Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika, nchini Ufaransa ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano huo kwa kushirikiana na Waziri Mkuu wa Norway na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Nishati Safi ya Kupikia Duniani na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huo pamoja na mambo mengine, unalenga kujadili mikakati ya namna ya kuimarisha Sera ya Ugharamiaji na Ushirikiano katika Kuimarisha Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Wizara katika kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini ni pamoja na kusambaza kwa wananchi mitungi ya gesi ya *LPG*, gesi asilia na majiko banifu; kutekeleza *program* mbalimbali za kuhamasisha

matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwa ni pamoja na kuendesha Kongamano la Wanawake la Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika hapa Dodoma tarehe 9 Machi, 2024; na kushirikiana na Jeshi la Magereza ili kuwezesha Jeshi hilo (Magereza, Kambi za Makazi ya Watumishi, Ofisi, Vyuo, Shule na Hospitali) kutumia nishati safi ya kupikia kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee pia sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia. Mwaka 2023/2024 Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuendeleza sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia nchini katika maeneo ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta na gesi ambapo utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Majadiliano ya Mkataba wa Utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(LNG)* yaliendelea ili kuboresha rasimu ya awali za mikataba hiyo kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi nyingine za Serikali;

(ii) Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati vya Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi - Wembere, Songo Songo Magharibi na Vitalu Na. 4/1B na Na. 4/1C ziliendelea kwa kuchukua hatua mbalimbali kama inavyofafanuliwa kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali iliridhia kutolewa kwa leseni ya uendelezaji wa gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la Ntorya katika kitalu cha Ruvuma kwa *TPDC* kwa niaba ya mwekezaji kwa kampuni ya *ARA Petroleum*. Uendelezaji wa gesi iliyogunduliwa Ntorya unatarajiwa kuiwezesha nchi yetu kupata gesi takribani futi za ujazo milioni 60 kwa siku katika kipindi cha awali cha miaka miwili, na kuongeza hadi kufikia uzalishaji wa futi za ujazo milioni 140 kwa siku katika kipindi hicho na hivyo kuimarisha upatikanaji wa gesi asilia hapa nchini;

(iii) Kufanikisha ununuzi wa 20% ya hisa za Kampuni ya Wentworth katika Mkataba wa Uendeshaji wa Kitalu cha Uzalishaji wa gesi asilia cha Mnazi Bay kilichopo Mtwara ambapo *TPDC* imeongeza uwekezaji wake wa kitalu hicho kwa 20%;

(iv) Miradi ya usambazaji wa gesi asilia viwandani, katika taasisi na majumbani iliendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kujenga bomba la gesi asilia lenye urefu wa kilometa 12.4 kutoka Mwenge - Mbezi hadi Dar es Salaam, linalowezesha uunganishwaji wa miundombinu ya gesi asilia kwa viwanda, hoteli mbalimbali na kujenga bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka BVS 3 kuelekea Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo Mkoani Lindi lenye urefu wa kilometa 10.04 ili kuwezesha kuunganisha nyumba 209 kuziunganisha na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kukamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi wa kujenga miundombinu ya kuunganisha nyumba 451 Mkoani Lindi (Kata ya Mnazi Mmoja na Mingoyo) na nyumba 529 Mkoa wa Pwani huko Mkuranga;

(v) Ujenzi wa vituo vya kujaza gesi asilia *(Compressed Natural Gas-CNG)* katika magari, unaoendelea kushirikisha Sekta Binafsi. *TPDC* na *GPSA* ziliendelea na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi ili kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa michoro wa kihandisi na Tathmini ya Athari ya Mazingira na Jamii ili kuwezesha *GPSA* kujenga vituo vya *CNG* katika bohari za Dar es Salaam na Dodoma, ikiwa ni hatua ya kuwezesha vyombo vya moto vinavyomilikiwa na Serikali kuanza kutumia *CNG*. Aidha, sekta binafsi iliendelea kutumia fursa ya matumizi ya *CNG* katika vyombo vya moto kwa kujenga vituo vya *CNG*, Dar es Salaam, Pwani na karakana nane za kubadilisha mifumo ya matumizi ya *CNG* kwenye magari ambapo ni nyenzo muhimu ya kuchochea

matumizi ya *CNG* kwenye magari. Hatua hizi zimeendelea kuimarisha matumizi ya gesi asilia *(CNG)* katika magari.

(vi) Hali ya upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya petroli nchini imeendelea kuwa vizuri, ikiwemo kutengamaa kwa bei za mafuta ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa dola za Marekani kwa ajili ya kulipia mafuta yaliyoagizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda hadi Tanga - *Tanzania (East African Crude Oil Pipeline – EACOP)* kwa kukamilisha malipo ya fidia ya shilingi bilioni 34.93 kwa wananchi 9,823 kati wananchi 9,904 waliopisha utekelezaji wa mradi. Hii ni sawa na 99.2%; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 340 sawa na 100% ya makazi mbadala kwa wananchi 294 waliopisha mradi huu kupisha mkuza huo; kukamilika kwa ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa upashaji joto kwenye mabomba; na kuendelea na ujenzi wa maeneo 14 ya makambi.

Mheshimiwa Spika, aidha, mabomba yenye urefu wa Kilometa 400 yameshawasili nchini tayari na zoezi la kuwekewa mfumo wa kupasha joto na usalama na mawasiliano wa bomba linaendelea. Vilevile hadi kufikia Machi, 2024, Serikali ilikuwa imelipa jumla ya Dola za Marekani milioni 289.78 sawa na 94% ya kiasi cha mchango wa Serikali kwenye Kampuni ya *EACOP Ltd.* Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia 27.1%.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(PURA)* na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* iliendelea kusimamia na kudhibiti Sekta ya Nishati kuhakikisha utekelezaji wa shughuli za Sekta hiyo unazingatia sheria na taratibu zilizopo pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi. *PURA* iliendelea na maandalizi ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kupitia duru ya Tano kwa kuandaa rasimu ya Mkataba Kifani wa Ugawaji wa Mapato wa Mwaka, 2024 kwa ajili ya kutumika katika zoezi hilo na kukamilisha Mwongozo wa

kupata kampuni za kijiofizikia zitakazoshiriki na *PURA* katika zoezi la kunadi vitalu ambapo taratibu za kupata kampuni hizo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma ya Serikali kuhakikisha wananchi wananufaika na uwekezaji katika rasilimali zilizopo katika maeneo yao, Serikali kupitia *PURA* na *TPDC* imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii *(Corporate Social Responsibility)* katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi unaotarajia kukamilika mwishoni mwa Juni, 2024. Aidha, maandalizi ya rasimu yamehusisha wadau mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali ikiwemo Mikoa ya Lindi, Mtwara pamoja na Pwani.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* iliendelea kusimamia na kudhibiti shughuli za mafuta, gesi na umeme ambapo Mamlaka hiyo ilitoa leseni 34 kwa kampuni za mafuta kwa ajili ya kuagiza na kuuza mafuta kwa jumla; vibali vya ujenzi *(construction approvals)* 237 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafuta; miundombinu ya kuhifadhi *LPG;* na matumizi binafsi ya ghala za kuhifadhi mafuta na leseni 1,163 kwa wataalam wenye sifa za kufunga mifumo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuimarisha usimamizi, udhibiti na utoaji wa huduma, *EWURA* iliboresha Kanuni *(Rules)* mbalimbali ikiwemo, *The Petroleum Wholesales Storage, Retail and Consumer Installation Rules* ya mwaka 2023; na *The Petroleum, Retail and Operations in Townships and Villages as Amended Rules* za Mwaka 2023 na *Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products Price Setting)* kama ilivyorekebishwa ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto ambazo naomba niziseme kwa kifupi. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2023/2024, Sekta ya Nishati ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uzalishaji wa umeme na gesi asilia kutoendana na mahitaji kutokana na ukuaji wa uchumi na shughuli za kijamii; pia uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme. Kutokana na hatua hizo, Serikali ilichukuliwa hatua ikiwemo kuharakisha utekelezaji wa miradi ya uzalishaji wa umeme pamoja na ukarabati na matengenezo ya miundombinu ambayo yanafanyika

kwa haraka. Hali ya upatikanaji wa umeme nchini unaokidhi mahitaji imeendelea kuimarika na kuwa nzuri hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine iliyopo ni vitendo vya hujuma na uhalifu katika miundombinu ya umeme. Serikali imeendelea kuwachukulia hatua za kisheria wanaobainika kufanya vitendo hivyo vya uhujumu. Aidha, Serikali inaendelea kutoa wito kuwa, Serikali itaendelea kuchukua hatua kali tena bila kumfumbia macho mtu yeyote wa aina yoyote atakayebainika anahujumu miundombinu. Kwa sababu, kufanya kazi ya kuhujumu miundombinu ni kuturudisha nyuma kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyobainisha hapo awali, tulikabiliwa pia na changamoto ya upatikanaji wa Dola za Kimarekani kwa ajili ya kulipia mafuta yaliyoagizwa hapa nchini. Hali hii ilisababisha wafanyabiashara kupunguza kiasi cha mafuta kilichoagizwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania na wadau wengine, ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya mikataba ya uagizaji wa mafuta na kuruhusu matumizi ya fedha za kigeni zikiwemo fedha ya Uingereza *(British Pound),* Umoja wa Ulaya *(Euro)* na Umoja wa Nchi za Uarabuni.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ya Nishati kupitia *EWURA* iliimarisha ukaguzi wa vituo vya mafuta ili kuhakikisha kuwa mafuta yanapatikana kwa wakati wote katika maeneo yote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo juu ya taarifa na changamoto tulizopitia kwa mwaka wa fedha uliopita, naomba sasa nieleze juu ya Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2024/2025. Baada ya kutoa taarifa hii, mwaka 2024/2025, utekelezaji wa majukumu ya Wizara utaongozwa na vipaumbele vilivyojikita katika kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kufikisha gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kingine ni kupeleka nishati vijijini, ikiwemo katika vitongoji ili kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia ikiwemo Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(LNG)*.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kingine ni ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza na kusimamia shughuli za utafutaji na uendelezaji katika vitalu vya kimkakati vya uwekezaji na usambazaji wa gesi asilia viwandani katika taasisi, majumbani na kuimarisha matumizi ya *CNG* kwenye magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vingine ni kuendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking)* nchini pamoja na upatikanaji wa nishati ya mafuta vijijini kupitia uanzishwaji wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo. Vilevile, kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya petroli pamoja na ufanisi katika kushughulikia upatikanaji wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuimarisha uwekezaji na ushiriki wa sekta binafsi wa shughuli za utafutaji mafuta, uendelezaji wa gesi asilia pamoja na uzalishaji na usambazaji wa umeme na kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma na tija katika uendeshaji wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ambayo ni *TANESCO, TPDC, EWURA, PURA* na *PBPA* pamoja na Kampuni Tanzu zake.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara itaendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia pamoja na rasilimali watu ya Wizara na Taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2024/2025 pamoja na mambo mengine, umezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwaka 2020, Maagizo ya Viongozi wa Kitaifa katika Sekta ya Nishati, Mwongozo wa Maendeleo ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/2025 pamoja na Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano na miongozo mingine iliyozingatia Sera, Mikakati na

Programu mbalimbali za Kisekta na Kitaifa pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa *(SDGs)* ya Mwaka 2030 kuhusu masuala ya nishati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu C ya hotuba yangu, ukurasa wa 119 hadi 173 inatoa maelezo na ufafanuzi wa kina kuhusu programu, miradi na mikakati ya kazi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha unaokuja. Kwa ufupi Wizara itatekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu. Moja ya kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa uhakika wakujitosheleza. Umeme wa uhakika utatokana na vyanzo mbalimbali *(energy mix)*. Hii ni kwa kuzingatia umuhimu wa nishati katika maendeleo ya nchi yetu na uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza azma hiyo, Wizara imepanga kukamilisha mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere wa megawati 2,115 ambapo kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la mitambo *(power house)*, ufungaji wa mitambo saba ya kuzalisha umeme ambayo sasa ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Wizara itaendelea kutekeleza Mradi wa Uzalishaji Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi. Pamoja na kwamba tunaweka nguvu kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini gesi asilia hatujaiacha. Tunaendelea kukamilisha ujenzi huo kwa kujenga, kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilometa 19 kutoka Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Kinyerezi kwenda Gongo la Mboto na Mbagala Jijini Dar es Salaam na kufunga *transformer* eneo la Gongo la Mboto na Mbagala ambako kuna matatizo makubwa ya umeme kukatikakatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya uzalishaji wa umeme itakayotekelezwa ni Mradi wa Uzalishaji wa Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi, Megawatt 49.5, mradi huu mkandarasi yuko *site*. Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Shinyanga, Megawatt 150, mkandarasi yuko

*site*. Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Hale; Mradi wa kuzalisha umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono, megawati 87.8 na Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji ya Mto Kikonge, megawati 321. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali vilevile itaendelea kuelekeza nguvu katika kutekeleza uzalishaji wa umeme wa jotoardhi, ambapo itakamilisha uchorongaji wa visima vitatu vya uhakiki, ili kuhakiki hifadhi ya joto ardhi kwa ajili ya kuzalisha umeme. Vilevile Serikali itaanza kutekeleza programu ya uchorongaji wa visima vinne vya uhakiki katika Mradi wa Kiejo Mbaka, Mbeya, wenye uwezo wa kuzalisha Megawatt 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Kusafirisha Umeme, miundombinu imara ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini ni msingi thabiti wa kuwa na umeme wa uhakika. Hatua nyingine zitakazochukuliwa na Serikali katika mwaka 2024/2025 ni pamoja na kukamilisha mradi wa kusafirisha umeme kutoka *Julius Nyerere Hydro Power Plant* hadi Chalinze.

Mheshimiwa Spika, mradi huo una msongo wa Kilovoti 400 na Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kumalizia kazi zilizobaki katika kituo hicho ikiwemo majengo, barabara, njia ya kusafirisha umeme na marekebisho mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma yenye urefu wa kilometa 345 na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Dodoma. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha kusafirisha umeme unaotoka katika Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere hadi Chalinze kwenda kwenye Mkoa wa Dodoma na kuusambaza katika maeneo mengine nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya usafirishaji wa umeme itakayotekelezwa ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Kinyerezi mpaka Mkuranga. Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na msongo wa Kilovoti 220 kutoka Segera hadi Tanga. Ujenzi

wa njia ya kusafirisha umeme wa Kilovoti 220 kutoka Chalinze hadi Bagamoyo hadi Ununio, Dar es Salaam na ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli, Shinyanga wa Kilovoti 400/220/33. Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma kupitia Mradi wa *TAZA* na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa kuimarisha Gridi ya Taifa kupitia Mradi wa Gridi Imara kwa kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme. Pia Serikali itaendelea kufanya matengenezo ya mitambo ya kusafirisha umeme ili kuwa na miundombinu imara itakayoweza kubeba umeme wote unaozalishwa na kuwafikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024/2025 Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* itaendelea kuchukua hatua za kupeleka umeme vijijini ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii katika maendeleo na miradi mbalimbali. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kupeleka umeme kwenye vitongoji 20,000 ambapo kazi zinazofanyika ni pamoja na ununuzi wa wakandarasi na kutekeleza mradi, kufanya usanifu wa kina wa mradi na kuanza ujenzi wa miundombinu ya miradi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji na mikoa ya Songwe na Kigoma na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme wa msongo mdogo, kufunga *transformer* na kuunganisha wateja. Vilevile Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika Vitongoji 3,060 (vitongoji 15 kwa kila Jimbo) kwa kujenga miundombinu ya mradi, kufunga *transformer* na kuunganisha wateja na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine itakayotekelezwa ni Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili B, Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili C, Mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya vijijini - miji. Mradi wa kusambaza umeme katika migodi midogo, maeneo ya kilimo na

viwanda, mradi wa kupeleka umeme katika minara ya mawasiliano na simu na mradi wa ufungaji wa mifumo ya umeme jua kwenye makazi yaliyopo visiwani, yaliyopo mbali na gridi ya Taifa *(Off Grid)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nishati Safi ya Kupikia. Katika Mwaka wa fedha unaokuja wa 2024, Serikali itaendelea kutekeleza hatua mbalimbali madhubuti za kuimarisha matumizi ya Nishati Safi ya kupikia nchini. Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kutekeleza mradi wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Mwaka 2024 – 2034 kwa kupatia ufumbuzi vikwazo vya matumizi ya nishati hiyo, ikiwemo gharama kubwa ya nishati hiyo, upatikanaji hafifu na uhaba wa miundombinu yake. Pia kukosekana kwa elimu ya matumizi ya nishati hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara itaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Programu ya Nishati Safi ya Kupikia itakayowawezesha wanawake Barani Afrika Kutumia Nishati Safi ya Kupikia kwenye Programu ya *African Women Clean Cooking Support Programme*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Majiko Banifu kwenye kaya zilizopo katika maeneo ya Vijijini na Vijiji-Miji; kutoa ruzuku kwa wazalishaji wa mkaa mbadala kwa ajili ya ununuzi wa mashine zitakazotumika katika uzalishaji wa mkaa huo; kuendelea kushirikiana na Jeshi la Magereza katika kujenga miundombinu ya nishati ya kupikia katika maeneo 211 pamoja na kuendelea na usambazaji wa gesi asilia majumbani, hususan katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nielezee Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi. Serikali itaendelea kusimamia na kuendeleza Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi kwa kuchukua hatua mbalimbali ili kuwa na lengo, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa mchango wa sekta hii katika maendeleo na uchumi wa nchi yetu unaimarika. Serikali itaendelea na shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati na kujenga bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka kitalu cha Ruvuma, Ntorya, – Madimba, lenye urefu wa kilometa 34.2 na uwezo

wa kubeba futi za ujazo milioni 140 kwa siku. Aidha, Serikali inatarajia kukamilisha majadiliano ya mikataba ya miradi ya kuchakata na kusindika Gesi Asilia Kuwa Kimiminika *(LNG)* ili utekelezaji wake uanze.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mtwara, Lindi pamoja na Pwani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya tathmini ya athari ya mazingira na jamii, usanifu wa kihandisi pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwenye viwanda vya Mkuranga pamoja na Kongani za Viwanda ya Kwala Mkoani Pwani; kukamilisha ujenzi wa vituo vya *CNG (Mother station* katika Eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Vituo Vidogo vya Kairuki na Muhimbili) Mkoani Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa vituo vitano vya *CNG* vinavyohamishika *(mobile CNG stations)* vitakavyotoa huduma kwenye Jijini la Dar es Salaam. Aidha, sekta binafsi itaendelea kushiriki katika ujenzi wa vituo vya *CNG* pamoja na karakana za kubadili mifumo ya matumizi ya nishati ya gesi asilia ya magari.

Mheshimiwa Spika, vilevile *TPDC* itakamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa usambazaji wa gesi asilia nchini kwa ufadhili wa *REA* ambapo nyumba 980 zitaunganishwa katika mikoa ya Lindi na Pwani kwa kuanza awamu ya pili ya mradi huo kwa kuendelea kusambaza gesi asilia maeneo ya Mkuranga, mkoani Pwani.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine itayakayotekelezwa ni Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima – Uganda hadi Tanga – Tanzania; na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara na ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa kimkakati wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *PURA* inatarajia vilevile kuendesha Duru ya Tano ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa lengo la kutangaza kwa wawekezaji vitalu vilivyo wazi katika eneo la bahari na nchi kavu. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuandaa nyaraka za zabuni zitakazoongoza mnada wa vitalu hivyo, kufanya maonesho ya kitaalamu kuhusu vivutio vya vitalu na

kuzindua Duru ya Tano ya kunadi vitalu. Aidha, *EWURA* itaendelea kusimamia udhibiti wa huduma za nishati nchini kwa kuwasimamia watoa huduma kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma iliyo bora na ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhusiano wa kikanda na kimataifa, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Nishati inashirikiana na washirika mbalimbali wa Maendeleo, Jumuiya za Kikanda, nchi wahisani na wadau wengine. Kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru kwa moyo wa dhati Washirika wa Maendeleo, Jumuiya za nchi wahisani ambao wameendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua kwa mchango wao Benki ya Maendeleo Afrika *(AFDB),* Benki ya Dunia, *Arab Bank for Economic Development,* Mfuko wa Uendelezaji wa *Economic Development Cooperation Fund* wa Korea, Jotoardhi *(Geothermal Risk Mitigation Facility)* pamoja na Taasisi za Mashirika ya *JICA* ya Japan, *KFW* wa Ujerumani, *AFD* ya Ufaransa, Shirika la Fedha Duniani *(IMF),* Sida ya Sweden, *NORAD* ya Norway, Umoja wa Ulaya *(EU)*, Shirika la Mitaji ya Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)*, Shirika la Maendeleo la Canada *(CIDA)* na *USAID* ya Marekani, *OPEC Fund for International Development,* Abu-Dhabi *Fund for Development* na Saudi *Fund for Development*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii pia kutoa shukrani kwa Serikali za Afrika ya Kusini, Algeria, Burundi, Canada, China, *DRC* Congo, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Iceland, India, Japan, Kenya, Korea Kusini, Malawi, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, Norway, Rwanda, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uingereza, Zambia na nchi nyingine ambazo tumeendelea kuwa na ushirikianonao kwenye Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki na Ukanda wa *SADC* na kwenye Jumuiya ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kuwa, kwa kutambua umuhimu wa nishati kuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya

uchumi wa nchi yetu kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Wizara ya Nishati itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kusimamia, kuimarisha na kuendeleza nishati kwa lengo la kuhakikisha kuwa sekta hii inachangia ipasavyo katika maendeleo ya Taifa letu na watu wake kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia mijini na vijijini ili kulinda afya za watu wetu. Aidha, Wizara itaendelea kuipa suluhu ya kudumu changamoto ya upatikanaji wa umeme wa uhakika hapa nchini, kuimarisha usambazaji wake na kuimarisha uhakika wa umeme wenyewe.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara itaendelea kuimarisha usambazaji wa nishati hiyo pamoja na kuimarisha uzalishaji wa gesi asilia utakaoendana na mahitaji kwa kuzingatia kiwango cha ugunduzi wa nishati hiyo hadi sasa hapa nchini na hatua za utafutaji zinazoendelea kuchukuliwa. Pia Wizara itaendelea kuelekeza nguvu katika kuimarisha utoaji wa huduma mbalimbali zitakazotolewa kupitia taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi trilioni 1,883,759,455,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Shilingi 1,794,866,832,000 sawa na 95.28% ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,536,020,274,000 ni fedha za ndani na shilingi 258,846,558,000 ni fedha za nje.

(ii) Shilingi bilioni 84, naomba nirudie hapo. Shilingi bilioni 88,892,623,000ambayo ni sawa na 4.72%, ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 69,524,201,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 19,368,422,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Nieleze

tu kuwa hotuba hii inapatikana kwenye Tovuti ya Wizara yetu ambayo ni *www.nishati.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, vilevile hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatanishwa kwa ajili ya ufafanuzi na masuala mbalimbali yanayohusu Wizara yetu, vimeambatanishwa kwenye tovuti hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA DKT. DOTO MASHAKA BITEKO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2024/25 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2024/25.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2024/25. Aidha, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kama Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati katika Serikali ya Awamu ya Sita (6) na kuwasilisha Hotuba hii, kwa namna ya kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

Uteuzi huu ni dhamana na heshima kubwa kwangu katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Nishati inakidhi matarajio ya Watanzania ya kupata umeme wa uhakika pamoja na kuendeleza rasilimali za mafuta na gesi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu. Nitumie fursa hii

kuahidi, na kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha, kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu mkubwa kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu pamoja na wadau wengine katika Sekta ya Nishati.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 29 Februari, 2024 Taifa letu lilimpoteza aliyekuwa Rais mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Ali Hassan Mwinyi. Aidha, kabla ya hapo, tarehe 10 Februari, 2024 Taifa lilimpoteza aliyekuwa Waziri Mkuu mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Edward Ngoyai Lowassa. Kwa masikitiko makubwa naungana na Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, familia, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi wetu hawa, tuliwapenda lakini Mwenyezi Mungu amewapenda zaidi. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za wapendwa wetu mahali pema peponi, Amina.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** Julai mosi, 2023, Bunge lako Tukufu lilimpoteza Mhe. Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali. Aidha, tarehe 8 Aprili 2024, Bunge lako lilimpoteza Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani, Zanzibar. Naungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wote walioguswa na misiba hiyo. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Vilevile, naungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, kuwapa pole watanzania wenzetu waliopatwa na majanga mbalimbali katika mwaka 2023/24, ikiwemo yaliyotokana na mafuriko na maporomoko ya mawe na matope katika maeneo ya Hanang Mkoani Manyara; Kibiti na Rufiji Mkoani Pwani pamoja na Malinyi, Ulanga, Ifakara na Mlimba Mkoani Morogoro.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nawashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), kwa uongozi na juhudi zao katika kuleta maendeleo ya Taifa letu na kwa ushirikiano wanaonipa katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Wizara ya Nishati. Nikiri kuwa

maelekezo na miongozo ya viongozi wetu hawa ni msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati. Aidha, napenda kumpongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kusimamia kwa umahiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza kwa dhati wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Hii ni heshima kubwa na Tunu kwa Watanzania wote kwa ujumla kwa kuthaminiwa na kutambuliwa katika medani za kimataifa. Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu ili azidi kukupa nguvu na hekima zaidi katika kutekeleza majukumu yako.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii tena kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Bi. Nenelwa Mwihambi, Katibu wa Bunge kwa usimamizi wa shughuli za Bunge. Ni dhahiri kuwa, chini ya uongozi wenu Bunge letu limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ipasavyo katika kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza wajibu wa kuwaletea wananchi maendeleo.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na manaibu Waziri walioteuliwa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nampongeza Mhe. Jerry William Silaa (Mb), aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mhe. Deogratius John Ndejembi (Mb), aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mhe. Alexander Pastory Mnyeti (Mb), aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo; Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb), aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi; Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb), aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii; Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb.) aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati; Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb), aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mhe. Zainab Athuman Katimba (Mb), aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri

wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza, Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa jimbo la Mbarali kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo kuwa mwakilishi wa wananchi katika jimbo hilo. Hakika ni heshima kubwa uliyopewa na wananchi wa Mbarali na ninakutakia kila la kheri katika kutekeleza jukumu lako la uwakilishi katika Bunge letu Tukufu.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nampongeza Mhe. Dkt. David Mathayo David (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mhe. Kilumbe Shaban Ng'enda (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Vilevile, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maoni yao katika kuendeleza na kusimamia Sekta ya Nishati kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa letu na watu wake.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati kwa kuendelea kunisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Mha. Felchesmi Jossen Mramba kwa utendaji kazi wake mahiri na ushirikiano anaonipa katika kutekeleza shughuli zangu za kila siku za Wizara. Nampongeza pia, Dkt. James Peter Mataragio kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati. Nawashukuru pia Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara kwa ujumla kwa ushirikiano na juhudi zao katika kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya Wizara.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge wao. Kutokana na majukumu ya kitaifa kama Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kuna wakati wananikosa jimboni, lakini kwa wema wao wanaendelea kunivumilia na kunipa ushirikiano mkubwa. Nawaahidi

kuendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu katika kutekeleza shughuli za maendeleo. Aidha, namshukuru mke wangu mpendwa Benadetha Clement Mathayo kwa maombi na upendo wake wa dhati kwangu na watoto wetu. Amekuwa mvumilivu katika kipindi chote ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya Ubunge, Uwaziri na Unaibu Waziri Mkuu na kukubali kubeba na kutekeleza baadhi ya majukumu ya kifamilia.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie pia fursa hii kuvishukuru na kuvipongeza Vyombo vya Habari vikiwemo redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia Wizara ya Nishati kwa mwaka 2023/24. Vyombo hivyo vimekuwa mstari wa mbele katika kufuatilia kwa karibu miradi na shughuli zinazotekelezwa na Wizara ya Nishati na kuelimisha pamoja na kuhabarisha umma kuhusu mafanikio yaliyopatikana. Ni matumaini yangu kuwa, ushirikiano huu utazidi kuimarika katika Mwaka wa Fedha wa 2024/25 kwa manufaa ya Taifa letu na wananchi kwa ujumla katika upatikanaji wa taarifa kuhusu Sekta ya Nishati.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2023/24 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2024/25.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2023/24, pamoja na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2024/25.

## B. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2023/24 uliongozwa na vipaumbele mbalimbali vilivyojikita katika kukamilisha miradi mbalimbali ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme pamoja na kuendelea kuchukua hatua nyingine za kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini; kuendelea kupeleka umeme vijijini, vitongojini, katika visiwa na maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa, vituo vya afya na pampu za maji, wachimbaji

wadogo wa madini, maeneo ya kilimo na viwanda na katika shule na mahakama za mwanzo vijijini; pamoja na kutekeleza mikakati na programu mbalimbali za kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia (*clean cooking*) nchini.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vingine vilikuwa ni kuanza maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG*); kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda Hadi Tanga – Tanzania (EACOP), shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Kimkakati, usambazaji wa gesi asilia viwandani, majumbani na nchi jirani, kuimarisha matumizi ya Gesi Asilia Iliyoshindiliwa *(Compressed Natural Gas-CNG)* katika magari pamoja na kunadi vitalu (*licencing round*) vilivyo wazi katika maeneo ya nchi kavu na baharini ili viendelezwe.

**18.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilielekeza pia nguvu katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli, kutokana na umuhimu wake katika ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja kuimarisha ufanisi katika kushughulikia bidhaa hizo. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya TANESCO, TPDC, REA, EWURA na PURA pamoja na Kampuni Tanzu ili yatoe huduma bora kwa mujibu wa matarajio ya wadau, kuimarisha mapato pamoja na tija na ufanisi katika uendeshaji. Kwa kuzingatia gharama katika utekelezaji wa miradi ya nishati, Wizara iliendelea pia kuelekeza nguvu katika kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya nishati.

**Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2023/24**

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara ya Nishati iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi **Trilioni Tatu na Bilioni Arobaini na Nane, Milioni Mia Sita Thelathini na Mbili, Mia Tano Kumi na Tisa Elfu** (**Shilingi 3,048,632,519,000)** ambapo Shilingi **Trilioni Mbili, Bilioni Mia Sita na Tisa, Milioni Mia Moja Hamsini na Sita, Mia Moja Ishirini na Nane Elfu** (**Shilingi 2,609,156,128,000)** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya

maendeleo na **Shilingi Bilioni Themanini na Saba, Milioni Mia Tisa Ishirini na Tisa, Mia Sita Tisini na Nane Elfu (Shilingi 87,929,698,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane Kumi na Tatu na Milioni Ishirini na Sita, Mia Moja Arobaini na Saba Elfu, Mia Moja Hamsini na Sita (Shilingi 1,813,026,147,156)**, ambapo Shilingi **Bilioni Ishirini na Saba na Milioni Sabini na Tisa na Ishirini na Sita Elfu, Mia Saba Kumi na Sita** (**Shilingi 27,079,026,716**) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **Trilioni Moja, Bilioni Mia Saba Themanini na Tano, Milioni Mia Tisa Arobaini na Saba, Mia Moja Ishirini Elfu, Mia Nne Arobaini (Shilingi 1,785,947,120,440)** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.


**B.1 SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU**


**B.1.1 HALI YA UZALISHAJI NA UPATIKANAJI WA UMEME NCHINI**

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Serikali iliendelea kuchukua hatua za kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa umeme nchini ambapo hadi kufikia Machi, 2024 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulifikia jumla ya MW 2,138 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.2 ikilinganishwa na MW 1,872.1 za Mei, 2023. Katika kiasi hicho MW 836.3 (asilimia 39.1) ni umeme unaotokana na nguvu ya maji, MW 1,198.8 (asilimia 56.1) gesi asilia, MW 92.4 (asilimia 4.3) mafuta mazito na MW 10.5 (asilimia 0.5) tungamotaka (*biomass*) kama inavyofafanuliwa katika *Kielelezo Na. 1*.

***Kielelezo Na.1:*** **Uwezo wa Mitambo ya Kufua Umeme katika Gridi ya Taifa hadi Machi, 2024 na Hali ya Uzalishaji**

| **Chanzo** | **Uwezo wa Mitambo** | | **Hali ya Uzalishaji** | |
|---|---|---|---|---|
| | **MW** | **Asilimia** | **MW** | **Asilimia** |
| Maji | 836.3 | 39.1% | 755.5 | 43.1% |
| Gesi Asilia | 1,198.8 | 56.1% | 935.1 | 53.2% |
| Mafuta | 92.4 | 4.3% | 65.8 | 3.7% |
| Tungamotaka | 10.5 | 0.5% | - | - |
| **Jumla** | **2,138.0** | **100%** | **1,756.4** | **100%** |




**22.** ***Mheshimiwa Spika***, Ongezeko la uwezo wa uzalishaji wa umeme limetokana na kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (MW 2,115) ambapo MW 235 zimeanza kuzalishwa kupitia mtambo Namba 9 pamoja na kukamilika

kwa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo ambao unachangia MW 26.7 katika Gridi ya Taifa. *Kiambatisho Na. 1* ni mchanganuo wa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme katika Gridi ya Taifa hadi Machi, 2024.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2024, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme ambayo haijaungwa katika Gridi ya Taifa ni MW 33.4 ambazo zinajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO yenye uwezo wa kufua MW 28.4 na MW 5 zitokanazo na nguvu ya jua kutoka kwa mzalishaji binafsi. Aidha, Wizara kupitia TANESCO inanunua umeme wa MW 31 kati ya hizo MW 21 kutoka Uganda kwa ajili ya Mkoa wa Kagera na MW 10 kutoka Zambia kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, bado uzalishaji huo ulikuwa haukidhi mahitaji ya nchi ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na changamoto za upungufu wa maji na gesi asilia katika vituo vya kufua umeme, hitilafu katika mitambo ya uzalishaji pamoja na kufanyika kwa matengenezo katika mitambo ya uzalishaji wa umeme. Mahitaji ya juu ya umeme nchini yamekua na kufikia MW 1,590.1 zilizofikiwa tarehe 26 Machi, 2024 saa 3.00 usiku sawa na ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na MW 1,470.5 zilizofikiwa tarehe 12 Juni, 2023 saa 2:00 usiku. *Kielelezo Na.2* ni mwenendo wa ukuaji wa mahitaji ya umeme katika mwaka 2022/23 na 2023/24.

***Kielelezo Na. 2*: Ukuaji wa Mahitaji ya Umeme (Megawati) Nchini kwa Mwaka 2022/23 na Mwaka 2023/24**

| MWEZI | | JULAI | AGOSTI | SEPTEMBA | OKTOBA | NOVEMBA | DESEMBA | JANUARI | FEBRUARI | MACHI | WASTANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MWAKA | 2022/23 | 02.2 | 1,321.0 | ,341.3 | ,336.1 | ,315.6 | 1,354.6 | 1391.7 | 1,402.7 | 1401.9 | 1351.9 |
| | 2023/24 | 66.1 | 1,482.8 | 1413.5 | 1399.9 | 389.5 | 1339.7 | 1434.4 | 1,510.3 | 1590.1 | 1447.4 |
| **ONGEZEKO (%)** | | **11.2** | **10.9** | **5.11** | **4.6** | **5.3** | **-1.1** | **3.0** | **7.1** | **11.8** | **7.1** |

## B.1.2 HALI YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA UMEME

**25. *Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa usafirishaji wa umeme, miundombinu ya kusafirisha umeme imeendelea kuimarika na kufikia jumla ya urefu wa kilometa 7,745.4 ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.8 ikilinganishwa na kilometa 6,363.3 za mwaka 2022/23. Ongezeko hili limetokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ya njia za kusafirisha umeme, ikiwemo msongo wa Kilovoti 400 kutoka Julius Nyerere Hydro Power Plant hadi Chalinze, Singida- Arusha- Namanga pamoja na msongo wa Kilovoti 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme (SGR Lot II).

**26. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha miundombinu ya usambazaji umeme nchini ambapo imeongezeka na kufikia kilometa 176,750.9 ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.9 ikilinganishwa na kilometa 168,548.5 za mwezi Mei, 2023.

Kwa upande wa njia za kusambaza umeme, kilometa 58,886.6 ni za msongo wa Kilovoti 33, kilometa 12,476.6 za msongo wa Kilovoti 11 na kilometa 105,387.7 za msongo wa Kilovoti 0.4. *Kielelezo Na.3* ni mwenendo wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme.

***Kielelezo Na.3*: Njia za Kusafirisha na Kusambaza Umeme hadi Kufikia Machi, 2024**

| Na. | Njia za Usafirishaji wa Umeme | Urefu (Km) | |
|---|---|---|---|
| | | Mei, 2023 | Machi, 2024 |
| 1. | Njia za msongo wa kV 400 | 670.0 | 1,244.8 |
| 2. | Njia za msongo wa kV 220 | 3,477.7 | 4,095.6 |
| 3. | Njia za msongo wa kV 132 | 1,672.6 | 1,825.0 |
| 4. | Njia za msongo wa kV 66 | 543.0 | 580.0 |
| | **Jumla** | **6,363.3** | **7,745.4** |
| | ***Njia za Usambazaji wa Umeme*** | | |
| 1. | Njia za msongo wa kV 33 | 55,045.6 | 58,886. 6 |
| 2. | Njia za msongo wa kV 11 | 12,986.3 | 12,476.6 |
| 3. | Njia za msongo wa kV 0.4 | 100,516. 6 | 105,387.7 |
| | **Jumla** | **168,548.5** | **176,750.9** |

***Chanzo: TANESCO***

**B.1.3 HUDUMA KWA WATEJA**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Serikali kupitia TANESCO imetekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa huduma ikiwa ni pamoja na:

i. Kuongeza wigo wa mawasiliano na wateja kwa kuanzisha mfumo unaomuwezesha mteja kuhudumiwa kwa haraka zaidi bila kupiga simu kwa njia ya ujumbe wa simu (CHATBOT). Mfumo huu umekamilika kwa asilimia 95;

ii. Kupanua kituo cha huduma kwa wateja *(Call Center)* kwa kuongeza vifaa na wapokea simu kutoka mawakala 63 mpaka 100. Kwa sasa, Shirika linakamilisha taratibu za ununuzi wa vifaa;

iii. Kuanzisha mfumo utakaowawezesha wateja kupata taarifa maalumu za hali ya upatikanaji wa umeme kwa haraka kwa njia ya ujumbe wa simu kwenye simu zote janja na simu za kiswaswadu kuhusu Makatizo ya Umeme *(Automatic Power Interruption Notification sytem)* na hivyo kuwezesha wateja kujipanga ipasavyo na kupunguza malalamiko ya ukosefu wa umeme; na

iv. Kuanzisha mfumo wa benki ya taarifa na elimu *(DESA SYTEM knowledge based)* ili kuweza kutatua changamoto za wateja kwa kuwapa elimu na taarifa mbalimbali zitakazotatua changamoto zao bila mafundi. Uanzishwaji wa mfumo huu umefikia asilimia 99 ili uweze kuanza kutumika.

## B.1.4 MIRADI YA KUZALISHA UMEME

### a) Miradi Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji

#### (i) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP – MW 2,115)

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 2,115 katika maporomoko ya maji ya Mto Rufiji, wenye gharama ya **Shilingi trilioni 6.55** zinazogharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, sasa tupo katika hatua za mwisho za kukamilisha mradi huu ambapo hadi kufikia Machi, 2024 utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 97.43 na uzalishaji kuanza kupitia mtambo Namba 9 unaoingiza katika Gridi ya Taifa jumla ya MW 235. Aidha, mtambo Namba 8 wa mradi huu upo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji ili uanze uzalishaji wa MW nyingine 235. Kazi zinazoendelea kukamilishwa ni pamoja na ujenzi wa barabara za kudumu katika eneo la mradi ambao umefikia asimilia 85.6, ujenzi wa nyumba za makazi na ofisi ambao umefikia asilimia 98.5, ujenzi wa Daraja la kudumu ambao

umefikia asilimia 97.2 na ufungaji wa mitambo saba (7) yenye uwezo wa kuzalisha MW 235 kila mmoja ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ufungwaji.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension– MW 185**

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Serikali ilikamilisha ujenzi wa mitambo ya kufua umeme ya Kinyerezi I Extension MW 185 ambapo kwa sasa mitambo yote minne (4) inafua umeme. Aidha, hadi kufika Machi 2024, kazi ya upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi ilikuwa imefikia asilimia 97.6 ambapo transfoma mbili zenye uwezo wa MVA 175 zilikuwa zimefungwa kwenye misingi yake; na ujenzi wa barabara, ufungaji wa taa na mifumo ya ulinzi ulikuwa unaendelea. Vilevile, vituo vya Mbagala na Gongolamboto vinaongezewa uwezo kufikia MVA 170 kutoka uwezo wa awali wa MVA 50. Pia, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye urefu wa kilometa 19.2 ya msongo wa Kilovoti 132 kutoka Kinyerezi hadi Mbagala kupitia Gongolamboto umefikia asilimia 55.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80**

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha uzalishaji wa umeme wa MW 80 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera na umejengwa kwa ushirikiano wa nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa wa umeme kwa kila nchi. Mradi umekamilika na kuanza uzalishaji wa umeme ambapo kila nchi inapata MW 27. Aidha, kwa upande wa Tanzania mradi ulihusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa Kilovoti 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilometa 94.1 pamoja na miradi ya kijamii ambayo imekamilika kwa asilimia 100.

**(iv) Ukarabati wa Mitambo katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale**

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na ukarabati wa miundombinu ya kuzalisha umeme katika Kituo cha Hale chenye

uwezo wa kuzalisha MW 21 ambapo kwa sasa kiasi kinachozalishwa ni MW 10.5 kutokana na uchakavu wa miundombinu ya kuzalisha umeme. Hadi kufikia Machi, 2024, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 61 na kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha uundaji wa mitambo, matengenezo ya kituo cha kupoza umeme, ujenzi wa barabara mpya yenye urefu wa kilometa 1.3 na uchimbaji wa njia ya chini ya ardhi. Mradi unatarajiwa kukamilika Agosti, 2025.

**(v) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5**

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 49.5 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 132 yenye urefu wa kilometa 54 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe, mkoani Kigoma. Aidha, tayari Mkandarasi ameanza ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme na mradi unatarajiwa kukamilika Oktoba, 2027. Vilevile, Mkandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme anaendelea na kazi za ujenzi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 15.6 na mradi unatarajiwa kukamilika Aprili, 2025.

**(vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Jua Mkoani Shinyanga – MW 150**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu unahusisha ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa Megawati 150 kwa kutumia nguvu ya jua Mkoani Shinyanga. Hadi kufikia Machi, 2024 Serikali ilikuwa imekamilisha ulipaji wa fidia ya **Shilingi bilioni 2.6** kwa wananchi 109 waliopisha mradi. Aidha, Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha umeme na mradi unatarajiwa kukamilika Januari, 2025.

**(vii) Miradi ya Kuboresha Upatikanaji wa Umeme Mikoa ya Kusini (Lindi na Mtwara)**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa Mtwara (MW 300) ambapo maandalizi ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha

eneo la ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme yanaendelea. Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na JICA kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**36.** ***Mheshimiwa Spika*****,** ikiwa ni hatua ya kuhakikisha Mikoa ya Lindi na Mtwara inakuwa na umeme wa uhakika na unaoendana na ukuaji wa mahitaji, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kufunga mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa MW 20 katika eneo la Hiyari, Mkoani Mtwara ambao umeanza uzalishaji wa umeme, pamoja na kufufua mtambo Na.13 (MW 4.3) na mtambo Na. 8 (MW 2) mkoani Mtwara na mtambo Na.3 (MW 2.5) Somanga mkoani Lindi. Hatua hizo zimeimarisha upatikanaji wa umeme na kuondoa mgao wa umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Aidha, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuiunganisha Mikoa ya Lindi na Mtwara katika Gridi ya Taifa kwa kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Songea-Tunduru-Masasi-Mahumbika ifikapo Agosti, 2025. *Kielelezo Na. 4* ni mtambo wa kuzalisha umeme kiasi cha MW 20 ukiwa eneo la kufungwa Mkoani Mtwara.

***Kielelezo Na.4*****: Mtambo wa Kuzalisha Umeme Kiasi cha MW 20 Ukiwa Katika Eneo la Kusimikwa Mkoani Mtwara**







b) **Miradi ya Uzalishaji wa Umeme Iliyopo katika Hatua za Utayarishaji**

(i) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na utekelezaji wa mradi huu unaohusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 358 kwa

kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji mkoani Njombe na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 yenye urefu wa kilometa 170 kutoka Ruhudji hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa. Tayari uthamini wa mali za wananchi watakaolipwa fidia ili kupisha eneo la mradi kwa ajili ya ujenzi umekamilika na taratibu za kulipa fidia zinaendelea. Aidha, vyeti vya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii kwa upande wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme vimeshatolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Vilevile, tathmini ya gharama za miundombinu wezeshi imekamilika na taratibu za kupata fedha za kutekeleza mradi na ujenzi wa miundombinu hiyo zinaendelea.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 222 kwa kutumia maji ya Mto Rumakali mkoani Njombe na njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 64.5 kutoka kwenye mitambo hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya.

***Mheshimiwa Spika,*** hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza mradi huu ni pamoja na kukamilisha uthamini wa mali za wananchi watakaolipwa fidia ili kupisha eneo la mradi kwa ajili ya ujenzi ambapo taratibu za kulipa fidia zinaendelea. Aidha, vyeti vya mazingira kutoka NEMC kwa upande wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme vimetolewa na tathmini ya gharama za miundombinu wezeshi zimekamilika ambapo taratibu za kupata fedha za kutekeleza mradi na ujenzi wa miundombinu wezeshi zinaendelea.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87.8**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme katika Gridi ya Taifa na upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme wa MW 87.8 kwa kutumia

maporomoko ya maji ya Mto Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 38. Hadi kufika Machi, 2024, Serikali ilikuwa inaendelea na tathmini ya mali za wananchi 126 wanaopisha mradi na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi zinatarajiwa kukamilika Juni, 2024. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zitafuata baada ya kukamilika kwa kazi ya Mshauri Mwelekezi.

**(iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kikonge – MW 321**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 321 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhuhu mkoani Ruvuma na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 96 kutoka Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Serikali inaendelea na taratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu pamoja na kukamilisha taarifa muhimu za mradi ikiwemo tathmini ya kina ya Athari za Kijamii na Mazingira (*detailed ESIA*), uwekaji wa mipaka katika eneo la uzalishaji wa umeme, usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni za mradi (bwawa la kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme). Aidha, maandalizi ya kufanya tathmini katika eneo la bwawa la uzalishaji umeme yameanza. Vilevile, hatua za awali za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kazi za Mazingira zinaendelea.

## B.1.5 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME

**a) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji**

**(i) Mradi wa Kusafirisha Umeme kutoka Julius Nyerere Hydro Power Plant hadi Chalinze – Kilovoti 400 na Kituo cha Kupoza Umeme, Chalinze**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kilovoti 400 yenye urefu wa kilometa 160 kutoka JNHPP hadi Chalinze umekamilika kwa

asilimia 99.5 na njia hiyo imeanza kutumika kusafirisha umeme. Aidha, kituo kipya cha kupoza umeme cha Chalinze cha Kilovoti 400/220/132 kimekamilika kwa asilimia 93.1 na kimeanza kutumika kuingiza umeme katika Gridi ya Taifa. Kazi zilizobaki zinatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2024.

**(ii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na mradi wa kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi. Aidha, zoezi la uunganishwaji wa wateja linaendelea ambapo wateja 3,046 wameshapata huduma ya umeme kati ya wateja 5,646 na mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2024.

**(iii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga**

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 yenye urefu wa kilometa 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Babati na Arusha ambapo umekamilika kwa asilimia 99.4. Aidha, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Arusha hadi Namanga yenye urefu wa kilometa 114.3 umefikia asilimia 97.5 na kituo cha kupoza umeme cha Lemugur kimekamilika kwa asilimia 100 na kuwashwa.

**(iv) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Serikali ilikusudia kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waliosalia wakati wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 94 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi ambao tayari umekamilika kwa asilimia 100. Hadi kufika Machi 2024, wananchi wote waliosalia walikuwa wamelipwa fidia zao.

**(v) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilometa 620 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma na Sumbawanga. Serikali iliendelea na zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi ambalo limefikia asilimia 89. Aidha, tayari imesainiwa Mikataba kati ya TANESCO na wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na vituo viwili vya kupoza umeme vya Sumbawanga na Tunduma. Vilevile, vituo vya Iringa, Kisada na Mbeya vipo katika hatua za mwisho za kupata idhini ya Benki ya Dunia ya kuendelea na taratibu za kusaini Mikataba. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Desemba, 2025 na unalenga pia kuunganisha Gridi ya Taifa na Nchi za Kusini mwa Afrika *(Southern African Power Pool – SAPP)*.

**(vi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilometa 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi pamoja na usambazaji wa umeme katika vijiji 18 vilivyopo katika eneo la mradi. Hadi kufika Machi 2024, utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme ulikuwa umefikia asilimia 94.98 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2024 kwa mujibu wa Mkataba. Aidha, Mkataba wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi umesainiwa na utekelezaji unatarajiwa kukamilika Desemba, 2026.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa njia ya msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma, Serikali imechukua hatua ya dharura ya kufunga transfoma katika kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe itakayowezesha kufikisha umeme wa

Gridi ya Taifa wa msongo wa Kilovoti 220 katika Mkoa wa Kigoma ifikapo Juni, 2024.

**(vii) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Projects)* – Gridi Imara**

**48. *Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu uimarishaji wa miundombinu ya umeme katika mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 220 na 132 na kuongeza uwezo wa nyaya za kusafirisha umeme, ujenzi wa njia za kusambaza umeme msongo wa Kilovoti 33, ujenzi wa vituo vya kupoza umeme na kuongeza uwezo wa baadhi ya vituo pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika maeneo ya usambazaji (*switching station*). Mradi huu unatekelezwa kwa Awamu Tano ambapo Awamu ya Kwanza inahusisha miradi 27.

**49. *Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya Awamu ya Kwanza kufuatia kusainiwa kwa mikataba baina ya Serikali na Wakandarasi. Aidha, upembuzi yakinifu wa njia za kusafirisha, kusambaza na vituo vya kupoza umeme umefanyika pamoja na usanifu wa michoro, ununuzi wa vifaa kwa baadhi ya miradi pamoja na kuanza kazi za awali za ujenzi. Vilevile, utambuzi wa miradi ya Awamu ya Pili umefanyika na hatua za awali za utekelezaji zimeanza. *Kiambatisho Na.2* ni hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Gridi Imara. Kutokana na umuhimu wa miradi hii katika kuondoa changamoto za upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini, Serikali itaendelea kuhakikisha fedha zinazotengwa kila mwaka zinapatikana.

**(viii) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa *(Grid Rehabilitation and Upgrading) TTGRUP***

**50. *Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo nane (8) vya kupoza umeme, kurefusha Mkongo wa Mawasiliano (*Optic Fiber*) na kuboresha miundombinu ya mawasiliano kwa kuondoa *earth wire* na kuweka *optical ground wire* pamoja na kuimarisha mfumo wa uendeshaji na udhibiti wa Gridi ya Taifa. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la

Maendeleo la Ufaransa (AFD) pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadi kufikia Machi, 2024, utekelezaji wa mradi wa ukarabati na uboreshaji wa vituo nane (8) ulikuwa umefikia asilimia 21.0; uboreshaji wa miundombinu ya mawasiliano kwa ujumla umefikia asilimia 70.0 na kazi za kuimarisha mfumo wa uendeshaji na udhibiti wa Gridi ya Taifa kwa ujumla umefikia asilimia 23.4. Mradi unatarajiwa kukamilika Desemba, 2024.

**(ix) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka yenye urefu wa kilometa 166.2 itakayounganisha Mkoa wa Kagera katika Grid ya Taifa. Serikali kupitia TANESCO imekamilisha uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi na kazi zinazoendelea ni pamoja na taratibu za kufanya malipo ya fidia na majadiliano na Mshauri Mwelekezi aliyekidhi vigezo ili kusaini mkataba Aprili, 2024. Mradi unatarajiwa kukamilika Desemba, 2026.

**(x) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot II)**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea kutekeleza mradi huu ambapo tayari umekamilika kwa asilimia 99 na majaribio ya kupitisha umeme kutoka Msamvu, Morogoro hadi Zuzu, Dodoma yamefanyika kwa mafanikio.

**(xi) Mradi wa Njia ya Kusafirishi Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot V)**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 230 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Serikali kupitia TANESCO imekamilisha tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi na taratibu za malipo ya fidia

zinaendelea. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi Mjenzi zimekamilika na ameanza kufanya kazi za awali za utafiti wa udongo na njia ya kusafirisha umeme. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mei, 2025.

**(xii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze - Kinyerezi - Mkuranga (*NEG Phase 1*)**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu inahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze, Kinyerezi hadi Mkuranga yenye urefu wa kilometa 135 na vituo vya kupoza umeme vya Chalinze, Kinyerezi, Mkuranga na Morogoro. Hadi kufikia Machi 2024, Serikali ilikuwa imekamilisha ununuzi wa Mkandarasi Mjenzi wa njia ya kusafirisha umeme ambaye anaendelea na utekelezaji wa mradi. Mradi unatarajiwa kukamilika Aprili, 2026.

**(xiii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Dodoma (*NEG Phase 2*)**

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma yenye urefu wa kilometa 345 na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Dodoma. Mradi huu utawezesha kusafirisha umeme unaotoka JNHPP kupitia Chalinze kwenda Dodoma na kuusambaza katika Mikoa mbalimbali nchini (*power evacuation*). Hadi kufikia Machi, 2024, Serikali ilikuwa imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi 2,760 kati ya 2,860 wanaopisha mradi sawa na asilimia 92 na taratibu za ulipaji wa fidia zinaendelea. Aidha, Mkandarasi anaendelea na utekelezaji wa mradi na unatarajia kukamilika Desemba, 2025.

**(xiv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na Msongo wa Kilovoti 220 Segera – Tanga**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Segera - Tanga na vituo cha kupoza umeme vyenye uwezo wa MVA 800 Segera na Tanga. Kwa

sasa Serikali inaendelea na taratibu za kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huu ambao kukamilika kwake kutawezesha kusafirisha umeme kutoka Chalinze kwenda Tanga. Aidha, Serikali imekamilisha kazi ya Upembuzi Yakinifu na inaendelea na taratibu za kutathmini mali za wananchi watakaopisha mradi ili waweze kulipwa fidia.

**(xv) Mradi wa Kuboresha Utendaji Kazi wa TANESCO *(Corporate Management System – CMS)***

**57.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuboresha hali ya utendaji kazi wa TANESCO kwa kuweka mifumo itakayowezesha kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi. Mradi huu unatekelezwa sambamba na mradi wa kusafirisha umeme wa *Tanzania – Zambia Interconnector Transmission Project (TAZA)* kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 34.8** sawa na **Shilingi bilioni 81.6**.

**58.** ***Mhesimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO inaendelea na utekelezaji wa kazi za ufungaji wa vifaa vya miundombinu ya mradi *(data center infrastructure)* na kufanyiwa majaribio utendaji wake. Aidha, usimikaji wa mfumo wa taarifa za kijiografia za miundombinu ya umeme na wateja (GIS) umekamilika pamoja na mafunzo kwa wataalam. Vilevile, miundombinu ya mawasiliano ya mradi *(network infrastructure)* imekamilika kwa asilimia 80 na hatua ya kwanza ya utengenezaji wa mfumo imefikia asilimia 85 ambapo hatua ya pili ya mradi imefikia asilimia 43. Pia, yamefanyika mafunzo ya matumizi ya mfumo kwa Mameneja na Timu Maalumu (*Champions Team*) na yanaendelea kwa wafanyakazi wote. Kwa ujumla mradi umetekelezwa kwa asilimia 61 na unatarajiwa kukamilika Agosti, 2024.

**b) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua ya Utayarishaji**

**(i) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Segera- Same- Arusha (*Lemugur*)**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Segera hadi Arusha kupitia Same, kituo cha kupoza umeme cha Same na upanuzi wa

vituo vya kupoza umeme vya Segera na Lemugur. Kazi za Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Mazingira na Kijamii zinaendelea na zinatarajika kukamilika Agosti, 2024.

**(ii) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli, Shinyanga 2x315 MVA**

**60.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha kujenga kituo kipya chenye uwezo wa Kilovoti 400/220 na kusimika transfoma kubwa mbili zenye ukubwa wa MVA 315 kila moja katika eneo la Ibadakuli mkoani Shinyanga ili kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya kanda ya Ziwa na maeneo jirani kwa lengo la kuchochea shughuli za kiuchumi, hususan uchimbaji wa madini, usafirishaji kwa kutumia (SGR) na mradi wa Bomba la Mafuta kutoa Uganda hadi Tanga (EACOP). Kwa sasa Mkandarasi anaendelea na usanifu wa kituo.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Makutopora hadi Tabora kwa ajili Uendeshaji wa Treni ya Umeme (*SGR Lot 3*)**

**61.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 347 kutoka Makutopora hadi Tabora kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme (SGR). Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 212.58**. Hadi kufikia Machi 2024, kazi zilizokuwa zinatekelezwa ni pamoja na Upembuzi Yakinifu ambao umefikia asilimia 25 na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya usanifu wa kina wa mradi. Aidha, tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi zitaanza baada ya kukamilisha Upembuzi Yakinifu.

**(iv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Tabora hadi Isaka kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (*SGR Lot 4*)**

**62.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu unaokadiriwa kuwa kilometa 195 kutoka Tabora hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni

ya umeme. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 131.66**. Hadi kufikia Machi 2024, kazi zilizokuwa zinatekelezwa ni pamoja na Upembuzi Yakinifu ambao umefikia asilimia 12.5 na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya usanifu wa kina wa mradi. Aidha, tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi zitaanza baada ya kukamilisha Upembuzi Yakinifu.

**(v) Ujenzi wa njia ya Kusafirisha Umeme *(Submarine Cable)* Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Tanzania Bara (Ununio) Hadi Zanzibar (Unguja)**

**63.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 kwenda Zanzibar kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa umeme Zanzibar. Kukamilika kwa mradi huu kutatatua changamoto ya kuzidiwa kwa miundombinu ya kusafirisha umeme kwenda Zanzibar iliyopo kwa sasa. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni kukamilisha taratibu za ununuzi wa Mshauri Mwelekezi atakayefanya Upembuzi Yakinifu wa mradi ambazo zinatarajiwa kukamilika Juni, 2024. Taratibu za utafutaji wa fedha za kutekeleza mradi huu zinaendelea ambapo AfDB imeonyesha nia ya kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa mradi huu.

**(vi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme *(Submarine Cable)* Msongo wa Kilovoti 132 kutoka Tanzania Bara (Tanga) Hadi Zanzibar (Pemba)**

**64.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 132 kutoka Tanga kwenda Pemba ili kuimarisha upatikanaji wa umeme Pemba. Kukamilika kwa mradi huu kutatatua changamoto ya kuzidiwa kwa miundombinu ya kusafirisha umeme kwenda Pemba iliyopo kwa sasa. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni kukamilisha taratibu za ununuzi wa Mshauri Mwelekezi atakayefanya Upembuzi Yakinifu wa mradi. Taratibu za utafutaji wa fedha za kutekeleza mradi huu zinaendelea ambapo AfDB ameonesha nia ya kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa mradi huu.

**(vii) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Manyoni (Manyoni Substation - MVA 2x30, 220/33kV)**

**65.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unalenga ujenzi wa kituo cha kupoza umeme chenye uwezo wa MVA 60 katika Kata ya Mkwese, Wilaya ya Manyoni, Mkoa wa Singida na unatarajiwa kugharimu **Shilingi bilioni 38.05**. Hadi kufikia Machi 2024, Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii ilikuwa imekamilika na kuwasilishwa NEMC kwa ajili ya kupata cheti cha mazingira. Aidha, tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi inaendelea ambapo inatarajiwa kukamilika Juni, 2024. Serikali inaendelea na taratibu za utafutaji wa fedha za kutekeleza mradi huu.

**(viii) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Masaka - Ibadakuli)**

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 yenye urefu wa kilometa 617 kutoka Ibadakuli – Nyakanazi – Kyaka hadi Masaka Uganda pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka. Upembuzi Yakinifu umekamilika na kazi zinazoendelea ni kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira pamoja na tathmini ya wananchi watakaopisha mradi. Taratibu za upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi zinaendelea.

**(ix) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Chalinze – Bagamoyo**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 kutoka Chalinze - Bagamoyo yenye urefu wa kilometa 90 na kituo cha kupoza umeme cha Bagamoyo. Hadi kufikia Machi, 2024 Upembuzi Yakinifu wa mradi ulikuwa umekamilika na kazi zinazoendelea ni pamoja na kufanya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi na kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huu.

**(x) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma Kupitia Mpanda (Km 480) na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda**

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenye urefu wa kilometa 480. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 200.4** sawa na **Shilingi bilioni 512.02** kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme na **Dola za Marekani milioni 50** kwa ajili ya kituo cha kupoza umeme. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Exim Benki ya Korea zimeonesha nia ya kufadhili mradi huu. Hadi kufikia Machi 2024, Serikali kupitia TANESCO ilikuwa imekamilisha uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu na usanifu wa mradi wa awali na inaendelea na taratibu za kutafuta fedha za kutekeleza mradi.

**(xi) Utekelezaji wa Miradi Mingine na Matengenezo ya Mitambo**

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO imeendelea kufanya ukaguzi wa miundombinu ya umeme pamoja na kuifanyia matengenezo. Mitambo ya kuzalisha umeme iliyofanyiwa matengenezo kinga makubwa na madogo ni pamoja na kituo cha Tegeta, Kituo cha Kinyerezi II, Kituo cha Ubungo I na Kituo cha Mtera. Matengenezo hayo yaliimarisha uzalishaji wa umeme kwa wastani wa MW 115 kwenye Gridi ya Taifa ambao ulikuwa hauzalishwi kutokana na ubovu wa mitambo. *Kiambatisho Na. 3* ni mitambo iliyofanyiwa matengenezo makubwa na madogo.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uwezo wa miundombinu ya usafirishaji na kupunguza upotevu wa umeme, TANESCO inafanya maboresho kwenye njia mbalimbali za kusafirisha umeme ikiwemo njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kilovoti 132 yenye urefu wa kilometa 97 kutoka Ubungo hadi Chalinze. Kwa sasa njia hiyo ina uwezo wa kusafirisha kiasi cha MW 150, ikilinganishwa na kiasi cha MW 94 kilichokuwa kinasafirishwa awali hivyo kufanya uwezo wa kusafirisha umeme kuongezeka kwa asilimia 78. Aidha, Shirika linabadilisha miundombinu ya msongo wa Kilovoti 11 na kuwa msongo wa Kilovoti 33, pamoja na kuongeza transfoma kwenye maeneo mbalimbali. Kazi

ya ukarabati ni endelevu na inaendelea katika mkoa wa Tanga kwa kuboresha njia ya kilometa 172 ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kilovoti 132 kutoka Chalinze mpaka Hale.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada nyingine zinazofanyika ili kuimarisha miundombinu ya usafirishaji umeme nchini ni kufanya ukaguzi wa kina ili kubaini maeneo yenye changamoto na kuyafanyia ukarabati. Ukarabati huo unahusisha ubadilishaji wa nyaya chakavu, vikombe vilivyopasuka, vyuma vilivyoibiwa, kuondoa nguzo za miti na kuweka nguzo za zege pamoja na ukarabati wa sehemu zilizoathiriwa na mmomonyoko wa udongo na kusafisha njia tengefu.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu uboreshaji wa mifumo ya uendeshaji wa Gridi, Serikali kupitia TANESCO ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mradi wa uboreshaji na kuongeza uwezo wa mitambo ya kuongoza/kuendesha Gridi ya umeme (*SCADA/EMS*). Mradi huu, wenye lengo la kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa gridi kupitia teknolojia ya kidijitali unatarajiwa kukamilika Juni, 2025.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO imefanikiwa kuweka mifumo ya kisasa ya mawasiliano katika vituo tisa (9) vya kupoza umeme ili viendeshwe kidijitali (*unmanned substations*). Hadi sasa kituo kimoja cha Buzwagi kimekamilika na vituo nane (8) vilivyobaki vinatarajiwa kukamilika Desemba 2024. Vituo hivyo ni *New City Centre (Posta)*, Kurasini, Dege, Mbagala na Gongo la Mboto vilivyopo mkoani Dar es Salaam pamoja na vituo vya Musoma, Geita na Bulyanhulu ambavyo vipo katika majaribio ya kuendeshwa kidijitali. Jitihada za kuweka mifumo ya kidijitali kwenye vituo vingine zinaendelea.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada za maboresho zinafanyika pia katika mifumo ya kisasa ya usambazaji umeme (*distribution network automation*), ikiwa ni pamoja na kubadilisha mita za wateja wakubwa T2 na T3 kwa kufunga mita zenye ufanisi. Zoezi hili limeanza kwa mkoa wa Dar es Salaam na maeneo mengine yatafuatia. Aidha, TANESCO inakamilisha taratibu za ununuzi wa mfumo wa mita janja (*smart meters*) zitakazomuwezesha mteja wa kawaida kununua umeme na kisha mita hiyo kupokea moja kwa moja umeme badala na mfumo wa sasa.

## B.1.6 UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO

### a) Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO)

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 ETDCO iliendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya usafirishaji wa umeme. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 132 wenye urefu wa kilometa 383 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Sikonge, Ipole na Inyonga unaotarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2024; na mradi wa kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Urambo na kutoka Urambo hadi Kidahwe Mkoani Kigoma. Aidha, ETDCO ilikamilisha kwa asilimia 99 ujenzi wa njia nne za kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 33 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Mpomvu (Geita) hadi kituo cha kupoza umeme cha Mgodi wa Geita Gold Mine ili kuunganisha mgodi na umeme wa Gridi ya Taifa.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** ETDCO iliendelea na utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini katika Mikoa ya Geita na Kigoma kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ambapo hadi kufikia Machi, 2024 ilikuwa imekamilika kwa asilimia 40 kwa upande wa Mkoa wa Geita na asilimia 20 kwa upande wa mkoa wa Kigoma. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ufungaji wa transfoma 20 kati ya 45 na kuwasha mitaa 20 kati ya 45 kwa upande wa mkoa wa Geita; na kufunga transfoma 6 kati ya 59 na kuwasha umeme mitaa sita kati ya 59 katika mkoa wa Kigoma. Miradi hii kwa ujumla wake inatarajia kukamilika mwishoni mwa Desemba, 2024.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** kampuni ya ETDCO iliendelea pia na utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini katika mikoa ya Katavi (REA III, Round II) ambao umekamilika kwa asilimia 96, Mbeya (REA III, Round II) ambao umekamilika kwa asilimia 92, Kigoma (REA III, Round I) ambao umekamilika kwa asilimia 99 na Arusha (REA III, Round I) ambao umekamilika kwa asilimia 100. Pia kampuni hiyo ilianza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia za kusambazia umeme katika nyumba zinazojengwa Msomera wilayani Handeni kwa ajili ya familia zinazohama kutoka Hifadhi ya Ngorongoro ambapo mradi huo pia utahusisha nyumba zitakazojengwa Saunyi wilayani Kilindi na Kitwai B

wilayani Simanjiro. Pamoja na hayo, Serikali inaendelea kusimamia kwa karibu utendaji wa Kampuni hii ikiwemo kuimarisha uongozi wa kampuni ili iweze kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

### b) Kampuni ya Kuzalisha Nguzo za Umeme za Zege Tanzania (TCPM)

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuhakikisha uzalishaji wa nguzo za zege unaimarika nchini, Serikali kupitia TCPM ilianza taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa kiwanda cha kwanza cha kuzalisha nguzo za zege Mkoani Tabora. Aidha, kazi za ujenzi wa kiwanda zinatarajiwa kuanza Mei, 2024. Vilevile, taratibu za kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha pili Mkoani Mbeya zinaendelea.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TCPM itashirikiana na Wawekezaji binafsi walioonyesha nia ya kushirikiana kwa mfumo wa ushirikiano wa *joint venture* katika uzalishaji wa nguzo za zege. Hadi kufikia Machi, 2024 mazungumzo ya awali yamefanyika na Wawekezaji 17 waliowasilisha maombi ya kushirikiana na TCPM. Aidha, uchambuzi wa taarifa za mapendekezo ya kifedha na kiufundi unaendelea ili kupata wawekezaji wenye uwezo wa kushirikiana nao.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** TCPM ilisanifu, kusimamia uzalishaji na kusambaza nguzo za zege 1,482 za mita 17 kwa Kampuni ya ETDCO kwa ajili ya mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 132 kutoka Mkoa wa Tabora kwenda Mkoa wa Katavi na Wilaya ya Urambo. TCPM pia ilisambaza nguzo 940 za saizi tofauti kwa ETDCO kwa ajili ya miradi mbalimbali. Aidha, kampuni hii ilisambaza nguzo 4,479 za saizi tofauti kwa mikoa mbalimbali ya TANESCO kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa njia za kusambaza umeme.

### c) Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi (TGDC)

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini kupitia vyanzo mbalimbali, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme kupitia jotoardhi, ambapo kipaumbele kilielekezwa katika miradi mitano (5) ya Ngozi (MW 70) na Kiejo-Mbaka (MW 60) iliyopo

mkoani Mbeya, Songwe (MW 5) mkoani Songwe, Luhoi (MW 5) mkoani Pwani na Natron (MW 60) mkoani Arusha.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TGDC inaendelea na taratibu za kuwapata Wakandarasi wa kuchoronga visima vya uhakiki (*drilling contractor*), tathmini ya visima (*well testing services*) na ununuzi wa bidhaa/malighafi za uchorongaji wa visima vya uhakiki vya jotoardhi Ngozi na shughuli za uchorongaji wa visima hivyo zinatarajiwa kuanza Juni, 2024. Aidha, mradi wa Ngozi utatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inatarajiwa kuanza na uzalishaji wa MW 30 na inatarajiwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 144** sawa na takribani **Shilingi bilioni 367.9.** *Kiambatisho Na. 4* ni mtambo wa uchorongaji ukiwa umesimikwa kwa ajili ya uhakiki wa jotoardhi katika eneo la mradi wa jotoardhi wa Ngozi.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa katika miradi ya jotoardhi ni pamoja na:

i. Kuendelea na taratibu za kuajiri Mshauri Mwelekezi (*drilling consultant*) kwa ajili ya kusanifu na kusimamia uchorongaji (*drilling program*) wa visima vya uhakiki vya jotoardhi katika Mradi wa Kiejo–Mbaka pamoja na tathmini ya ardhi na ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha utekelezaji wa mradi. Aidha, maandalizi ya kupata mtambo mdogo wa kuzalisha umeme (*well head generator*) yanaendelea. Mradi huu utatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inatarajiwa kuanza na MW 10. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 75** sawa na takribani **Shilingi bilioni 191.6**;

ii. Taratibu za upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uchorongaji wa visima vya uhakiki vya jotoardhi na kujenga uelewa kwa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu manufaa ya mradi kupitia warsha mbalimbali zimekamilika katika mradi wa Songwe. Maandalizi ya uchoronganji wa visima vya uhakiki katika eneo la mradi yanaendelea. Gharama za kutekeleza mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 32** sawa na takribani **Shilingi bilioni 81.8**;

iii. Maandalizi ya uchorongaji wa visima vinne (4) vya uhakiki vya jotoardhi pamoja na kufanya upembuzi yakinikifu wa matumizi mengineyo unaendelea katika mradi wa Luhoi. Gharama za kutekeleza mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 32** sawa na takribani **Shilingi bilioni 81.8**; na

iv. Kuendelea na taratibu za kuajiri Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina (*detailed geoscientific surface exploration*) Aprili, 2024 ili kuanza utafiti wa kina wa kijiosayansi katika mradi wa Natron MW 60. Gharama za kutekeleza mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 288** sawa na takribani **Shilingi bilioni 735.8**.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TGDC ilikamilisha taratibu za kukidhi vigezo vya kupata ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ikiwemo mfuko wa *Geothermal Risks Mitigation Facility (GRMF)* unaoratibiwa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa ajili ya kupata fedha za kuendeleza vyanzo hivyo. Vilevile, Mfuko wa *Climate Action Africa* kupitia Serikali ya Canada umeridhia kutoa msaada wa kiufundi (*Technical Assistance*) kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina wa kijiosayansi katika eneo la mradi wa Meru Mkoani Arusha na mfuko wa *GRMF HEAT* umeridhia kutoa **Dola za Marekani milioni 1.6** kwa ajili ya utafiti wa kina wa kijiosayansi kwa mradi wa jotoardhi Manyara mkoani Manyara. Jitihada nyingine zinazoendelea ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu manufaa ya miradi ya jotoardhi.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuhamasiaha uwekezaji na matumizi ya rasilimali za jotoardhi, Tanzania itakuwa mwenyeji wa Kongamano la 10 la Jotoardhi (*African Rift Geothermal Conference-ARGeo C10*) litakalofanyika Novemba, 2024 Jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo litahusisha Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki zilizopitiwa na bonde la ufa.

### B.1.7 UZALISHAJI WA UMEME KUPITIA SEKTA BINAFSI

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO inanunua umeme kutoka kwa wazalishaji wadogo wa umeme ambao wanasaidia

kuongeza upatikanaji wa umeme nchini. Wazalishaji hao wanachangia jumla ya MW 31.8 ambapo MW 26.8 zimeingizwa katika Gridi ya Taifa na MW 5.00 nje ya Gridi ya Taifa. Changamoto wanazokutana nazo wazalishaji hao ni pamoja na upungufu wa malighafi za kuzalisha umeme ikiwemo maji, magome ya miti na mabaki ya miwa kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na hivyo kuathiri uzalishaji wao. *Kiambatisho Na. 5* ni Wazalishaji Wadogo wa Umeme (SPPs) waliosajiliwa.

**87.** ***Mheshimwa Spika,*** Serikali imeingia mikataba na wawekezaji 20 ambao bado wapo katika hatua ya ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji wa umeme ambao kwa ujumla wataongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme kiasi cha MW 86.31.

**B.1.8 MIRADI YA NISHATI VIJIJINI**

**a) Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II)**

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini iliendelea kutekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unaolenga kukamilisha kupeleka umeme kwenye vijiji 4,071 vilivyobaki kati ya vijiji vyote 12,318. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya vijiji 11,837 sawa na asilimia 96.37 ya vijiji vyote Tanzania Bara vilikuwa vimepelekewa umeme. Aidha, REA imejenga njia za umeme za Msongo wa Kati zenye urefu wa kilometa 22,578 kati ya kilometa 23,619 sawa na asilimia 95.6 pamoja na njia za umeme wa Msongo Mdogo zenye urefu wa kilometa 8,214 kati ya kilometa 12,159 sawa na asilimia 67. Vilevile, transfoma 3,686 kati ya 4,071 sawa na asilimia 90.54 zimefungwa hivyo kuunganisha wateja 54,626. Kutokana na hatua zinazochukuliwa za kupeleka umeme vijijini, jumla ya taasisi 63,509 zinazotoa huduma kwa ajamii ikiwa ni pamoja na za Elimu, Biashara, Pampu za Maji, Vituo vya Afya na Nyumba za Ibada zilikuwa zimeunganishiwa umeme kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na.*6 ikilinganishwa na taasisi 43,925 za Aprili, 2023.

**b) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – *(Hamlet Electrification Project – HEP)***

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Serikali iliendelea kutekeleza azma ya kuhakikisha vitongoji vyote nchini vinapatiwa huduma ya umeme ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii vitongojini. Hadi kufikia Machi, 2024 Wakandarasi wa kutekeleza miradi ya kuunganisha umeme katika vitongoji 667 katika Mikoa ya Songwe na Kigoma walikuwa wanaendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu ya umeme katika vitongoji hivyo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Juni, 2025. Aidha, REA ipo katika hatua za ununuzi wa wakandarasi wa kutekeleza Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji 15 kwa kila Jimbo.

**c) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B**

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye vitongoji ambavyo vimepitiwa na njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa Kati katika mikoa tisa (9) ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe na Songwe. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya kilometa 103 za umeme wa Msongo Mdogo zimejengwa na nguzo kilometa 1,458 zimesimikwa kati ya 3,860. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Novemba, 2025.

**d) Mradi wa Ujenzi wa Gridi Ndogo (*Mini Grids*) katika Maeneo ya Visiwa na Maeneo Yaliyo Mbali na Gridi ya Taifa**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi unahusisha kupeleka umeme katika visiwa kwa kutumia gridi ndogo zinazozalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua kwenye maeneo ya visiwa ambavyo havijafikiwa na Gridi ya Taifa. Hadi kufikia Machi, 2024 kazi zilizotekelezwa ni kuchambua maombi yaliyowasilishwa, kusaini mikataba miwili (2) kati ya saba (7) na kuanza kutekeleza mradi ambapo wateja 1,403 wameunganishiwa umeme kati ya 14,168 katika vijiji 34 kati ya 85.

**e) Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kuuzia Bidhaa za Petroli Vijijini kwa Njia ya Mikopo**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu kusogeza huduma ya bidhaa ya mafuta ya petroli kwa wananchi wanaoishi vijijini kwa kutoa mikopo kwa waendelezaji wa vituo vya mafuta ili waweze kuwekeza katika maeneo ya vijijini. Tayari zoezi la kuwapata waendelezaji wa vituo hivyo vijijini limefanyika kupitia Wakala wa Nishati Vijijini ambapo maombi ya waendelezaji 10 yaliyokidhi vigezo vya kiufundi yamewasilishwa Benki ili kufanyiwa tathmini ya kifedha. Kufuatia uzoefu uliopatikana katika maombi yaliyowasilishwa wakati fursa hii ilipotangazwa awali, vigezo na masharti ya utolewaji wa mikopo hiyo vimepitiwa upya na kuboreshwa ili kuwawezesha waombaji wengi kunufaika na fursa hiyo na hivyo kuimarisha ujenzi wa vituo hivyo vijijini. Aidha, tarehe 25 Machi 2024, Wakala ulitangaza Awamu ya Pili ya fursa za upatikanaji wa mikopo hiyo ambapo kwa sasa hakuna ukomo wa uwasilishwaji wa maombi. Kupitia utaratibu huu, kwa maombi yatakayobainika kutokidhi vigezo, waombaji husika watakuwa na nafasi ya kufanya marekebisho ya maombi yao katika maeneo yenye upungufu na kuyawasilisha tena.

**f) Programu ya Kuwezesha Waendelezaji wa Miradi Midogo ya Nishati Jadidifu Vijijini chini ya Utaratibu wa Kusaidia Uandaaji wa Miradi (PPSF)**

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusu kuwawezesha waendelezaji miradi ya nishati jadidifu vijijini ambao wana upungufu wa mitaji ili waweze kuandaa maandiko ya miradi ikiwemo Mpango wa Biashara. Hadi kufikia Machi, 2024 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kusaini mikataba miwili (2) iliyopatikana katika *Call for Proposal* Awamu ya Kwanza na kuendelea na uchunguzi wa kina kwa waendelezaji waliokidhi vigezo baada ya tathmini iliyofanyika (*due diligence*). Aidha, Wakala unaendelea kuandaa kabrasha kwa ajili ya kutangaza fursa hizo kwa Awamu ya Nne.

**g) Mpango wa Uendelezaji Miradi ya Nishati Jadidifu Inayofua Umeme kwa Kutumia Maporomoko ya Maji**

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango huu unahusisha Serikali kutoa ruzuku kwa Waendelezaji wa miundombinu ya miradi midogo ya kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji vijijini ili wapate motisha ya kuiendeleza. Hadi kufikia Machi, 2024 Serikali kupitia REA iliendelea kutoa ruzuku kwa waendelezaji wa Miradi midogo ya kufua umeme kwa kutumia nguvu ya maji. Jumla ya miradi minne (4) imepata ruzuku ikijumuisha Ijangala (kW 360) uliopo Makete – Shilingi milioni 426; Lupali (kW 317) uliopo Ludewa Shilingi bilioni 2.9; Lugarawa (kW 1,700) uliopo Njombe Shilingi milioni 495 na Kilolo/Maguta (kW 2,400) uliopo Kilolo Iringa Shilingi milioni 969.9. Aidha, ujenzi wa Mradi wa Ijangala umekamilika na kuzinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango Oktoba 2023. Pia, utekelezaji wa Mradi wa Lupali umefikia asilimia 90; Mradi wa Lugarawa asilimia 75; na Mradi wa Kilolo umefikia asilimia 92.

**B.1.9 UTEKELEZAJI WA MIKAKATI NA MIPANGO MBALIMBALI YA UENDELEZAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU**

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati imeendelea kuandaa na kutekeleza Mipango na Mikakati mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Nishati kama ifuatavyo:

**a) Uhuishaji wa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2020 (*Power System Master Plan Update 2020)***

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuhakikisha uwekezaji katika Sekta Ndogo ya Umeme unaendana na mahitaji yanayotokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, Serikali iliendelea na zoezi la kuhuisha Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2020. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ukusanyaji wa mahitaji ya umeme kwa kila mkoa Tanzania Bara na Zanzibar; na utambuzi wa maeneo ya uwekezaji wa miradi ya nishati jadidifu na kiwango cha nishati jadidifu (jua na upepo) kinachotakiwa kuingizwa

kwenye Gridi ya Taifa. Kazi hii inafanyika kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na inatarajiwa kukamilika Agosti, 2024.

**b) Mkakati wa Nishati Jadidifu na Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati *(Renewable Energy Strategy and its Implementation Roadmap)***

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini, Serikali inaandaa Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Nishati Jadidifu. Kwa sasa Mshauri Mwelekezi anakamilisha uandaaji wa Mkakati baada ya kupokea maoni ya wadau. Kazi hii inafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa *Tanzania Rural Energy Expansion Programme-TREEP* na inatarajiwa kukamilika Juni, 2024.

**c) Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati na Uhuishaji wa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati *(Energy Efficiency Strategy and Update of the Energy Efficiency Action Plan)***

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inashirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kuandaa Mkakati na Mpango kazi wa Matumizi Bora ya Nishati. Mkakati huo unaandaliwa ili kukidhi matakwa ya kitaifa na kimataifa ya kupunguza matumizi ya nishati yasiyo ya lazima, upotevu na gharama za nishati, kuhamasisha utunzaji wa mazingira pamoja na kukuza mchango wa nishati katika maendeleo ya nchi. Tayari Mkakati huo umeandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau kwa maoni kabla ya kukamilishwa na kuanza kutumika.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la uandaaji wa Mkakati huo limehusisha pia uaandaji wa viwango vya matumizi ya vifaa vya nishati vinavyoruhusiwa *(minimum energy performance standards and labelling)*; uboreshaji wa taarifa za matumizi na watumiaji wakubwa wa nishati; kuandaa na kutekeleza miongozo ya watumiaji wakubwa wa nishati; kuandaa sifa za wataalamu katika usiamamizi na ukaguzi wa matumizi ya nishati (*professional qualification and skills in energy management and audit*) na kujenga uelewa kwa umma kuhusu faida na fursa za matumizi bora ya nishati.

**d) Mkakati wa Kitaifa wa Nishati ya Tungamotaka *(Biomass Energy Strategy – BEST)***

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha majadiliano na Umoja wa Ulaya ya kuwezesha kupata ufadhili kwa ajili ya kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Nishati ya Tungamotaka ili kuwa na mwongozo thabiti wa uendelezaji wa rasilimali ya tungamotoka ambayo ni endelevu na isiyokuwa na athari kubwa za kiafya na mazingira.

**e) Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kupeleka Nishati Vijijini *(Rural Energy Master Plan-REMP)***

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA inaendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Master Plan-REMP*) ili kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 huduma ya nishati vijijini iwe inapatikana kwa asilimia 100 na asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

**f) Mikakati na Mipango Mbalimbali ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeidhinisha Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa mwaka 2024 - 2034. Mkakati huu pamoja na mambo mengine, unalenga kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa watanzania kwa kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uhakika ya nishati safi ya kupikia; kupunguza gharama za nishati safi, vifaa na majiko sanifu ya kupikia; kuandaa, kuhuisha na kuoanisha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo wezeshi ya kufanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; kuhamasisha uwekezaji katika nishati safi ya kupikia; kuongeza wigo wa tafiti na ubunifu wa teknolojia zinazohusu nishati ya kupikia; na kuimarisha uelewa wa jamii kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau iliratibu na kushiriki katika mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai Novemba-Desemba, 2023. Katika Mkutano huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua Programu ya Nishati Safi ya kupikia

itakayowawezesha Wanawake Barani Afrika (*African Women Clean Cooking Support Programme-AWCCSP)* kutumia nishati safi ya kupikia. Aidha, Mei, 2024 kutafanyika mkutano wa Wakuu wa Nchi kuhusu Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika, Paris Ufaransa ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan atakuwa Mwenyekiti Mwenza wa mkutano huo kwa kushirikiana na Waziri Mkuu wa Norway, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Nishati Duniani *(International Energy Agency-IEA)* na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mkutano huo pamoja na mambo mengine, unalenga kujadili na kuweka mikakati ya namna ya kuimarisha Sera, ugharamiaji na ushirikiano katika kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuhakikisha Umma wa Watanzania unapata elimu kuhusu nishati safi ya kupikia, Wizara iliandaa kongamano la wanawake la nishati safi ya kupikia lililofanyika Mkoani Dodoma tarehe 9 Machi, 2024 katika kipindi cha siku ya wanawake duniani. Kongamano hilo pamoja na mambo mengine, lilihusisha utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu nishati safi ya kupikia, pamoja na ugawaji wa mitaji na vitendea kazi vya nishati safi ya kupikia. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na UNCDF kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya inaanda mpango wa kuzijengea miundombinu ya nishati safi ya kupikia taasisi za kijamii zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wizara ya Nishati kupitia Wakala wa Nishati Vijijini, imesaini mkataba wa ushirikiano na Jeshi la Magereza ili kuwezesha Jeshi hilo pamoja na vituo inavyovisimamia ikiwemo Magereza 129, Kambi za Makazi ya Watumishi 47, Ofisi 26, Vyuo vinne (4), Shule moja (1) na Hospitali moja (1) kutumia nishati safi ya kupikia. Katika maeneo hayo, jumla ya mifumo 126 ya bayogesi, 64 ya LPG pamoja na majiko banifu itajengwa na kuwezesha ununuzi wa mashine 61 za kuzalisha mkaa mbadala. Sambamba na hilo, jumla la mitungi 15,920 ya gesi ya LPG itagawiwa kwa Watumishi wa Jeshi hilo. Aidha, Wakala wa Nishati Vijijini unakamilisha taratibu za kuwezesha Jeshi la Kujenga Taifa

pamoja na taasisi nyingine hususan za elimu na afya kutumia nishati safi ya kupikia.

**g) Kuridhiwa kwa Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009 *(Statute of the International Renewable Energy Agency – IRENA, 2009)***

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuvutia uwekezaji, utaalamu, teknolojia, utafiti na mitaji katika uendelezaji wa nishati jadidifu, Tanzania ilijiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009 *(Statute of the International Renewable Energy Agency – IRENA, 2009)*. Hatua hii itaongeza kasi ya uendelezaji wa nishati jadidifu nchini na hivyo mchango wa chanzo hicho katika uzalishaji wa nishati ya umeme iliyo nafuu, ya gharama nafuu na rafiki wa mazingira.

## B.2 SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuendeleza Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia nchini katika maeneo ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta na gesi, ambapo mafanikio mbalimbali yaliweza kupatikana.

### B.2.1 MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

**a) Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini kilichopo bahari ya kina kifupi Kusini Mashariki mwa Tanzania. Hadi kufika Machi 2024, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuanza majadiliano na Kampuni ya Maurel & Prom (M&P) ambayo imeonesha nia ya kushirikiana na TPDC katika kazi za utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwenye kitalu hiki ikiwemo uchorongaji wa visima vya utafiti. Aidha, maombi ya leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu husika yapo katika hatua ya uidhinishwaji.

**b) Kitalu cha Eyasi– Wembere**

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha utafutaji wa mafuta katika kitalu cha Eyasi – Wembere kilichopo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilisha kazi ya kukusanya na kuchakata taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D zenye urefu wa kilometa 260 katika awamu ya kwanza, kukamilisha tafsiri ya awali, kuandaa mpango wa awamu ya pili wa ukusanyaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D zenye urefu wa kilometa 1,100; na kukamilika kwa kazi ya ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathiriwa na zoezi la ukusanyaji wa taarifa za mitetemo. Aidha, TPDC inaendelea na hatua ya kumpata mkandarasi wa kufanya tafsiri ya tathmini ya kina ya taarifa za awamu ya kwanza na mkandarasi atakayekusanya taarifa za awamu ya pili ya kazi hii.

**c) Kitalu cha Songo Songo Magharibi**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Songo Songo Magharibi ili kuimarisha upatikanaji, uzalishaji na usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi mbalimbali nchini. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuanza taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa uchorongaji wa visima ambaye atafanya mapitio ya taarifa za kijiolojia na kijiofizikia katika Kitalu na kuandaa rasimu ya Mpango wa Uchorongaji wa visima vya utafiti. Aidha, katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa mradi husika, TPDC kwa kushirikiana na Kampuni ya Pertamina ya nchini Indonesia inaratibu mafunzo kwa vitendo nchini Indonesia kwa Wataalamu 100 ili kuwajengea uwezo katika masuala ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia. Aidha, awamu ya kwanza Watalaamu watano (5) wameshapelekwa kwenye mafunzo hayo.

**d) Vitalu Namba 4/1B na 4/1C**

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu namba 4/1B na 4/1C ili kuongeza upatikanaji, uzalishaji na usambazaji gesi asilia. Hadi kufikia Machi, 2024 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha taratibu za kusaini Makubaliano ya Awali *(Memorandum of Understanding – MoU)* ya

mashirikiano kati ya TPDC na kampuni ya CNOOC kutoka China. Makubaliano hayo yanalenga kushirikiana katika tafiti za awali kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo vitalu hivyo.

### B.2.2 MIRADI YA UTAFUTAJI NA UENDELEZAJI WA MAFUTA NA GESI KATIKA VITALU KUPITIA PSA

**Kitalu cha Ruvuma (Ntorya)**

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusisha uendelezaji gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la Ntorya katika kitalu cha Ruvuma. Hadi kufikia Machi, 2024 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha tafsiri ya taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D zilizokusanywa katika eneo la kilometa za mraba 334.9 na kuendelea na maandalizi ya ukarabati na majaribio ya visima *(well tests)* kwa visima vya Ntorya 1 na Ntorya 2. Aidha, Mkandarasi anaendelea na hatua za ununuzi wa mtambo wa kuchoronga kisima cha Chikumbi-1. Vilevile, Baraza la Mawaziri limeridhia kutolewa kwa leseni ya uendelezaji wa Kitalu hiki ambapo taratibu za utoaji wa leseni hiyo kwa TPDC kwa niaba ya mwekezaji (Kampuni ya ARA Petroleum) zinakamilishwa.

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, maandalizi ya ujenzi wa bomba la kutoa gesi Ntorya kupeleka kwenye kiwanda cha kuchakata gesi cha Madimba yanaendelea ambapo Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIA) imekamilika na Mshauri Mwelekezi wa uhandisi na ujenzi anakamilisha upembuzi yakinifu wa kihandisi ili kuwezesha zabuni ya ujenzi wa bomba kutangazwa.

### B.2.3 MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA KUWA KIMIMINIKA *(LIQUEFIED NATURAL GAS – LNG)*

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unatekelezwa katika eneo la Likong'o mkoani Lindi na utahusisha usindikaji wa gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu Na. 1, 2 na 4 vilivyopo katika kina kirefu cha bahari. Serikali kupitia Timu yake ya Majadiliano *(Government Negotiation Team)* imekwishafanya uchambuzi wa rasimu za Mkataba wa Nchi Hodhi (*Host Government Agreement - HGA*) na Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato Ulioboreshwa (*Amended Production Sharing*

*Agreement – PSA*) kwa ajili ya kuboreshwa kupitia majadiliano na wawekezaji kabla ya kuidhinishwa na Serikali kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi nyingine za Serikali katika rasimu za awali za Mikataba hiyo.

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TPDC imeendelea kushirikiana na Kampuni za Shell na Equinor kufanya maandalizi ya kutekeleza miradi ya uboreshaji wa hali ya maisha kwa wananchi waliopisha eneo la mradi (*post compensation livelihood restoration program*), ikiwemo kusaini Mkataba wa Makubaliano ya ujenzi wa shule ya msingi ya Likong'o iliyopo Manispaa ya Lindi.

### B.2.4 UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA

#### a) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa njia ya mabomba. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa bomba lenye urefu wa kilometa 12.4 kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach lililowezesha kuunganishwa kwa miundombinu ya gesi asilia kwenye viwanda viwili (2) vya Chemi and Cotex Industrial Ltd na Cotex Ltd pamoja na kuunganisha miundombinu ya gesi asilia katika hoteli sita (6) za White Sand Hotel, Land Mark Hotel, Serene Beach Resort, Ramada Resort, Giraffe Hotel na Jangwani Sea Breeze. Vilevile, kiwanda cha Sapphire Float Glass (Tanzania) Co. Ltd kiliunganishwa na miundombinu ya gesi asilia katika Mkoa wa Pwani.

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zilizotekelezwa ni kufanya tafiti na kuandaa andiko la mradi wa kuunganisha gesi asilia katika gereza la Ukonga na nyumba za askari katika magereza ya Ukonga na Keko.

#### b) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa njia ya mabomba katika Mikoa ya Lindi na

Mtwara. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kupunguza msukumo wa gesi *(Pressure Reduction Station – PRS*) na miundombinu ya umeme yenye urefu wa kilometa 3.8 kutoka makutano ya Mahumbika hadi Valvu Namba 3 (BVS 3) na bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka BVS 3 kuelekea Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo mkoani Lindi lenye urefu wa kilometa 10.04. Bomba hilo limewezesha kuunganisha nyumba 209 ambazo zilikuwa na miundombinu ya gesi asilia tangu awali. *Kiambatisho Na.7* ni miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini.

**c) Usambazaji wa Gesi Asilia Kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini - Awamu ya Kwanza na Pili**

**119.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unatekelezwa na TPDC kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na unalenga kusambaza gesi asilia na kuimarisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia katika maeneo ya vijijini. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi wa kujenga miundombinu ya kuunganisha nyumba 451 mkoani Lindi (Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo) na nyumba 529 mkoani Pwani (Mkuranga). Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili wa REA kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.82** kama sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia katika maeneo ya vijijini.

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, TPDC imekamilisha utafiti wa kubaini mahitaji ya gesi asilia katika mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara. Maeneo ya vijijini katika mikoa hiyo yatajengewa miundombinu ya kusambazia gesi asilia kwa ajili ya kupikia ikilenga makazi na taasisi za kibiashara na zisizo za kibiashara ili kupunguza matumizi ya kuni na mikaa kama sehemu ya utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo.

**d) Ujenzi wa Vituo vya Kujaza Gesi Asilia (*Compressed Natural Gas-CNG*) katika Magari kwenye Bohari za Dar es Salaam na Dodoma**

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024 TPDC na GPSA ziliendelea na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa michoro ya kihandisi na Tathmini ya

Athari ya Mazingira na Jamii ili kuwezesha GPSA kujenga vituo vya CNG katika bohari za Dar es Salaam na Dodoma unaotarajiwa kuanza mwaka 2024/25. Lengo la mradi huu ni kuhamasisha matumizi ya gesi asilia katika vyombo vya moto vinavyomilikiwa na Serikali kwa kuongeza upatikanaji wake katika maeneo mbalimbali nchini.

### e) Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Ujenzi na Uendeshaji wa Vituo vya Kujaza Gesi Asilia (CNG) katika Magari

**122.** ***Mheshimiwa Spika****,* kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, vituo viwili vya kujaza gesi asilia (CNG) katika magari vilijengwa na kuanza kutoa huduma Novemba, 2023. Vituo hivyo ni kinachomilikiwa na Kampuni ya TAQA-Dalbit kilichopo pembezoni mwa barabara ya Nyerere karibu na Kiwanja cha Ndege (*Terminal II*) na kituo kinachomilikiwa na Kampuni ya Dangote kilichopo Mwanambaya, Mkuranga mkoani Pwani.

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, karakana nane (8) za kubadilisha mifumo ya matumizi ya nishati ya gesi asilia (CNG) kwenye magari ambayo ni nyenzo muhimu ya kuchochea matumizi ya gesi asilia katika magari zimejengwa na zinamilikiwa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi. Karakana hizo ni NK CNG Auto Limited (Mbezi Beach, Dar es Salaam), MOL CNG Limited na TEMESA (Keko, Dar es Salaam), Kleenair CNG (Kigamboni, Dar es Salaam), TAQA Dalbit (Kipawa, Dar es Salaam), DIT (Dar es Salaam), BQ Contractors Limited (Goba, Dar es Salaam) na Kampuni ya Dangote ambayo imejenga karakana yake katika eneo la kiwanda Mkoani Mtwara kwa ajili ya kuhudumia magari ya kiwanda hicho. Jitihada hizi zimewezesha kuongezeka kwa magari yanayotumia mfumo wa gesi asilia kutoka 3,100 hadi 4,500.

### f) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kusimamia Usambazaji wa Gesi Asilia Nchini

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inashirikiana na JICA kutekeleza mradi wa kujenga uwezo wa kusimamia usambazaji wa gesi asilia nchini (*Capacity Development of Natural Gas Utilization in Tanzania*). Mradi huu unalenga kuhuisha Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (*Natural Gas Utilization Master Plan - NGUMP*), kufanya usanifu

wa mtandao wa usambazaji (*network design*) wa gesi asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Pwani na kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara na Taasisi. Hadi kufikia Machi, 2024, kazi zilizofanyika ni ukusanyaji wa takwimu mbalimbali za kuwezesha uhuishaji wa NGUMP ikiwemo mahitaji, uzalishaji na matumizi ya gesi asilia nchini. Mradi huu unatarajiwa kukamilishwa Oktoba, 2025.

### B.2.5 MRADI WA BOMBA LA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KUTOKA TANZANIA HADI UGANDA

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda. Mradi unalenga kusafirisha gesi asilia pamoja na kuunganisha maeneo yatakayopitiwa na bomba hilo. Hadi kufikia Machi, 2024 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuridhiwa kwa makubaliano ya mikataba mahsusi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Uganda (*Bilateral Agreement*) kwa ajili ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu wa mradi.

### B.2.6 MRADI WA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KUTOKA DAR ES SALAAM (TANZANIA) HADI MOMBASA (KENYA)

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam kwenda Mombasa - Kenya na pia unatarajiwa kunufaisha Mikoa ya Pwani, Tanga, Arusha na Kilimanjaro. Hadi kufikia Machi, 2024 Kamati ya Pamoja ya Wataalamu imekamilisha maboresho ya nyaraka za maridhiano kwa ajili ya kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya upembuzi yakinifu wa mradi.

### B.2.7 MIRADI YA KUHIFADHI NA KUSAFIRISHA MAFUTA

#### a) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda hadi Tanga - Tanzania *(East African Crude Oil Pipeline – EACOP)*

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu unaendelea katika mwaka 2023/24 ambapo hadi kufikia Machi, 2024 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi ya **Shilingi**

**bilioni 34.93** kwa wananchi 9,823 kati ya 9,904 waliopisha utekelezaji wa mradi, sawa na asilimia 99.2; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 340 sawa na asilimia 100 ya makazi mbadala kwa wananchi 294 waliopoteza makazi na kupisha mkuza; kukamilika kwa ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa upashaji joto kwenye mabomba; na kuendelea na ujenzi wa maeneo 14 ya makambi. Aidha, mabomba yenye urefu wa kilometa 400 yameshawasili nchini na zoezi la kuwekewa mfumo wa kupasha joto, usalama na mawasiliano wa bomba *(thermal insulation and fiber optic cables)* linaendelea.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za awali za ujenzi wa matenki zimefikia asilimia 32, usanifu wa kina wa matenki umefikia asilimia 85, ujenzi wa jeti umefikia asimilia 33 na zoezi la upimaji na uwekaji mawe ya mpaka kwenye mkuza wa bomba umekamilika kwa asilimia 100. Aidha, hadi kufikia Machi, 2024, Serikali ilikuwa imelipa jumla ya **Dola za Marekani milioni 289.78** sawa na asilimia 94 ya kiasi kinachotakiwa kuchangiwa kama mtaji katika Kampuni ya EACOP Ltd. Utekelezaji wa Mradi kwa ujumla umefikia asilimia 27.1.

***Kielelezo Na. 5:*** **Uzinduzi wa Karakana ya Kuweka Mfumo wa Kupasha Joto Mabomba kwenye Kijiji cha Sojo Wilayani Nzega**





**b) Mradi wa Bomba Jipya la TAZAMA**

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa bomba jipya la TAZAMA lenye uwezo wa kusafirisha aina mbalimbali za mafuta safi kutoka Dar es Salaam hadi Zambia kwa kutumia mkuza wa bomba la TAZAMA. Tarehe 23 hadi 25 Oktoba, 2023 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya ziara ya kikazi nchini Zambia ambapo pamoja na mambo mengine, alifanya mazungumzo na Rais wa Zambia kuhusu utekelezaji wa mradi huu. Aidha, kupitia mazungumzo hayo ilikubalika mradi utekelezwe sambamba na ujenzi wa matenki ya kuhifadhia mafuta kwa ukubwa wa tani 380,000 kwa upande wa Dar es salaam - Tanzania na tani 120,000 kwa upande wa Ndola – Zambia. Hadi kufikia Machi, 2024, Timu ya Wataalamu imeundwa kwa ajili ya kuangalia namna bora ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba jipya. Sambamba na hilo mkutano wa Mawaziri wa Nishati wa nchi hizi mbili umefanyika kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa utekelezaji wa mradi.

**c) Uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*)**

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu uanzishaji wa hifadhi ya kimkakati ya mafuta ambayo inahitaji pia uwepo wa maghala ya kuhifadhia mafuta na ununuzi wa mafuta yenyewe. TPDC ipo katika hatua za kutafuta Mshauri Mwelekezi wa kufanya tathmini ya mradi pamoja na uendeshaji utakaoshirikisha Wizara, TPDC na Sekta Binafsi.

Maeneo yaliyopo kwa ajili ya uanzishwaji wa SPR ni pamoja na Chongoleani (Tanga), Zuzu (Dodoma), Isaka (Kahama), Makambako (Njombe) na Kigamboni (Dar es Salaam).

### B.2.8 MRADI WA KUJENGA UWEZO WA KUSIMAMIA NA KUENDELEZA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA RASILIMALI ZA ASILI TANZANIA

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu ulianza kutekelezwa Juni, 2017 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mfuko wa Maendeleo wa Afrika (AfDB) na umefikia asilimia 86 ya utekelezaji wake. Kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2023/24 ni pamoja na kukamilisha uundaji wa mfumo wa uondoshaji shehena mipakani kwa Tanzania Bara na Zanzibar; ununuzi na usimikaji wa vifaa mbalimbali katika bandari ya Dar es Salaam na Zanzibar, uhuishaji wa Mkataba Kifani wa Ugawanaji Mapato *(Model Production Sharing Agreement - MPSA)* kupitia PURA na kugharamia mafunzo kwa wataalam kutoka Wizara ya Nishati, PIU, PSC, PURA na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Jumla ya watumishi 77 wamenufaika na mafunzo hayo.

### B.2.9 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMPUNI TANZU ZA TPDC

#### a) TANOIL Investments Limited (TANOIL)

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** TANOIL iliendelea kushiriki katika biashara ya mafuta kama kampuni ya kununua na kuuza mafuta (*Oil Marketing Company - OMC*). Aidha, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, TANOIL iliweza kuagiza kiasi cha lita milioni 34.2 za dizeli ambapo lita milioni 33.1 zimeshauzwa na lita milioni 16.8 za petroli ziliagizwa na zote zimeshauzwa. Katika kipindi hiki, TANOIL imefanikiwa kupata faida ya **Shilingi bilioni 6.8**. Vilevile, TANOIL katika kipindi husika imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 9.8** kati ya **Shilingi bilioni 29** za madeni chechefu kutoka kwa wadaiwa sugu na jitihada za kukusanya madeni yaliyosalia zinaendelea.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa vituo vya mafuta, TANOIL imekamilisha ukarabati wa vituo viwili vya mafuta

katika Mikoa ya Singida na Geita. Vituo hivyo vitaendeshwa kwa mtindo wa kukodisha kwa kampuni binafsi zinazofanya biashara ya mafuta (*Company Owned Dealer Operated Model -CODO)* kwa makubaliano ya kulipa kodi na kununua mafuta kutoka TANOIL. Aidha, ujenzi wa vituo vya Musoma na Tarime (Mara), Segera (Tanga) na Makuyuni (Arusha) vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Hatua hii itaisaidia TANOIL kuweza kushiriki kwenye biashara ya mafuta katika mnyororo wote wa usambazaji na hivyo kuleta tija kwenye ushindani wa sekta.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kukamilika kwa uchunguzi dhidi ya watumishi wa TANOIL walioisababishia hasara kampuni hiyo kwa mujibu wa Taarifa za Hesabu za mwaka 2021/22, Serikali tayari imekwishachukua hatua za kinidhamu ambapo watumishi watatu wamefukuzwa kazi na mmoja kupewa adhabu ya kupunguzwa mshahara kwa asilimia 15. Utekelezaji wa adhabu hizo ni kwa mujibu wa taarifa na mapendekezo ya Kamati ya Uchunguzi iliyoundwa na kwa kuzingatia Taratibu na Miongozo katika Utumishi wa Umma. Aidha, TAKUKURU inaendelea na uchunguzi wa tuhuma za kijinai dhidi ya watumishi hao.

**b) GAS Company – GASCO**

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** GASCO imepewa jukumu la kuendesha na kufanya matengenezo *(Operations and Maintenance - O & M)* ya miundombinu yote ya Taifa ya gesi asilia *(National Natural Gas Infrastructure - NNGI)* inayohusisha mitambo ya kuchakata gesi ya Madimba na Songo Songo pamoja na bomba la kusafirisha gesi kutoka Mtwara na Songo Songo hadi Dar es Salaam. GASCO imeendelea kutekeleza jukumu hilo kwa kuzingatia na kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa vya usalama mahala pa kazi katika kuhakikisha Usalama wa Watu, Miundombinu na Mazingira *(Health Safety and Environment - HSE)*.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024, kazi za uendeshaji na matengenezo zilifanyika kikamilifu bila kupata ajali au kusimamisha shughuli za uzalishaji (*Zero Lost Time Injury (LTI =0*). Vilevile, jumla ya matenegenezo 21,164 ya mitambo mbalimbali yalifanyika kwa ufanisi

sawa na asilimia 95.85 ya mpango kwa kipindi husika. Matengenezo mengine yanaendelea kufanyika baada ya ununuzi wa vipuri kukamilika. Ufanisi huu umewezesha miundombinu yote ya gesi asilia kuwa na utayari (*reliability and availability)* wa asilimia 100 wa kufikisha gesi asilia kwa wateja wake wote.

## B.2.10 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SEKTA YA NISHATI KUPITIA PURA NA EWURA

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) iliendelea kusimamia na kudhibiti Sekta ya Nishati ili kuhakikisha utekelezaji wa shughuli za sekta hiyo unazingatia sheria na taratibu zilizopo pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

### B.2.10.1 MAMLAKA YA UDHIBITI MKONDO WA JUU WA PETROLI (PURA)

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA imeendelea kusimamia shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu mbalimbali nchini kulingana na mikataba ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA) kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na.8*. Hadi kufikia Machi 2024, uzalishaji wa gesi asilia umeendelea kuimarika na kufikia wastani wa futi za ujazo milioni 236.21 kwa siku zilizozalishwa katika vitalu vya Songo Songo (120.27 mmscfd) na Mnazi bay (115.94 mmscfd). Gesi hiyo ilitumika katika matumizi mbalimbali ikiwemo viwandani, majumbani, katika taasisi, katika magari na kwa ajili ya uzalishaji wa umeme.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA inatarajia kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kupitia Duru ya Tano (5). Lengo kuu la zoezi hili ni kuwezesha ugunduzi zaidi wa rasilimali za mafuta na gesi asilia nchini kwa kufanya shughuli za utafutaji katika vitalu vilivyowazi vyenye viashiria vya uwepo wa rasilimali hizo. Hadi kufikia Machi, 2024 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha mapitio na maboresho ya Mkataba Kifani wa Ugawanaji Mapato *(Model Production Sharing Agreement-MPSA)* wa mwaka, 2013 ambapo rasimu ya MPSA (MPSA, 2024) imeandaliwa; na kukamilishwa kwa

Mwongozo wa Kupata Kampuni za Kijiofizikia *(Geophysical Multiclient Company)* zitakazoshirikiana na PURA katika zoezi la kunadi vitalu ambapo taratibu za kupata kampuni hizo zinaendelea.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia PURA imekamilisha zoezi la utengaji wa vitalu vinavyopendekezwa kufanyiwa mnada na kwa sasa zoezi linaloendelea ni kuandaa vifurushi vya taarifa *(data packages)* za vitalu hivyo. Zoezi la kunadi vitalu linatarajiwa kuzinduliwa mara baada ya kuidhinishwa kwa MPSA, 2024 na marekebisho ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** kaguzi na usimamizi wa shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia umeendelea kufanyika katika vitalu vya Tanga, Namba 1, 2 & 4, Nyuni, Ruvuma, Ruvu na Kiliwani North. Aidha, katika Eneo la Eyasi-Wembere shughuli ya uchakataji wa data zilizochukuliwa za mfumo wa 2D imekamilika na taratibu za kumpata Mkandarasi wa kutafsiri data hizo zinaendelea. Katika Kitalu cha Ruvuma, kazi ya kutafsiri taarifa za mitetemo zilizochukuliwa katika eneo la kilometa za mraba 334 imekamilika na kuanza kwa maandalizi ya uendelezaji wa gesi asilia iliyogunduliwa ikiwemo ukarabati wa visima vya Ntorya-1 na Ntorya-2 vitakavyotumika kuzalisha gesi asilia na uchorongaji wa kisima cha utafutaji cha Chikumbi-1. *Kiambatisho Na.* 9 ni ramani inayoonesha hali ya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mfuta na gesi asilia nchini.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia azma ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wananufaika na uwekezaji katika rasilimali zilizopo katika maeneo yao, Serikali kupitia PURA na TPDC imeandaa rasimu ya Miongozo ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii *(Corporate Social Responsibility – CSR)* katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia nchini inayotarajiwa kukamilika mwishoni mwa Juni, 2024. Aidha, maandalizi ya rasimu yamehusisha wadau kutoka maeneo mbalimbali ikiwemo mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Serikali inapata stahiki zake kwa mujibu wa mikataba iliyoingiwa kati yake na Wawekezaji katika shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini, PURA imeendelea kufanya kaguzi za gharama katika mikataba ya PSA ambapo hadi kufikia Machi 2024, kaguzi hizo ziliwezesha jumla

ya **Shilingi bilioni 211** kutolewa kwenye madai ya gharama za uwekezaji na kurudishwa kwenye mfuko wa ugawanaji mapato kati ya Serikali na Wawekezaji.

### B.2.10.2 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

#### a) Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Kati na Chini wa Gesi Asilia

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA iliendelea kusimamia na kudhibiti shughuli za gesi asilia kwa kufanya kaguzi za mara kwa mara katika miundombinu ya uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia na vituo vya kujazia gesi kwenye magari (CNG) katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya kaguzi za kawaida 25 kwenye miundombinu ya gesi asilia zilifanyika na kaguzi moja maalum ya kitaalam na kiusalama kwenye vituo vitatu (3) vya kujazia gesi kwenye magari na karakana saba (7) za kuongeza mfumo wa gesi asilia kwenye magari ulifanyika. Ukaguzi huu maalumu ulishirikisha EWURA, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB). Lengo ni kuhakikisha usalama kwenye eneo la utaalam, vifaa na mazingira ya utekezaji wa shughuli zinazohusu matumizi ya gesi asilia katika magari. Kupitia kaguzi hizo, imebainika miundombinu na shughuli zote zinazohusisha gesi asilia hapa nchini zipo katika hali nzuri inayokidhi viwango vya ubora na usalama.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2024, EWURA ilitoa vibali sita (6) kwa ajili ya ujenzi *(construction approvals)* wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia viwandani na vituo vya CNG. Vibali hivyo vilitolewa kwa TPDC kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikuu *(mother station)* cha kuzalisha CNG kwenye eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vituo vidogo viwili (2) *(daughter stations)* vya kupokea CNG katika kiwanda cha Kairuki (Kibaha) na hospitali ya Taifa ya Muhimbili na vibali vingine viwili (2) kwa ajili ya ujenzi wa mabomba ya kuunganisha gesi asilia kwenye kituo cha kujazia gesi kwenye magari cha Dangote na kwenye kiwanda cha kampuni ya KEDA vilivyopo Mkuranga.

Aidha, EWURA ilitoa kibali cha ujenzi kwa kampuni ya PanAfrican Energy Tanzania (PAET) kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi la kuunganisha kituo cha kujazia gesi asilia kwenye magari cha kampuni ya TAQA Dalbit - Kipawa.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** EWURA pia ilitoa leseni mbili (2) za uendeshaji *(operational licence)* kwa vituo viwili vya kujazia gesi asilia kwenye magari *(CNG filling station)*. Vituo hivyo vinamilikiwa na Kampuni za TAQA Dalbit (Kipawa - Dar es Salaam) na Dangote (Mkuranga – Pwani) vinavyohudumia watumiaji wa nishati ya gesi asilia kwenye maeneo husika.

**b) Shughuli za Bidhaa za Mafuta ya Petroli**

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na usimamizi wa ubora wa vituo vya mafuta ili kuimarisha upatikanaji, usalama na ubora wa bidhaa za mafuta kwa watumiaji katika maeneo yote nchini. Aidha, imeendelea kusimamia mazingira chanya ya uwekezaji wa ujenzi wa vituo vya mafuta vyenye ubora ambapo hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya vituo 2,522 vilivyopo mijini na vijijini vilikidhi vigezo vya ubora na usalama na kupewa leseni ikilinganishwa na vituo 2,297 katika kipindi hicho mwaka 2022/23, sawa na ongezeo la asilimia 9.80. Kati ya vituo hivyo, vituo 434 vimejengwa katika maeneo ya vijijini ikilinganishwa na vituo 287 vilivyojengwa vijijini kwa kipindi hicho mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 51.22.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, EWURA ilitoa leseni, vibali, kuboresha Kanuni na kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta kama ifuatavyo:

i. Ilitoa leseni 34 kwa kampuni za mafuta (wholesalers) kwa ajili ya kuagiza na kuuza mafuta kwa jumla, ambapo leseni 30 zilitolewa kwa kampuni mpya;

ii. Ilitoa leseni mpya 4 kwa kampuni za kuagiza na kuuza Gesi itokanayo na Petroli (LPG) kwa jumla (*LPG Wholesalers*). Pia, ilitoa leseni 27 kwa Mawakala wa Kusambaza LPG *(LPG Distributors)*. Kati ya leseni hizo, leseni 26 zilitolewa kwa Mawakala wapya;

iii. Ilitoa leseni saba (7) kwa kampuni zenye miundombinu binafsi ya kuhifadhi na kujaza mafuta (*consumer installation facilities*). Kati ya leseni hizo, leseni sita (6) zilitolewa kwa kampuni mpya;

iv. Ilitoa leseni mpya moja (1) ya ghala la kuhifadhia mafuta (*petroleum storage*);

v. Ilitoa leseni moja (1) ya uwakala wa *condensate.*

vi. Ilitoa vibali vya ujenzi (*construction approvals*) 237 ambapo vibali 233 vilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafuta, kimoja (1) kwa ajili ya miundombinu ya kuhifadhia LPG, viwili (2) kwa ajili ya matumizi binafsi (*consumer installations*) na kimoja (1) kwa ajili ya ghala ya kuhifadhia mafuta;

vii. Ilisimamia taratibu za uagizaji na usambazaji wa mafuta ili kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini;

viii. Ilisimamia ubora wa bidhaa za mafuta nchini kwa kufanya kazi ya kuchukua sampuli za mafuta kutoka kwenye vituo vya mafuta na maghala ya kuhifadhia mafuta na kupeleka maabara kwa ajili ya vipimo. Aidha, jumla ya sampuli 318 zilichukuliwa kutoka katika miundombinu tajwa kwa ajili ya kupima ubora na sampuli 303 sawa na asilimia 95.3 zilifaulu kwa kuwa na viwango stahiki vya ubora. EWURA inachukua taratibu za kisheria ikiwemo kufungia wahusika kutoendelea kufanya biashara pindi wanapobainika kuwa na dosari hadi hapo wanapokidhi matakwa ya leseni zao. Pia, EWURA inaendelea kutoa elimu na ushauri kwa wadau ili waendelee kutoa huduma stahiki;

ix. Ilifanya maboresho ya Kanuni zikiwemo *The Petroleum (Wholesales Storage Retail and Consumer Installation) Rules,* 2023 ili kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za biashara ya mafuta kutoka kwa wafanyabiashara wa mafuta wa jumla pamoja na maghala ya kuhifadhia mafuta; *the Petroleum (Retail Operations in Townships and Villages) (Amendment) Rules,* 2023 ambazo zilifanyiwa maboresho ili kuwezesha ukusanyaji wa takwimu za

biashara ya mafuta kutoka kwenye vituo vya mafuta; na the *Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products Price Setting) (Amendment) Rules, 2023* ambazo zilifanyiwa maboresho ya jedwali la ukokotoaji wa bei za mafuta;

x. Ilikagua ubora wa miundombinu ya mafuta na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta kwa wananchi bila kuhatarisha afya, usalama na mazingira. Katika kipindi hiki, ukaguzi ulifanyika kwenye miundombinu ya mafuta 446 na miundombinu ya mafuta 338 sawa na asilimia 75.78 ilikidhi viwango stahiki vya ubora. EWURA inaendelea kutoa elimu kuhusiana na usalama na mazingira ya miundombinu ya mafuta kwa wahusika; na

xi. Ilitoa bei elekezi za mafuta kila mwezi na kusimamia utekelezaji wake.

**c) Udhibiti wa Biashara ya Vilainishi**

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla upatikanaji na ubora wa vilainishi nchini ni wa kuridhisha. Serikali kupitia EWURA inaendelea na usimamiaji wa ubora wa vilainishi vinavyoingizwa nchini ambapo leseni 99 za wauzaji wa jumla wa vilainishi na leseni 6 za wafanyabiashara wanaotengeneza vilainishi nchini zimetolewa. Vilevile, EWURA inaendelea kushirikiana na Tume ya Ushindani (FCC) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kudhibiti ubora wa bidhaa za vilainishi zinazoingizwa nchini kwa kufanya kaguzi kwa pamoja. Aidha, EWURA imeanza kusajili vilainishi vinavyozalishwa na kuagizwa kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuhakikisha vilainishi vyenye ubora uliothibitishwa na Taasisi za ndani na kimataifa vinatumika nchini. EWURA inaendelea kutoa elimu kwa watumiaji kununua bidhaa hizo kutoka kwa wauzaji waliothibitishwa.

**d) Uwekaji Vinasaba katika Mafuta**

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA iliendelea na jukumu la kusimamia na kukagua soko la ndani la mafuta ili kuhakikisha kuwa mafuta yanayouzwa nchini yana viwango stahiki vya vinasaba kwa lengo la kudhibiti ubora na kuimarisha mapato ya Serikali kupitia kodi.

Uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta unafanywa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ambapo hadi kufikia Machi 2024, kiasi cha lita bilioni 1.18 za mafuta ya petroli, lita bilioni 1.70 za mafuta ya dizeli na lita milioni 6.18 za mafuta ya taa ziliwekewa vinasaba nchini. Aidha, katika kipindi hicho EWURA ilipima mafuta kwenye vituo 307 ambapo vituo 299, sawa na asilimia 97.39, vilifaulu kwa kuwa na kiwango stahiki cha vinasaba. Vituo ambavyo vilikutwa na mafuta ambayo hayana kiwango stahiki cha vinasaba vilichukuliwa hatua za kisheria.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TBS inafanya maboresho ya kutumia teknolojia *(automation)* katika kuweka vinasaba kwenye mafuta na hadi sasa mifumo ya kuweka vinasaba kwa teknolojia hiyo imeunganishwa katika maghala sita na TBS inaendelea na taratibu za kujenga vituo vya kupima vinasaba kwa hiari kabla mafuta hayajafika kituoni (*voluntary check points*). Vituo hivi vitawezesha wafanyabiashara kuhakikisha uwepo wa vinasaba kwenye mafuta kabla ya kufikisha mafuta vituoni.

### e) Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Umeme

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024 Serikali kupitia EWURA ilitekeleza yafuatayo:

a) Ilitoa leseni tatu (3) za Muda Mfupi *(Provisional Licence)* zenye uwezo wa kuzalisha Megawati 14.5 kwa Kampuni tatu ambazo ni Bugando Natural Energy Limited MW 5; Lilondi Hydropower Limited MW 4.5; na Tangulf Nakatuta Energy Company Limited MW 5;

b) Ilitoa leseni 1,163 kwa wataalamu wenye sifa za kufunga mifumo ya umeme nchini ili kusaidia katika juhudi za Serikali za kusambaza umeme kwa mujibu wa kifungu namba 5(a) na 8(1) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131. Kati ya hizo Daraja A (51); Daraja B (105); Daraja C (699); Daraja D (306) na Daraja S1 (2);

c) Ilikagua miundombinu ya umeme ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji, upatikanaji wa huduma bora, na uzingatiwaji wa

Sheria kwa mujibu wa kifungu namba 31(2) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131. Miundombinu ya umeme iliyokaguliwa ni:

i. Miundombinu ya TANESCO ya kusambaza na kugawa umeme katika mikoa 17 nchini. Mikoa hiyo ni; Mwanza, Simiyu, Tabora, Mbeya, Songwe, Arusha, Mtwara, Dodoma, Tanga, Morogoro, Mara, Lindi, Pwani, Kagera, Ruvuma, Rukwa na Songwe. Pia EWURA ilifanya ukaguzi wa miundombinu ya kusamabaza umeme kwa kampuni ya Mwenga Power Services;

ii. Mitambo 14 ya kuzalisha umeme. Mitambo hiyo ni Kinyerezi I (MW 150.00), Kinyerezi I Extension (MW 185.00), Kinyerezi II, Ubungo I (MW 102.00), Ubungo II (MW 129.00), Ubungo III (112.50), Tegeta (MW 45.0), Songas (189.0), Mtera (MW 80.00), Andoya Hydro Power Plant (1.00), Yovi Hydro Power Company Ltd (0.95), Mwenga Hydro Ltd (4.00), Kidatu (204.00) na Kihansi (180.00); na

iii. Miundombinu ya kusafirisha umeme kwenye laini ya Ubungo-Chalinze (Kilovoti 132) pamoja na vituo vyake vya kupozea umeme vya Ubungo, Mlandizi na Chalinze.

d) Ilikagua miradi ya kuzalisha umeme inayotekelezwa ili kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wake, kwa mujibu wa Sheria ya Umeme. Miradi hiyo ni:

i. Mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere Hydropower Project (2115MW);

ii. Mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo Hydropower Project (80MW); na

iii. Mradi wa kuzalisha umeme wa Kikagati-Murongo Hydropower Plant (14MW).

e) Iliridhia mkataba wa mauziano ya umeme *(Power Purchase Agreement)* wa Megawati 26.67 kati ya TANESCO na Rusumo Power Company Limited (RPCL). Mradi huu umechangia kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme kwenye mfumo wa Gridi ya Taifa;

f) Iliridhia jumla ya mikataba 14 yenye jumla ya Megawati 79.2 ya kuuziana umeme *(Standardized Power Purchase Agreement- SPPA)* kati ya TANESCO na wazalishaji wadogo *(Kiambatisho Na. 10)* ili kuimarisha upatikanaji wa huduma ya nishati ya umeme kwa wananchi waliounganishwa katika Gridi ya Taifa na nje ya Gridi ya Taifa; na

g) Ilifanya marekebisho ya Kanuni za Shughuli za Ugavi wa umeme na Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji Umeme za Mwaka 2023 kwa ajili ya kuboresha taratibu za kufanya ukaguzi.

## B.2.11 USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI NA USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA

**154. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kampuni za wazawa na watalaam wazawa wanashiriki kikamilifu kwenye mnyororo wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia nchini, Serikali kupitia EWURA na PURA zimeendelea kuhuisha kanzidata za watoa huduma na wataalamu wa ndani *(Local Suppliers and Service Providers Database (LSSP)* na *Local Professional Database)* kupitia mfumo wa "*Common Qualification System –CQS*". Kupitia mfumo huo, EWURA imesajili kampuni za wazawa 2,029 na wataalam wazawa 198 kwenye kanzidata ya EWURA na jumla ya Kampuni 157 zimesajiliwa na zinapata fursa za kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali kwenye Miradi inayoendelea na wataalamu 187 wa ndani wenye ujuzi mbalimbali katika tasnia ya mafuta na gesi asilia wamesajiliwa katika mfumo na kanzidata ya shughuli za petroli. Aidha, takribani kampuni 250 zilipata zabuni za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja katika mradi wa EACOP na miradi mingine katika Sekta Ndogo ya Gesi Asilia.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** takribani Watanzania 3,227 walikuwa wameajiriwa katika miradi ya mafuta na gesi asilia hususani katika mradi wa EACOP na Watanzania 212 wameajiriwa katika vitalu vya uzalishaji wa gesi asilia vya Mnazi Bay na Songo Songo. Aidha, shughuli za utafutaji wa gesi asilia pia huzalisha ajira za muda ambapo jumla ya Watanzania 148 waliajiriwa katika kazi ya uchukuaji wa data za mitetemo za 3D katika Kitalu cha Songo Songo na 250 waliajiriwa katika kazi ya uchukuaji wa data za mitetemo za 2D katika Kitalu cha Eyasi Wembere. Sambamba na ajira, takribani **Dola za Marekani milioni 44.5** zilitumiwa na kampuni za kigeni zilizowekeza katika shughuli za mafuta na gesi asilia kununua bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa na kupatikana nchini.


## B.2.12 HALI YA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NCHINI

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli nchini, Serikali imeendelea kutumia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja *(Bulk Procurement System - BPS)*. Mfumo huu ulianzishwa mwaka 2011 na kuanza kutumika rasmi Januari, 2012 ambapo pamoja na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wakati wote pia uagizaji wa mafuta umeendelea kufanyika kwa ufanisi na hivyo mlaji wa mwisho kulipia mafuta kwa bei stahiki. Aidha, mfumo huu umewezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za bidhaa za mafuta ya petroli yanayoingia nchini na kwenda nchi jirani na pia kurahisisha udhibiti wa ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya lita bilioni 6.28 za bidhaa za mafuta ya petroli ziliingizwa nchini kwa kutumia mfumo wa BPS kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024. Bidhaa hizo ziliingizwa kupitia Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, ambapo dizeli ilikuwa lita bilioni 3.77, petroli lita bilioni 2.29 na mafuta ya ndege/taa lita milioni 224. Aidha, mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 6.07 ikilinganishwa na kiasi kilichoingizwa Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Vilevile, kiasi cha mafuta yaliyoingizwa kwa ajili ya kwenda nchi jirani kilipungua kwa asilimia 4.76 kutokana na changamoto ya upatikanaji wa Dola za Marekani. Kati ya mafuta


yaliyoingizwa Julai, 2023 hadi Machi, 2024 lita bilioni 3.37 sawa na asilimia 53.7 yalikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita bilioni 2.9 sawa na asilimia 46.3 yalikuwa kwa ajili ya nchi jirani. *Kielelezo Na. 6* kinaonesha uwiano wa bidhaa za mafuta zilizoingizwa nchini kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024. *Kielelezo Na.7* ni jumla ya kiasi cha mafuta kilichoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani na nchi jirani katika kipindi hicho.

***Kielelezo Na.6:*** **Uwiano wa Bidhaa za Mafuta Zilizoingizwa Nchini kwa Kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024**




*Chanzo:* ***PBPA***

***Kielelezo Na.7*: Jumla ya Kiasi cha Mafuta Kilichoingizwa kwa Ajili ya Matumizi ya Ndani na Nchi Jirani, Julai 2023 hadi Machi 2024**




*Chanzo:* ***PBPA***

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya zabuni 88 zilitolewa kwa njia ya ushindani wa kimataifa kwa kigezo cha gharama ndogo za uletaji wa mafuta nchini (*premium*). Aidha, wastani wa zabuni 9 hadi 12 zilishindanishwa kila mwezi ambapo wastani wa wazabuni wanne (4) hadi sita (6) hushinda zabuni hizo kila mwezi. Katika zabuni hizo TPDC imekuwa ikishiriki na hivyo kuongeza ushindani na kuchangia upatikanaji wa gharama stahiki za uagizaji wa mafuta.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto ya upatikanaji wa Dola za Marekani imeendelea kuikabili nchi yetu kama ambavyo nchi nyingi Duniani zinapitia changamoto hiyo. Makali ya tatizo hili yanatokana na vita baina ya Urusi na Ukraine na mabadiliko ya sera ya fedha za Marekani. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, Taasisi zinazohusika katika mnyororo wa biashara ya mafuta pamoja na Sekta Binafsi zilishirikiana kuchukua hatua mbalimbali. Benki Kuu ya Tanzania ilisimamia suala hili ikiwemo kuruhusu benki kuuziana fedha za kigeni hususan Dola za Marekani ili kuchagiza upatikanaji wake katika soko la ndani; kuruhusu ulipiaji wa mafuta kwa kutumia fedha

nyingine za kigeni; na kuongeza kiwango cha ukomo wa ukopaji kwa wanunuzi wa mafuta (*OMC's borrowing limit*) katika benki za biashara.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mpito kuelekea uwekezaji wa miundombinu ya kupokea mafuta kwa pamoja, Serikali imeendelea kutumia miundombinu ya Kampuni ya TIPER kama Kituo cha Kupokea Mafuta kwa Pamoja (*Single Receiving Terminal - SRT*) ambapo kina uwezo wa kupokea wastani wa meli moja hadi mbili (2) kwa mwezi. Idadi hii inafikia asilimia kati ya 30 hadi 60 ya meli mbili (2) hadi nne (4) zinazoingia nchini kila mwezi kushusha shehena ya mafuta ya dizeli. Hivyo meli zinazokosa nafasi ya kushusha mafuta TIPER hutumia muda mrefu kumaliza kushusha mafuta. Ikiwa ni hatua ya kuboresha ufanisi, TIPER inaendelea kusimika pampu za kuhamisha mafuta zenye uwezo mkubwa wa kusukuma hadi lita 800,000 kwa saa ili kuongeza kasi ya kuhamisha mafuta kwenda kwenye maghala ya kampuni za mafuta (OMCs) ambapo kazi hii inatarajiwa kukamilika Januari, 2025.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PBPA imekamilisha ufungaji na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki (SCADA) ili kusaidia udhibiti wa upotevu wa mafuta kwenda kwa wafanyabiashara wa mafuta ya jumla (OMCs) wakati wa upakuaji. Mfumo huu una uwezo wa kusoma kiasi cha mafuta yanayopita katika mita *(flowmeter)* za Serikali zilizopo Kurasini, Kigamboni, Tanga na Mtwara na kulinganisha kiasi cha mafuta yanayopita katika mita zilizopo kwenye maghala ya kuhifadhi mafuta. Upatikanaji wa taarifa hizi kutoka kwenye mita unawezesha Serikali kudhibiti upotevu wa mafuta.

## B.2.13 MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeendelea kufuatilia mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia ambapo kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 bei ya pipa la mafuta ghafi kwa wastani ilishuka kwa asilimia 7 na kufika wastani wa Dola za Marekani 84 kwa pipa ikilinganishwa na wastani wa Dola za Marekani 90 kwa pipa kwa kipindi kama hicho katika mwaka 2022/23. Kushuka huko kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia kulichangiwa na kudorora kwa uchumi wa dunia uliotokana na migororo ya kivita ikiwemo Urusi na

Ukraine pamoja na Israel na Palestina. Vilevile, kulichangiwa na kudorora kwa ukuaji wa uchumi wa mataifa makubwa kama China kulikosababishwa na athari zilizotokana na UVIKO-19. *Kielelezo Na.8* ni mwenendo wa bei za mafuta ghafi katika soko la Dunia.


***Kielelezo Na.8*: Mwenendo wa Bei ya Mafuta Ghafi katika Mwaka 2022/23 na 2023/24**

| **Mwezi** | **DOLA KWA PIPA** | |
|---|---|---|
| | **2023/24** | **2022/23** |
| Julai | 80 | 105 |
| Agosti | 85 | 98 |
| Septemba | 92 | 91 |
| Oktoba | 91 | 93 |
| Novemba | 83 | 87 |
| Disemba | 78 | 82 |
| Januari | 80 | 80 |
| Februari | 82 | 84 |
| Machi | 85 | 79 |
| Wastani | 84 | 89 |
| **Badiliko** | **-6%** | |

Chanzo: ***EWURA***

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** kushuka kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia, kulisababisha kushuka kwa wastani wa asilimia 8 ya bei za mafuta yaliyosafishwa ambapo bei ya mafuta ya petroli ilishuka kwa asilimia 1, dizeli kwa asilimia 13 na mafuta ya taa/ndege kwa asilimia 10. Hadi kufikia Machi 2024, bei za mafuta yaliyosafishwa katika soko la Dunia kwa wastani zilikuwa Dola za Marekani 785 kwa tani ya petroli, Dola za Marekani 797 kwa tani ya dizeli na Dola za Marekani 832 kwa tani ya mafuta ya taa/ndege ikilinganishwa na wastani wa Dola za Marekani 795 kwa tani ya mafuta ya petroli, Dola za Marekani 919 kwa tani ya dizeli na Dola za Marekani 925 kwa tani ya mafuta ya taa/ndege katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. *Kielelezo Na.9* ni wastani wa mwenendo wa bei za mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kwa Mwaka 2022/23 na 2023/24

***Kielelezo Na.9:*** **Wastani wa Mwenendo wa Bei za Mafuta Yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kwa Mwaka 2022/23 na 2023/24**




Chanzo:**EWURA**


### B.2.14 MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

**164. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA iliendelea kupanga bei za ndani za mafuta kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Aidha, bei za mafuta nchini zilionesha kutengamaa ikilinganishwa na mwaka uliopita. Mathalani kwa mkoa wa Dar es Salaam wastani wa bei za mafuta kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 zilishuka kwa asilimia 7 kwa mafuta ya taa/ndege, asilimia 2 kwa mafuta ya dizeli; na yalipanda kwa asilimia 2 kwa mafuta ya petroli, ambapo wastani wa bei ya petroli kwa lita ilikuwa **Shilingi 3,129**, dizeli **Shilingi 3,113** na mafuta ya taa **Shilingi 3,047** ikilinganishwa na wastani wa bei za mafuta hayo kwa kipindi hicho mwaka 2022/23 ambapo zilikuwa petroli **Shilingi 3,081**, dizeli **Shilingi 3,167** na mafuta ya taa **Shilingi 3,282** kwa lita.

**165. *Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa bei nchini kulitokana na kushuka kwa bei ya mafuta ghafi kwenye soko la Dunia, hatua zilizochukuliwa na Serikali za kutoruhusu kutumia fedha za kigeni zilizopo ndani ya nchi kulipia mafuta yanayokwenda nchi jirani (*transit cargoes*) pamoja na kuruhusu kutumia aina tofauti za fedha za kigeni kuagiza

mafuta yanayotumika nchini. *Kielelezo Na. 10* kinaonesha wastani wa mwenendo wa bei za mafuta nchini.

***Kielelezo Na.10*: Wastani wa Mwenendo wa Bei za Mafuta Nchini**




Chanzo**: EWURA**

**B.2.15 KUIMARISHA UTENDAJI KAZI NA UTOAJI HUDUMA**

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kukamilisha Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba unaotekelezwa na Mkandarasi- Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambapo hadi kufikia Machi, 2024 ujenzi huo ulifikia asilimia 75.1 na matarajio ya Wizara ni kuhamia katika jengo hilo katika mwaka 2023/24. Ukamilishwaji wa jengo hilo ni hatua ya kuhakikisha Watumishi wanakuwa na mazingira bora ya utekelezaji wa majukumu kwa tija na ufanisi.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Taasisi zilizo chini ya Wizara zinaimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma, Wizara ilisimamia watumishi kujisajili katika mfumo mpya wa Usimamizi na Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS). Aidha, Wizara iliendelea kuwajengea uwezo watumishi wake pamoja na Taasisi zilizo chini yake ambapo jumla ya watumishi 59 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu

na watumishi 3,048 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika kada mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, watumishi wa Wizara walikuwa 53, TANESCO 2,320, TPDC 248, REA 100, PURA 51, PBPA 48 na EWURA 228.

**168. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ili zifanye kazi kwa tija inayotarajiwa. Kufuatia hatua ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuteua Wenyeviti wa Bodi ya Wakurugenzi ya REA na TANESCO, Wizara iliteua Wajumbe wa Bodi hizo ili kuimarisha usimamizi na utendaji kazi wa Taaasisi hizo.

## B.2.16 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

**169. *Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mbalimbali yamepatikana katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2023/24. Mafanikio hayo ni pamoja na:

1. Uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa umeongezeka na kufikia MW 2,138 Machi, 2024 kutoka MW 1,872.1 zilizozalishwa mwaka 2022/23, ikiwa ni ongezeko la asimia 14.2;

2. Kuanza kwa uzalishaji wa umeme kupitia Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) wenye uwezo wa kuzalisha MW 2,115 ambapo tayari uzalishaji umeanza kwa MW 235 kupitia mtambo Namba 9. Aidha, matarajio ni mradi huu kukamilika Desemba, 2024 kwa mitambo yote nane (8) yenye uwezo wa kuzalisha MW 235 kila moja kuwa inazalisha umeme;

3. Kukamilisha ujenzi wa mitambo ya kufua umeme ya Kinyerezi I Extension MW 185 ambapo kwa sasa mitambo yote minne (4) inafua umeme kiasi cha MW 40 kila mmoja unaoigizwa katika gridi ya Taifa;

4. Miundombinu ya kusafirisha umeme imeongezeka na kufikia jumla ya urefu wa kilometa 7,745.4 ikiwa ni ongezeko la asilimia 21.7 ikilinganishwa na kilometa 6,363.3 za mwaka 2022/23;

5. Kuanza kutumika kwa njia ya kusafirisha umeme wa Kilovoti 400 kutoka JNHPP hadi Chalinze pamoja na kituo kipya cha kupoza umeme cha Chalinze cha Kilovoti 400/220/132 kinachotumika kupoza na kusafirisha umeme unaotoka JNHPP na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa;

6. Kukamilika kwa asilimia 99 kwa Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme (*SGR Lot II*);

7. Kukamilika kwa asilimia 99.4 kwa Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga. Aidha, ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Arusha hadi Namanga yenye urefu wa kilometa 114.3 umefikia asilimia 97.5 na kituo cha kupoza umeme cha Lemugur kimekamilika kwa asilimia 100 na kuwashwa;

8. Miundombinu ya kusambaza umeme imeongezeka na kufikia kilometa 176,750.9, ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.9 ikilinganishwa na kilometa 168,548.5 za mwezi Mei, 2023;

9. Jumla ya wateja 4,784,297 wameunganishiwa umeme hadi kufikia Machi, 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.4 ikilinganishwa na wateja 4,319,258 waliokuwa wameunganishiwa umeme Juni, 2023;

10. Kuweka mifumo ya kisasa ya mawasiliano katika vituo tisa (9) vya kupoza umeme ili viendeshwe kidigitali (*unmanned substations*) ambapo kituo kimoja cha Buzwagi kimekamilika;

11. Jumla ya vijiji 11,837 sawa na asilimia 96.37 ya vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara vimeunganishwa na umeme hadi kufikia Machi, 2024;

12. Kuandaliwa na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri kwa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa mwaka 2024 - 2034. Mkakati huu ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha angalau asilimia 80 ya watanzania kuwa wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034 kwa kutatua vikwazo mbalimbali vinavyokwamisha matumizi ya nishati hiyo ikiwa ni pamoja na gharama kubwa, upatikanaji hafifu na uhaba wa miundombinu yake; kukosekana kwa elimu ya kutosha kuhusu madhara ya nishati zisizo safi na salama za kupikia pamoja na baadhi ya mila, desturi na tamaduni zinazochochea matumizi ya nishati zisizo safi na salama za kupikia;

13. Kuzinduliwa kwa Programu ya Nishati Safi ya Kupikia inayoloenga Kuwawezesha Wanawake Barani Afrika Kutumia Nishati Safi ya Kupikia (*African Women Clean Cooking Support Programme – AWCCSP*), iliyozinduliwa Desemba 2023 katika Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan; na

14. Kufanikisha ununuzi wa asilimia 20 ya hisa za Kampuni ya Wentworth kwenye Mkataba wa Uendeshaji wa Kitalu cha Uzalishaji gesi asilia cha Mnazi Bay kilichopo Mtwara. TPDC imeongeza uwekezaji katika kitalu hicho kwa asilimia 20;

### B.2.17 CHANGAMOTO ZILIZOPO NA UTATUZI WAKE

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2023/24, Sekta ya Nishati ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo zifuatazo:

a) Uzalishaji wa umeme na gesi asilia kutoendana na mahitaji kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme imekuwa ikichangia pia kutokidhi mahitaji ya upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa wananchi. Kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali, ikiwemo kuharakisha utekelezaji wa miradi ya uzalishaji wa umeme pamoja na kukarabati na kufanya matengenezo ya miundombinu ya umeme, hali ya upatikanaji wa umeme nchini unaokidhi mahitaji imeendelea kuimarika hadi kufikia Machi, 2024.

   Aidha, Serikali iliendelea kuchukua hatua za kuimarisha upatikanaji wa gesi asilia, ikiwa ni pamoja na kukarabati na kuongeza msukumo wa gesi asilia kwenye visima na mabomba katika Kitalu cha Songo Songo; kutoboa maeneo mapya ya kuzalishia gesi asilia (*perforation*) katika visima viwili (2) na kuchoronga visima viwili katika kitalu cha Mnazi Bay; pamoja na uendelezaji wa kitalu cha Ruvuma katika eneo la Ntorya.

b) Vitendo vya hujuma/uhalifu katika miundombinu ya umeme. Serikali inaendelea kuwachukulia hatua za kisheria wanaobanika kutekeleza vitendo hivyo na inaendelea kutoa wito kwa wananchi wasio na nia njema kuacha vitendo hivyo, kwa kuzingatia hasara na usumbufu mkubwa unaojitokeza kwa watumiaji wa umeme kutokana na vitendo hivyo.

c) Changamoto ya upatikanaji wa Dola za Marekani kwa ajili ya kulipia mafuta yaliyoagizwa nchini iliyosababisha wafanyabishara kupunguza kiasi cha mafuta kilichokuwa kinaagizwa. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania na wadau wengine ilichukua hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya mikataba ya kuagiza mafuta na kuruhusu matumizi ya fedha za kigeni zikiwemo fedha ya Uingereza (*British Pound*), Umoja wa Ulaya (*Euro*) na Umoja wa Nchi za Uarabuni (*Dirham*). Aidha, Wizara ya Nishati kupitia EWURA iliimarisha ukaguzi katika vituo vya mafuta ili kuhakikisha mafuta yanapatikana wakati wote katika maeneo yote nchini.

## C. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2023/24, sasa napenda kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25.

**172.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2024/25 utekelezaji wa majukumu ya Wizara utaongozwa na vipaumbele mbalimbali vinavyojikita katika kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kufikisha gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia; kupeleka nishati vijijini, ikiwemo katika vitongoji; kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia ikiwemo mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG Project*), ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*) na upelekaji wa gesi asilia katika nchi jirani za Kenya, Uganda, Zambia na Malawi. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati; usambazaji wa gesi asilia viwandani, katika taasisi na majumbani na kuimarisha matumizi ya CNG katika magari.

**173.** ***Mheshimiwa Spika*****,** vipaumbele vingine ni kuendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking)* nchini pamoja na upatikanaji wa nishati ya mafuta vijijini kupitia uanzishwaji wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo; kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja na ufanisi katika kushughulikia upatikanaji wa bidhaa hizo; kuimarisha uwekezaji na ushiriki wa Sekta Binafsi katika shughuli za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia pamoja na uzalishaji na usambazaji wa umeme na kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma, tija na ufanisi katika uendeshaji wa Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya TANESCO, TPDC, EWURA, PURA na PBPA pamoja na Kampuni Tanzu. Wizara pia itaendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia pamoja na rasilimali watu ya Wizara ya Taasisi zake na upatikanaji wa vitendea kazi muhimu.

**174. *Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/25 pamoja na mambo mengine, umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) 2021/22 – 2025/26, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Maagizo ya Viongozi wa Kitaifa katika Sekta ya Nishati, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26). Miongozo mingine iliyozingatiwa ni Sera, Mikakati na Programu mbalimbali za Kisekta na Kitaifa pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) ya mwaka 2030 kuhusu masuala ya nishati.

## C.1 SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

### C.1.1 MIRADI YA KUZALISHA UMEME

**175. *Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza awali, moja ya kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha nchi yetu inakuwa na umeme wa kutosha kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadaye kutokana na kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii. Ili kutimiza azma hiyo Wizara imepanga kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme kama ifuatavyo:

**a)Miradi ya Kuzalisha Umeme Iliyopo Katika Hatua za Utekelezaji**

**(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115**

**176. *Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2024/25 ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la mitambo (*power house*) na ufungaji wa mitambo saba (7) ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Jumla ya **Shilingi bilioni 620** fedha za ndani zimetengwa ili kukamilisha mradi huu.

### (ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilometa 19.2 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi kwenda Gongolamboto hadi Mbagala Jijini Dar es Salaam na kufunga transfoma maeneo ya Gongolamboto na Mbagala, ikiwemo kukamilisha kazi za mitambo ya uzalishaji zilizobaki kwa uangalizi.

### (iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na uangalizi wa njia ya kusafirisha umeme kwa kipindi cha matazamio *(defect liability period)* hadi Aprili 2025, pamoja na kufanya malipo ya mwisho (retention money). Jumla ya **Shilingi Bilioni 4** fedha za ndani zimetengwa**.**

### (iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 49.5 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi, mkoani Kigoma kwa gharama ya **Dola za Marekani Milioni 144.14** (sawa na **Shilingi bilioni 364.67**) na unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB). Serikali inaendelea na ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme pamoja na njia ya kusafirisha na kusambaza umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.1** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

### (v) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua Shinyanga – MW 150

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itakamilisha ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua wa MW 150. Ujenzi unaendelea na unatarajiwa kamilika Januari, 2025.

**(vi) Ukarabati wa Mitambo katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale**

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itakamilisha ukarabati wa miundombinu ya kuzalisha umeme katika Kituo cha Hale ili kiwe na uwezo wa kuzalisha MW 21. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.3** fedha za ndani zimetengwa kwa kazi hiyo.

**(vii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87.8**

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kujenga Bwawa la kuzalisha umeme MW 87.8 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera, mkoani Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 38.7. Kazi zilizopangwa ni kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi, kupata Mkandarasi Mjenzi na kuanza utekelezaji wa mradi.

**b)Miradi ya Kuzalisha Umeme Iliyopo katika Hatua za Maandalizi**

**(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji ya mto Kikonge–MW 321**

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inalenga kujenga kituo cha kuzalisha umeme wa MW 321 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhuhu mkoani Ruvuma na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 96 kutoka Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Kazi zitakazofanyika ni kuendelea na tathmini ya Athari ya Mazingira, uwekaji wa mipaka katika eneo la uzalishaji wa umeme, usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni za mradi (bwawa la kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme). Jumla ya **Shilingi milioni 500** fedha za ndani zimetengwa**.**

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 358 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji na njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kiloviti 400 yenye urefu wa kilometa 170 kutoka Ruhudji mkoani Njombe hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa. Gharama za ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani millioni 867.41** na njia ya kusafirisha umeme **Dola za Marekani millioni 100.9**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi, ujenzi wa miundombinu wezeshi ya barabara na kuendelea na taratibu za kupata ufadhili wa mradi. Kiasi cha **Shilingi bilioni 37** fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222**

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 222 kwa kutumia maji ya Mto Rumakali mkoani Njombe na njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 65 kutoka kwenye mitambo hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya. Gharama za mradi huu kwa pamoja zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 612.78** kwa upande wa mitambo ya kufua umeme. Gharama za njia ya kusafirisha umeme ni **Dola za Marekani milioni 21.72**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi, ujenzi wa miundombinu wezeshi na kuendelea na taratibu za kupata ufadhili wa mradi. Kiasi cha **Shilingi bilioni 2** fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara (MW 300)**

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga ujenzi wa mitambo ya kufua umeme wa MW 300 kwa kutumia gesi asilia mkoani Mtwara pamoja na ujenzi wa njia za kusaifirisha umeme ya Kilovoti 400 kutoka Mtwara hadi Somangafungu na vituo vya kupoza umeme ili

kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini ikiwemo katika mikoa ya Mtwara na Lindi. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la ujenzi wa kituo cha kufua umeme pamoja ya njia ya kusafirisha umeme na kutafuta fedha za ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.55** fedha za ndani zimetengwa kwa kazi hiyo.

### (v) Mradi wa Kinyerezi III wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia MW 600

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuzalisha umeme wa MW 600 katika eneo la Kinyerezi III. Kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha/ufadhili na kuanza taratibu za ununuzi. Jumla ya **Shilingi milioni 200** fedha za ndani zimetengwa kwa kazi hiyo.

### (vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Upepo MW 100 Kititimo Mkoani Singida

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme MW 100 kwa kutumia upepo pamoja na njia ya kusafirisha umeme ya kilometa 8 ya msongo wa kilovoti 220 na kituo cha kupoza umeme. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 153**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na upembuzi yakinifu, kufanya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi pamoja na kutafuta fedha/ufadhili na kuanza taratibu za ununuzi. Jumla ya **Shilingi bilioni 3** fedha za ndani zimetengwa kwa kazi hiyo.

### (vii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Jua MW 100 Wilaya ya Manyoni

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa MW 100 kwa kutumia jua pamoja na kituo cha kupoza umeme Wilayani Manyoni. Gharama za mradi huu kwa pamoja zinakadiriwa **kuwa Dola za Marekani milioni 120**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na upembuzi yakinifu, kufanya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi na kulipa fidia. Serikali

inaendelea kutafuta fedha/ufadhili na kuanza taratibu za manunuzi. Jumla ya **Shilingi milioni 400** zimetengwa kwa kazi hiyo.

**(viii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Jua MW 60 Zuzu Dodoma**

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa MW 60 kwa kutumia jua Mkoani Dodoma. Gharama za mradi huu kwa pamoja zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 77.66**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na upembuzi yakinifu na kuanza utekelezaji. Serikali inaendelea kutafuta fedha/ufadhili na kuanza taratibu za ununuzi. Jumla ya **Shilingi milioni 25** fedha za ndani zimetengwa kwa kazi hiyo.

## C.1.2 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** umeme ukishazalishwa, hauna budi kusafirishwa ili kuweza kuwafikia walaji, hivyo upatikanaji wa umeme wa uhakika ni pamoja na kuwa na miundombinu madhubuti ya usafirishaji na usambazaji wa umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme. Kutokana na changamoto ya muda mrefu ya miundombinu chakavu na isiyotosheleza ya kusafirisha na kusambaza umeme, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya usafirishaji na usambazaji wa umeme katika mwaka 2024/25 kama ifuatavyo:

**a) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua za Utekelezaji**

**(i) Mradi wa Kusafirisha Umeme kutoka Julius Nyerere Hydro Power Plant hadi Chalinze – Kilovoti 400 na Kituo cha Kupoza Umeme, Chalinze**

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kilovoti 400 kutoka JNHPP hadi Chalinze na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze Kilovoti 400/220/132. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kumalizia kazi zilizobaki katika kituo cha kupoza umeme ikiwemo majengo, barabara, njia ya kusafirisha

umeme na marekebisho mbalimbali. **Shilingi bilioni 2** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

**(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Dodoma**

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma yenye urefu wa kilometa 345 na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Dodoma. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 245** fedha za ndani zimetengwa kwa kazi hiyo.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze - Kinyerezi - Mkuranga**

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** awamu ya kwanza ya mradi huu inahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze, Kinyerezi hadi Mkuranga na vituo vya kupoza umeme vya Chalinze, Kinyerezi, Mkuranga na Morogoro. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 7** fedha za ndani zimetengwa kwa kazi hizo.

**(iv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na Msongo wa Kilovoti 220 Segera – Tanga**

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na Msongo wa Kilovoti 220 Segera – Tanga, na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Segera na Tanga. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya fidia, kuanza ununuzi wa Wakandarasi na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.21** zitatumika kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi.

**(v) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Chalinze – Bagamoyo hadi Ununio Dar es salaam**

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 kutoka Chalinze – Bagamoyo hadi Ununio na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Bagamoyo na Ununio. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya fidia, kuanza manunuzi ya Wakandarasi na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha na vituo vya kupoza umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.3** fedha za ndani zimetengwa kwa kazi hiyo.

**(vi) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli Shinyanga Kilovoti 400/220/33**

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha msongo wa Kilovoti 400/220/33 Ibadakuli - Shinyanga. Gharama ya mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 50**. Serikali itaendelea kutekeleza mradi huu ambapo kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na ununuzi wa vifaa na nyenzo zote zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 37.5** fedha za ndani zimetengwa.

**(vii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilometa 620 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma na Sumbawanga. Aidha, mradi huu unalenga pia kuunganisha Gridi ya Taifa na Nchi za Kusini mwa Afrika *(Southern African Power Pool – SAPP)*. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme ikiwemo kukamilisha ulipaji wa fidia. Jumla ya **Shilingi bilioni 51** fedha za nje zimetengwa kwa kazi hizo.

**(viii) Mradi wa Kuboresha Utendaji Kazi wa TANESCO (*Corporate Management System – CMS*)**

**199. *Mhesimiwa Spika***, mradi huu unalenga kuboresha hali ya utendaji kazi wa TANESCO kwa kuanzisha mifumo itakayowezesha kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. Mradi huu ni sehemu ya Mradi wa Tanzania – Zambia *Interconnector Transmission Project* (TAZA). Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 34.8** sawa na **Shilingi bilioni 81.61**. Kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kumalizia kazi za ufungaji wa vifaa vya miundombinu vya mradi (*data center infrastructure*) na kufanyiwa majaribio utendaji wake. Aidha, mafunzo kwa wafanyakazi wote yataendelea kutolewa. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.9** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizopangwa.

**(ix) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma**

**200. *Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kiloviti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilometa 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na usambazaji umeme katika vijiji 18 vilivyopo katika eneo la mradi. Utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme umefikia asilimia 94.98. Kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na Kidahwe na miundombinu ya usambazaji umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi.

**(x) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Project)* – Gridi Imara**

**201. *Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu utekelezaji wa awamu ya kwanza ya miradi 27 ya uimarishaji wa miundombinu ya umeme katika mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme za msongo wa kilovoti 220 na 132 na kuongeza uwezo wa nyaya za kusafirisha umeme (*re-conductoring*), ujenzi wa njia za kusambaza umeme za msongo wa kilovoti 33, ujenzi wa vituo vya

kupoza umeme na kuongeza uwezo wa baadhi ya vituo na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika maeneo ya usambazaji (*switching station*). Kazi zitakazofanyika ni kuendelea kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi, ujenzi wa njia za kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme. Mradi unatarajiwa kukamilika Desemba 2025. Jumla ya **Shilingi bilioni 200** fedha za ndani zimetengwa.

**(xi) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa *(Grid Rehabilitation and Upgrading)-TTGRUP***

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo vya kupoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini na unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi zitakazofanyika ni ukamilishaji wa usanifu, uagizaji wa vifaa na kukamilisha mradi.

**(xii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka**

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka yenye urefu wa kilometa 166.17. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 105.4** sawa na **Shilingi bilioni 263.5**. Kazi zitakazofanyika ni kulipa fidia, kuanza kazi za usanifu, utafiti wa udongo, uagizaji wa vifaa na kuanza kazi za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme vya Benaco na Kyaka. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.4** fedha za nje na **Shilingi bilion 6.2** fedha za ndani zimetengwa**.**

**(xiii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Makutopora hadi Tabora kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot 3)**

**204.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 347 kutoka Makutopora hadi Tabora kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa ni **Dola za Marekani milioni**

**90.65** sawa na **Shilingi bilioni 212.58**. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ukamilishaji wa upembuzi yakinifu ikiwemo tathmini ya mazingira, kufanya uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi, kulipa fidia na kuanza taratibu za kupata Wakandarasi. Jumla ya **Shilingi bilioni 15** zimetengwa kupitia Fungu la SGR.

**(xiv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Tabora hadi Isaka kwa ajili Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot 4)**

**205.** ***Mhesimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu unaokadiriwa kuwa kilometa 195 kutoka Tabora hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Gharama za mradi huu inakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 56**.1 sawa na **Shilingi bilioni 131.7**. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ukamilishaji wa upembuzi yakinifu ikiwemo tathmini ya mazingira, kufanya uthamini wa mali za wananchi wataopisha mradi, kulipa fidia, na kuanza taratibu za kupata Wakandarasi. Jumla ya **Shilingi bilioni 10** zimetengwa kupitia Fungu la SGR.

**(xv) Mradi wa Njia ya Kusafirishi Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot V)**

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 230 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Kazi zitakazotekelezwa ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kuendelea na malipo ya fidia. Jumla ya **Shilingi Bilioni 14** zimetengwa kupitia Fungu la SGR kwa ajili ya malipo ya fidia na **Shilingi bilioni 45** za utekelezaji wa mradi.

## b) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua za Maandalizi

### (i) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Sumbawanga hadi Kigoma Kupitia Mpanda (Km 480) na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi pamoja kuweka mipaka ya mkuza wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Sumbawanga kupitia Mpanda hadi Kigoma, na kutafuta fedha za kutekeleza mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 600** fedha za ndani zimetengwa kutekeleza kazi hizo.

### (ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Segera – Same – Lemugur (Kisongo) Arusha

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Segera – Same – Lemugur (Kisongo) Arusha na kituo cha kupoza umeme kilovoti 220/132/33 cha Mwanza. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu, Athari za Mazingira na Jamii (ESIA), usanifu wa mradi, kufanya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi, kuanza kulipa fidia na kuendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 9** fedha za ndani zimetengwa kutekeleza kazi hizo.

### (iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme *(Submarine Cable)* Msongo wa Kilovoti 220 Kutoka Tanzania Bara (Ununio) hadi Zanzibar (Unguja)

**209.** ***Mhesimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mshauri Mwelekezi itakamilisha Upembuzi Yakinifu, Athari za Mazingira na Jamii (ESIA) na usanifu wa mradi**.** Aidha, Serikali itaendelea kutafuta fedha za kutekeleza mradi huu.

**(iv) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Manyoni (Manyoni Substation - MVA 60)**

**210.** ***Mhesimiwa Spika,*** Serikali itakamilisha kazi ya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi, na kulipa fidia. Aidha, itaendelea na taratibu za kutafuta fedha kiasi cha **Dola za Marekani milioni 16.36** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi pamoja na kutafuta Mkandarasi Mjenzi. Jumla ya **Shilingi milion 500** fedha za ndani zimetengwa kutekeleza kazi hizo.

**(v) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Masaka - Ibadakuli)-UTIP**

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Masaka - Ibadakuli) yenye urefu wa kilometa 617 na kituo cha kupoza umeme Kilovoti 220/33 cha Kyaka. Serikali itakamilisha kazi ya kufanya uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi na kuanza kulipa fidia na pia itaendelea na taratibu za kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi kiasi cha **Dola za Marekani milioni 383.9.** Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji.

**(vi) Miradi ya Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Kuunga Gridi ya Taifa na Nchi za Jirani kwa Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Tanzania Hadi Malawi (TAMA); Kilovoti 400 Kutoka Tanzania Hadi Msumbiji (MOTA) na Kilovoti 400 Kutoka Tanzania hadi DRC**

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi hii inahusu ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kwa ajili ya kuunga Gridi ya Taifa na nchi za jirani kwa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Malawi (TAMA); Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Msumbiji (MOTA) na Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi DRC. Kazi zitakazofanyika ni kufanya uthamini wa mali na Upembuzi Yakinifu. Serikali itaendelea kutafuta fedha za kutekeleza kazi hizo. Jumla ya **Shilingi milioni 800** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji.

**(vii) Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme Msongo wa Kilovoti 220 katika Jiji la Dodoma, Mbeya, Arusha, Mwanza**

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo kuu la mradi huu ni kuandaa Mpango Kabambe wa Usambazaji umeme utakaoiongoza TANESCO kuendelea kutekeleza miradi ya usambazaji umeme ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya umeme na kupunguza upotevu wa umeme katika njia za usambazaji katika Majiji hayo. Aidha, mpango huu unalenga kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika *(reliability)*. Vilevile, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia za mzunguko *(ring circuirts)* za kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 220 na ujenzi wa vituo vipya vya kupoza umeme pamoja na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vilivyopo. Kwa kuwa utekelezaji wa miradi hii inahitaji fedha nyingi, maandalizi ya utekelezaji yameanza na Majiji manne ambayo ni Arusha, Mwanza, Dodoma na Mbeya. Kazi zitakazofanyika ni kuendelea na shughuli ya upembuzi yakinifu.

**(viii) Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma**

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekusudia kulibadilisha jiji la Dodoma kimazingira kwa kuhakikisha miundombinu ya umeme haiwi sehemu ya vitu vinavyolifanya jiji hilo kutokuwa na muonekano mzuri. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeanza maandalizi ya mradi wa kubadilisha miundombinu ya usambazaji umeme kwa kutumia nguzo na kuelekea kwenye miundombinu ya usambazaji inayopita chini ya ardhi. Aidha, mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya usambazaji katika jiji la Dodoma kwa kubadilisha njia za kusambazia umeme pamoja na transfoma zake. Vilevile, katika utekelezaji wa mradi huu, kutakuwa na upanuzi wa vituo vidogo vilivyopo katikati ya jiji ili kuviongezea uwezo. Hatua hii itawezesha kuendelea kusambaza umeme wenye kukidhi mahitaji kwa wateja wapya wanaoongezeka katikati ya jiji. Hata hivyo mradi huu upo katika hatua za awali na tayari Exim Bank ya Korea imeonyesha nia ya kuufadhili na kufanya upembuzi yakinifu. Kazi zinazotarajiwa kufanyika katika mwaka 2024/25 ni upembuzi yakinifu pamoja na kuandaa usanifu wa awali wa mradi. Kiasi cha **Shilingi milioni 200** za ndani zimetengwa.

### (ix) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme katika Kila Wilaya Nchini

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Gridi ya Taifa katika Wilaya zote nchini. Mradi utatekelezwa chini ya mradi wa Gridi imara katika awamu tano (5) ambapo katika kila awamu vitajengwa vituo vya kupoza umeme kumi na tano (15). Utekelezaji wa mradi unalenga kuboresha miundombinu ya usambazaji na kupunguza upotevu wa umeme unaotokana na umbali mrefu wa njia za usambazaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Shilingi trilioni 4.20.**

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Serikali kupitia TANESCO itaanza utekelezaji wa mradi huu kwa kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi, Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii, tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi, na kuanza kutafuta fedha za ujenzi wa mradi. Serikali imetenga **Shilingi bilioni 5.4** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. *Kiambatisho Na.11* ni mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa katika kila Wilaya kwa kila awamu.

## C.1.3 MIRADI MINGINE ITAKAYOTEKELEZWA YA MATENGENEZO YA MITAMBO

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** TANESCO kupitia mapato yake ya ndani itafanya matengenezo kinga katika vituo vya kuzalisha umeme, kufanya matengenezo makubwa na madogo katika miundombinu ya kusafirisha, kusambaza na vituo vya kupoza umeme. Aidha, Shirika litaendelea kutekeleza miradi inayolenga kuongeza uwezo wa miundombinu ya kusafirisha umeme, kuboresha mifumo ya uendeshaji Gridi, kuweka mifumo ya kisasa ya mawasiliano katika vituo vya kupoza umeme, kujenga vituo vidogo vya kuendesha Gridi *(unmanned substations)* na kuweka mfumo wa "*Advance Metering Infrastructure-AMI*" wa kufunga Mita Janja (*Smart Meter*).

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** TANESCO pia itatekeleza miradi ya kupeleka umeme katika maeneo mbalimbali pamoja na kufanya maboresho

kwenye miundombinu ya usambazaji ili kuondoa adha za kuwa na umeme mdogo kwa wananchi na kuunganisha wateja wapya. Jumla ya **Shilingi bilioni 959.792** fedha za ndani zimetengwa kutumika kwa ajili ya kazi hizo ili kuimarisha uwezo wa miundombinu ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme iliyopo.

## C.1.4 UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO (TCPM NA ETDCO)

### a) Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO)

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya ETDCO, imepanga kukamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Urambo na kutoka Urambo hadi Kidahwe Mkoani Kigoma. Aidha, ETDCO itakamilisha utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini katika Mikoa ya Geita na Kigoma inayosimamiwa na REA. Vilevile, ETDCO imepanga kujenga mradi wa njia ya kusafirisha Umeme Kilovoti 220 Masasi – Mahumbika yenye urefu wa kilometa 128 katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

### b) Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania (TCPM)

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya TCPM inatarajia kuzindua kiwanda chake cha kwanza cha kuzalisha nguzo za zege Mkoani Tabora. Kampuni itaendelea kuingia ushirikiano *(joint venture)* na Wawekezaji binafsi ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa nguzo za zege na kurahisisha zoezi la usafirishaji wa nguzo hizo katika maeneo mbalimbali nchini.

### c) Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi (TGDC)

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Serikali kupitia TGDC itatekeleza yafuatayo:

i. Itakamilisha uchorongaji wa visima vitatu (3) vya uhakiki *(exploratory wells)* ili kuhakiki hifadhi, kiwango na ubora wa

rasilimali ya jotoardhi katika mradi wa Ngozi (Mbeya) wenye uwezo wa kuzalisha MW 30 katika awamu ya kwanza pamoja na kuanza ujenzi wa mtambo mdogo wa kuzalisha umeme *(wellhead generator)* wa MW 5. Jumla ya **Shilingi bilion 2.9** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

ii. Itaanza utekelezaji wa programu ya uchorongaji wa visima vinne (4) vya uhakiki, kutekeleza miradi ya matumizi mengineyo pamoja na maandalizi ya upatikanaji wa mtambo wa kuzalisha umeme katika mradi la Kiejo Mbaka (Mbeya) wenye uwezo wa kuzalisha MW 60. Jumla ya **Shilingi bilioni 14.56** zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa shughuli hizo;

iii. Itakamilisha taratibu za umiliki wa ardhi na maandalizi ya uchorongaji wa visima vinne (4) vya uhakiki katika mradi wa Songwe (Songwe) wa MW 5. Jumla ya **Shilingi milioni 560** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo;

iv. Kufanya maandalizi ya programu ya uchorongaji wa visima vitatu (3) vya uhakiki pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa matumizi mengineyo katika eneo la mradi wa Luhoi (Pwani) MW 5. Jumla ya **Shilingi milioni 350** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo;

v. Kukamilisha utafiti wa kina wa kijiosayansi wa juu ya ardhi *(detailed surface exploration)* pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufanya tafiti katika eneo la mradi la Natron MW 60 (Arusha) ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 1.28** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi husika;

vi. Kufanya utafiti wa kina wa kijiosayansi wa juu ya ardhi (*detailed surface exploration*) katika eneo la mradi wa Meru (Arusha) wa MW 60 pamoja na kuajiri Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya kazi ya utafiti huo. Jumla ya **Shilingi milioni 700** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi husika; na

vii. Kuratibu Kongamano la 10 la Jotoardhi *(African Rift Geothermal Conference-ARGeo C-10)* litakalofanyika Novemba, 2024 Jijini Dar es Salaam.

### C.1.5 USHIRIKISHWAJI WA SEKTA BINAFSI KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UMEME

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO itaendelea na taratibu za kutekeleza miradi ya kufua umeme inayotarajiwa kutekelezwa na wawekezaji binafsi, ikiwemo miradi ya umeme jadidifu na vyanzo vingine. Wawekezaji binafsi wanaendelea kukaribishwa kujitokeza katika kutekeleza miradi ya upepo, jua, makaa ya mawe, maji na gesi katika maeneo mbalimbali nchini. Kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2024/25 ni uchambuzi, uthamini na ulipaji wa fidia katika maeneo ya miradi, kutangaza zabuni na kuingia mikataba ya makubaliano na wawekezaji binafsi pamoja na kufanya upembuzi yakinifu.

**223.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya usafirishaji wa umeme, Serikali kupitia TANESCO itaendelea kuwashirikisha wawekezaji binafsi katika utekelezaji wa miradi hii, hususan katika maeneo ya viwanda na migodi. Kazi zitakazofanyika ni uchambuzi wa maeneo ya miradi na kuingia makubaliano na wawekezaji binafsi kwa utekelezaji wa miradi hiyo.

### C.1.6 MIRADI YA NISHATI VIJIJINI

**224.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2024/25, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini itaendelea kuchukua hatua za kupeleka nishati vijijini ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii katika maeneo hayo. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali kupia Wakala wa Nishati Vijijini itatekeleza miradi ifuatayo:

#### a) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji 20,000

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vitongoji 20,000 ambavyo bado havijafikiwa na miundombinu ya umeme. Jumla ya **Shilingi**

**bilioni 350** fedha za ndani zimetengwa. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuandaa kabrasha la zabuni, ununuzi wa wakandarasi, kufanya usanifu wa kina wa mradi na kuanza ujenzi wa miundombinu ya mradi.

**b) Mradi wa Kupeleka Umeme Katika Vitongoji katika Mkoa wa Songwe na Kigoma**

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vitongoji 677 vya Mkoa wa Kigoma na Songwe ili kuwezesha ujenzi wa njia za umeme Msongo wa Kati zenye urefu wa kilometa 726.24; ujenzi wa njia za umeme wa Msongo Mdogo zenye urefu wa kilometa 1,308; ufungaji wa transfoma 653 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 14,352. Kazi zitakazofanyika ni kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme Msongo Mdogo, kufunga transfoma na kuunganisha wateja. Jumla ya **Shilingi bilioni 26.60** kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kupitia dirisha la *Extended Credit Facility* zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi.

**c) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji 3,060**

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vitongoji 3,060 ikiwa ni vitongoji 15 kila Jimbo, ujenzi wa njia za umeme Msongo wa Kati zenye urefu wa kilometa 258; ujenzi wa njia za umeme wa Msongo Mdogo zenye urefu wa kilometa 6,118; ufungaji wa transfoma 3,060 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 100,947. Kazi zitakazofanyika ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya mradi, kufunga transfoma na kuunganisha wateja.

**d) Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili B (*Densification IIB*)**

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kupeleka umeme kwenye vitongoji 1,686 katika mikoa 9 ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe na Songwe ambapo kazi za ujenzi zinahusisha ujenzi wa njia za msongo mdogo zenye urefu wa kilometa 3,860, ufungaji wa transfoma 1,272 na kuunganisha wateja wa awali 95,334. Katika Mwaka 2024/25, Wakala wa Nishati Vijijini

utaendelea kukamilisha kazi za ujenzi wa miundombinu ya mradi, kufunga transfoma na kuunganisha wateja. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.40** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**e) Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili C (*Densification IIC*)**

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umelenga kufikisha huduma za umeme kwenye vitongoji 1,880 katika mikoa 7 ya Manyara, Iringa, Rukwa, Mtwara, Ruvuma, Simiyu na Mara ili kujenga kilometa 5,640 za Msongo Mdogo, kufunga transfoma 1,880 na kuunganisha wateja wa awali 94,000. Katika Mwaka 2024/25, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini itakamilisha kazi za ujenzi wa njia za umeme Msongo Mdogo, kufunga transfoma na kuunganisha wateja. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.41** fedha kutoka Benki ya Dunia zimetengwa ili kukamilisha kazi hizo.

**f) Mradi wa Kupeleka Umeme Katika Maeneo ya Vijijini-Miji (*Peri Urban*)**

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kutekelezwa katika mikoa 8 ya Geita, Kigoma, Kagera, Mbeya, Mtwara, Singida, Tabora na Tanga ambapo jumla ya maeneo 416 yatafikishiwa huduma ya umeme kupitia ujenzi wa njia za umeme wa Msongo wa Kati zenye urefu wa kilometa 379; ujenzi wa njia za umeme wa Msongo Mdogo zenye urefu wa kilometa 753; ufungwaji wa transfoma 314 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 16,369 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 76.9** kutoka Serikali ya Tanzania. Katika Mwaka 2024/25, kazi zilizopangwa kufanyika ni ujenzi wa njia za umeme Msongo wa Kati na Mdogo, kufunga transfoma na kuunganisha wateja ambapo **Shilingi bilioni 2** fedha za ndani zimetengwa.

**g) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Migodi Midogo, Maeneo ya Kilimo na Viwanda**

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu kupeleka umeme katika maeneo 581 ya wachimbaji wadogo wa madini, maeneo ya kilimo na viwanda Tanzania Bara kupitia ujenzi wa njia za Msongo wa Kati zenye urefu wa kilometa 1,370; ujenzi wa njia za umeme wa Msongo Mdogo zenye urefu wa kilometa 1,097; ufungwaji wa transfoma 517 pamoja

na kuunganisha wateja wa awali 17,119. Katika Mwaka 2024/25, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini itaendelea kukamilisha kazi za kupeleka umeme katika jumla ya maeneo ya migodi, kilimo na viwanda 581 ambapo **Shilingi bilioni 5.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi hizo.

**h) Mradi wa Kupeleka Umeme Katika Minara ya Mawasiliano ya Simu**

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu kupeleka umeme katika minara 754 ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini. Katika Mwaka 2024/25, Wakala wa Nishati Vijijini utaendelea kushirikiana na *Universal Communications Services Access Fund (UCSAF)* ili kupelekea umeme katika minara ya mawasiliano kwenye maeneno ya vijijini ambapo **Shilingi bilioni 12.00** fedha za ndani zimetengwa .

**i) Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme Jua kwenye Makazi Yaliyopo Visiwani na Yaliyopo Mbali na Gridi ya Taifa**

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu kufunga na kusambaza mifumo itakayozalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika makazi yaliyo vijijini ambayo hayatafikiwa na gridi ya Taifa kwa kufunga mifumo ipatayo 7,000. Gharama za mradi ni **Shilingi bilioni 9.4**. Katika Mwaka 2024/25, kazi zitakazotekelezwa ni kutangaza mradi, kufanya tathmini ya maombi yaliyowasilishwa, kufanya *due diligence*, na kuanza kutekeleza mradi ambapo **Shilingi bilioni 3.53** fedha kutoka Benki ya Dunia zimetengwa.

**j) Mradi wa Kusambaza Majiko Banifu kwenye Kaya Zilizopo katika Maeneo ya Vijijini na Vijiji-Miji**

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusambaza majiko banifu katika maneo ya vijijini na vijiji-miji (*Peri Urban*). Mradi utasambaza majiko banifu 70,000 yaliyotengenezwa kwa teknolojia yenye ubunifu wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa pamoja na kupunguza uharibifu wa mazingira. Gharama za mradi ni **Shilingi bilioni 14.10**. Katika Mwaka 2024/25, Wakala wa Nishati Vijijini utaandaa kabrasha la mradi na kutangaza ili kuwapata wazalishaji/wasambazaji

wa majiko, kufanya tathmini ya maombi yaliyowasilishwa, kufanya *due diligence*, na kuanza kutekeleza mradi ambapo **Shilingi bilioni 4.7** kutoka Benki ya Dunia zimetengwa.

**k) Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya nishati ya kupikia katika taasisi za umma na binafsi ambazo zinahudumia zaidi ya watu 300 kwa siku. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoaja na kutoa ruzuku kwa wazalishaji wa mkaa mbadala kwa ajili ya ununuzi wa mashine zitakazotumika katika uzalishaji; kutoa ruzuku kwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili waweze kununua na kufunga mashine mbili (2) za kuzalisha mkaa bora wa kupikia kutokana na makaa ya mawe, kutoa ruzuku kwa Jeshi la Magereza kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya nishati ya kupkia katika maeneo 211 pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya tathmini ya aina za nishati safi ya kupikia zilizopo Tanzania Bara. Tathmini hii itahusisha pia kuainisha teknolojia zilizopo, nishati safi zilizopo, watoa huduma (waendelezaji au wasambazaji) wa nishati safi ya kupikia waliopo, na kupendekeza aina ya mifumo ya ufadhili ili kufikisha nishati ya kupikia katika maeneo husika.

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** mpango wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia utahusisha kutoa elimu kupitia makongamano, semina na vyombo vya habari kuhusu madhara ya nishati chafu na manufaa ya matumizi ya nishati iliyo safi katika kipikia. Jumla ya **Shilingi bilioni 24.5** ya fedha ndani zimetengwa.

**l) Mpango wa Utoaji Ruzuku kwa Waendelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu**

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango huu unahusisha kuchangia gharama za uendelezaji wa gridi ndogo (*mini grids*) kwa kutoa ruzuku ili kuzalisha umeme unaotokana na nishati jadidifu. Mpango unahusisha ujenzi wa mitambo ya kufua umeme yenye uwezo wa hadi kufikia Megawati 10 kutoka vyanzo vya maji, jua, upepo na tungamotaka. Jumla ya **Shilingi bilioni 10** fedha za ndani zimetengwa.

**m) Mradi wa Uwezeshaji Upanuzi wa Miundombinu ya Msongo Mdogo (*Distribution Network*) na Ujenzi wa *"Interconnection Line"* kwa Waendelezaji Wadogo**

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha kutoa ruzuku kwa waendelezaji wa miradi ya nishati vijijini ili waweze kujenga miundombinu ya kuunganisha umeme kutoka kwenye chanzo kwenda kwenye miundombinu ya TANESCO na kusambaza umeme katika vitongoji vinavyoendelezwa na Waendelezaji wa Miradi (*Franchaise Area under Standardized Power Purchase Agreement*). Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kuchambua maombi yatakayowasilishwa, kufanya *due diligence* na kusaini mikataba kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mradi ambapo **Shilingi bilioni 15** fedha za ndani zimetengwa.

**n) Ukuzaji na Uhamasishaji wa Ufanisi wa Matumizi Bora ya Nishati Pamoja na Matumizi ya Umeme katika Uzalishaji**

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi hii itahusisha kumpata mtoa huduma wa kukuza na kuhamasisha ufanisi wa matumizi bora ya nishati ikiwemo vifaa vinavyotumia umeme, tabia ya watumiaji kuhusu matumizi sahihi katika uzalishaji mali kwa kutumia umeme. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kumtafuta Mshauri Mwelekezi wa kuandaa Mkakati wa kuhamasisha Matumizi bora ya Umeme katika uzalishaji mali katika maeneo yaliyounganishwa na umeme vijijini. Hatua hii itawezesha kuongeza thamani katika maeneo yaliyopelekewa umeme kupitia miradi mbalimbali ya umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 1.50** fedha kutoka Benki ya Dunia zimetengwa.

**o) Tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijijini**

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA inatarajia kufanya tathmini mbalimbali ili kuhuisha na kuandaa nyaraka za kitalaamu zitakazoongoza jitihada za uendelezaji na utekelezaji wa miradi ya kusambaza nishati vijijini. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kutafuta Washauri Elekezi kwa ajili ya kuandaa upembezi yakinifu wa kuibua aina za Nishati Jadidifu katika kutekeleza miradi ya umeme vijijini; kufanya tathmini ya vijiji na vitongoji vyote visivyo na umeme na

vinavyohitaji ujazilizi katika maeneo yote ya visiwani; na Mshauri Mwelekezi wa kusimamia mradi wa ufungaji wa mifumo midogo ya umeme jua pamoja na gridi ndogo katika maeneo ya vijijini hususan visiwani. Jumla ya **Shilingi bilioni 7.5** kutoka Benki ya Dunia zimetengwa.

### C.1.6 UTEKELEZAJI WA MIKAKATI NA MIPANGO MBALIMBALI YA UENDELEZAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu nchini, Serikali kupitia Wizara ya Nishati itakamilisha kuandaa mipango na mikakati mbalimbali ili ianze kutekelezwa. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha uhuishaji wa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme *(Power System Master Plan 2020)* pamoja na kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Kupeleka Nishati Vijijini *(Rural Energy Master Plan)* ambao umejikita katika kupeleka nishati ya umeme katika vitongoji na nishati safi ya kupikia katika maeneo ya vijijini.

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kuendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programu ya Nishati Safi ya Kupikia inayoloenga Kuwawezesha Wanawake Barani Afrika Kutumia Nishati Safi ya Kupikia *(African Women Clean Cooking Support Programme – AWCCSP;* Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034) pamoja na mradi wa Matumizi Bora ya Nishati na Mkakati wa Maboresho katika Sekta Ndogo ya Umeme (*Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap – ESI-RSR)*. Pia Serikali kupitia Wizara ya Nishati itafanya tathmini ya vyanzo vyote vya nishati jadidifu vilivyopo nchini ili kutambua maeneo vilivyopo na uwezo, teknolojia inayohitajika kuviendeleza na kuandaa ramani kwa lengo la kuviendeleza.

### C.2 SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kusimamia na kuendeleza Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi kwa kuchukua hatua mbalimbali,

lengo likiwa ni kuhakikisha mchango wa sekta hii katika maendeleo ya Taifa letu unaimarika.

### C.2.1 MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

#### a) Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa za kitaalamu kuhusu kitalu hiki zimeonesha uwepo wa mashapo yenye uwezekano wa kuwa na gesi asilia. Serikali kupitia TPDC imeshampata mbia wa kimkakati (Maurel & Prom (M&P)) ambaye ameonyesha nia ya kushirikiana katika shughuli za utafutaji na uendelezaji wa kitalu hiki. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na uchorongaji wa visima vya utafiti pamoja na kukamilisha taratibu za upatikanaji wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Jumla ya **Shilingi bilioni 2**, fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizi.

#### b) Kitalu cha Eyasi – Wembere

**245.** ***Mheshimiwa Spika,*** TPDC itaendelea na shughuli za utafiti wa awali wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Eyasi – Wembere ambapo kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendelea na uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D zenye urefu wa kilometa 1,100 ili kutambua maeneo ambayo visima vya utafutaji vitachorongwa, kutafuta mbia wa kimkakati wa kushirikiana naye katika uwekezaji pamoja na kukamilisha taratibu za upatikanaji wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizi.

### C.2.3 MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA KUWA KIMIMINIKA (*LIQUEFIED NATURAL GAS – LNG*)

**246.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu Na.1, 2 na 4 vilivyopo katika kina kirefu baharini ili kuwa kimiminika na kuweza kuuzwa katika soko la dunia. Mradi huu pia utasaidia kuongeza upatikanaji, uzalishaji na usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi ya ndani ya nchi.

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatarajia kukamilisha majadiliano ya Mikataba ya mradi huu na Wawekezaji, ikiwemo Mkataba wa Nchi Hodhi (HGA) na Mkataba wa Ugawanaji Mapato (APSA); kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu na manufaa ya mradi; kushiriki katika shughuli za ufuatiliaji na tathmini za mradi; na kushiriki katika utafiti na utoaji elimu ya upatikanaji wa huduma na bidhaa za ndani ikiwemo wataalam watakaohitajika katika mradi. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kuwezesha uanzishwaji wa ofisi ya mradi na ujenzi wa shule ya msingi Likong'o mkoani. Jumla ya **Shilingi bilioni 5** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### C.2.4 MIRADI YA UENDELEZAJI, UCHAKATAJI, USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI GESI ASILIA

#### a) Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Kutoka Ntorya katika Kitalu cha Ruvuma hadi Madimba

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha kuendeleza gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la Ntorya katika kitalu cha Ruvuma. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kujenga bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka kitalu cha Ruvuma (Ntorya) hadi Madimba lenye urefu wa kilometa 34.2 litakalokuwa na uwezo wa kubeba futi za ujazo milioni 140 kwa siku. Aidha, TPDC imeshapata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya usanifu wa kina na kihandisi. Jumla ya **Shilingi bilioni 101.6** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha kazi hizo kutekelezwa.

#### b) Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya tathmini ya athari kwa mazingira na jamii, usanifu wa kihandisi pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwenye viwanda vya Mkuranga pamoja na Kongani ya Viwanda ya Kwala Mkoani Pwani; kukamilisha ujenzi wa vituo vya CNG (Kituo Mama katika eneo la

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Vituo vidogo vya Kairuki na Muhimbili) mkoani Dar es Salaam; na ununuzi wa vituo vitano (5) vya CNG vinavyohamishika *(mobile CNG stations)* vitakavyotoa huduma katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, miradi ya ujenzi wa vituo vya CNG inayotekelezwa na Sekta Binafsi itakayokamilika katika mwaka 2024/25 ni pamoja na kituo cha TAQA kitakachojengwa barabara ya Sam Nujoma; kituo cha Energo kinachoendela kujengwa katika eneo la Mikocheni mkabala na Coca Cola; kituo cha BQ Contractors kitakachojengwa Mbezi Beach karibu na Hospitali ya Masana; na vituo sita (6) vya PUMA vitakavyojengwa barabara ya Mandela, makutano ya barabara Mwenge, Mbezi Tanki Bovu, DART Mbagala, DART Ubungo na Tegeta.

**250.** ***Mheshimiwa Spika,*** TPDC pia itakamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa usambazaji wa gesi asilia chini ya ufadhili wa REA ambapo nyumba 980 zitaunganishwa katika mikoa ya Lindi na Pwani; na kuanza awamu ya pili ya mradi huo kwa kuendelea kusambaza gesi asilia maeneo ya Mkuranga, mkoani Pwani. Jumla ya **Shilingi bilioni 28.4** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya miradi hii ya usambazaji gesi katika mikoa minne.

### C.2.5 MIRADI YA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KWENDA NCHI JIRANI

#### a) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania hadi Uganda

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha nyaraka muhimu za miradi ikiwemo Kanuni za Pamoja za Ununuzi *(Joint Procurement Rules)* na Hadidu za Rejea za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 483.8** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kufanikisha shughuli hiyo.

#### b) Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Mombasa (Kenya)

**252.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na uandaaji wa nyaraka za mradi zikiwemo *Bilateral Agreements, Joint*

*Procurement Rules & Terms of Reference* (ToR) na nyaraka za zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu. Jumla ya **Shilingi milioni 502.2** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha kazi hizo kutekelezwa.

## C.2.6 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUHIFADHI MAFUTA

### a) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda hadi Tanga - Tanzania *(East African Crude Oil Pipeline – EACOP)*

**253.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mradi wa EACOP unaendelea ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kupokea shehena za mabomba, kuendelea na ujenzi wa bomba la mafuta, ujenzi wa matenki ya kuhifadhia mafuta na jeti katika eneo la Chongoleani na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo kwa maeneo yanayopitiwa na mradi na kuendelea kuchangia mtaji na kushirikiana na Wanahisa wengine kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za mkopo. Jumla ya **Shilingi bilioni 50** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kufanikisha shughuli hizo.

### b) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Dar es Salaam - Tanzania hadi Ndola – Zambia

**254.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam hadi Zambia lenye urefu wa takribani kilometa 1,710 ambalo litatumia mkuza wa bomba la kusafirisha mafuta la TAZAMA. Wamiliki wa bomba tajwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zambia. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha idhini ya nyaraka muhimu za mradi na kupata Mshauri Mwelekezi wa kufanya uchambuzi wa kina wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 415.8** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

### c) Ujenzi wa Miundombinu ya Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta Pamoja na Miundombinu ya Kuwezesha Biashara ya Mafuta

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** uanzishaji wa Hifadhi ya Taifa ya Mafuta ya Kimkakati (SPR) unatekelezwa kwa kujenga maghala ya kuhifadhi mafuta *(tank farms)* katika maeneo ya kimkakati nchini ili kurahisisha usambazaji wa mafuta. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi atakayeandaa Mpango wa Kina (*Detailed Road Map)* kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya SPR. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.4** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

### d) Ukarabati wa Tenki Namba 8

**256.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha tathmini ya athari kwa mazingira na jamii na usanifu wa tenki pamoja na kuanza kazi ya ukarabati wa tenki hilo kwa ajili ya hifadhi ya mafuta. Jumla ya **Shilingi bilioni 14.4** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

### e) Ujenzi wa Maghala Sita (6) Eneo la Kigamboni

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya ujenzi wa matenki sita (6) katika eneo la Kigamboni itafanyika kwa awamu ambapo awamu ya kwanza itaanza kwa ujenzi wa matenki matatu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 81,000. Jumla ya **Shilingi bilioni 49.8** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa maghala hayo.

## C.2.7 MRADI WA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA RASILIMALI ZA ASILI TANZANIA

**258.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa kupitia mradi huu ni pamoja na kuwezesha Duru ya Tano ya kunadi vitalu vilivyo wazi ili kuvutia uwekezaji katika utafutaji wa mafuta na gesi, kufadhili utafiti na maandalizi ya Mkakati wa Uendelezaji na Uhamasishaji wa matumizi ya gesi ya mitungi *(Liquefied Petroleum Gas – LPG)* na gesi iliyoshindiliwa (*Compressed Natural Gas – CNG)*, kununua kituo kinachotembea cha kujazia gesi kwenye magari *(Mobile CNG Station)*, kufadhili uanzishaji wa vituo vya kujenga uwezo kwa

Wananchi chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) pamoja na kukamilisha awamu ya mwisho ya programu ya kujenga uwezo kwa Wataalam wa Wizara ya Nishati, PURA, TPDC na Watumiaji wa Mfumo wa Uondoshaji Shehena Mipakani.

### C.2.8 MAJUKUMU YATAKAYOTEKELEZWA NA KAMPUNI TANZU ZA TPDC (TANOIL & GASCO)

#### a) TANOIL Investments Limited (TANOIL)

**259.** ***Mheshimiwa Spika,*** TPDC kupitia Kampuni yake tanzu ya TANOIL itaendela kushiriki katika biashara ya mafuta kama kampuni ya kununua na kuuza mafuta (*Oil Marketing Company* - OMC). Kampuni ya TANOIL imepanga kutumia **Shilingi bilioni 240.95** katika biashara hiyo na itaendelea kukamilisha ukarabati wa vituo vitatu (3) vya Musoma, Tarime (Mara) na Segera (Tanga) pamoja na kujenga kituo kipya kimoja (1) Makuyuni (Arusha) kupitia Kampuni mama (TPDC).

#### b) Gas Company (GASCO)

**260.** ***Mheshimiwa Spika,*** TPDC kupitia kampuni Tanzu ya GASCO itaendelea kuendesha miundombinu ya Taifa ya Gesi Asilia nchini. TPDC kupitia GASCO imepanga kutumia **Shilingi bilioni 76.41** kwa ajili ya kulipia gharama za uendeshaji na usimamizi wa miundombinu ya kuchakata gesi asilia iliyoko Songo Songo na Madimba, bomba la gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam na mtandao wa mabomba ya usambazaji gesi asilia iliyopo Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam.

### C.2.9 UDHIBITI WA MASUALA YA MKONDO WA JUU WA PETROLI KUPITIA PURA

**261.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA inatarajia kutekeleza Duru ya Tano (5) ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Zoezi hili lina lengo la kutangaza kwa wawekezaji vitalu vilivyo wazi vinavyopendekezwa katika eneo la bahari na nchi kavu. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na; kuandaa nyaraka za zabuni

zitakazoongoza mnada wa vitalu, kufanya maonesho ya kitaalamu kuhusu vivutio vya vitalu na kuzindua Duru ya Tano (5) ya kunadi vitalu. Zoezi la kunadi vitalu linatarajiwa kuzinduliwa mwishoni mwa mwaka 2024 baada ya kukamilika kwa maandalizi yote yanayoendelea. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** zimetengwa.

**262.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA itaendelea kusimamia shughuli za ukarabati wa visima katika vitalu vya uzalishaji wa gesi asilia pamoja na shughuli za uendelezaji katika Kitalu cha Ruvuma, kufanya mapitio ya kanuni mbalimbali, kuendelea kusimamia, kufanya ukaguzi na kuhakikisha ushiriki wa Watanzania katika Vitalu vyote vya utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia nchini pamoja na kusimamia shughuli za awali zinazoendelea katika vitalu Namba 1, 2 & 4 vitakavyohusika katika mradi wa LNG. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.77** fedha za ndani zimetengwa ili kutekeleza kazi hizi.

### C.2.10 UDHIBITI WA MASUALA YA NISHATI KUPITIA EWURA

**263.** ***Mheshimiwa Spika,*** EWURA itaendelea kusimamia udhibiti wa huduma za nishati nchini kwa kuwasimamia watoa huduma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma iliyo bora na uhakika. Pia, ili kufikisha huduma karibu na wananchi EWURA imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 1.7** kwa ajili ya kuendelea na taratibu za ujenzi wa Ofisi za Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini na Kati.

### C.2.11 KUIMARISHA UTENDAJI KAZI NA UTOAJI HUDUMA

**264.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha taasisi zilizo chini yake ili ziweze kujiendesha kwa tija na ufanisi na kutoa huduma bora kwa wananchi na wadau. Aidha, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 56 na kuwahamishia Wizarani watumishi 76 ili kukabiliana na upungufu wa watumishi uliopo. Vilevile, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 4,219.

## D. USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

**265.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ya Nishati inashirikiana na Washirika mbalimbali wa Maendeleo, Jumuiya za Kikanda, nchi wahisani na wadau wengine. Kwa niaba ya Serikali, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo, Jumuiya na nchi wahisani ambao wameendelea kushiriki katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maendeleo ya Sekta ya Nishati kwa ujumla. Napenda kutambua mchango wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); Arab Bank for Economic Development in Africa (BADEA); Mfuko wa Uendelezaji wa Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea); Jotoardhi (Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya JICA (Japan), KfW (Germany), AFD (Ufaransa); Shirika la Fedha Duniani (IMF); Sida (Sweden), NORAD (Norway); Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Mitaji ya Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCDF), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) na USAID (Marekani); OPEC Fund for International Development; Abu - Dhabi Fund for Development (ADFD); na Saudi Fund for Developmnet (SFD).

**266.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii pia kutoa shukrani kwa Serikali za Afrika Kusini, Algeria, Burundi, Canada, China, DRC Congo, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Iceland, India, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, Norway, Rwanda, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Zambia, na nchi nyingine kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Nazishukuru pia Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu Sekta ya Nishati.

## E. HITIMISHO

**267.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa nishati katika kuchochea na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa letu, katika mwaka 2024/25 Wizara ya Nishati itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kusimamia, kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Nishati, kwa lengo la kuhakikisha sekta hii inachangia

ipasavyo katika maendeleo ya Taifa letu na watu wake kama inavyotarajiwa.

***268. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia mijini na vijijini ili kulinda afya za wananchi na mazingira. Aidha, Wizara itaendelea kuipatia suluhu ya kudumu changamoto ya upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini, kuimarisha usambazaji wa nishati hiyo pamoja na kuimarisha uzalishaji wa gesi asilia unaoendana na mahitaji, kwa kuzingatia kiwango cha ugunduzi wa nishati hiyo hadi sasa nchini na hatua za utafutaji zinazoendelea kuchukuliwa. Wizara pia itaendelea kuelekeza nguvu katika kuimarisha utoaji wa huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi zake.

***269. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane Themanini na Tatu, Milioni Mia Saba Hamsini na Tisa, Mia Nne Hamsini na Tano Elfu** (**Shilingi 1,883,759,455,000)** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

**(i)** **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Saba Tisini na Nne, Milioni Mia Nane Sitini na Sita, Mia Nane Thelathini na Mbili Elfu (Shilingi 1,794,866,832,000)** sawa na asilimia **95.28** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Tano Thelathini na Sita na Milioni Ishirini, Mia Mbili Sabini na Nne Elfu (Shilingi 1,536,020,274,000)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Mia Mbili Hamsini na Nane, Milioni Mia Nane Arobaini na Sita, Mia Tano Hamsini na Nane Elfu (Shilingi 258,846,558,000)** ni fedha za nje; na

**(ii)** **Shilingi Bilioni Themanini na Nane, Milioni Mia Nane Tisini na Mbili, Mia Sita Ishirini na Tatu Elfu (Shilingi 88,892,623,000)** sawa na **asilimia 4.72** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Sitini na Tisa, Milioni Mia Tano Ishirini na Nne, Mia Mbili na Moja Elfu (Shilingi 69,524,201,000)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Tatu Sitini na Nane, Mia Nne Ishirini na Mbili Elfu (Shilingi**

**19,368,422,000)** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**270.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.nishati.go.tz. Vilevile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo aje awasilishe hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea ninaomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 na maoni ya Kamati kuhusu bajeti ya mwaka 2024/2025 ni kutokana na majukumu ya msingi Kamati iliyopewa kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na imegawanyika katika sehemu tano, kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, msingi na muundo wa taarifa hii;

(ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na namna Wizara ilivyotekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati;

(iii) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Sehemu ya Nne, inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

(v) Sehemu ya Tano, ni hitimisho na shukrani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na uzingatiaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, inaweka masharti kwa Kamati za Kisekta kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inayosimamia na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa hayo, kuanzia tarehe 20 hadi 28 Machi, 2024 Kamati ilitekeleza wajibu huo kwa kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho dhidi ya

Mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati ilijielekeza kwenye maeneo yafuatayo: -

(i) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2023/2024;

(ii) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iv) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2024; na

(v) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa minne ambayo ni Dodoma, Arusha, Dar es Salaam na Pwani na kukagua miradi minne inayotekelezwa chini ya Wizara ya Nishati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mradi wa kwanza ni ujenzi wa jengo la Wizara Mtumba, Dodoma. Mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa sita kwa ajili ya Ofisi ya Wizara ya Nishati na unatekelezwa katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 25.2 na kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1.55 ni kwa ajili ya Wakandarasi washauri na shilingi bilioni 23.7 ni kwa ajili ya Mkandarasi wa Ujenzi *(NHC)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 12 Machi, 2024, utekelezaji wake ulikuwa umefikia 75.09% na kiasi cha shilingi bilioni 16.5 sawa na 65.33% ya gharama za mradi kilikuwa

kimeshalipwa kwa Wakandarasi wanaotekeleza na kusimamia mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu na kuangalia utekelezaji wake ilibaini kasi ndogo ya utekelezaji wake. Hivyo, inashauri Wizara iimarishe usimamizi ili kuhakikisha mradi unakamilika ndani ya muda wa mkataba na jengo hilo kutoa huduma inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili ni ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Lemugur, Kisongo - Arusha. Ujenzi wa Kituo hiki unahusu upanuzi wa Kituo cha Kupoza Umeme *(substation)* cha Lemugur, Arusha na unagharimu Dola za Kimarekani milioni 36. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 utekelezaji ulikuwa umefikia 99.27% na sasa mradi upo katika hatua ya majaribio.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mafanikio ya awali kutokana na ujenzi wa kituo hiki ni pamoja na kuiwezesha *TANESCO* kuanza mradi wa ujenzi wa njia nane za kusambaza umeme msongo wa Kv 33, ili kupunguza mzigo Kituo cha Kupoza Umeme cha Njiro, kutokana na ongezeko la wateja katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

Mheshimiwa Spika, mradi wa tatu ni ujenzi wa miundombinu ya Vituo vya Kujaza Gesi Asilia kwenye Magari *(CNG)*, Dar es Salaam. Kamati ilitembelea na kukagua vituo vya *CNG, mother stations* viwili vya kujaza gesi asilia kwenye magari ambavyo viko Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Kipawa na Ubungo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kituo cha *TAQA-Dalbit* kilichopo Uwanja wa Ndege wa Julius Kambarage Nyerere, Kipawa, Dar es Salaam, kituo hiki kina pampu sita zenye uwezo wa kuhudumia magari 1,000 kwa siku. Kituo hiki kinakabiliwa na changamoto ya kutegemea nishati ya umeme pekee kujiendesha na hivyo kinashindwa kuhudumia wateja umeme unapokatika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali itoe kipaumbele katika upatikanaji wa umeme kwenye maeneo yanayotoa huduma ya kujaza gesi kwenye magari ili yatoe huduma muda wote.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha *Pan-African Energy Tanzania Limited* na *TPDC* kilichopo Ubungo, Dar es Salaam kinachomilikiwa kwa ubia kati ya *TPDC* na *PAET* kina pampu mbili zenye kuhudumia magari 700 kwa siku. Kamati ilibaini msongamano mkubwa wa magari yanayohitaji huduma hiyo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kushughulikia tatizo hili ikiwemo kujenga vituo vingine ili kuboresha, kueneza huduma na kushawishi watu kuanza kutumia gesi asilia kwenye magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Umeme Vijijini *(REA)* Halmashauri ya Chalinze - Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, kwa maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa mradi huu ni kama ilivyooneshwa ukurasa wa nne hadi wa 14 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele 14. Kamati imebaini kuwa kwa sehemu kubwa Wizara imetekeleza vipaumbele ingawa baadhi ya vipaumbele utekelezaji wake haukuwa wa kuridhisha. Miongoni mwa vipaumbele vilivyotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha ni pamoja na ujenzi wa kuzalisha umeme, ikiwemo miradi ya Julius Kambarage Nyerere ambao hadi Februari, 2024 utekelezaji wake ulikuwa umefikia 96%; mradi wa kuzalisha umeme Rusumo *MW* 27 ambao umekamilika; na mradi wa kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme wa gesi asilia katika Kituo cha Kinyerezi *I extension* cha *MW* 185 ambao pia umekamilika.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa vipaumbele ambavyo utekelezaji wake haukuwa wa kuridhisha ni kinachohusu kupeleka umeme katika vitongoji 36,336. Hadi Februari, 2024 utekelezaji wake ulikuwa umefikia 10.2%. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele yanapatikana katika ukurasa wa 14 hadi 16 wa taarifa kamili.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia mwezi Februari, 2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipangiwa kukusanya shilingi milioni 20.4 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi milioni 9.9 sawa na 49% ya lengo. Ukusanyaji huo ni chini ya lengo na Kamati imeshauri Wizara ibuni vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Nishati (Fungu 58) iliidhinishiwa na Bunge shilingi trilioni 3.05 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 87.93 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na 2.9% ambapo shilingi bilioni 16.3 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 71.64 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)*. Aidha, Miradi ya Maendeleo iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.96 sawa na 97.1% ya bajeti yote ambazo zinajumuisha fedha za ndani shilingi trilioni 2.61 na fedha za nje shilingi bilioni 351.55.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kuwa hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea shilingi trilioni 1.31 sawa na 52.27% ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 24 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.57 zilipokelewa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* haukuwa wa kuridhisha kutokana na kutokupokelewa kwa shilingi bilioni 53.2 za *IMF* kutoka nje. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ihakikishe inafuatilia upatikanaji wa fedha hizo ili kutoendelea kuathiri mipango iliyokusudiwa kutekelezwa. Maelezo zaidi kuhusu upatikanaji wa fedha yanaoneshwa katika ukurasa wa 17 hadi 19 wa taarifa yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliyowasilishwa Bungeni mwezi Mei, 2023 pamoja na mambo

mengine, ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo yapatayo 24 ili yafanyiwe kazi. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ni kama ilivyoonekana kwenye ukurasa wa 20 na 21 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(a) Uchambuzi wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(b) Uchambuzi wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(d) Ulinganisho kati ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025; na

(e) Uchambuzi wa masuala mahususi ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2024/2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara iliomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 8,000,000/= kutoka kwenye vyanzo vyake viwili. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya ni pungufu ya kiasi cha shilingi milioni 12.34 sawa na 60.8% ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo yalikuwa shilingi milioni 20.34.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Wizara imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati katika mwaka wa fedha

2022/2023 inayohusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli kuendana na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya fedha mwaka 2024/2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.9 ambazo zinajumuisha shilingi bilioni 88.89 za matumizi ya kawaida sawa na 4.7% ya bajeti yote ya Wizara. Shilingi trilioni 1.79 ni kwa ajili ya maendeleo sawa na 95.3% ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika fedha hizo, shilingi bilioni 19.34 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 69.52 ni kwa ajili ya matumizi mengine ambapo shilingi bilioni 53.2 ni fedha za nje *(IMF)* kwa ajili ya matumizi mengineyo pamoja na kutekeleza miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa na Umeme wa Vijijini *(REA)*. Katika fedha za maendeleo shilingi trilioni 1.54 ni fedha za ndani, shilingi bilioni 258.85 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kwa kiasi cha shilingi trilioni 1.2 sawa na 38.21% ikilinganishwa na bajeti ya Wizara hii ya kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ilielezwa kwamba ni kutokana na ukomo wa bajeti ya Wizara na kukamilika kwa Mradi wa Julius Nyerere ambao bajeti ilikuwa shilingi trilioni 1.5 sawa na 51.72% ya bajeti yote ya maendeleo iliyotengwa kwa Wizara. Maelezo zaidi ni kama ilivyooneshwa katika ukurasa wa 25 na 26 ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati, baada ya uchambuzi huu, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo: -

(i) Kutokana na umuhimu wa jengo la Wizara linalojengwa katika Mji wa Serikali, Mtumba na kutokana na kasi ya utekelezaji wake kuonekana siyo ya kuridhisha, Wizara iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike kwa muda uliopangwa na kwa viwango stahiki; na

(ii) Kutokana na kutokupokelewa kwa fedha za nje shilingi bilioni 53.2 kwa ajili matumizi mengineyo, Wizara ifuatilie na kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ili kutoathiri utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Umeme *TANESCO*, Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutokea Singida hadi Namanga ulihusisha kupeleka umeme kwenye vijiji 19 vilivyopitiwa na mradi huo. Hata hivyo, ni wateja 608 tu kati ya 10,000 waliokusudiwa ndiyo wameunganishiwa umeme, idadi ambayo ni ndogo sana. Kwa kuwa, kumekuwepo na tatizo la aina hii katika maeneo mengi nchini, Serikali ihakikishe:-

(i) *TANESCO* inashirikiana na *REA* kubuni mbinu zitakazoamsha ari ya wananchi na kuhamasisha matumizi ya umeme kwenye shughuli zao;

(ii) *TANESCO* iongeze kasi katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ili kuwezesha nchi kuwa na utoshelevu na uhakika wa umeme; na

(iii) *TANESCO* iongeze kasi ya kutekeleza miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa ili kuondoa changamoto ya kukatika kwa umeme kutokana na uchakavu wa miundombinu na umeme kupungua nguvu na kupotea kutokana na kusafiri umbali mrefu bila kupozwa.

Mheshimiwa Spika, nne, kwa kuwa nchi imeanza kujitosheleza kwa kiwango kikubwa cha umeme wa uhakika kutokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo Julius Nyerere, Rusumo pamoja na Kinyerezi *I Extension*, Serikali ihakikishe maeneo ya uzalishaji kama vile migodi, viwanda na skimu za umwagiliaji yanapata umeme wa kutosha na wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali ihakikishe ujenzi wa njia za kusafirishia umeme ambao umepangwa kutekelezwa katika mwaka

wa fedha 2024/2025 unahusisha kuunganisha mikoa iliyosailia kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, aita, mpango wa kuzalisha umeme wa *Megawatt* 200 kutokana na makaa ya mawe ya Kiwira - Mbeya ni wa muda mrefu bila kuanza utekelezaji, jambo linaloikosesha nchi fursa ya kunufaika na rasilimali za asili zilizopo. Serikali ihakikishe utekelezaji wa mradi huu unaanza ili nchi iweze kunufaika na rasilimali hiyo kama ilivyo katika nchi nyingine zenye rasilimali ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali iongeze kasi ya uhamasishaji, uwezeshaji na utekelezaji wa mradi wa nishati safi ya kupikia kwa kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa utoshelevu na bei nafuu. Mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia tungamotaka ya mabaki ya miwa nchini ina uwezo wa kuzalisha *Megawatt 10.5*. Hata hivyo, mitambo hiyo haifanyi kazi kikamilifu kutokana na kutegemea mabaki ya miwa na ingawa inaweza kutumia tungamotaka nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe mitambo hiyo inazalisha umeme kwa kutumia tungamotaka za aina mbalimbali kama vile taka laini zinazozalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu, Wakala wa Umeme Vijijini – *REA*, ili kuondoa tofauti ya gharama za kuunganishiwa umeme katika vijiji ambapo baadhi hulipa shilingi 27,000.00 na wengine zaidi ya shilingi 300,000.00 mfano Kijiji cha Tukamisasa, Chalinze - Bagamoyo, jambo linaloleta malalamiko miongoni mwa wananchi, Serikali ifanye mapitio ili kuwianisha gharama hizo na hivyo kuondoa malalamiko hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze kasi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 32,030 vilivyosalia ambavyo ni asilimia 49.5 ya vitongoji vyote nchini ili kuwezesha wananchi wa maeneo hayo kupata na kunufaika na nishati ya umeme nchini kama ilivyo kwa maeneo yenye huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme pembezoni mwa miji *(peri urban)* awamu ya tatu unasuasua licha ya kubakiza muda mfupi miezi nane kukamilika. Hadi Februari, 2024 mradi

huo ulikuwa umefikisha umeme kwenye maeneo 83 kati ya 420, sawa na asilimia 19.8 ya lengo na hivyo kuibua malalamiko miongoni mwa maeneo ambayo hayajafikiwa. Ili kuondoa malalamiko hayo, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Maendeleo la Petroli *(TPDC)*, usambazaji wa gesi asilia viwandani, majumbani na kwenye taasisi kwa ajili ya kupikia na kuendeshea mitambo na magari unasuasua. Hivyo basi, *TPDC* iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili kuongeza uzalishaji viwandani, kuchochea matumizi ya nishati safi ya kupikia na matumizi ya gesi asilia kwenye magari.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi asilia unaelezwa kupungua kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa gesi asilia na kuongezeka kwa matumizi ya gesi hiyo kwenye maeneo mengine ili kuondokana na athari hizo, Serikali iongeze uzalishaji kwenye vitalu vilivyopo na ianze uzalishaji katika vitalu vipya kama vile Kitalu cha Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe kampuni tanzu ya *TPDC* ya *TANOIL* inaongeza kasi ya ukusanyaji wa madeni chechefu yaliyofikia shilingi bilioni 21 kutoka kwa wadaiwa sugu na kuhakikisha haizalishi tena madeni mengine yasiyolipika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli – *PURA*, Serikali iharakishe mchakato wa kunadi vitalu vya gesi vilivyo wazi maeneo ya nchi kavu na baharini katika duru ya tano ili kuongeza uzalishaji wa gesi hasa ikizingatiwa kuwa mahitaji ya gesi nchini yameongezeka kuzidi kiwango cha uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi la kutayarisha miongozo kuhusu uwajibikaji wa kampuni kwa jamii *(CSR)* katika sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia nchini, linatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024, Serikali ihakikishe *PURA* inatoa elimu ya kutosha kuhusu mwongozo huo kwa wadau ili kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*, uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta

unaofanywa kwa kutumia njia ya mkono umeonesha kutokuwa na vipimo sahihi jambo linalozua manung`uniko miongoni mwa wafanyabiashara ya mafuta kwa kudai kuwa wanapigwa faini ukaguzi unapofanyika. Ili kuondokana na malalamiko hayo na kuleta ufanisi kwenye uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta, Serikali ianzishe uwekaji wa vinasaba kwa njia za kielekroniki.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa bei tofauti za gesi asilia miongoni mwa viwanda vinavyotumia gesi katika uzalishaji, umesababisha malalamiko miongoni mwa watumiaji hao. Kwa kuwa jukumu mojawapo la *EWURA* ni kupanga bei ya gesi ili kuweka usawa miongoni mwa watumiaji, Serikali ihakikishe taasisi hiyo inatekeleza jukumu lake kama ilivyo kwenye mafuta, maji na umeme.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la uuzaji holela wa mafuta ya dizeli na petroli maeneo ya vijijini unahatarisha usalama wa raia na mali zao. Serikali ihakikishe kwamba *EWURA* inaimarisha usimamizi wa biashara ya mafuta katika maeneo hayo ili kuepusha uwezekano wa kutokea majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu, Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja *(PBPA)*. Mfumo wa kudhibiti upotevu wa mafuta *(SCADA)* unaomilikiwa na *PBPA* una changamoto ya kutokuonesha mtiririko wa mafuta baada ya kupakuliwa kutoka kwenye meli. Hali hiyo inasababisha mamlaka husika kushindwa kubaini upotevu wa mafuta unaotokea wakati yanasafirishwa kwa njia ya bomba. Ili kudhibiti hali hiyo, Serikali iboreshe mfumo huo na kuuwezesha kuonesha mwenendo wa mtiririko wa mafuta na upotevu unaoweza kutokea wakati wa usafirishaji kwa njia ya bomba.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa maghala ya kuhifadhia mafuta nchini ikiwemo mafuta ya ndani na mafuta kwa ajili ya kupeleka nchi jirani *(on transit)* unaifanya nchi kukosa uhakika na usalama wa hifadhi ya mafuta na hivyo kuchangia kupanda kwa bei mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuanzisha mradi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta *(Strategic Petroleum Reserve - SPR)* ili kutatua changamoto hiyo. Hata hivyo,

Kamati inashauri kasi ya utekelezaji iongezeke ili kuwezesha nchi kuwa na uhakika na usalama wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, uzio wa eneo la *flow meters* pale Kigamboni, Dar es Salaam umezungukwa na makazi binafsi ya watu. Kamati inashauri maeneo hayo yatawaliwe na Serikali kwa makubaliano kusudi mabomba yale yawe salama na wenye maeneo hayo ili kusudi mabomba yake yawe salama.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa namna ya pekee naendelea kukushukuru na kukupongeza wewe kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge letu Tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Namshukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika kuendesha vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia mimi pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge, ambao umetuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu ya Kamati kwa ufanisi. Kwa namna ya pekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa ushirikiano anaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge na Naibu Waziri wa Nishati, kwa jinsi anavyoshirikiana na Kamati na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felschesmi Mramba; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. James Mataragio, kwa namna wanavyowaongoza watendaji wa Wizara na taasisi zake na hivyo kurahisisha utendaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Nishati **(Fungu 58)** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025**.** Uchambuzi wa

[1] 118 (9) Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja.

utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 na maoni ya kamati kuhusu bajeti ya mwaka 2024/2025 ni kutokana na majukumu ya msingi iliyopewa Kamati kwa mujibu wa kanuni ya 117(2) ikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[2].

## 1.1 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na imegawanyika katika sehemu zifuatazo:

a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, msingi na muundo wa taarifa hii;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na namna Wizara ilivyotekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

d) Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, inaweka masharti kwa Kamati za Kisekta

---

[2] 7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa yafuatayo:- (a) kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata[3]. Kwa kuzingatia matakwa haya, kuanzia tarehe 20 hadi 28 Machi, 2024 Kamati ilitekeleza wajibu huo kwa kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho dhidi ya mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilijielekeza kwenye maeneo yafuatayo: -

(a) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha mwaka wa fedha 2023/2024;

(b) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(c) Uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(d) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2024; na

(e) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati;

### 2.1 Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge[4], inaweka masharti kwa Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha (2023/2024). Katika kuzingatia masharti hayo, Kamati ilifanya

---

[3] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata

[4] Toleo la Februari 2023

ziara katika mikoa minne ambayo ni Dodoma, Arusha, Dar es Salaam na Pwani na kukagua miradi minne (4) inayotekelezwa chini ya Wizara ya Nishati.

Lengo la ukaguzi huo ni kutathmini utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kubainisha mafanikio na changamoto ili kuweza kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua katika kuisimamia Serikali. Uchambuzi kuhusu miradi hiyo na matokeo ya ukaguzi ni kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wizara (Na. 6389) Mtumba, Dodoma

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) kwa ajili ya ofisi za Wizara ya Nishati na unatekelezwa katika mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.
Gharama za mradi ni **shilingi 25,224,256,613.88,** na kati ya kiasi hicho **shilingi 1,547,480,194.89** ni kwa ajili ya wakandarasi washauri na **shilingi 23,676,776,415.9** ni kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi (NHC).

Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 12 Machi, 2024, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 75.09** na kiasi cha **shilingi 16,480,633,639.89** sawa na **asilimia 65.33** ya gharama za mradi kilikuwa kimelipwa kwa wakandarasi wanaotekeleza na kusimamia mradi.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 22 Novemba, 2021 na ulitakiwa kukamilika tarehe 29 Novemba, 2023. Hata hivyo, mradi haukukamilika katika muda huo kutokana na mkandarasi kuchelewa kuwasilisha malighafi za ujenzi kutoka nje ya nchi. Kamati ilielezwa kuwa sababu ya kuchelewa huko ni uhaba wa fedha za kigeni (dola za marekani). Sababu hiyo ilifanya muda wa mkataba kurefushwa kwa miezi sita (6) na sasa unatarajiwa kukamilika ifikapo 29 Mei, 2024 baada ya changamoto ya uhaba wa dola za kimarekani kutatuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea mradi huu na kuangalia utekelezaji wake ilibaini kasi ndogo ya utekelezaji wake na hivyo kuleta mashaka iwapo utekekelezaji wake utakamilika kwa wakati ikilinganishwa na muda wa takribani miezi mitatu iliyobaki. **Ni ushauri**

**wa Kamati kwamba, Wizara iimarishe usimamizi ili kuhakikisha mradi unakamilika ndani ya muda wa mkataba na jengo hilo kutoa huduma inayokusudiwa**.

### 2.1.2 Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Lemugur (Na. 3175), Kisongo-Arusha

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki ni sehemu ya nne (Lot 4) kati ya sehemu sita (six lots) za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia yenye urefu wa kilometa **414.3** ya kusafirisha umeme wa msongo wa **Kv 400** kutoka Singida hadi Namanga. Kwa ujumla utekelezaji wa sehemu zote sita za mradi unagharimu Dola za Marekani **milioni 258.82**, kati ya hizo **asilimia 83** zinatolewa na wafadhili AfDB na JICA na **asilimia 17** Serikali ya Tanzania.
Ujenzi wa Kituo hiki unahusu upanuzi wa kituo cha kupoza umeme (substation) cha Lemugur, Arusha na unagharimu Dola za Marekani **milioni 36** na hadi kufikia mwezi Machi, 2024 utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 99.27** na sasa mradi upo katika hatua ya majaribio.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mafanikio ya awali kutokana na ujenzi wa kituo hiki ni pamoja na kuiwezesha TANESCO kuanza mradi wa ujenzi wa njia nane (8) za kusambaza umeme msongo wa **Kv 33.** Lengo la mradi huo ni kukipunguzia mzigo kituo cha kupoza umeme cha Njiro kutokana ongezeko la wateja katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

Gharama za mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika Agosti, 2024 ni Dola za Marekani **Milioni 1.56** na shilingi **14,295,364,097.20** ambazo zinatolewa na Serikali ya Tanzania. Wakati Kamati inatembelea mradi huu, utekelezaji ambao ulianza Machi, 2023 ulikuwa umefikia **asilimia 35**. **Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili kuboresha huduma ya ugavi katika maeneo yanayohudumiwa na kituo cha Njiro**.

**Mheshimiwa Spika,** faida nyingine za utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na:-

(a) Kuwezesha Tanzania kuunganishwa na umeme wa pamoja wa upande wa mashariki mwa Afrika (East African Power Pool-EAPP) na hivyo kuingia katika biashara ya nishati na nchi nyingine; na

(b) Kuimarisha uwezo wa usambazaji wa umeme katika nchi za Kenya, Tanzania na eneo la mashariki mwa Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi wa mradi huu, Kamati ilipata taarifa kuhusu utekelezaji wa sehemu ya tano (Lot 5) ambayo ilihusu usambazaji wa umeme katika vijiji kumi na tisa (19) vilivyopitiwa na mradi kwa gharama ya Dola za Marekani **Milioni 4.4.** Mradi umekamilika na jumla ya **wateja 10,000** walikusudiwa kunufaika na mradi huu kwa kuunganisha umeme. Hata hivyo ilibainika kuwa ni **wateja 608** sawa na **asilimia 6.08 tu** ndio waliokuwa wameunganishwa.

### 2.1.3 Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kujaza gesi asilia kwenye magari (CNG) (Na. 3162), Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua vituo vikuu (CNG mother stations) viwili vya kujaza gesi asilia kwenye magari ambavyo viko Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Kipawa na Ubungo, katika mkoa wa Dar es Salaam. Uchambuzi kuhusu ukaguzi wa kila kituo ni kama ifuatavyo: -

#### (a) Kituo cha TAQA-*Dalbit* kilichopo Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Kipawa, Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki kilianza kazi tarehe 11 Novemba, 2023 na kina pampu sita zenye uwezo wa kuhudumia magari sita kwa wakati mmoja. Ni miongoni mwa vituo mama (mother CNG stations) kwa kuwa kinapokea gesi asilia moja kwa moja kutoka kwenye bomba lililojengwa na kampuni ya *PanAfrican Energy Tanzania Ltd* (PAET) kwa kushirikiana na TPDC. Aidha, kituo hiki kina karakana ya kuweka mfumo wa kutumia gesi kwenye magari ambayo yameingizwa nchini yakiwa hayana mfumo huo.

Kamati ilifahamishwa kuwa, kituo hiki chenye uwezo wa kujaza gesi asilia takribani **magari 1000** kwa siku kinafanya kazi saa 24 jambo linalosaidia kupunguza msongamano na hivyo kuwawezesha wateja kutumia muda mfupi kwenye kupata huduma. Wakati wa ukaguzi, kamati ilishuhudia ufanyaji kazi wa mfumo wa kuigandamiza gesi inayopokelewa kutoka kwenye bomba ili iweze kutumika kwa ajili ya magari, uwekaji wa mfumo wa gesi kwenye magari na ujazaji wa gesi kwenye magari kwa kuhudumia idadi kubwa ya wateja bila ya kusababisha msongamano.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ufanisi ulioshuhudiwa na kamati katika uendeshaji wa kituo hiki, zipo changamoto kadhaa zinazokikabili kituo hiki ikiwa ni pamoja na kituo kutegemea nishati ya umeme pekee kujiendesha. Hali hii inasababisha kukosekana kwa huduma ya kujaza gesi kwenye magari mara umeme unapokatika. **Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali itoe kipaumbele katika upatikanaji wa umeme kwenye maeneo yanayotoa huduma ya kujaza gesi kwenye magari, ili kuwawezesha wamiliki wa vituo hivyo kutoa huduma muda wote, hasa ikizingatiwa kwamba utumiaji wa kangavuke (*generator*) unaweza kusababisha gharama za kujaza gesi kuwa kubwa**.

**(b) Kituo cha PAET/TPDC kilichopo Ubungo, Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki ni miongoni mwa vituo mama (CNG mother stations) vya kujaza gesi kwenye magari na kinamilikiwa kwa ubia baina ya TPDC na Kampuni ya PAET. Kituo hiki kinachofanya kazi saa 24 kutokana na pampu mbili zilizopo, kina uwezo wa kuhudumia wastani wa magari 750 kwa siku.

Kutokana na eneo kilipo kituo hiki, wateja wengi huvutiwa kujaza gesi hapo, jambo linalosababisha msongamano mkubwa wa magari yanayosubiri kujaza gesi hasa nyakati za asubuhi na mchana. Aidha, kamati ilijulishwa kuwa idadi ya watumiaji wa gesi kwenye magari imekuwa ikiongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta.

Kamati ilipohoji kuhusu uwezekano wa kuongeza pampu ili kukabili msongamano, ilijulishwa kwamba suala hilo haliwezekani kutokana na ufinyu au udogo wa eneo la kituo. **Baada ya uchambuzi, Kamati**

**iliishauri Serikali kuhakikisha inatatua tatizo la foleni katika eneo hilo ndani ya muda mfupi ikiwemo ujenzi wa vituo vingine hatua ambayo itasaidia kuhamasisha watu wengi kujiunga na matumizi ya gesi asilia kwenye magari**.

### 2.1.4 Mradi wa ujenzi bomba la kusafirisha gesi asilia kwa ajili ya kupikia na viwandani (Na. 3162), Mwenge-Mbezi Beach, Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua ujenzi wa bomba kutokea Mwenge hadi Afrikana, Mbezi beach na viwanda vinavyotumia gesi asilia kuendeshea mitambo. Ujenzi wa bomba hilo umekamilika na tayari wateja wameomba kuunganishiwa huduma hiyo hususani baadhi ya viwanda na hoteli ambao wameanza kuandaa miundombinu itakayowawezesha kutumia gesi asilia.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa wateja wanaotumia gesi asilia kuendeshea mitambo ni kiwanda cha mabati cha **Kiboko** na kiwanda cha kuzalisha karatasi laini na vifungashio cha **TanPack Tissue Ltd** vilivyopo Mikocheni, Dar es Salaam. Gesi inayotumika katika viwanda hivi inatokana na bomba lililojengwa kwa ubia baina ya TPDC na Kampuni ya PAET. Kamati ilijulishwa kuwa matumizi ya gesi kwenye viwanda hivyo ni nafuu zaidi kwa wastani wa **asilimia 25** ikilinganishwa na matumizi ya umeme na mafuta.

Pamoja na unafuu huo wa matumizi ya gesi, wamiliki wa viwanda hivyo walilalamika kununua gesi hiyo kwa bei ya juu ikilinganishwa na bei wanayotozwa wamiliki wa viwanda vingine vinavyotumia nishati hiyo. Ilielezwa kwamba, wakati viwanda hivyo vinanunua *unit* moja ya gesi kwa kiasi cha Dola za Marekani **9.3**, viwanda vingine vinanunua *unit* hiyo kwa Dola za Marekani **6.7**. Kamati ilipohoji juu ya tofauti hiyo ya bei, ilijulishwa kwamba viwanda hivyo vinauziwa gesi na Kampuni ya PAET ambayo bei yake iko juu ikilinganishwa na gesi inayouzwa na TPDC. **Ni maoni ya Kamati kwamba Serikali iangalie namna ya kuwianisha bei ya gesi asilia kwa wateja wote ili kuondoa malalamiko na kuweka mazingira sawa ya kibiashara**.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu gharama za nishati mbalimbali za kupikia umebaini kwamba, matumizi ya gesi asilia (LNG) ni nafuu zaidi ikilinganishwa na matumizi ya nishati nyingine. Kielelezo Na.1kinafafanua zaidi.

**Kielelezo Na. 1:** Ulinganisho wa bei za nishati mbalimbali katika kupikia

| Nishati ya Kupikia | Tshs/MMbtu | Kuokoa Gharama |
|---|---|---|
| Gesi asilia (LNG) | 27,738.09 | Benchmark |
| Mkaa | 40,523.41 | 32% |
| Gesi ya Mitungi (LPG) | 76,670.40 | 64% |
| Umeme | 105,420.60 | 74% |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Wizara ya Nishati na Usanifu wa Kamati*

### 2.1.5 Mradi wa Umeme Vijijini (REA) (Na. 3113) Halmashauri ya Chalinze, Bagamoyo, Mkoa wa Pwani

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ufungaji wa mashine umba **22** na kupeleka umeme kwenye **vijiji 22** ambavyo vilikuwa havijafikiwa katika halmashauri ya Chalinze. Gharama za mradi ni **shilingi 7,827,305,757** na utekelezaji wake ulianza Agosti, 2021 na kukamilika Machi, 2024. Mradi ulikusudiwa kufikishia umeme wateja **1,452,** hata hivyo wakati Kamati inatembelea mradi huu, ni wateja **1,236** ndiyo walikuwa wameunganishiwa umeme kwenye nyumba zao sawa na **asilimia 85** ya lengo. Kwa upande wa uunganishaji wa umeme kwenye taasisi za umma zikiwemo shule, hospitali, misikiti na makanisa, utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 91**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kujiridhisha na hali halisi ya huduma ya umeme vijijini, Kamati ilitembelea Kijiji cha Tukamisasa ambacho ni cha mwisho kufikiwa na huduma ya umeme kwa gharama ya **shilingi Milioni 466**. Kamati ilielezwa kuwa, umeme katika Kijiji hicho una wigo wa wateja wa **awali 64**, lakini hadi wakati wa ukaguzi ni **wateja 23** tu ndio walikuwa wameunganishwa. Kamati ilipohoji kuhusu idadi ndogo

ya wateja kuunganishiwa umeme sababu mbalimbali zilitolewa kama ifuatavyo:

(a) Uhamasishaji hafifu kutoka kwa viongozi kutokana na uwepo wa taarifa kuwa mradi wa REA ambao ndio unaolipiwa **shilingi 27,000** umefikia ukomo na umebaki mradi wa TANESCO ambao gharama yake ni zaidi ya **shilingi 300,000**;

(b) Umeme kutokufika kwenye vitongoji vilivyo nje ya barabara zilizojengwa miundominu ya umeme;

(c) Kaya nyingi kutokuandaa miundombinu ya kupokelea umeme kwenye nyumba zao; na

(d) Ukosefu wa mashine umba (transfoma) katika baadhi ya vitongoji licha ya kupitiwa na miundombinu ya umeme.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa sababu zilizoelezwa katika halmashauri ya Chalinze hususani kijiji cha Tukamisasa kwa watu wengi kutokuunganisha umeme kwenye nyumba zao licha ya umeme kufika katika vijiji vyao, kwa sehemu kubwa ndizo changamoto zilizoko katika vijiji vingi nchini.

Wakala wa Umeme Vijijini (REA) pia unatekeleza mradi wa kupeleka umeme kwenye migodi midogo na maeneo ya kilimo kwenye jumla ya maeneo kumi na nne (14) katika wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya **wateja tarajiwa 78**. Mradi huo utakaogharimu **shilingi 2,456,801,235.70** ulianza kutekelezwa Machi, 2023 na unategemewa kukamilika Septemba, 2024. Hadi wakati wa ukaguzi, maeneo manne **(4)** tu sawa na **asilimia 28** ya lengo ndio yalikuwa yamepata huduma ya umeme.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele kumi na nne **(14).** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa sehemu kubwa Wizara imetekeza

vipaumbele hivyo kwa kiasi cha kuridhisha. Aidha, utekelezaji wa baadhi ya vipaumbele haukuwa wa kuridhisha.

Miongoni mwa vipaumbele vilivyotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha ni ujenzi wa miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo mradi wa Julius Nyerere (JNHPP-**MW2,115**) ambao hadi Februari, 2024 utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 96**, mradi wa kuzalisha umeme Rusumo **MW 26.67** ambao umekamilika na mradi wa kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme wa gesi asilia katika kituo cha kinyerezi I extension **MW 185** ambao pia umekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa vipaumbele ambavyo utekelezaji wake haukuwa wa kuridhisha, Kamati imetoa ushauri kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wake kufanyika kadri ulivyopangwa. Vipaumbele hivyo ni pamoja na: -

(a) Kupeleka umeme katika vitongoji **36,336** sawa na **asilimia 56** ya vitongoji **64,760** vya Tanzania bara. Hadi Februari, 2024 utekelezaji wa kipaumbele hiki ni **asilimia 10.2** ambapo kazi zilizofanyika ni ununuzi wa vifaa na kusimika nguzo katika mkoa wa Songwe na Kigoma kwa lengo la kufikisha umeme kwenye **vitongoji 654.** Aidha, tathmini kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa kutekeleza mradi huu katika **vitongoji 3,060** imekamilika.

(b) Kuhakikisha upatikanaji wa umeme nchini kupitia mradi wa kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization) ambapo kazi zilizofanyika ni kukamilisha taratibu za kuwapata wakandarasi na kusainiwa kwa mikataba ya miradi yote ya gridi imara, ukaguzi wa njia za kusafirishia umeme, upembuzi yakinifu wa njia za kusafirishia umeme, usanifu wa michoro, ununuzi wa vifaa kwa baadhi ya miradi pamoja na kuanza kazi za ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa sababu za kutokutekelezwa ipasavyo kwa kipaumbele hiki ni pamoja na kutolewa kwa kiasi kidogo cha fedha kwani hadi Februari, 2024, ni **shilingi Bilioni 132.6** tu kati ya **shilingi Bilioni 473.4** zilizotengwa sawa na utekelezaji wa asilimia **28.02**.

### 2.3 Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli hadi kufikia mwezi Februari, 2024

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya **Shilingi 20,392,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 9,942,015** sawa na **asilimia 49** ya lengo. Kielelezo Na. 2 kinafafanua.

**Kielelezo Na. 2: Makusanyo ya Maduhuli hadi Februari, 2024**

| Chanzo cha Mapato | Kiasi kilichopangwa | Kiasi kilichokusanywa | Asilimia ya lengo |
|---|---|---|---|
| Stakabadhi nyinginezo | 1,000 | 0 | 0 |
| Marejesho ya fedha za Umma | 20,391,000 | 9,942,015 | 49 |
| Stakabadhi za aina mbalimbali | 1,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **20,393,000** | **9,942,015** | **49** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara hii ulikuwa chini ya lengo. Hata hivyo, ilielezwa kuwa hali hiyo imesababishwa na Wizara kutegemea kwa asilimia kubwa (99.9%) makusanyo kutoka chanzo kimoja ambacho ni urejeshaji wa masurufu (*imprest)*. **Ni mtazamo wa Kamati kwamba Wizara ibuni vyanzo vipya vya mapato**.

## 2.4 Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2024

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Nishati (**Fungu 58**) iliidhinishiwa na Bunge **Shilingi 3,048,632,519,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni **Shilingi 87,929,698,000.00** sawa na **asilimia 2.9** ya fedha yote ambapo **Shilingi 16,292,586,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (P.E) na **Shilingi 71,637,112,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Miradi ya Maendeleo iliidhinishiwa **Shilingi 2,960,702,821,000.00** sawa na **asilimia 97.1** ya bajeti yote ambazo zinajumuisha fedha za ndani **Shilingi 2,609,156,128,000.00** na fedha za nje **Shilingi 351,546,693,000.00**

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 1,310,852,090,180.49** sawa na **asilimia 52.27** ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 24,089,029,668.19** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo **shilingi 11,386,327,902.48** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **Shilingi 12,702,701,765.71** sawa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, zilipokelewa **shilingi 1,569,534,870,633.73** sawa na **asilimia 53.42** ya kiasi kilichotengwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,324,485,523,330.90** ni fedha za ndani na **Shilingi 245,049,347,302.73** ni fedha za nje. Mchanganuo wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.3**.

**Kielelezo Na. 3:** Upatikanaji wa Fedha kwa Wizara ya Nishati kwa kipindi cha Julai, 2023 - Februari, 2024

| Aina | Kilichoidhinishwa | Kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Mishahara** | **16,292,586,000** | **11,386,327,902.48** | **69.88** |
| **Oc** | **71,637,112,000** | **12,702,701,765.71** | **17.73** |
| **Maendeleo Ndani** | **2,609,156,128,000** | **1,324,485,523,330.90** | **50.76** |
| **Maendeleo Nje** | **351,546,693,000** | **245,049,347,302.73** | **69.70** |
| **JUMLA** | **3,048,632,519,000** | **1,310,852,090,180.49** | **52.27** |

***Chanzo**: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umebaini kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) haukuwa wa kuridhisha. Kamati ilipohoji kuhusu hali hiyo ilielezwa kuwa ilisababishwa na kutokupokelewa kwa fedha za IMF kutoka nje jumla ya **shilingi Bilioni 53.2. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ihakikishe inafuatilia upatikanaji wa fedha hizo ili kutoendelea kuathiri mipango iliyokusudiwa kutekelezwa.**

## 2.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliyowasilishwa Bungeni mwezi Mei, 2023 pamoja na mambo mengine, ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo yapatayo 24 ili yafanyiwe kazi na Wizara.

Katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 20 Machi, 2024, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Tathmini inaonesha kuwa, Wizara imetekeleza ushauri na mapendekezo yaliyotolewa kwa kiwango cha kuridhisha isipokuwa kwa baadhi ya hoja chache zifuatazo: -

(a) TANESCO kulipa deni lote inalodaiwa na TPDC kiasi cha **shilingi Bilioni 720** katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hoja hii haikutekelezwa kutokana na mapato ya TANESCO kuwa kidogo ikilinganishwa na mahitaji. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, kutokulipwa kwa fedha hizi kunaathiri uwezo wa TPDC katika kutekeleza kikamilifu shughuli zake ikiwa ni pamoja na miradi ya uzalishaji wa gesi asilia ambayo ni muhimu pia kwa ajili ya TANESCO katika kuzalisha umeme; na

(b) Taasisi zote zinazodaiwa na TANESCO ankara za umeme jumla ya **shilingi Bilioni 334.8** kulipa madeni yote katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hadi Februari, 2024 deni linalodaiwa na TANESCO ni **shilingi Bilioni 86.3.** Kamati ilielezwa kuwa, madeni haya yanatokana na taasisi zinazotumia mita za umeme za zamani kutokana na kuwa na matumizi makubwa ya umeme ambayo hayawezi kutumia mita za LUKU kama ilivyo kwenye nyumba za makazi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokulipwa kwa madeni haya kikamilifu kunaathiri utendaji wa TANESCO na kuipunguzia uwezo wa kutekeleza miradi yake. Ni msisitizo wa Kamati kuwa, Serikali isimamie na kuhakikisha taasisi zinazodaiwa na TANESCO zinalipa madeni stahiki kwani zinaidhinishiwa katika bajeti fedha za kununua umeme.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

a) Uchambuzi wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

b) Uchambuzi wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

c) Uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

d) Ulinganisho kati ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025; na

e) Uchambuzi wa masuala mahsusi ya kisekta.

### 3.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umebaini kuwa, malengo na vipaumbele vya Wizara vimezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati wa Mwaka 2021/2022-2025/2026.

Ili kufikia malengo ambayo yamefafanuliwa kwa kina kupitia mpango mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/2022-2025/2026, Wizara inakusudiwa kutekeleza jumla ya vipaumbele tisa (9). Baadhi ya vipaumbele hivyo ni: -

a) Kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kufikisha gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia;

b) Kuendelea kupeleka nishati vijijini, ikiwemo kusambaza umeme katika vitongoji vya Tanzania Bara, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa nishati ya mafuta vijijini kupitia uanzishwaji wa vituo vya mafuta;

c) Kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia ikiwa ni pamoja na mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (*Liquefied Natural Gas-LNG Project*) na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline -EACOP*);

d) Kutekeleza shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati pamoja na kusambaza gesi asilia viwandani, taasisi, makazi na magari;

e) Kuendelea kuimarisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia (clean cooking) nchini; na

f) Kuendelea kuhakikisha nchi inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya vipaumbele vya mwaka wa fedha 2024/2025 vilikuwepo katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo, vipaumbele vya mwaka wa fedha 2024/2025 vimepungua kutoka kumi na nne (14) hadi tisa (9) kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pomoja na baadhi ya miradi kukamilika na kupungua kwa bajeti ya Wizara kwa asilimia 38 ikilinganishwa na mwaka unaoisha.

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **shilingi 8,000,000.00** kutoka kwenye vyanzo vyake viwili. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya ni pungufu kwa kiasi cha **shilingi 12,392,000** sawa na **asilimia 60.8** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo yalikuwa **shilingi 20,392,000.00**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Wizara imezingatia ushauri uliowahi kutolewa na Kamati katika mwaka wa fedha 2022/2023 uliohusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli kuendana na uhalisia. Kielelezo Na. 4 kinaeleza kuhusu ulinganisho wa maduhuli.

Kielelezo Na. 4: **Ulinganisho wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| CHANZO | 2023/2024 | 2024/2025 | ONGEZEKO /UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Marejesho ya Fedha za Umma (Recovery of Public Money) | **20,391,000** | **7,999,000** | **12,392,000** | **60.8** |
| Stakabadhi nyinginezo | **1,000** | **1,000** | **0** | **0** |
| Stakabadhi za aina mbalimbali | **1,000** | **-** | **-** | **-** |
| **JUMLA** | **20,393,000** | **8,000,000** | **12,392,000** | **60.8** |

***Chanzo**: Randama ya Wizara ya makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na usanifu wa Kamati*

3.3 **Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Nishati inaomba kuidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 1,883,759,455,000.00**. Fedha hizi zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 88,892,623,000/=** sawa na **asilimia 4.7** ya bajeti yote ya Wizara. Katika fedha hizo, **shilingi 19,368,422,000.00** ni kwa ajili ya mishara (PE) na **shilingi 69,524,201,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Kamati ilielezwa kuwa, katika fedha za matumizi mengineyo (OC), kiasi cha **shilingi 53,200,000,000.00** ni fedha za nje (IMF) kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) pamoja na kutekeleza miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa na umeme vijijini (REA-HEP).

Aidha, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ni shilingi **1,794,866,832,000.00** sawa na **asilimia 95.3** ya bajeti yote ya Wizara, ambapo **shilingi 1,536,020,274,000.00** ni fedha za ndani na **shilingi 258,846,558,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kwa kiasi cha **shilingi 1,164,873,084,000.00** sawa na **asilimia 38.21** ikilinganishwa na bajeti ya Wizara hii ya mwaka wa fedha 2023/2024. Kielelezo Na.5 kinafafanua ulinganisho huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kutokana na kupungua kwa ukomo wa bajeti (Budget ceiling) iliyotolewa na Serikali ikilinganishwa na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo ukomo wa bajeti ulikuwa juu. Vilevile, kupungua kwa bajeti katika mwaka ujao wa fedha kunahusianishwa na kukamilika kwa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao bajeti yake ilikuwa **shilingi 1,500,000,000,000.00** sawa na **asilimia 51.72** ya bajeti yote ya maendeleo iliyotengwa kwa Wizara.

Kielelezo Na. 5: **Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| WIZARA YA NISHATI - FUNGU 58 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2023/2024** | **2024/2025** | **ONGEZEKO/UPUNGUFU** | **ASILIMI A** |
| **Maendeleo** | Fedha za Ndani | 2,609,156,128,000 | 1,536,020,274,000 | 1,073,135,854,000 | 41.13 |
| | Fedha za Nje | 351,546,693,000 | 258,846,558,000 | 92,700,135,000 | 26.37 |
| | **Jumla ndogo** | **2,960,702,821,000** | **1,794,866,832,000** | **1,165,835,989,000** | **39.38** |
| **Matumizi ya kawaida** | Mengine yo (OC) | 71,637,112,000 | 69,524,201,000 | 2,112,911,000 | 2.95 |
| | Mishahara (PE) | 16,292,586,000 | 19,368,422,000 | 3,075,836,000 | 18.88 |
| | **Jumla ndogo** | **87,929,698,000** | **88,892,623,000** | **962,925,000** | **1.1** |
| **JUMLA KUU** | | **3,048,632,519,000** | **1,883,759,455,000** | **1,164,873,064,000** | **38.21** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Wizara kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 na Usanifu wa Kamati*

### 3.4 Ulinganisho baina ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulienda mbali zaidi kwa kulinganisha Bajeti ya Wizara hii na Bajeti ya Taifa. Ulinganisho huo uliangalia bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambayo ni **shilingi 3,048,632,519,000** na bajeti ya 2024/2025 ambayo ni **shilingi 1,883,759,455,000** dhidi ya bajeti ya Taifa kwa kipindi hicho ambayo ni **shilingi 44,388,100,000,000** mwaka 2023/2024 na **shilingi 49,345,700,000,000** mwaka 2024/2025. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali yafuatayo: -

a) Bajeti ya Wizara kwa ujumla dhidi ya Bajeti ya Taifa imeshuka kutoka **asilimia 6.87** mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia **asilimia 3.8** kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

b) Katika upande wa matumizi mengineyo, bajeti ya Wizara imeshuka kutoka **asilimia 0.66** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **asilimia 0.26** mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na bajeti ya Taifa.

c) Katika bajeti ya maendeleo, fedha za ndani za Wizara zimepungua kutoka **asilimia 21.97** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **asilimia 12.64** mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na bajeti ya Taifa.

d) Katika bajeti ya maendeleo, fedha za nje zimepungua kutoka **asilimia 10.71** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **asilimia 7.11** mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti ya Wizara imepungua katika nyanja zote ilihali bajeti ya Taifa imeongezeka.

**Kielelezo Na. 6:** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

| **BAJETI YA TAIFA DHIDI YA BAJETI YA WIZARA MWAKA 2024/2025** | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI YA TAIFA** | **BAJETI YA NISHATI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 33,556,600,000,000 | 1,794,866,832,000 | 5.35 |
| **Mishahara** | 11,997,800,000,000 | 19,368,422,000 | 0.16 |
| **Maendeleo ndani** | 12,148,300,000,000 | 1,536,020,274,000 | 12.64 |
| **Maendeleo nje** | 3,640,800,000,000 | 258,846,558,000 | 7.11 |
| **Deni la Serikali** | 15,746,700,000,000 | - | - |
| **JUMLA KUU** | **49,345,700,000,000** | **1,883,759,455,000** | **3.8** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Randama ya Wizara ya Nishati mwaka wa fedha 2024/2025 na Usanifu wa Kamati.*

### 3.5 **Uchambuzi wa Masuala Mahsusi**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi wa bajeti, Kamati imejiwekea utaratibu wa kufuatilia masuala mahsusi ya kisekta kwa kuwa yana maslahi kwa wananchi na nchi kwa ujumla. Masuala hayo ni mwenendo wa upatikanaji wa umeme pamoja na mwenendo wa biashara ya mafuta nchini. Uchambuzi kuhusu masuala hayo ni kama ifuatavyo: -

#### 3.5.1 **Mwenendo wa Upatikanaji wa Umeme**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, hali ya upatikanaji wa umeme nchini imekuwa ikibadilika katika vipindi tofauti. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 hali haikuwa ya kuridhisha na hivyo kusababisha mgao katika sehemu kubwa ya nchi. Katika kipindi cha Januari hadi Aprili, 2024, hali ya upatikanaji wa umeme imeonekana kuimarika na hivyo mgao kupungua.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusiana na mitambo ya kuzalisha umeme, hadi Februari, 2024 uwezo wa mitambo kuzalisha umeme (*installed capacity*) ulikuwa **MW 2,129.85.** Kiwango hiki ni ongezeko la **MW 307.8** ikilinganishwa na uwezo wa mitambo wa **MW 1,822.05** mwezi Februari, 2023. Licha ya uwezo wa mitambo kuwa juu, uzalishaji halisi (production capacity) hadi Februari, 2024 ulikuwa wastani wa **MW 1,756.42** sawa na uwezo wa uzalishaji wa **asilimia 82.5** ikilinganishwa na uwezo wa mitambo iliyosimikwa. Kielelezo Na.7 kinafafanua zaidi.

Kielelezo Na. 7: **Mchanganuo wa uwezo wa mitambo katika gridi ya Taifa hadi Mwezi Februari, 2024**

| **Chanzo** | **Uwezo wa Mitambo (Installed Capacity)** | | **Uzalishaji unaopatikana (Available production)** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **MW** | **Uwezo wa mitambo (%)** | **Chanzo** | **MW** | **Uzalishaji (%)** |
| Maji | 836.61 | 39.3 | Maji | 755.56 | 90.31 |
| Gesi Asilia | 1,198.82 | 56.3 | Gesi Asilia | 935.11 | 78 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mafuta | 83.92 | 3.9 | Mafuta | 65.75 | 78.35 |
| Tungamotaka | 10.5 | 0.5 | Tungamotaka | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2,129.85** | **100** | **Jumla** | **1,756.42** | **82.5** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mitambo iliyopo inazalisha umeme chini ya uwezo wake kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uchakavu wa miundombinu ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme na upungufu wa uzalishaji wa gesi asilia ikilinganishwa na mahitaji ya gesi yaliyopo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya umeme vijijini, hadi Februari, 2024, jumla ya **vijiji 11,837** kati ya **vijiji 12,318** vilivyopo nchini vimefikiwa na huduma ya umeme, sawa na **asilimia 96.1**. Aidha, kwa upande wa vitongoji, hadi kufikia Februari, 2024 asilimia **50.54** (**vitongoji 32,730** kati ya **vitongoji 64,760)** vilivyoko nchini vilikuwa vimefikiwa na huduma ya umeme.

Ili kuhakikisha maeneo yote ya nchi yanapata umeme, Serikali ilianzisha mradi wa umeme maeneo ya pembezoni mwa miji (*peri urban)* ambao utekelezaji wake uko awamu ya Tatu. Awamu hii imepangwa kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2024. Hata hivyo, utekelezaji wake unasuasua kwani hadi Februari, 2024 ulikuwa umefikia **asimilia 19.8 tu** kwa kufika katika maeneo **83** kati ya **420** yaliyokusudiwa, na kuunganishia umeme wateja **1,166** kati ya **18,426.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la uhitaji wa umeme nchini kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo idadi kubwa ya wananchi wanaosubiri kuunganishiwa umeme hususani maeneo ya vijijini, pembezoni mwa miji na maeneo ya uzalishaji ikiwemo wachimbaji wadogo na viwanda. **Kamati inasisitiza Serikali kuendelea kukamilisha miradi ya kuzalisha umeme inayotekelezwa ikiwemo, mradi wa umeme wa jua Shinyanga (MW 150) na Julius Nyerere (JNHPP MW 2115) ili kupunguza upungufu wa**

**umeme katika maeneo yaliyosalia ambayo hayajapata huduma ya umeme.**

### 3.5.2 Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu uagizaji wa mafuta nchini kupitia Wakala wa Uagizaji wa mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa kutumia mfumo wa manunuzi ya pamoja (*Bulk Procurement System* – BPS). Uchambuzi wa Kamati kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta unaonesha kuwa, nchi ina akiba ya mafuta inayotosheleza mahitaji. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 akiba ya mafuta nchini ilikuwa **siku 25** ambazo ni juu ya wastani wa mahitaji (**siku 15**).

Katika kipindi hicho, jumla ya **Tani 4,453,479** ziliingizwa nchini kupitia zabuni **78** zilizotolewa na PBPA. Kiasi hicho ni ongezeko la **Tani 190,234** za mafuta sawa na **asilimia 4.46** ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 ambapo uagizaji ulikuwa **Tani 4,263,245.** Katika kiasi hicho kilichoingizwa nchini, Tani **2,228,238** sawa na **asilimia 50.03** ni kwa ajili ya matumizi ya ndani (*local*) na kiasi cha **Tani 2,225,241** sawa na **asilimia 49.97** ni mafuta yanayopita kwenda nchi jirani (*on transit*).

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa na akiba toshelezi ya mafuta nchini, bei ya mafuta iliendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupanda kwa gharama za usafiri na ongezeko la bima ya meli zinazosafirisha mafuta kutokana na vita vya Ukraine na Urusi, uhaba wa Dola za Marekani na kuongezeka kwa gharama za kubadilisha fedha za kigeni *(exchange rate*). **Ni msisitizo wa Kamati kuwa Serikali iendelee na jitihada za kupunguza athari za bei ya mafuta kuwa juu nchini ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia kwenye magari**.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huu, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kama ifutavyo:-

4.1 **Wizara ya Nishati**

a) Kutokana na umuhimu wa Jengo la Wizara linalojengwa katika mji wa Serikali mtumba, na kutokana na kasi ya utekelezaji wake kuonekana sio ya kuridhisha, Wizara iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike katika muda ulioongezwa na kwa viwango stahiki.

b) Kutokana na kutokupokelewa kwa fedha za nje **shilingi 53,200,000,000.00** kwa ajili matumizi mengineyo, Wizara ifuatilie na kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ili kutoathiri utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa.

4.2 **Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO)**

a) Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutokea Singida hadi Namanga ulihusisha kupeleka umeme kwenye vijiji kumi na tisa (19) vilivyopitiwa na mradi huo. Hata hivyo, ni **wateja 608** tu kati ya **10,000** waliokusudiwa ndio wameunganishiwa umeme idadi ambayo ni ndogo sana. Kwa kuwa kumekuwepo na tatizo la aina hii katika maeneo mengi nchini, Serikali ihakikishe TANESCO inashirikiana na REA kubuni mbinu zitakazoamsha ari ya wananchi na kuhamasisha matumizi ya umeme kwenye shughuli zao;

b) TANESCO iongeze kasi katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ili kuwezesha nchi kuwa na utoshelevu na uhakika wa umeme;

c) TANESCO iongeze kasi ya kutekeleza miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa ili kuondoa changamoto ya kukatika kwa umeme kutokana na uchakavu wa miundombinu, na umeme kupungua nguvu na kupotea kutokana na kusafiri umbali mrefu bila kupozwa;

d) Kwa kuwa nchi imeanza kujitosheleza kwa kiwango na uhakika wa umeme kutokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya kuzalisha umeme (JNHPP, Rusumo na Kinyerezi I Extension),

Serikali ihakikishe maeneo ya uzalishaji kama vile migodi, viwanda na skimu za umwagiliaji, yanapata umeme wa kutosha na wa uhakika;

e) Serikali ihakikishe ujenzi wa njia za kusafirishia umeme ambao umepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 unahusisha kuunganisha mikoa iliyosailia kwenye gridi ya Taifa;

f) Mpango wa kuzalisha umeme (**MW 200)** kutokana na makaa ya mawe ya Kiwira, Mbeya ni wa muda mrefu bila kuanza utekelezaji, jambo linaloikosesha nchi fursa ya kunufaika na rasilimali za asili zilizopo. Serikali ihakikishe utekelezaji wa mradi huu unaanza ili nchi iweze kunufaika na rasilimali hiyo kama ilivyo katika nchi nyingine zenye rasilimali ya aina hii;

g) Serikali iongeze kasi ya uhamasishaji, uwezeshaji na utekelezaji wa mradi wa nishati safi ya kupikia kwa kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa utoshelevu na bei nafuu; na

h) Mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia tungamotaka ya mabaki ya miwa nchini ina uwezo wa kuzalisha **MW 10.5.** Hata hivyo, mitambo hiyo haifanyi kazi kikamilifu kutokana na kutegemea mabaki ya miwa tu ingawa inaweza kutumia tungamotaka nyingine. Serikali ihakikishe mitambo hiyo inazalisha umeme kwa kutumia tungamotaka za aina mbalimbali kama vile taka laini zinazozalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

4.3 **Wakala wa Umeme Vijijini – REA**

a) Ili kuondoa tofauti ya gharama za kuunganishiwa umeme katika vijiji ambapo baadhi hulipa shilingi 27,000.00 na wengine zaidi ya shilingi 300,000.00 (mfano kijiji cha Tukamisasa, Chalinze-Bagamoyo), jambo linaloleta malalamiko miongoni mwa wananchi, Serikali ifanye mapitio ili kuwianisha gharama hizo na hivyo kuondoa malalamiko yaliyopo;

b) Serikali iongeze kasi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 32,030 vilivyosalia (ambavyo ni asilimia 49.5 ya vitongoji vyote nchini) Ili kuwezesha wananchi wa maeneo hayo kupata na kunufaika na nishati ya umeme nchini kama ilivyo kwa maeneo yenye huduma ya umeme; na

c) Utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme pembezoni mwa miji (peri urban) awamu ya tatu unasuasua licha ya kubakiza muda mfupi (miezi nane) kukamilika. Hadi Februari, 2024 mradi huo ulikuwa umefikisha umeme kwenye **maeneo 83** kati ya **420**, sawa na **asilimia 19.8** ya lengo na hivyo kuibua malalamiko miongoni mwa maeneo ambayo hayajafikiwa. Ili kuondoa malalamiko hayo, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu.

4.4 **Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC)**

a) Usambazaji wa gesi asilia viwandani, majumbani na kwenye taasisi kwa ajili ya kupikia na kuendeshea mitambo na magari unasuasua. Hivyo basi, TPDC iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili kuongeza uzalishaji viwandani, kuchochea matumizi ya nishati safi ya kupikia na matumizi ya gesi asilia kwenye magari;

b) Uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi asilia unaelezwa kupungua kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa gesi asilia na kuongezeka kwa matumizi ya gesi hiyo kwenye maeneo mengine. Ili kuondokana na athari hizo, Serikali iongeze uzalishaji kwenye vitalu vilivyopo na ianze uzalishaji katika vitalu vipya kama vile kitalu cha Ruvuma; na

c) Serikali ihakikishe Kampuni Tanzu ya TPDC ya TANOIL inaongeza kasi ya ukusanyaji wa madeni chechefu yaliyobakia (shilingi bilioni 21) kutoka kwa wadaiwa sugu na kuhakikisha haizalishi madeni mengine yasiyolipika.

4.5 **Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli – PURA**

a) Serikali iharakishe mchakato wa kunadi vitalu vya gesi vilivyo wazi maeneo ya nchi kavu na baharini katika duru ya tano ili kuongeza uzalishaji wa gesi hasa ikizingatiwa kuwa mahitaji ya gesi nchini yameongezeka kuzidi kiwango cha uzalishaji; na

b) Kwa kuwa zoezi la kutayarisha miongozo kuhusu Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR) katika sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia nchini linatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024, Serikali ihakikishe PURA inatoa elimu ya kutosha kuhusu muongozo huo kwa wadau ili kurahisisha utekelezaji wake.

4.6 **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**

a) Uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta unaofanywa kwa kutumia njia ya mkono umeonesha kutokuwa na vipimo sahihi jambo linalozua manung`uniko miongoni mwa wafanyabiashara ya mafuta kwa kudai kuwa wanapigwa faini ukaguzi unapofanyika. Ili kuondokana na malalamiko hayo na kuleta ufanisi kwenye uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta, Serikali ianzishe uwekaji wa vinasaba kwa njia za kielekroniki;

b) Uwepo wa bei tofauti za gesi asilia miongoni mwa viwanda vinavyotumia gesi katika uzalishaji umesababisha malalamiko miongoni mwa watumiaji hao. Kwa kuwa jukumu mojawapo la EWURA ni kupanga bei ya gesi ili kuweka usawa miongoni mwa watumiaji, Serikali ihakikishe taasisi hiyo inatekeleza jukumu lake kama ilivyo kwenye mafuta, maji na umeme; na

c) Ongezeko la uuzaji holela wa mafuta ya dizeli na petroli maeneo ya vijijini unahatarisha usalama wa raia na mali zao. Serikali ihakikishe EWURA inaimarisha usimamizi wa biashara ya mafuta katika maeneo hayo ili kuepusha uwezekano wa kutokea majanga ya moto.

### 4.7 **Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA)**

a) Mfumo wa kudhibiti upotevu wa mafuta (SCADA) unaomilikiwa na PBPA una changamoto ya kutokuonesha mtiririko wa mafuta baada ya kupakuliwa kutoka kwenye meli. Hali hiyo inasababisha mamlaka husika kushindwa kubaini upotevu wa mafuta unaotokea wakati yanasafirishwa kwa njia ya bomba. Ili kudhibiti hali hiyo, Serikali iboreshe mfumo huo na kuuwezesha kuonesha mwenendo wa mtiririko wa mafuta na upotevu unaoweza kutokea wakati wa usafirishaji kwa njia ya bomba;

b) Uhaba wa maghala ya kuhifadhia mafuta nchini ikiwemo mafuta ya ndani na mafuta kwa ajili ya kupeleka nchi jirani (on transit) unaifanya nchi kukosa uhakika na usalama wa hifadhi ya mafuta na hivyo kuchangia kupanda kwa bei mara kwa mara. Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuanzisha mradi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (Strategic Petroleum Reserve-SPR) ili kutatua changamoto hiyo. Hata hivyo, inashauri kasi ya utekelezaji iongezeke ili kuwezesha nchi kuwa na uhakika na usalama wa mafuta; na

c) Uzio wa eneo la *flow meters* zilizopo Kigamboni, Dar es Salaam umezungukwa na makazi binafsi, jambo ambalo linahatarisha usalama wa bomba la mafuta. Aidha, siku za nyuma uliripotiwa wizi wa mafuta kutoka kwenye bomba uliohusishwa na makazi binafsi. Ili kuepuka kujirudia kwa tatizo la wizi na hujuma kwenye bomba la mafuta, Serikali iangalie uwezekano wa kutwaa maeneo yenye makazi binafsi kuzunguka bomba na *flow meters*.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hoja ya Kamati kama ifuatavyo: -

## 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naendelea kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Namshukuru Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu, (Mb) pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika kuendesha vikao vya Bunge.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano mkubwa wananipatia mimi pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb) ambao umetuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu ya Kamati kwa ufanisi. Kwa namna ya pekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*hansard*) kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Sophia Hezron Mwakagenda, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. John Marko Sallu, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Eng. Samwel X. Hhayuma, Mb - Mjumbe

22. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumshukuru Mhe. Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa ushirikiano anaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, natoa shukrani zangu kwa Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb), Naibu Waziri wa Nishati, kwa anavyoshirikiana na Kamati na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Felschesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu Dkt. James Mataragio kwa namna wanavyowaongoza watendaji wa Wizara na Taasisi zake na hivyo kurahisisha utendaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi (*ndc*) pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya Kikatiba.

### 5.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati (**Fungu 58)** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dkt. David Mathayo David, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

24 Aprili, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada, tutaanza sasa uchangiaji lakini kabla hatujaanza, wapo wageni ambao wameingia hapa ndani baada ya kuwa tumeshatangaza wageni. Nitawatangaza hawa wageni kisha tutaendelea.

Kwanza, tunao wageni kumi waliopo Jukwaa la Spika ambao wageni wangu kutoka Bunge la Zambia na wageni hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya Uchukuzi; kwanza ni Mheshimiwa Mubika Mubika ambaye ni Mwenyekiti, karibu sana; Mheshimiwa Joel Chibuye, Makamu Menyekiti; Mheshimiwa Sunday Chanda, Mjumbe; Mheshimiwa Charles Mulenga, Mjumbe; Mheshimiwa Lloyd Lubozha, Mjumbe; Mheshimiwa Francis Kapyanga, Mjumbe; Mheshimiwa Mutotwe Kafwaya, Mjumbe; Mheshimiwa  Benard Kanengo Mjumbe; Mheshimiwa Emmanuel Musonda, Mjumbe; na Ndugu Darius Kunda ambaye ni Katibu wa Kamati. Karibuni sana wageni wetu kutoka Zambia. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ambao pia wameingia baada ya wengine kuwa wametoa nafasi hapo juu, kwa hiyo hatukupata nafasi ya kuwatangaza mapema.

Yupo Ndugu Halfani Halfani ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi - *PURA*, yupo Mhandisi David Ngula, Mwenyekiti wa Bodi - *EWURA – CCC*, yupo Ndugu Fadhili Manongi, Mjumbe wa Bodi *EWURA*, yupo Ndugu Stella Lupimo, Kaimu Katibu Mtendaji wa *EWURA CCC*. Karibuni sana.

Wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambapo pia wamepata nafasi ya kuingia baada ya wengine kuwa wamepisha kwenye majukwaa yetu ya wageni. Tunao wageni watatu ambao ni wageni wangu kutoka Umoja wa Vijana, Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ambao ni Wakurugenzi na Maafisa kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati. Wote wasimame kwa pamoja. Haya, siwaoni wakisimama, nadhani bado hawajapata nafasi labda. Ama wamesimama! Wametambulishwa wakiwa huku, haya karibuni sana Bungeni. Pia

Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko anao wageni wake ambao ni wadau wa sekta ya nishati, wasimame kwa pamoja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 109 wa Mheshimiwa George Simbachawene ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na hawa ni viongozi wa Jumuiya ya Wazazi Umoja wa Wanawake Tanzania na Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Kata zote za Jimbo la Kibakwe Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, nao ni wanafunzi 100 na wanachama wa Umoja wa Vijana, Chama cha Mapinduzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Elimu, karibuni sana Bungeni wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo la wageni, jambo moja ambalo nataka kusisitiza, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu katika siku hizi mbili pamoja na cheo kingine, yeye ni Waziri wa Nishati. Kwa hiyo, atakuwa anasikiliza hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kiti chake pale kipindi hiki cha siku mbili asikae mtu isipokuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati. Kama kuna jambo la kwenda pale, utaenda na kuondoka ili asikilize hoja za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimezungumza nikiwa nimesimama ili ukimwona mwingine pale, mkumbushe hata kama sikuwa nimekaa mimi hapa ili Mheshimiwa Waziri aweze kusikiliza hoja za Wabunge zinazohusu Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza sasa uchangiaji. *(Kicheko)*

*(Hapa Waziri wa Maji alikuwa ameketi katika kiti kilicho karibu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji alienda pale kwa ajili ya hoja maalum, maana unajua Mheshimiwa Waziri wa Maji na Mheshimiwa Waziri wa Nishati wanashirikiana kwa karibu sana. Kwa hiyo, ilikuwa ni muhimu yeye kuwepo pale wakati wanasikiliza hoja za Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, maana nyingine zinahusu maeneo yake ya

maji ambapo wanatoa umeme. Kwa hiyo, ilikuwa ni muhimu sana kuwepo hapo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza uchangiaji na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, na Mheshimiwa George Natany Malima, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kutoa ushauri wangu kwenye Wizara ya Nishati. Kwanza Waheshimiwa Wabunge naomba tupitishe bajeti hii kwa sababu ukisikiiza yaliyosemwa yanatia matumaini. Kwa hiyo, tuipitishe na ni kielelezo kwamba Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Rais inafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo napenda kusisitiza umuhimu wa vyanzo vipya vya umeme mwingi kwa ajili ya ukuaji wa uchumi wetu. Naomba nirudie hilo, umeme mwingi, kwa hiyo siyo tu *energy mix*, Hapana, ni umeme mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahali ambapo tunaanzia mpango wetu wa maendeleo ambao unaisha mwakani, tulisema kufika mwakani 2025 pato letu ukiligawa kwa kila mtu kwa mwaka zifikie dola 3,000 - *GDP per capital.* Kwa hiyo, tunavyojadili yote haya kwenye haya mambo ya bajeti lazima tujipime tumefika wapi?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mipango yetu ilipangwa kwamba kufika mwakani tunapaswa kuwa tumepata *Megawatt* 5,000, kwa hiyo, *GDP per capital* hatujaifikia, *Megawatt* 5000 hatujafikia, lakini tunaelekea huko. Kufikia huko ni lazima uchumi wetu ukue kwa asilimia nane hadi 10%. Sasa vyanzo vipya ni hivi vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vyanzo vipya ni sehemu ya vyanzo vingine ambavyo vipo duniani na Mheshimiwa Waziri wa Nishati ameongelea nishati jadidifu *(renewable energies),* dunia yote mapambano ya tabianchi yanataka tuwekeze kwenye *renewable energies*. Sasa hivi vyanzo ni vingi sana, ni 10 vingine 20 lakini muhimu sana ni saba.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha kwanza ni *solar*, cha pili ni *wind,* cha tatu *geothermal*, cha nne *bio energies (biomass, biogas),* umeme wa maji *(hydro),* mawimbi ya baharini *(ocean tides and waves)* na cha saba ni *hydrogen.* Samahani nikitaka kuyaweka kwenye Kiswahili nitatumia muda mwingi kujaribu kutafsiri, lakini nadhani wengi wanaelewa *hydrogen* ni nini.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini vinakuwa muhimu sana? Wanasayansi wamepiga hesabu kwamba jua lina uwezo wa kutupatia umeme wa kiasi cha 173,000 *trillion watts*. Sasa ukisikia nasema *trillion watts* maana yake ni *Megawatts* milioni moja. Kwa hiyo, jua linaweza likatupatia umeme ambao ni zaidi ya 10,000 ya umeme ambao tunauhitaji; jua peke yake, dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, tukichukua upepo una uwezo wa kutupatia umeme ambao ikifika mwaka 2040 tutakuwa tuna uhitaji yaani ni zaidi ya *trillion watts* 36,000.

**SPIKA:** Profesa, ili usikike vizuri…

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Ndiyo.

**SPIKA:** Hicho kitabu ulichoshika ukishikie pembeni kidogo ili kile kisemeo kiwe mbele yako moja kwa moja.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, utaniongeza muda. Walibadili kilikuwa kirefu wakaweka kifupi, sasa naona nimesogea kwenye hiki kirefu. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Zima kile kimoja.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Hapana, acha viwe viwili, leo tunaenda na viwili.

Mheshimiwa Spika, hapo unanisikia vizuri! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Nakusikia vizuri sasa, unaweza kuendelea.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kwamba hiki ninachokiongea ni lazima tuwekee maanani kweli kweli, maana yake tunang'ang'ana na vyanzo vingi. Mimi nataka kuwathibitishia vyanzo vya uhakika.

Mheshimiwa Spika, yaani jua linavyopiga ardhini *square meter* moja unapata kama *bulb* nne au tano za umeme; ni *watts* 342. Sasa nataka kuonesha kwa nini Tanzania twende huko tusiache mengine. Nimechukua mfano wa India na China.

Mheshimiwa Spika, India na China tulikuwa pamoja miaka ya 1950 na 1960, umasikini wetu ulikuwa unafanana. Sasa hivi mwezi uliopita Machi mwaka huu ule uwezo wa kuzalisha umeme *(installed capacity)* wa India kutokana na vyanzo hivyo; sikiliza vizuri sana. *Solar* ni *Gigawatts* 82. Kwa hiyo, ukisikia nasema *Gigawatts,* wewe zidisha kwa 1,000 upate *Megawatts.*

Mheshimiwa Spika, upepo wana *Gigawatts* 46, hii *biomass* aliyokuwa anaongea, ni karibu *Gigawatts* 10. Narudia tena. *Gigawatts* zidisha mara 1,000 halafu ukisikia *Terawatts* zidisha mara 1,000,000. Kwa hiyo, sisi kama Taifa tunataka kuendelea lazima tuwekeze kwenye *solar, wind, biomass* na vingine.

Mheshimiwa Spika, Mfano mwingine, India imepanga kufikia mwaka 2030, umeme wa kutokana na jua na upepo utakuwa *Gigawatts* 500 *(Megawatts 500,000).* Mwaka 2023 China kwenye *solar* walikuwa na *Gigawatts 430.* Siyo kwamba wanapanga, hizo ni *installed capacities* na mwaka huu wakichukua jua na upepo wana *Gigawatts* 609.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa nitoe shukurani kwa *REA,* wameanza kuona umuhimu wa umeme wa jua na ninadhani mfano mzuri utakuwa Jimboni kwangu, watakuja kuweka kule kisiwani umeme wa jua. Kwa hiyo, nitakuwa nao kwa ukaribu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aina ya pili ni upepo. Upepo ambao unaweza kuzalisha umeme lazima *speed* yake iwe karibu mita nne kwa sekunde, yaani kilometa kwa saa ziwe ni kati ya 12 na 14. Ikiwa 50

mpaka 60 kama *speed* ya gari uzalishaji unakuwa ni mkubwa sana, ikiwa zaidi ya 90 inaharibu *turbines.*

Mheshimiwa Spika, sasa angalia mfano wa nchi nyingine na ndiyo tunapaswa kwenda huko. India wana umeme wa upepo *Gigawatts* karibu 43, kwa hiyo ni *Megawatts* 43,000. Wanataka ikifika mwaka 2030 wafikishe *Gigawatts* 170 na hii tutaongea kwenye mipango. Tusiende na hizi *Megawatts* ndogo ndogo, haziwezi kukimbiza uchumi sana.

Mheshimiwa Spika, nakuja China, kwenye upepo wana *Gigawatts* 440 na wanategemea ikifika mwaka 2030 upepo na jua uweze kuzalisha umeme wa *Gigawatts* 1,300 (1,300,000 *Megawatts)*. Kwa hiyo, siyo ajabu mkaenda kununua vitu India na China kwa sababu huu umeme wao ni wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba jua na upepo hauwezi kutoa umeme wa viwanda. India na China wanatuonesha hapa, mwaka 2050 China inategemea ifikishe umeme wa upepo *Gigawatts* 1,000 (*Megawatts* 1,000,000). Kwa upande wa Afrika na Watanzania tujifunze kwa wenzetu Wakenya, wao ndio wana umeme mwingi kwa bara zima la Afrika, wana *Megawatts* karibu 440 na ni kule *Lake Turkana* Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, aina nyingine niliyotaka kuongelea, nimechukua tatu tu, yaani jua, upepo na joto ardhi *(geothermal)*. Nyuzi yaani *temperature* ambazo zinahitajika kuzalisha *geothermal*, maji yale yawe yanachemka kwa kiwango siyo chini ya 50 to 100 *Degree Celsius.* Ni kama majimoto, lakini yanaongezeka kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa kufikia mwaka 2023 joto ardhi duniani *capacity* yake ilikuwa karibu *gigawatts* 17 (*Megawatts* karibu 17,000) na mfano mzuri kwetu sisi Afrika tunaenda kuuchukua Kenya. Kenya ni ya kwanza kwa bara la Afrika, Kenya ni ya sita duniani kwa umeme unaotokana na joto ardhi. Wanazo *Megawatts* za joto ardhi karibu 1,000 ni 988, lakini *potential* yaani uwezo uliopo kwenye Bonde na unazalishwa kwenye bonde ni kati ya *Megawatts* 5,000 na *Megawatts* 10,000 kwa Kenya.

Mheshimiwa Spika, sasa ukichukulia Bonde la Ufa la Kenya ukilinganisha na la Tanzania, sisi tuna Bonde la Ufa refu zaidi, lakini hicho siyo kigezo muhimu, muhimu ni ule upana *(thickness)*. Ili upate joto ardhi zuri ni lazima ule upana wa ardhi yako uwe chini ya kilometa mbili, ndiyo wanaweza wakachimba, wakafika chini na kutoa huo mvuke ambao utaendesha *turbines* na kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi umeme wa Kenya ukilinganisha na wa Tanzania, zamani tulikuwa tunawazidi, au tunalingana nao lakini wao kwa ujumla umeme wao sasa hivi wana *Megawatts* 3,300. Kwa hiyo, ni karibu na *Gigawatts* 3.3. Sasa ukilinganisha za Kenya ambaye ana uchumi mkubwa Afrika Mashariki *Gigawatts tatu*, linganisha na nilizowapatia za China na India.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Ethiopia. Wenyewe walianza kuzalisha jotoardhi mwaka 1998, lakini sasa hivi wana *Megawatts* kidogo tu 7.5.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania, kwa mipango mizuri tuliyoisikiliza, tulitengeneza ramani inayoonesha maeneo ambayo tunaweza tukavuna umeme wa jua kwa wingi sana na eneo lililokuwa linaongoza ni Shinyanga, sasa inabidi hiyo ramani ipitiwe kwa sababu ya tabianchi, tunahitaji *panels* zifanye kazi. Tunahitaji 15 – 35 *degree Celsius,* hiyo ndiyo *temperatures* za chini kabisa za *solar panel* kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza wataalamu wetu wa *TANESCO* na *REA* wapitie *solar map*, *wind map* hata ikiwemo ile ya Makambako, *speed* yake ya umeme tupitie halafu na *Singida*. *Geothermal Map,* nawaambia *geologists* wapitie tena ile ramani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kumalizia ni kwamba hivi vyanzo ambavyo tunavyo kama tunataka kufikia hiyo *GDP per capita* ya 3,000 *US Dollars* ni lazima tuwe na umeme wa zaidi ya *Megawatts* 10,000 ambayo ni *Gigawatts* moja na tutaipata kutoka vyanzo hivyo nilivyovitaja ambavyo ni *solar, wind* na *geothermal*, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa George Natany Malima, na Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba nami nianze kwa kusema kwamba naunga mkono Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Kipekee nianze kwa kutambua na kupongeza kazi nzuri ambayo inafanywa na Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake wote.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa hiyo pia naomba kupongeza na kutambua Hotuba nzuri ya Mwenyekiti wangu wa Kamati na kwamba yale yote yaliyosemwa na Kamati, nayaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wizara ya Nishati, kwanza kwa ubunifu waliokujanao kwenye Wiki ya Nishati. Naweza kusema ile Wiki ya Nishati imemaliza hotuba yangu kama asilimia 80 na itakuwa hivyo karibu kwa Wabunge wote kwa sababu tulipata nafasi ya kutosha ya ku-*interact* na Mameneja wetu, lakini tulipata majibu mengine sahihi kwenye Wiki ya Nishati. Kwa hiyo, sasa ninachotaka kusema hapa, kwa kweli tofauti sana na Mwalimu wangu Profesa Muhongo, yeye alikuwa anafundisha, lakini mimi kidogo nitazungumza shida za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri amesema umeme umeongezeka kwa takribani asilimia 14 na hali ya umeme sasa imetulia. Tunaipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa ambayo imefanya na niipongeze pia Serikali kwa kujibu kiu ya wananchi. Wananchi walikuwa wanalalamika sana na maeneo mengi sasa hivi malamiko yamepungua. Kwa hiyo, nina uhakika kwamba hali hii itaendelea kuwa hivyo hata baada ya hizi mvua nyingi ambazo zinaendelea sasa hivi kwisha.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, amesema karibu wanakamilisha usambazaji wa umeme kwenye vijiji vyote Tanzania. Napongeza sana juhudi hizo. Kipekee mimi nianze kwenye Jimbo langu kwamba ninaishukuru sana Serikali. Sasa Jimbo

langu la Geita Mjini lina vijiji 15 na mitaa 65, karibu katika kila kijiji, vijiji vyote umeme umefika, na pia mitaa yote kazi inaendelea. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa hatua iliyokuja ya kupeleka umeme kwenye vitongoji. Sasa hapa nina maoni. Kule kwenye vijiji ambako tumepeleka umeme tumepeleka takribani watu wasiozidi 10 au 15. Kwa hiyo, unakuta katika kijiji kile kile ambacho umeme upo, wanaotaka umeme ni watu karibu 50, umeme umefikia watu 10 mpaka 15. Taasisi nyingi za eneo lile unakuta umeme haujafika, lakini tayari hesabu ya Serikali ni kwamba umeme umefika kwenye kila Kijiji.

Mheshimiwa Spika, kilio cha wananchi wa eneo lile ni kwamba umeme umefikia watu wachache. Sasa ombi langu ni kwamba mpango wa *diversification* ambao ulizungumzwa na Waziri, ungewekewa mkakati maalum ili wote wanaohitaji umeme kwenye vijiji ambavyo tumeshafikisha umeme wa *REA* waweze kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi namna ilivyo, umeme huu unatuchonganisha sana kwa sababu inabidi Diwani na Mwenyekiti wa Kijiji wawe wa mwisho, maana hao ni rahisi kumwambia Mkandarasi wapelekee kuliko wananchi kukosa halafu akapata Diwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maeneo mengi umeme umeenda. Walioomba ni wengi kuliko uwezo wa mkandarasi. Sasa naiomba Serikali, wakati tunafikiria kwenda kwenye vitongoji, Mheshimiwa Waziri na hapa nilitaka niweke kumbukumbu vizuri. Vitongoji vingi wananchi wako *scattered* na nimeona kwa *experience* ya kwenye vijiji nguzo zinazaoenda ni chache, kwa hiyo, matokeo yake umeme unakuwa *concentrated* kwenye *center* peke yake.

Mheshimiwa Spika, sasa sina uhakika na *study* iliyofanyika kwa sababu kwenye vitongoji vingi utakuta wanaotaka umeme wako zaidi ya mita 200 au 400 kutoka kwenye mji mwingine. Sasa hawa wote wanahitaji kupata haki hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa vizuri kabisa na Kamati, tulipofanya ziara tumegundua kwamba sehemu nyingi ambazo umeme wa *REA* umefika na baada ya *REA* kuondoka, wanapoanza kuomba *TANESCO* wanakutana na bei kubwa kwa sababu mkandarasi wa REA ameshaondoka, ambayo siyo tena shilingi 27,000 na kwa sababu ni bei ghali, wanakijiji wengi hawawezi kulipia shilingi 300,000.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba uje mpango ambao utaendeleza, siyo tu ionekane hawa watu 10 ndio waliopata hiyo bahati, hata baada ya wale wakandarasi wa *REA* kuondoka, basi uje mpango mahususi ambao utawawezesha wananchi katika maeneo yale kuendelea kupata umeme wa shilingi 27,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuongea kwenye eneo hili, tumekuwa na mpango wa kusambaza mitungi ya gesi. Tunakushukuru sana tulipata bahati ya kwenda India, tukafanya ziara kubwa na ya kutosha kama Kamati, tukajifunza namna ambavyo zoezi hili limeratibiwa na linafanyika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mitungi ambayo tunaisambaza kama kuchochea wananchi wengi kwenda kwenye nishati safi ni mitungi midogo ya kilo sita. Kwenye familia zetu huko vijijini, watu wachache ni watano. Mitungi hii inaweza kutumika kwa wiki mbili au wiki moja. Sasa shida iko wapi? Moja, nadhani sasa Wizara inatakiwa kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba upatikanaji wa hii gesi hasa kwenye vijiji unaratibiwa vizuri ipatikane kwa wingi ili kusudi mtu asifuate mtungi wa gesi kwa gharama kubwa kuliko gesi yenyewe anayoifuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule India tulijifunza nini? Kwanza walitambua watu ambao wanataka kuwapa punguzo la mitungi ya gesi na hawa ni karibu ya 50% ya *population* ya India. Kwa hiyo, Serikali ilichokifanya, iliwatambua na baada ya kuwatambua ikawasajili, ilipowasajili ikapeleka ile mitungi ya kati ya kilo 15.

Mheshimiwa Spika, ile mitungi ya kilo 15, hao watu waliopewa waliposajiliwa wamewekwa kwenye mfumo. Wale wasambazaji wote

wamesajiliwa na wamepewa namba na wale watumiaji wamesajiliwa. Kwa hiyo, kuna *token* ambayo inamwendea mtumiaji kila mwezi ambayo hii *token* ni punguzo la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yake ni nini? Kwenye mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba wanakwenda kwenye *energy* safi, wametengeneza *token* ambayo Serikali ime-*subsidize*. Kwa hiyo, mtungi huo hauwi tena na gharama kubwa, unakuwa na gharama ndogo kwa sababu huyu mwananchi unapoisha akipeleka ile *token* huyu muuzaji wa gesi moja kwa moja anaweza kumpa gesi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, sasa hili limewezesha asilimia tatu peke yake ya *population* ya watu wa India ambao ndio bado wanachanganya aina mbalimbali za nishati, lakini *the rest* wote wanatumia gesi safi kwa ajili ya matumizi ya majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili la usambazaji likisimamiwa vizuri, kama tunalenga kuhakikisha kwamba tunapunguza matumizi ya kuni, mkaa na uharibifu wa mazingira, ni lazima Serikali ifahamu kwamba inatakiwa kutengeneza mpango wa kudumu kama ulivyo mpango wa *TASAF* na *REA* ambao utafanya wananchi waliopo kijijini waipate hii nishati kwa ukaribu na kwa gharama nafuu. Wakati huo huo wasambazaji wahakikishe kwamba wana soko lao la uhakika. Hapo ndipo jambo litaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, tulipofanya ziara Dar es Salaam, tukatembelea vituo vingi ambavyo vinauza *compressed natural gas.* Kwanza naipongeza Serikali na Wizara kwa hatua hiyo ambayo imefikiwa. Hata hivyo, jambo tulilojifunza ni kwamba, vituo ni vichache, hamasa ni kubwa. Kwa hiyo, matokeo yake ni nini? Matokeo yake ni kwamba foleni ya kusubiri kuwekewa gesi ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda kwenye kituo kimoja tukakuta gari ya shule inasubiri kuwekewa gesi. Sisi tumefika pale takribani saa saba tukakuta gari lile limefika pale saa 12.00 linasubiri kuwekewa gesi na

foleni bado ni ndefu. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba eneo hili tunatakiwa tuongeze juhudi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunajielekeza katika kuhakikisha kwamba Serikali inakuwa mfano, ushauri wangu ni kwamba pengine tulegeze masharti ya uwekezaji kwenye eneo hili ili tuhamasishe zaidi wawekezaji binafsi waje waungane na hawa waliopo, kama tulivyokwenda kwenye viwanda mbalimbali na tukakuta vinatumia *natural gas* na viwanda hivi vinasema vinaokoa gharama kubwa sana ya umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo hili lifanyike kwa *speed* kubwa ili kuwafanya wananchi ambao wangetamani kutumia gesi kwenye gari zao, kwa sababu kwa kweli kwa foleni ya Dar es Salaam, mtu anayefanya biashara ya *taxi* au *UBA*, au usafirishaji kama anatumia *diesel* au *petrol* huyu ni lazima anakula hasara, lakini wale wanaotumia gesi, hata ukizungumza nao kwenye foleni, yeye amewasha *AC*, anapiga mziki na hana wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maoni yangu ni kwamba, naomba Wizara kufanya mkakati huu kuwa mkakati kabambe ili kuokoa mazingira na kuongeza matumizi ya gesi. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Natany Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, ajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia afya sote ya kuendelea kuwepo Bungeni tukihudumu.

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu, na kwa kweli matunda yake tunaendelea kuyaona.

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya

katika nchi yetu hasa ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na nishati ya kutosha. Vilevile namshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Judith Kapinga ambaye naye anasaidia kazi na wanaendelea vizuri. Pia, naishukuru timu nzima ya Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuona nchi yoyote ambayo inaendelea kwa kasi, moja ya *factor* ambazo utaziona pale ni uhakika wa umeme katika nchi hiyo. Nadhani hilo ndilo jambo ambalo nasi tunatakiwa kujikita sana. Nchi yetu inahitaji kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaongozwa na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeonesha nia ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba tatizo la umeme katika nchi yetu linatatulika. Ukitaka kujua hilo, utaona jinsi ambavyo miradi mingi ya kuzalisha umeme inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano hapa umetolewa wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere ambalo linatarajia kutoa *Megawatt* 2115. Vilevile kuna ile *Kinyerezi I* ambayo tunategemea itumie *natural gas* ambayo itatoa *Megawatt* 185, lakini ule Mto Kagera kule Rusumo tunategemea kutoa *Megawatt* 85 na miradi mingine ambayo inaendelea mahali pale.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho ningechukua fursa kuwashauri Wizara ya Nishati ni kuendelea kutafuta vyanzo vipya. Vyanzo vilivyopo bado havitoshi. Sisi kama nchi, tunatarajia tuwe na umeme wa kutosha, lakini pia tupate fursa ya kuuza katika nchi Jirani. Kwa namna hiyo tutahakikisha uchumi wetu utakuwa unaenda mbele.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini ambao unatekelezwa na *REA*. Mradi huu umekuwa mzuri sana, na kwa kweli ukienda vijijini, leo vile vijiji ambavyo tayari vina umeme, hata kama katika lile eneo dogo lakini vijana tayari wamejiajiri. Vijana wamejiajiri wanafanya biashara, wameanzisha viwanda vidogo vidogo na kwa kufanya hivyo wamekuza pato la familia zao na Pato la Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo, jambo hili ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, shida kubwa iliyoko sasa kwenye *REA* ni kasi ndogo ya kutekeleza mradi huu. Wamesema wengine kwamba ukienda kwenye kijiji utakuta kuna nguzo 20, 25. Kwa hiyo ni watu wachache ambao wamefikiwa na umeme huu, lakini asilimia kubwa ya wananchi wa vijijini kwenye kijiji husika utakuta hawana umeme. Kwa hiyo, hilo limekuwa tatizo na kumekuwa na kelele nyingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa upande wa vitongoji nilikuwa nafikiri tusianze kwenda kwenye vitongoji kwanza, tumalizie zile nyumba za kwenye kijiji. Zile nyumba zinazotakiwa kupata umeme katika Kijiji, zipate umeme ndipo twende kwenye vitongoji vyake. Hiyo itatusaidia sana kuliko kuruka kwenda kwenye kitongoji, wakati huku kwenye vijiji kuna watu kumi tu ndio wenye umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni muhimu kwa sababu umeme ukipatikana kwa maeneo yote, hata kelele za kuilaumu Serikali zitapungua sana. Kwa hiyo, nilikuwa nawashauri watu wa *REA* waongeze kasi ya utekelezaji wa mradi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kuwashukuru Wizara ya Nishati katika Jimbo langu la Mpwapwa ambapo bado vijiji vitatu na mkandarasi yuko *site*. Vijiji vyote vimepata umeme isipokuwa shida ni ile kasi ya vile vijiji vitatu, mkandarasi haendi kwa kasi inayotakiwa. Hata hivyo ninaamini Wizara itaweka msukumo ili hivyo vijiji vitatu vilivyobaki viweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni huduma za *TANESCO.* Miaka ya nyuma kulikuwa na huduma ambazo hazikuwa nzuri na hivyo zilisababisha wananchi kuilaumu sana Serikali, lakini nawapongeza kwamba leo wamekuja na *solution.* Sasa wanatumia mifumo kwa ajili ya mawasiliano, na kuna *call centers.* Mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma nilipata fursa ya kutembelea hii miradi ninayoisema ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, pia tumetembelea Makao Makuu ya *TANESCO* na tumeona mifumo ambayo imewekwa, kuna *call centers* na mawasiliano yako vizuri na wateja. Zamani ilikuwa tukipata shida ya umeme tunaweza kusafiri kutoka nyumbani mpaka kwenye Ofisi ya

*TANESCO* ndipo upate huduma. Leo unapiga simu mara moja na tatizo linatatulika ukiwa nyumbani kwako.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hili nawapongeza, ni hatua kubwa, lakini bado tunataka kuendelea kuboresha huduma kwa wateja, hii itatusaidia sana. Kwanza shirika lenyewe litapata fedha kwa wingi kwa sababu litatoa huduma kwa haraka na watakusanya mapato kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni uchakavu wa miundombinu. Kule Mpwapwa tumekuwa na shida ya kukatikakatika umeme, nadhani ni maeneo mengi katika nchi hii. Umeme unakatikakatika sana katika Wilaya yetu ya Mpwapwa kwa sababu ile miundombinu inayosafirisha umeme kutoka kwenye kituo chetu cha zuzu imechakaa na kwa hiyo, unakuta kila siku umeme unakatika bila taarifa na mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, napenda sana Wizara ya Nishati iangalie jambo hili sana, tunahitaji umeme wa uhakika. Ili uweze kufanya shughuli zako za kiuchumi lazima umeme uwe wa uhakika, uwe na uhakika kwamba leo unataka kufanya kazi masaa 12, basi ufanye kazi masaa 12, lakini unapanga masaa 12 umeme unakatika, unafanya kazi masaa mawili. Kwa kufanya hivyo, hatuwezi kukua kiuchumi, tutaendelea kudidimia, tutakuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji umeme kuliko kitu kingine chochote. Kwa hiyo, tatizo la kukatikakatika umeme bila sababu za msingi, naomba Wizara ishughulike nalo sana, kwa sababu vinginevyo hatuwezi kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, ajiandae.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, na pia nampongeza Naibu Waziri Judith Kapinga kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya Katika Wizara hii. Kwa moyo wangu wa dhati nampongeza Spika wangu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kazi kubwa anayoifanya na jinsi anavyoliongoza Bunge letu kwa weledi. Mwenyezi Mungu akujalie Spika wetu.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza hotuba aliyotoa Waziri wa Nishati na mipango yao. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu, mipango yenu iende ikakamilike ili Watanzania waweze kufurahia huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa kuhakikisha wanaleta mtandao wa umeme katika vijiji vyetu. Hata hivyo, kwa upande wa Jimbo langu la Mtwara Vijijini, jumla ya vijiji ambavyo vilitakiwa kuwashwa umeme ni vijiji 24; ambavyo vimewashwa ni vijiji 18 na ambavyo bado havijawashwa ni vijiji sita. Ni hatua kubwa sana. Nawashukuru na ninampongeza Naibu Waziri Mkuu, naipongeza Serikali, na pia nawapongeza wakandarasi ambao wanafanya kazi katika jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Mkandarasi, mpaka kufikia Mei, 25 vijiji vyote vitakuwa vimekamilika katika Jimbo la Mtwara Vijijini. Ninasisitiza na ninawaombea vijiji hivyo vilivyobaki viende vikakamilike ili wananchi wangu waweze kufurahia huduma hii muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi katika vijiji umeme umewashwa. Hata hivyo, changamoto iliyopo ni zile kilometa mbili za kuingia ndani bado hazijawafikia wananchi. Katika vitongoji bado umeme haujasambaa vizuri. Kwa hiyo, naomba zile sentimeta mbili zifuatiliwe vizuri ili umeme uweze kusambaa vizuri katika vitongoji ambavyo bado havijawaka umeme.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la umeme katika Kijiji cha Msimbati na Madimba. Katika Bunge la Bajeti lililopita nilizungumzia sehemu ambayo inatoka gesi asilia ya Msimbati na Madimba, umeme unawaka maeneo ya Barazani tu lakini maeneo mengi ya vijiji na vitongoji vyake, maeneo mengi niliorodhesha mpaka vijiji, hakuna umeme, haujafika, sehemu ambayo inatoka gesi, ninasikitika sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali mliangalie suala hili kwa upana wake. Niwaombe Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri wake mwende mkaliangalie suala hili katika Kijiji cha Msimbati na Kijiji cha Madimba, bado tuna changamoto ya umeme. Sehemu ambayo gesi ipo, sehemu ambayo gesi inachakatwa umeme hakuna. Naomba mliangalie suala hili kwa upana wake katika Kijiji cha Msimbati na Madimba.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Msimbati na Madimba ndiko inakotoka gesi asilia. Hata hivyo kwa masikitiko makubwa sehemu ambayo kuna mradi mkubwa ambao Serikali imewekeza bado wananchi wale hawanufaiki na rasilimali hizi ambazo zipo katika vijiji vyao.

Mheshimwia Spika, wananchi wa Kijiji cha Msimbati na Madimba bado wana changamoto kubwa sana. Ukiangalia yale maeneo ambayo yamezunguka mradi mkubwa wa gesi asilia bado kuna changamoto kubwa mno. Hii *CSR* bado ni ndogo na hainufaishi vijiji hivi vya Msimbati na Madimba. Naomba hawa watu wa *TPDC* waliangalie hili. Hii *CSR* inayotoka pale ni ndogo…

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia, kuna taarifa kutoka kwa jirani yako hapo Mheshimiwa Stella Fiyao.

**TAARIFA**

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba, *issue* ya *CSR*

imekuwa ni changamoto kubwa kwenye maeneo mengi yanayozungukwa na miradi mikubwa. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Miradi mikubwa ya umeme au miradi yote?

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ni miradi yote ikiwemo ya umeme. Hata kwenye Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere bado kuna changamoto kubwa sana ya *CSR*.

**SPIKA:** Mheshimiwa umeulizwa swali na umeshalijibu. Mheshimiwa Shamsia, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaipokea taarifa hii kwa umuhimu wake mkubwa. Inaumiza, kwa sababu wananchi hawa wa Msimbati na Madimba wametupwa. Wana miradi mikubwa ambayo imewazunguka katika kijiji chao lakini hawanufaiki na chochote.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wangu wa dhati namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, nilikwenda ofisini kwake nikamlilia shida iliyopo katika vijiji hivi viwili vya Msimbati na Madimba. Nashukuru Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Dkt. Doto alikuja. Mheshimiwa Dkt. Doto, Mwenyezi Mungu akujalie na akuweke uishi maisha marefu na afya nzuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Doto alikuja kwenye Jimbo langu la Mtwara Vijijini akajionea hali halisi iliyokuwepo kwenye jimbo langu. Yeye ndiye mtu wa kwanza aliyekwenda kuweka alama kwenye vijiji hivi. Baada ya kuzungumza ndipo tukaiona hiyo *CSR* inatoka na kwa mara ya kwanza sasa kituo cha afya kinajengwa ilhali mradi huu katika Jimbo la Mtwara Vijijini upo kwa muda mrefu, lakini hakuna chochote ambacho kinanufaisha vijiji hivi viwili vya Msimbati na Madimba. Ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, wale wananchi wako katika mazingira duni na wanaona Serikali imewekeza mradi mkubwa pale. Tunaona kwa wenzetu wanakochimba madini wananufaika na miradi yao, lakini sisi kule hakuna kinachoendelea. Inatia uchungu na inatia hasira. Sasa

hivi Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko amekuja kule kuweka alama ndipo kituo cha afya kimeanza kujengwa. Mheshimiwa Dkt. Doto Mwenyezi Mungu akujalie sana.

Mheshimiwa Spika, katika Vijiji hivi vya Madimba na Msimbati wanakuja wanasema wanataka watuwekee taa za barabarani. Hiyo barabara ya kutuwekea taa za barabarani iko wapi? Sehemu ambayo inatoka gesi asilia barabara ni mbovu na hazipitiki. Ukienda hali yake inatia uchungu. Siku moja uje utembelee jimbo langu ujionee hali halisi iliyopo huko inakotoka gesi. Hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, yaani ukiangalia maisha ya wananchi walioko kule ni duni. Sasa hivi ndiyo Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko amekuja kutuwekea kituo cha afya. Baada ya kuja yeye, sijui hiyo *CSR* ilikuwa inakwenda wapi? Pia hiyo *CSR* inayotoka ni ndogo. Watu wa *TPDC* mliangalie hili…

**MHE HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mtenga.

**TAARIFA**

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, eneo linalozungumzwa kutoka Mtwara Mjini mpaka unaelekea Msimbati lina kilometa 35. Pia tunapozungumza mradi wa gesi wa mabilioni ya shilingi, hasa tunazingatia miundombinu ya barabara. Leo likitokea tatizo lolote mfano moto, gari la *fire* haliwezi kufika Msimbati kwa wakati na mradi ule tunaweza tukaupoteza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili. Hiyo ndiyo hali halisi iliyopo katika Kijiji cha Madimba na Msimbati, kumetupwa kabisa. Serikali imewekeza miradi mikubwa kule *(billions of monies)* lakini hakuna kinachoendelea. Inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, nije kuzungumzia suala la Mtambo wa *Turbine* na hapa nimshukuru Naibu Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa kweli amekuwa mkombozi wa watu wa kusini sasa acha nimshukuru, nimpe maua yake tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Mtwara tuna changamoto kubwa sana ya umeme changamoto ambayo imetusumbua kwa muda mrefu lakini Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu tulikaa naye kikao tukamweleza changamoto iliyopo katika Mkoa wetu changamoto kubwa ya umeme, kwa usikivu wake Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko akasema Wabunge wa Mtwara nimewasikia kilio chenu nitawaleteeni mtambo kwa ajili ya kupunguza tatizo la umeme katika Mkoa wa Mtwara na Lindi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante katika Mkoa wa Mtwara na Lindi tunashukuru mtambo ule umefika katika Mkoa wetu wa Mtwara na umeanza kufanya kazi ili kuhakikisha wanamaliza tatizo la umeme katika Mkoa wa Mtwara na Lindi kwa hili tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu lakini ninachokuomba na ninachoshauri endelea kufuatilia mtambo ili huduma ya umeme katika Mkoa wa Mtwara na Lindi uweze kukaa sawasawa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia kuwepo hapa tukiwa na afya njema. Nimpongeze Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko na Waziri wa Nishati. Nimpongeze Katibu Mkuu, Ndugu Mramba; Naibu Katibu Mkuu,

Bwana Matarajio; na Watendaji wengine wa *REA* na *TPDC,* Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza hii Wizara imepata wazoefu Katibu Mkuu Mramba alianzia kuwa Meneja wa *TANESCO* mpaka sasa hivi amekuwa ni Katibu Mkuu. Vilevile Bwana Matarajio alikuwa *TPDC* na sasa hivi anaonyesha atatupa matarajio makubwa sana kwa uzoefu alioupata katika *TPDC* ili kutaka kutuletea maendeleo ya umeme Tanzania pamoja na gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kampeni yake kubwa ya kumtua mwanamke kuni, kwa kweli wanawake kwa niaba yao nasema Mwenyezi Mungu ambariki sana. Wanawake kwa muda mrefu wanahangaika kutafuta kuni maporini, lakini je utakapoendelea kukata kuni mwisho wake ni nini? Ni uharibifu wa mazingira na tutaifanya nchi iingie katika ukame, hivyo Mwenyezi Mungu azidi kumzidisha kumpa maisha marefu na afya njema, tushirikiane naye ili tuhakikishe hii kampeni ya kumtua mwanamke kuni inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tuliyokuwa nayo zaidi ya 95% Tanzania iko katika umeme na haya ni maendeleo. Kuwa na umeme ni maendeleo kwa vile mahitaji ya dunia ya sasa hivi ni teknolojia ambayo inakwenda na umeme. Ukitaka maji huwezi kuanza kufua maji bila umeme, huwezi kuendesha *petrol station* bila umeme, huwezi kuendesha shule bila umeme, huwezi kuendesha hata Bunge bila umeme. Hivyo kwa 95% hata nchi za jirani wanaona kama kwa kweli Tanzania tumefanya kazi kubwa sana ya kupeleka umeme mpaka vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Liwale Vijijini huko Mpigamiti wote unakuta kuna umeme, kwa kweli haya ni mabadiliko makubwa na maendeleo makubwa ambayo tunayatarajia. Hata hivyo, kuna changamoto, tumepeleka umeme mwingi vijijini huo wa *REA* na wa kawaida, changamoto ya kwanza miundombinu mibovu, hasa waya za umeme nyingi zimeshaoza, zimeshakuwa hazifai, tuna imani kuwa katika mabadiliko haya yanayokwenda *speed,* kinachotakiwa ni

kuhakikisha kwamba mfumo wowote ule ambao umewekwa ufanye kazi na uwe wa kisasa hii itaondoa changamoto ya kuzimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo maana yake nini? Tumeleta mitambo ya kisasa, waya mbovu, hivyo zinakuwa *overloaded,* ndio maana inalipukalipuka na kusababisha giza. La pili, baadhi ya matumizi ya kutumia hasa hii miti, miti mingi na mvua kama hivi inaoza na kuna mchwa, hivyo inahitajika sasa hivi tubadilishe kutoka matumizi ya miti kwenda katika zege. Niwapongeze sana kwa vile wameliweka katika mojawapo ya hoja itakayoenda nayo twende kwa *speed* ili tuweze kubadilisha ili angalau tusizidi kuingia gharama ambazo zingeweza kurekebishika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la miradi ambayo wanaizungumzia sana wenzetu. Tunalalamika na ni kweli hii nchi ina keki na hii keki lazima iliwe na watu wote. Tuna miradi mikubwa ambayo unaona ya gesi ambayo inatoka katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani; Mradi wa Songas Kilwa, Mradi wa Madimba na miradi mingine ambayo imewekwa Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha katika mgao wa *corporate social responsibility* hata Mtwara haikuwekwa kabisa, utashangaa miradi ya Tanga – Hoima lakini wamepewa wao tu, Mikoa ya Lindi na Mtwara haimo, maana yake nini? Hii inatufanya Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani ionekane ni mikoa maskini wakati kuna uwezo mkubwa kuivusha hii mikoa ikawa mikoa ya kitajiri. Tumeambiwa hii gesi ya *LNG* itatoka Lindi Mungu akijalia, lakini je, Lindi inafaidika nini? Kilwa inafaidika nini? Hakuna miradi yoyote, nitaongelea maeneo machache, mradi umepelekwa Tanga, mradi umepelekwa Dodoma, miradi mingine sitaki kuizungumzia, lakini Mtwara haimo katika mradi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajiuliza, ndio unakuta watu wa Mtwara wanataka wanufaike na ule mradi hata wa kuwajengea mahospitali, kuwainua vijana kiuchumi, lakini miradi ile haikupelekwa kule imepelekwa maeneo mengine ambayo kila siku wananufaika. Kuna muda niliwahi kuuliza Miradi ya *TANAPA* ilikuwa haiendi Lindi na Mtwara wanasema ninyi hamko katika ujirani mwema, sasa kwa nini miradi ya kule inapelekwa maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia miradi katika maeneo ya uchimbaji wa madini, haipelekwi Lindi na Mtwara wakasema zamani, kwa vile Lindi na Mtwara hamkuwa katika hiyo sekta. Sasa tunaomba tafadhali kama ni keki hawa wanaopanga mipango wasilete ubaguzi, itatufanya tuone kama kuna mikoa ya kunufaika zaidi na kuna mikoa inaachwa nyuma na inaonekana kama mikoa ya kimaskini. Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani mpaka Morogoro siyo mikoa maskini, tunahitaji sasa hivi wakakae tena, warekebishe hii hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii miradi ya *corporate social responsibility* ikatengenezwe tena upya na wafanye tathmini yake, matokeo yake hii itatugawa kwa kuonekana kwamba imepelekwa mingi katika maeneo ambayo hawana masuala haya ya gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia mabadiliko ya tabianchi na athari itakayoifanya Wizara ya Nishati na Madini kuingia katika athari kubwa sana. Tunataka Wizara nne zishirikiane, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Madini na Wizara ya Mazingira. Mimi ni mwana mazingira na napenda sana kufuatilia mabadiliko ya tabianchi kwa ukamilifu na Mheshimiwa Rais kama mdau namba moja katika mabadiliko ya tabianchi na hii nitaizungumzia kwa mapana. Bunge linaendeshwa kwa Mabaraza yake, Madiwani wanaendeshwa kwa Mabaraza yao, lakini vilevile Rais anakwenda kwa Mabaraza yake na Spika katika Mikutano yake ya *IPU* anakwenda kwa Mabaraza yao, nini maana yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anapokwenda katika mikutano ya mabadiliko ya tabianchi anakwenda na *delegation* haendi kama anakawenda kuzurura, anakwenda kule kufuata sheria inasema nini na masuala ya mikataba mbalimbali ya kimataifa. Kama Rais anakwenda kuhudhuria lakini bado kuna wataalam wanakwenda, lakini hatuna ripoti za mabadiliko ya tabianchi ambazo zinaweza zikatusaidia.

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Mhongo kuwa tunataka vyanzo hivi viendelee, lakini kama vyanzo hivi havisimamiwi nchi itaingia katika *disaster* kubwa sana. Kwa mfano, nataka nizungumzie kuna suala la *adaptation* ya mabadiliko ya tabianchi

inasema una-*adapt* mito kwenda katika Bahari, *adaptation of the rivers to the sea*, je, tumeisimamia hiyo *adaptation*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo unaiona Rufiji imeingia katika gharika ya maji *(floods)* kwa nini imeingia katika gharika? Imechafuliwa mito huko juu wafugaji wamechukua mito wakulima wame *bypass* mito imeingia katika mashamba yao matokeo yake maji yakawa *blocked*. Baada ya kuwa yame-*block* maeneo ya Rufiji hasa katika Daraja la Mkapa maji yanasambazwa kwa wanavijiji ambao wanaathirika na wanakuwa maskini kwa ajili gani? Hatukusimamia kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukajifunze wenzetu India walikuwa katika mabadiliko, hawakusimamia mabadiliko ya tabianchi, ilikuwa kila siku unasikia milima mito ya *Ganges* na mito mbalimbali, watu wanakufa kwa sababu gani? Hatukusimamia. Siyo hivyo tu tunaipeleka hii hali siyo katika Wizara hii peke yake, leo Wizara ya Ujenzi ikishirikiana na Wizara itajua madaraja yao yote yanafanya kazi na je, yale madaraja hayana mchanga. Nilizungumza Bunge lililopita, nimepita Rufiji tuta limejaa, ina maana maji yakitoka huko hayawezi kupita pale, hivyo yatahama yatakwenda Muhoro, yatakwenda Kibiti, hivyo wale wenzetu watakuwa katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii siyo kwa ajili ya Mto Rufiji peke yake, nenda Dar es Salaam, pale Magomeni watu wameuharibu ule mto. Baada ya kuuharibu ule mto maji yanaingia katika Mradi wa Mwendokasi, nchi imeingia katika gharika, mwendokasi haifanyi kazi tena, majengo yameshakufa pale, tunatafuta tena mindombinu mingine ya kuirekebisha, lakini je, wanaokwenda kwenye mikutano hii ya mabadiliko ya tabianchi wanatuletea ripoti? Mheshimiwa Rais anakwenda katika mabadiliko ya tabia nchi na mikutano yake, hatuna ripoti tunayopata ndani ya Bunge. Matokeo yake, tunajikuta maazimio na ajenda mbalimbali ambazo zinapitishwa katika Umoja wa Mataifa haziji chini na kama haziji kwetu sisi tumekaa hatujui kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoomba, wewe ni kiongozi mzuri na unakwenda unaona unayoyaona, tunataka ajenda zote

zinazopitishwa na maazimio yapitishwe kwa wakati, siyo leo. Ajenda ya mwaka 2012 ndio inakuja kupitishwa hapa, ina maana tumepitwa na wakati, hii ni Tanzania siyo kisiwa, tunahitaji maendeleo ambayo yataendana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo wakae na Wizara ya Nishati wahakikishe wanaolima kuanzia Morogoro kule kote, kilimo chao hakileti uharibifu wa mazingira. Wafugaji waliokimbilia kwenye mito wanakata miti na wanafanya vitu mbalimbali, vilevile waangaliwe je, haitaleta mazingira mabaya ili kufanya Wizara hii ya Nishati na Madini ambayo tunategemea Mradi mkubwa wa Mwalimu Nyerere na mradi ule ambao hautaathirika na mabadiliko ya tabianchi waufanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, nina imani sana na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kwa hili ninalolizungumzia tulifanyie kazi ili angalau pale mito yote ambayo inataka kumwaga maji baharini, narudia tena mito yote ambayo inataka kumwaga maji baharini inazibuliwa na hii itatusaidia baadhi ya Wizara nyingine zisiathirike na haya. Tunaiona leo Magomeni tunakuja Mbezi, Mto Mbezi ule umezibwa nyumba zote za *NSSF* zimeingia katika maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30, malizia Mheshimiwa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na ninachoomba tu kuwa ushirikiano wa Wizara wa mabadiliko ya tabianchi ni mzuri na utasaidia kutunza vyanzo ambavyo vitalisaidia Bwawa la Mwalimu Nyerere hata Bwawa la Mtera lisipoteze asili yake na liweze kufanya kazi na kuleta uchumi wa kinchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema ahsante na Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, kwa muda uliobaki hataweza kuchangia Mbunge mwingine kwa sababu muda wake utakuwa umebana. Dkt. Florence George Samizi.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Hotuba ya Wizara hii muhimu sana katika ustawi wa wananchi wetu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya katika nchi hii kwa kuwaondoa wananchi katika giza na kuwapeleka katika mwanga. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma na wa Muhambwe tunampongeza Rais kwa sababu ni yeye mwenyewe alifika Kigoma kwenda kuzima majenereta na kutuunganisha kwenye Gridi ya Taifa ili tuweze kupata umeme wa uhakika lakini umeme wa bei nafuu pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayofanya katika wizara hii ya kuendelea kutuletea umeme. Nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Judith Kapinga kwa kazi nzuri anayoifanya tunamwona jinsi gani anapambana kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwapongeza watendaji wote, Katibu Mkuu *Engineer* Mramba, lakini *Engineer* Gisima na Watendaji wote walioko kwenye Taasisi za Wizara hii ya Nishati kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi kuhakikisha kwamba wananchi wanapata nishati safi ya umeme kwa ajili ya ustawi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuipongeza Wizara hii ya Nishati kwa jinsi ambavyo imefanya kazi katika Jimbo langu la Muhambwe. Mimi ni mnufaika wa kupelekewa umeme katika vijiji, miaka mitatu ya kishindo ya Rais Samia Suluhu Hassan tumeweza kuunganishiwa umeme katika vijiji vyote 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021 wakati nikiomba kura tulikuwa na vijiji saba tu na leo ninaposimama hapa vijiji 50 vyote vimekwishafikishiwa umeme katika Jimbo la Muhambwe. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Muhambwe tunampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali na Wizara ya Nishati kwa sababu imefikisha umeme katika vijiji vyote 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isitoshe tumeshafikishiwa umeme kwenye vitongoji 223 kati ya vitongoji 420, ni karibu 50% ya vitongoji vyetu. Hii ni jitihada kubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma ya umeme kwa sababu umeme ni uchumi, umeme ni fursa, umeme ni biashara ili tuweze kufanya shughuli mbalimbali kutokana na kuwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika hili naomba nijielekeze kidogo kwenye changamoto tunayoipata. Changamoto tuliyonayo ni kweli umeme umefika kwenye vijiji vyote, lakini wote tunafahamu *scope* ya kusambaza umeme ilikuwa ni ndogo na hii nitatoa mfano katika Kata yangu ya Murungu ambayo kata nzima wameunganishiwa umeme wananchi 50. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba pamoja na kwamba umeme umefika katika vijij vyote, lakini bado wananchi hawajafikiwa. Namwamini *Engineer* Hassan kule *REA,* anafanya kazi nzuri sana na hii kazi anaiweza. Tunaomba usambazaji wa umeme hasa umeme jazilizi…

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:**...katika umeme jazilizi ambao… *(Makofi)*

**SPIKA:** Taarifa inatokea wapi? Aaa! Mheshimiwa Dkt. Samizi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Catherine Magige.

**TAARIFA**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mchangiaji hapo ameongelea changamoto kidogo, pamoja na sifa zote tunazoipa Wizara hii ya Nishati katika Wilaya ya Ngorongoro, eneo la Loliondo kuna changamoto kubwa ya umeme hata jana usiku ulikatika na leo asubuhi pia umeme umekatika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Samizi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naipokea taarifa ya Ndugu yangu Mheshimiwa Catherine.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, umeme umefika kwenye vijiji vyetu na kwenye kata, lakini Taasisi zetu muhimu hazijapelekewa umeme. Misikiti yetu haijapelekewa umeme, Makanisa yetu hayajapelekewa umeme, kule kwangu Murungu, Lugongwe umeme haujafika kwenye Makanisa. Makanisa haya yana vyombo vya muziki, yana vyombo vya matangazo vinashindwa kufanya kazi na vinaharibika kwa sababu havina umeme. Shule zetu za sekondari na za msingi hazina umeme, shule hizi zina *computer* ambazo zinatakiwa zitumie umeme bado hazijapata umeme, Sekondari yangu ya Kumgogo haina umeme na Sekondari yangu ya Kumsenga haina umeme na ina vifaa vya *computer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara ije na mkakati maalum wa kuzisaidia hizi taasisi kwa sababu kama hizi Taasisi hazitapata umeme kwanza kelele zake ni nyingi. Pili, hizi Taasisi zina uhakika wa kuchangia hasa makanisa kulipa hizi *revenue,* lakini vyombo walivyonavyo vitaharibika. Niombe Wizara ije na mkakati maalum wa kusaidia hizi taasisi ziweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, minara yetu ambayo tumejengewa minara ya mawasiliano *Halotel* na *Voda* haina umeme. Minara tunayo, lakini huduma za mawasiliano zinakuwa hafifu kwa sababu hatujapata umeme wa uhakika. Tunawaamini *REA,* tunamwamini sana *Engineer* Hassan aje na mkakati, tuliona kwenye mabanda angalau aje na hata huduma ya *solar* ya harakaharaka kwenye hizi shule kwa sababu huduma ya *solar* ni huduma ya mara moja, lakini pia ina gharama nafuu, ukishaweka mradi umeweka ili angalau hizi shule zipate umeme kwa haraka ili vifaa viendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Naibu Waziri Mkuu na kwa kweli apokee maua yake kwa Mkoa wetu wa Kigoma na jinsi ambavyo ameendelea kutuongezea umeme, tumeshuhudia utiaji saini wa mkataba wa kujenga umeme *megawatt* 49.5 kupitia Mto Malagarasi. Hata hivyo, isitoshe tumeona tuna *megawatt* tano za *solar* katika Mkoa wetu wa Kigoma na Waziri ametuthibitishia ataongeza mpaka *megawatt* 10. Kwa hiyo, hii umetupa *confidence* na *assurance* kwamba Mkoa wetu wa Kigoma utaendelea kupata

umeme wa kutosha na hii itatusaidia kwamba tuendelee kupata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, umeme wa Malagarasi umekuwa kwenye vitabu kwa muda mrefu lakini Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu amethubutu kuanza mradi huu kwa kweli apokee maua yake kwa maamuzi haya magumu ya kuanzisha huu mradi na nimeona kwenye ukurasa wa 49 amesema mradi huu utaisha mwezi Oktoba mwaka huu, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wizara ya Nishati na Madini kwa maonesho waliyofanya kwenye viwanja hivi, kwa kweli imetusaidia sana kufungua macho na kuelewa vizuri Wizara hii. Nilibahatika kutembelea banda moja la Kampuni ya Kuzalisha Nguzo za Umeme za Zege Tanzania, *TCPM*. Kampuni hii inasimamia wazalishaji wa Nguzo za Zege kwa mikataba ya kushirikiana na nimeona Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu amesoma kwenye taarifa yake kwamba wameshafanya majadiliano na Taasisi Binafsi au wadau 17 ambao wameonesha nia ya kuzalisha nguzo, ni jitihada kubwa, tunaipongeza sana Wizara kwa kufanya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nguzo za zege ni nguzo ambazo hazidhuriki na mvua, hazidhuriki na mchwa, hazidhuriki na mto, lakini ni rafiki wa mazingira. Tunafahamu jinsi ukataji wa miti kwa ajili ya nguzo unaleta madhara kwenye jamii yetu na hasa kuleta uharibifu wa mazingira. Nguzo hizi ni himilivu kwa maana kwamba hata dhoruba kama hii ya moto kama kule kwangu Muhambwe kwenye moto kichaa, watu wakiandaa mashamba wanachoma moto, ina maana nguzo hizo zitaendelea kusimama, lakini tumeshuhudia hata kule Rufiji pamoja na mafuriko yaliyotokea nguzo za miti zilianguka lakini nguzo za zege zilibaki zimesimama.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa za Wizara hii inaonesha kwamba wanatumia takribani bilioni 80 kwa ajili ya kubadilisha nguzo zinazoharibika kila wakati. Ni pesa nyingi ambazo wangezipeleka kwenye zege, basi tungeondoka kwenye hiyo hali, nguzo hizi zina *lifespan* ya zaidi ya miaka 70 mpaka 100.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa sababu nimeona ameongelea kwamba sasa kampuni hii itaenda kujengewa uwezo. Ijengewe uwezo kwa maana kwamba pamoja na kuingia mikataba na hizi Taasisi zingine yenyewe kama yenyewe ambayo ni Kampuni ya Serikali ipewe pesa nayo iweze kuzalisha nguzo kwa sababu gani? Itasimama katikati; kwanza, kusimamia ubora wa hizo nguzo; pili, kudhibiti bei lakini na pale *TANESCO* inapopata dharura au Tanzania hii itatoa nguzo hizi za zege kwa haraka na hatuwezi kuingia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, tunasema kila siku kwamba umeme ni usalama na kama umeme ni usalama basi tuwe na juhudi za makusudi kabisa kuiwezesha kampuni hii ya zege iweze kuzalisha kwa ajili ya usalama wa nchi yetu pale inapotokea kwamba tumepata shida. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwenye taarifa yake amesema kwamba, moja ya changamoto tuliyokuwa nayo kwenye nchi kuhusiana na umeme ni uchakavu wa miundombinu na uchakavu wa miundombinu huo ni pamoja na uchakavu wa nguzo ambazo zinaoza na zinaliwa na mchwa. Kwa hiyo nimpongeze Naibu Waziri Mkuu kuliona hili na tunaamini kabisa kwamba sasa taasisi hii itawezeshwa ili iweze kuzalisha nguzo za zege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taasisi hii isiwezeshwe kwa hisani kwa maana inategemea Waziri gani yupo pale au Katibu Mkuu gani yuko pale. Kuwe na sheria, taratibu na sera ya kuisimamia ili yeyote mwingine asije na *interest* zake akaisema leo nguzo za zege mwisho kwa matakwa ya mtu binafsi kwa ajili ya kuilinda nchi yetu, lakini ya kuilinda taasisi hii, ni ukweli usiopingika kwamba Wizara hii imefanya kazi vizuri sana na tunaamini kabisa hizi changamoto ndogondogo ambazo wananchi wanalalamika watakwenda kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa bei ya umeme, *REA* wanapokuja kutuwekea umeme wanaunganishia wananchi wetu kwa shilingi 27,000. Tunafahamu kabisa hata ilivyo mapambano kuzilipa hizo shilingi 27,000, lakini hata hivyo *REA* wanapoondoka *TANESCO* ikiendelea inaleta shilingi 300,000. Kwa kweli wananchi wetu hawawezi kulipia gharama ya 300,000, tunaomba Serikali iangalie

upya i-*review* hizi bei ili shilingi 27,000 ya kuunganishia ibaki pale pale, kwa sababu walikuja na tathmini na ile tathmini jimboni kwangu kata kama tatu walisema ni mjini; Kata ya Bitulana, Kata ya Bitale na Kata ya Kumwambu.

Mheshimiwa Spika, tangu wamefanya tathmini wananchi hawajaweza kuunganishiwa umeme. Kwa hivyo haina faida ya kubaki na ile shilingi 300,000 na kama walifanya tathmini miezi sita ilishapita, si kosa ku-*review* na kuona palipokosewa na kubadilisha. Tunaomba turudi kwenye bei ya shilingi 27,000 katika majimbo yetu na vijiji vyetu ili wananchi waweze kuunganisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, pongezi nyingi sana kwa Wizara hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza wa kikao chetu cha leo. Majina ya Wabunge ambao tutaanza nao uchangiaji mchana na wengine wataendelea kutajwa kwa kadiri muda utakavyokwenda, lakini wapo Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje na wengine wataendelea kutajwa huo mchana tutakapokutana.

Baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na uchangiaji.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea. Wachangiaji wetu watakaoanza, ninalo jina la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, ndiye atakayeanza kuchangia, atafuatia Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe na Mheshimiwa Benardeta Mushashu ajiandae.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuongoza gurudumu la maendeleo katika Taifa letu, vilevile kutuongoza katika amani na utulivu. Mimi kama Mbunge wa wanawake kutoka Mkoa wa Tabora na wanawake wenzangu, baba zetu na kaka zetu tutasimama na Mheshimiwa Rais na tutatembea naye 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napongeza hotuba nzuri ya bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Naipongeza sana Wizara nzima ya Nishati pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga kwa kazi kubwa anazofanya kwa kuhakikisha Wizara hii inaenda sambamba na mategemeo makubwa tulionayo wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote hizo, Mkoa wangu wa Tabora tuna changamoto kubwa sana ya umeme. Kama mikoa mingine ina changamoto za umeme, lakini kwetu naona tunaweza tukawa ni namba moja, tunaongoza na changamoto hizo zina sababu mbalimbali. Pamoja na changamoto hizo viongozi hawa, Mawaziri hawa wa Wizara hii, Naibu Waziri pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Nishati kaka yangu Doto Biteko wamekuwa pamoja na sisi mkoani kwetu kwa ziara mbalimbali. Hawajatuacha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoani kwetu tuna Miradi ya Ujenzi wa Vituo vya Kupozea Umeme, kimoja kimejengwa Sikonge, Kata ya Ipole na Urambo, Kijiji cha Umoja. Pamoja na ujenzi huo unaoendelea toka mwaka jana kwa vituo vyote vya wilaya zote hizo mbili tayari Mheshimiwa Naibu Waziri ameshakuja kwenye vituo hivyo. Alikuja Urambo kituo kikiwa kina asilimia 64 ya ujenzi, lakini haikuishia hapo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ambaye ni Waziri wa Nishati, naye amekuja mwezi Machi katika Wilaya ya Urambo kuangalia maendeleo ya vituo hivyo vya kupozea umeme ambavyo vikikamilika wananchi wa Mkoa wa Tabora, hususan Wilaya ya Urambo, Kaliua, Jimbo la Ulyankulu pamoja na Sikonge, watakuwa wamepunguza adha kubwa ya ukatikaji wa umeme. Umeme ambao hauna viwango vya kuwawezesha wananchi wa mkoa wetu kufanya shughuli zao mbalimbali hususan vijana na akinamama ambao wamejiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati alikuja kukagua kituo hicho kuna jambo moja ambalo linaendelea ambalo halijakaa sawa. Naiomba Wizara, kuna suala la mkandarasi anayeleta *line* ya umeme kutoka Tabora kuja mpaka Urambo iende Kaliua, ambaye ni *ETDCO,* amesaini mkataba toka 2021, lakini mpaka sasa hivi ana 20% tu ya kazi hiyo ambayo ameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vya kupozea umeme umeshafika 84%, karibu na kumalizika. Wanachokisubiri ni zile *line* zitoke Tabora kuja kufika pale Urambo, kisha aweze kuwasha kwa ajili ya majaribio. Kwa hiyo, unakuta mkandarasi B amekamilisha kituo na ameanza mwaka jana, ameshamaliza, lakini anamsubiri mkandarasi anayeleta *line* ya umeme kutoka Tabora kuja Urambo ambaye bado yuko kwenye 20%. Mkataba unasema anatakiwa akabidhi kazi Juni, 2024, lakini mpaka sasa hivi tuko Aprili, 2024, kazi bado iko kwenye 20%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara na Waziri wa Nishati, wananchi wa Urambo watafarijika sana kwenye hotuba yake, atakapokuwa amesimama hapa atwambie mkandarasi huyu *ETDCO,* ambaye ni kampuni tanzu ya *TANESCO,* wana mpango gani naye kwa ufanyaji kazi huu ambao hauridhishi? Anatuletea hasara kubwa

kwa sababu, inabidi kumlipa mkandarasi ambaye ameshamaliza kazi yake, lakini inabidi amsubiri mkandarasi mzembe ambaye hajaifanya kazi yake kwa wakati kama inavyotakiwa. Kwa hiyo, inabidi tuendelee kumlipa, ili aendelee kuwepo *site* mpaka mkandarasi A atakapokamilisha. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati akisimama hapo kuhitimisha, awaeleze Wanatabora waweze kujua hatima yao kuhusu umeme, lakini na huyu mkandarasi anayetuchelewesha ni nini hatima yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuipongeza Serikali na Wizara kwa ujumla kwa kazi ambayo wanaifanya kwa mradi mkubwa ambao tunao katika nchi hii, Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mradi huu umekuja kuwa ni mkombozi wa upatikanaji wa umeme wa kutosha katika nchi hii na tayari tunaambiwa mgao utapungua. Kama kuna mgao sehemu siyo kwa sababu, nchi haina umeme ila ni kwa sababu ya miundombinu ambayo ni chakavu na mvua nyingi ambazo zinasababisha nguzo kudondoka na hitilafu mbalimbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Wizara, kama tunafanya matengenezo ya *line,* tunabadilisha *line* hizi za umeme na tumeshatengeneza vituo vya kupozea umeme, basi naomba twende sambamba na ubadilishaji wa hizi nguzo za miti ambazo kwa Mkoa wangu wa Tabora nyingi zipo maeneo ambayo yana maji sana. Kipindi hiki cha mvua, Mwenyezi Mungu ametujaalia mvua ya kutosha, umeme unakuwa unakatika kwa sababu nguzo nyingi zinadondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati yule mkandarasi anatengeneza *line* za kupeleka umeme, basi mkandarasi wa nguzo za zege naye awe anaanza ili ziende kwa pamoja ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vituo vya kupozea umeme, ambavyo ilikuwa ni kilio kikubwa sana kwa mkoa wetu, navyo vimekamilika. Changamoto ikija kutokea tena kwamba, umeme umekatika kwa sababu tu maji yamejaa, wananchi hawatatuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanachohitaji ni umeme wa kutosha. Mwananchi hajui Bwawa la Mwalimu Nyerere na hasa ndugu zangu mimi tulioko Tabora, hatujui Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa

sababu haliko Tabora. Hatujui sijui nguzo zimekaa kwenye maji kwa sababu, sisi siyo wakandarasi, tunachotaka ni umeme wa kutosha. Hatujui kwamba, sijui *line* nazo zinatakiwa kufanyiwa *service,* tunachojua ni zile nyaya ambazo huwa zimewekwa zinatakiwa tu kuwepo milele na milele kwa hiyo, wao wanachotaka ni kuona umeme unawaka. Naishauri Wizara ijitahidi, inapofanya matengenezo ya *line* basi pia, itengeneze pamoja na nguzo za kupitishia nyaya za umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacquiline, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula wajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza na kumtia moyo Mheshimiwa Rais wetu kwamba, pamoja na watu wachache ambao siyo waadilifu kutweza utu wake ameendelea kuwa ni mtu ambaye amekaa kimya na kunyamaza. Nasema wakati mwingine kunyamaza ni ibada. Mwenyezi Mungu amsaidie aendelee kunyamaza ili ibada zake ziendelee kuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutusaidia kupata umeme kwenye vijiji vyote 72 ambavyo viko ndani ya Jimbo la Momba pamoja na kwamba, vitongoji bado, lakini vijiji vyote 72 kwa *scope* ya kilometa moja umeme unawaka. Pia, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na timu yake yote bila kumsahau Naibu Waziri wake, hongereni kwa kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku ya leo nina maneno machache tu. Nina maombi pamoja na ushauri. Ombi la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye ni Waziri wa Nishati, alipofanya ziara pale Jimbo la Momba mwaka 2021 akiwa ni Waziri wa Madini, tulimpeleka kwenye Mradi wa Chumvi Itumbula, Ivuna,

pale kuna chanzo cha majimoto. Kwa hiyo, katika hotuba yake umesema wanaviangazia hivyo vyanzo kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa umeme nchini. Naiomba taasisi ambayo inahusika na mambo haya ifike kwa ajili ya uchunguzi zaidi, kinaweza kikatumika kikawa chanzo kizuri cha umeme kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, ndani ya Jimbo la Momba tuna changamoto ya kupata umeme ambao siyo toshelevu, *low voltage,* kiasi kwamba inavunja moyo na kutokuakisi yale malengo ambayo Serikali imepeleka umeme vijijini, wakati mwingine hata watu ambao wanataka kuchomelea hawawezi kufanya hizo shughuli kwa sababu, umeme ni mdogo. Kwa hiyo, naomba jambo hili kwa Jimbo la Momba na maeneo mengine kama changamoto hiyo ipo tusaidiwe, ili lile jambo la umeme vijijini ambalo limekusudiwa liweze kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la tatu ni ukosefu wa mita ndani ya Jimbo la Momba. Mimi mwenyewe toka nimejenga nyumba yangu kijijini kwetu Ihende mwaka 2022 sina umeme kwa sababu, hakuna mita. Sasa *you can imagine* Mbunge hana mita, wananchi wa kawaida hali ikoje? Wakati mwingine kutokana na jambo hili, vishoka wamekuwa wakiwadanganya wananchi kwamba watawaletea mita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwa Wizara juu ya mambo machache tu. Ushauri wa kwanza kwa Wizara ni namna ambavyo Wizara ya Nishati wanatoa taarifa. Ni kweli nia yenu kwa Watanzania ni njema, mfano, kama sasa hivi wametupa taarifa na siku wakati tunafunga maonesho yenu pale walisema kwamba, wamezalisha kiwango cha umeme kikubwa kuliko matumizi ambayo tunayataka. Naamini ni nia njema, lakini wakati mwingine taarifa hizi zinaenda tofauti na uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi huko nyuma kipindi kile ambacho mvua bado hazijaanza, miezi mitano au sita kurudi nyuma, walikuwa wanasema kukatikakatika kwa umeme kunasababishwa na kukosekana kwa maji. Mvua zikaanza kuja kuanzia mwezi Desemba, Januari na Februari, wananchi mtaani wakaanza kuuliza, mbona

mvua zipo za kutosha, zimezidi na zinaharibu miundombinu, lakini umeme bado unakatika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, wazungu wanasema kwamba, *action speaks,* matendo huongea zaidi kuliko maneno. Kwa hiyo, naomba waache *actions* zi-*speak louder than words.* Watekeleze kwanza halafu ndipo sisi tuanze kuona, kuliko sasa hivi wanatupa taarifa, wanatupa matumaini makubwa. Wakati mwingine taarifa za umeme nazichukulia ni kama taarifa za utabiri wa hali ya hewa, namna wanavyotoa taarifa za umeme, ndivyo watu wengine wanazichukua taarifa hizo wanaanza kuzifanyia kazi. Labda mtu anataka kufungua kiwanda chake, mtu anataka kuagiza samaki wengi, lakini taarifa zao zinavyokinzana na ule uhalisia kwenye jamii ndiyo mambo ambayo yanazua taharuki. Huku wanafanya wananchi wanakuwa wanaongelea hilo jambo na kuona kama Serikali ilikuwa inawahadaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba taarifa nzuri walizonazo ndani ya Wizara waende kwanza wakazifanyie *action,* halafu matendo yao yata-*speak very louder* na sisi tutaanza kujiuliza, mbona sasa hivi watu wa nishati wanafanya mambo mazuri? Kwa hiyo, taarifa zao zinakinzana na uhalisia ambao uko kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la ushauri ni kuhusiana na umeme kwenye vijiji. Ni kweli tunatambua kwamba, vijiji vyote vimepata umeme kwa *scope* ya urefu wa kilometa moja. Jambo hili kwa sisi tunaotokea vijijini wakati mwingine wananchi wamekuwa hawatuelewi. Unakuta urefu wa kilometa moja kijiji kingine kina urefu wa kilometa saba mpaka nane. Wakati mwingine wananchi inakuwa ni ngumu kuelewa kwamba, huu ni mkakati wa Serikali kwa hiyo sisi tuombe nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili liende kwa haraka kwa sababu, kule vijijini linaleta mpasuko na linawagawanya wananchi. Wakati mwingine wananchi wanakuwa wanafikiria watu wa kundi fulani ambao nguzo zimepita pale wamependelewa labda kwa manufaa fulani, kumbe hakuna hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba upelekaji wa umeme vitongojini kwa hizi *scope* za kilometa mbili ambazo wamekusudia kuongeza ziende kwa kasi ili kuwafikia wananchi kwenye maeneo mengine ambayo bado hawajapata umeme kwenye vitongoji. Pia, litaakisi uhalisia ule ambao tulikuwa tumesema tunataka kupeleka umeme vijijini. Kiukweli tuseme urefu wa kilometa moja tunaotoka huko vijijini ni mdogo na wakati mwingine wananchi hawatuelewi, ni ushauri wangu kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho ambalo nimekusudia kuwashauri watu wa Wizara ni juu ya kukatikakatika kwa umeme. Tunafahamu inawezekana labda wakati mwingine umeme unakatika nje ya mipango ya watu wa Wizara, labda walikuwa na mpango fulani au wanataka kunusuru jambo fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unakuta kuna mechi imetangazwa, Simba na Yanga, inajulikana itachezwa siku kumi mbele. Mtu amenunua kifurushi chake, amejitangaza pale mtaani labda ana kibanda umiza chake na amenunua vinywaji, mtu ana *bar,* watu wanaenda kuangalia mpira kwa sababu kile ni chanzo chake cha mapato, lakini unakuta *TANESCO* wanajua hilo jambo na wanajua kabisa watani wa jadi wanapocheza au mechi yoyote inapochezwa Watanzania hicho ndicho kiburudisho chao wanakifurahia, lakini *TANESCO* siku hiyo ndiyo wanakata umeme. Hata kama hilo jambo liko nje ya uwezo wao walishindwa kukata hata jana na juzi, leo wawavumilie wawaachie furaha yao iweze kutekelezeka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine huko mtaani kuna *notion* ambayo inaonekana kwamba, wapo baadhi ya vigogo wa Serikali ambao wanafanya biashara za jenereta. Sasa wakati mwingine inapokuwa ni siku ya mechi au siku ya tukio muhimu umeme unapokatwa inaonekana kwamba, wale vigogo wa Serikali wanaongea na watu huko *TANESCO* kwamba, kateni umeme ili labda tuuze mafuta sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Jacquiline, wakati mwingine wananchi hawataki kusikia mambo

mengi, wananchi wanachotaka ni kuona umeme, leo ni siku ya mpira wa Simba na Yanga tuangalie mpira. Sasa mtu amekusanya watu chumba cha kutosha, anajua leo atapata shilingi laki mbili alipe ada ya mtoto wake, *TANESCO* wanakata umeme na wanajua kabisa watu wanapenda mpira. Tunazua taharuki kwenye jamii, watu wanaendelea kuitukana Serikali na wanaendelea kuisema vibaya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaomba waangalie na matukio. Tunaamini kwamba, wanaweza wakajipanga watoe taarifa kama ambavyo huwa wanatoa kwenye nyakati nyingine. Watoe taarifa, lakini wanakatakata umeme kupitiliza hata kwenye matukio ambayo ni ya muhimu, kiukweli hata mimi jambo hili huwa linanikera. Umekaa hapo na wananchi, sasa Mheshimiwa hebu ona, sasa mbona wanakata umeme, kwa kweli inatukera, tunaomba siku za mechi ya Simba na Yanga wasiwe wanakata umeme ili tuweze kufurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nawapongeza sana watu wa Wizara ya Nishati. Naipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa namna ambavyo inafanya kazi vizuri. Nampongeza Mheshimiwa Rais wetu na tuendelee kumtia moyo kwamba, Mheshimiwa Rais wetu amejitahidi sana na amefanya kazi yake vizuri. Aliipokea nchi katika kipindi ambacho watu hawakufikiria kama angeweza kuifikisha nchi hapa, lakini amejitahidi amefanya zaidi ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe. Sasa atafuata Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, ajiandae Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula na baadaye atakuja Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo. Karibu Mheshimiwa.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hoja hii. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri

wa Nishati, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walio katika Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya. Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, tunamfahamu, utendaji wake tunaujua, kila Wizara aliyokabidhiwa imefanya vizuri sana. Kwa bahati nzuri sana amepewa Naibu Waziri kijana, yeye mwenyewe ni mtu ambaye anajiamini na mchapakazi, najua sasa wanaenda kufanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti waliyoleta mbele yetu ni nzuri sana, haijapata kuonekana. Nimesoma kitabu chao, 95.28% ya fedha zote ambazo watapewa Wizarani zinaenda kwenye miradi ya maendeleo, haijapata kuonekana. Nampongeza kwa Wiki ya Nishati, kwa kweli walituonesha mambo mengi, wakatufungua macho. Nilifurahi sana nilipoona mikoa yote inaonesha ni kwa jinsi gani na kwa kiasi gani umeme umeweza kusambaa vijijini, kwa sababu kila mkoa, kila wilaya ilioneshwa ni vijiji vingapi vimeweza kupata umeme kupitia Mradi wa *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakatuonesha pia na jinsi gani teknolojia imekua nchini maana yake tumeona hata magari yanayotembea kwa mfumo wa gesi. Vilevile, wakaweza kutupeleka kwenye Bwawa la Kufua Umeme la Nyerere bila kufika kule kwa kupitia *virtual reality,* tukaona jinsi ambavyo mradi mzima unafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendelea kutoa hela na kuwezesha miradi yote ya kimkakati kukamilika. Tukumbuke alipoingia madarakani huu Mradi wa Kufua Umeme wa Mwalimu Nyerere ulikuwa kwenye kama 30% hivi. Sasa hivi mradi umeshatekelezwa umefikia 95.8%, ahsante sana Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mtambo mmoja wameuwasha umeweza kuingiza kwenye Gridi ya Taifa *megawatts* 235 na ghafla mgao uliokuwa unawatesa wananchi ukapungua sana, karibu na kwisha. Tunasema Mama ahsante sana, yeye ana maono makubwa na nchi yetu. Sisi Watanzania tunampenda na tunasema, mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutuletea umeme vijijini. Kati ya vijiji 662 vilivyopo Mkoa wa Kagera vijiji 613 tayari vina umeme, tunasema ahsanteni sana. Kati ya vitongoji 3,365 vilivyopo Mkoa wa Kagera vitongoji 1,450 vina umeme. Hapo unaona kwamba bado tuko chini kwenye umeme katika vitongoji. Ombi letu kwa Serikali ni kwamba tunaomba waongeze bajeti ya kusambaza umeme mkoani Kagera ili vijiji vyote 49 ambavyo havijapata umeme vipatiwe umeme na vitongoji vyote viweze kupatiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanakagera tunaamini kwamba umeme ni ajira, umeme ni fursa, umeme ni maisha, umeme ni maendeleo, tunachoomba kwako Mheshimiwa Waziri ni umeme. Tunaipongeza Serikali kwa ule mradi ambao ulikuwa unaendeshwa na nchi tatu: Tanzania, Rwanda na Burundi wa pale Rusumo Ngara, umekamilika na Tanzania tumeweza kupata *megawatts* 27, tunasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera karibu wote unapata umeme kutoka Uganda. Huu umeme unakatika katika haijapata kuonekena unaweza ukakatika mara tatu au mara nne kwa siku. Kwa hiyo, watu wana adha kubwa kwa umeme huo ambao unakatika katika kila wakati, hii ni kwa sababu hatuko kwenye *grid* ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kile Kituo cha Nyakanazi kukamilika angalau sasa Wilaya za Ngara na Biharamulo zinaweza kupata umeme kutoka kwenye Kituo cha Nyakanazi, kwa hiyo wanapata kutoka kwenye *grid* ya Taifa. Uko Mradi wa Benaco - Kyaka, ule ndiyo unaweza kuwa mkombozi wa Mkoa wa Kagera kama utakamilika, kwa sababu utaweza kuingiza Wilaya za Muleba, Bukoba Vijijini, Bukoba Mjini, Misenyi, Karagwe, Kyerwa, wote wataweza kuingizwa kwenye *grid* ya Taifa na waweze kupata umeme wa uhakika na unaotosha ili waondokane na hii adha ya umeme kukatika katika kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumebahatika, Mwenyezi Mungu ametupa vyanzo vingi ambavyo tunaweza kuvitumia kuzalisha

umeme ikiwemo *biomass*, *natural gas*, *hydro* (maji), makaa wa mawe, *geothermal*, upepo, jua vilevile na madini ya *uranium* ambayo tunayo hapa nchini. Ukiangalia kwenye *energy mix* ya nchi yetu 63% ya umeme tunaupata kutoka kwenye *natural gas*, 32% tunapata kutoka kwenye maji, asilimia nne tunatoa kwenye mafuta na asilimia chini ya moja tunapata kwenye *biomass*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba tujue tuna mabadiliko ya tabianchi. Kuna wakati ukame utakuwa mkubwa kwa hiyo vyanzo vya maji vinaweza vikakauka au maji yakapungua sana. Kwa hiyo, kuwa tunategemea maji 32% inaweza ikawa ni hatari. Napenda kuishauri Wizara kwamba sasa tuangalie upande wa nishati jadidifu, vyanzo jadidifu, zile *renewables* kama upepo. Ukienda pale Ujerumani utatembea kilometa nyingi, unaona yale mawimbi *(panels)* yanavyozunguka. Ukienda pale Morroco unaenda *acres and acres of land* unakuta zile *solar panels* wana-*generate* umeme mkubwa sana. Kwa hiyo, nashauri kwamba na upande huo tuangalie kwamba tuingize *renewables* kwenye *energy mix* ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *geothermal*, nimeanza kusikia umeme wa *geothermal* bado nasoma shule nikiwa mdogo hadi leo bado wako kwenye utafiti. Wanasema wameshapata maeneo kama 50 ambayo yana *hot springs*, mahali ambapo kunatoka maji kwenye *surface*. Hata kwetu kule Kyerwa kuna sehemu inaitwa Mtagata maji yapo, kwa hiyo maeneo yanafahamika, basi wachimbe angalau tuone hata mradi mmoja uanze kuzaa matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa Mkutano wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa *COP28* alizindua Mpango wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia. Analenga kwamba ifikapo mwaka 2034, Watanzania 80% wawe wanatumia nishati safi ya kupikia. Tunasema Mama ahsante jitihada tunaziona, tumepewa majiko, tumeenda tumegawa. Nilishuhudia Wizara wanagawa majiko kwa akinamama ntilie na akinababa ntilie. Wale watu wa kawaida kabisa wa chini zaidi ya 1,000 sijui elfu ngapi, wakawapa majiko banifu, majiko sanifu na mitungi ya gesi. Napenda kupendekeza kwamba tunaomba bajeti iongezwe kusudi mitungi zaidi iendelee kugawiwa.

Vilevile, tuwashawishi wale wenye uwezo na wao waendelee kununua hiyo mitungi. Vilevile napendekeza kwamba hiyo gesi sasa ifike kule vijijini, kwa sababu mtu hawezi kutembea kilometa 20 mpaka 30 kwenda kujaza mtungi. Kwa hiyo tuhakikishe tunaweka *system* kwamba hiyo gesi itafika mpaka kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napendekeza kwamba sasa hivi bado bei ya gesi iko juu. Kwa hiyo, iwezekane waweze kuuza gesi katika ule ujazo mdogo ambao mtu wa kawaida anaweza kununua. Vilevile, ikiwezekana Serikali waweke ruzuku kwenye hiyo mitungi kusudi bei iteremke na kila mtu aweze kunufaika. Mwisho, tutoe elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa kutumia nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni nzuri, naomba wenzangu wote tuwaunge mkono, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benardeta. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, atafuatia Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu Mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwa wazima wenye afya na tuko hapa tunajadili bajeti ya Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kutuletea maendeleo Watanzania. Nisibaki nyuma, nimpongeze Naibu Waziri Mkuu ambaye ni Waziri wa Nishati kwa kweli amefanya kazi kubwa sana, hotuba ni nzuri hata sisi wenyewe wachangiaji tunaona kama hotuba imesheheni kila kitu. Kwa namna ya pekee sana nampongeza Naibu Waziri wetu, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge kijana, Mbunge mahiri, Mbunge msikivu, anapokea simu, anajibu *message* na anatusikiliza sana Waheshimiwa Wabunge wenziwe. Nampongeza sana Mheshimiwa Judith Kapinga, sisi vijana wenzake ametuheshimisha, tunamupongeza sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najielekeza kwenye mchango wangu na nitachangia maeneo mawili. Nitachangia upande wa gesi asilia, lakini pia nitachangia eneo la umeme. Kwenye gesi asilia hapa, nitazungumzia mambo mawili, nitazungumzia gesi ya magari, lakini pia nitazungumzia gesi ya majumbani. Mheshimiwa Rais alianzisha kampeni ya kumtua mama kuni kichwani, kampeni ambayo Wizara waliitendea vizuri, tumeona matamasha makubwa yamefanyika. Wananchi wamegawiwa mitungi ya gesi, Waheshimiwa Wabunge hapa, kila mmoja jimboni kwake ameenda kugawa mitungi ya gesi. Hakika hilo ni jambo kubwa sana ambalo limefanyika tunampongeza Mama Samia na pia tunawapongeza Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilikuwa na ushauri kwenye hii gesi ya majumbani. Tunafahamu kabisa vipato vya Watanzania ni vidogo sana na tunafahamu kabisa wananchi wamehamasika na wako tayari kutumia nishati safi ya kupikia. Changamoto yao ni moja, kwanza, ni gharama ya hizi gesi. Pia, huko mitaani gunia la mkaa ni shilingi 20,000 mpaka shilingi 30,000. Leo ukienda mtaani kuna mkaa wa shilingi 2,000, ule mkaa wa shilingi 2,000 unatosha kupikia siku nzima. Naishauri nini hapa Wizara? Sisi kama Wizara inabidi twende mbele zaidi, kwa sababu Watanzania wamehamasika kutumia gesi. Tunatamani kuona tunakuja na mpango ambao hautamlazimisha mtumiaji wa gesi awe na shilingi 25,000 apate mtungi wa kilo sita. Tunatamani kuona mpango ambao hautamlazimisha mtumiaji wa gesi awe na shilingi 58,000 aweze kupata mtungi wa kilo 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani kuona, kama ilivyo kwa magari, leo mtu mwenye gari siyo lazima aweke *full tank*, unaenda *petrol station* na shilingi 15,000 unaweka mafuta ya shilingi 15,000, mafuta ya shilingi 20,000, mafuta ya shilingi 30,000. Tunatamani kuona tunakuja na mpango ambao tutapata ujazo tofauti tofauti ili watu wote, leo nikiwa na shilingi 3,000 nyumbani kwangu niweze kwenda kununua gesi ya shilingi 3,000 nipikie ikiisha nikanunue tena. Ukichukua hii shilingi 25,000 kwa mtungi wa kilo sita ni wastani wa shilingi 4,000 kwa kilo moja. Sasa kama mtu anaweza akawa na shilingi 4,000 akaenda kuweka kilo moja na akaweza kupikia hiyo itaturahisishia sana sisi Watanzania kuondokana na matumizi mabaya ya nishati na kwenda kwenye nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye gesi za magari, tumeona Watanzania wamehamasika na naipongeza Wizara tumeona kwenye hotuba zaidi ya magari 3,000 yamebadilisha mfumo wa gesi. Tunasema, Watanzania wanatamani kuendelea kutumia gesi kwenye magari yao kwa sababu gesi ni gharama nafuu. Changamoto inakuja, tumeona mna mpango wa kuongeza vituo lakini bado vituo ni vichache, foleni inakuwa kubwa kusubiri gesi. Pia, bado vifaa vya kubadilishia mifumo ni gharama sana ambavyo vinafanya ubadilishaji wa mifumo uwe bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiwa na gari yako unataka kubadilisha mfumo kwenda kwenye mfumo wa gesi siyo chini ya shilingi milioni mbili, kwa hiyo, gharama hizi bado ni kubwa. Kwa hiyo, naishauri Serikali ione namna nzuri ya kufanya ili Watanzania wengi magari yao yafunge mfumo wa gesi. Tunaweza tukapunguza kodi kwenye vifaa hivi vya kubadilishia mfumo. Tunaweza kuwashirikisha wadau wa sekta binafsi wakawekeza katika mifumo hii ya kubadilisha magari yetu kwenda kwenye mfumo wa gesi, ili magari ya watu wengi yabadilishwe kwenda kwenye mfumo wa gesi, wapunguze matumizi ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejiuliza hapa, sijaona Serikali kama yenyewe ndiyo inasema inasimamia jambo hili, hamasa ipi inatupa kama Serikali? Wao kama Serikali ni magari mangapi ambayo tayari yana mfumo wa gesi? Wao kama Serikali wameanza kitu gani kutuonesha kwamba *now* wako *serious* na jambo hili. Kwa hiyo, ningependa sana kuona jambo hili linachukuliwa kwa uzito wake hasa na Wizara na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia pia kuhusu umeme. Tumekuwa na *phase* nyingi za mabadiliko ya matumizi ya umeme. Tulianza na mafuta, tukaja na gesi kwa zaidi ya 65%, sasa hivi tumeenda kwenye maji, lakini ukiangalia gharama za umeme bado ziko juu. Leo kwa zaidi ya miaka mitano *unit* moja ya umeme bado bei ni ile ile. Tulitarajia kwa kuwasha mitambo hii ambayo imewashwa basi gharama za umeme zingepungua walau hata kidogo. Leo mwananchi ananunua *unit* moja kwa shilingi 350 lakini tulitarajia kwa sababu gharama za uzalishaji zimepungua, tunatarajia kuona na

gharama za umeme zinapungua ili kuleta unafuu kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaambia vijana wajitokeze, wafanye biashara, waanzishe viwanda vidogo vidogo, wanahamasika lakini bado gharama za umeme ziko juu. Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati waliangalie jambo hili kwa kina. Tunatamani kuona vijana wengi wanafanya biashara, wanajiajiri, tunaomba waliangalie jambo hili kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendelea pia kwenye suala la umeme, umeme wa *REA*. Tumeona hapa kila Mbunge anayesimama anasema *REA,* wanafanya kazi nzuri lakini mimi binafsi nasimama hapa kwa masikitiko makubwa. Sisi wananchi wa Mkoa wa Rukwa bado jambo hili halijafanyika vizuri. Sisi wananchi wa Mkoa wa Rukwa bado tuna vijiji havijafikiwa na umeme. Sasa haiwezekani Wabunge hapa wanasema kwamba umeme umefika, tuna umeme mwingi mpaka mashine zinazimwa lakini bado sisi wananchi wa Mkoa wa Rukwa kuna vijiji havijafikiwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkandarasi Rukwa tumempa vijiji 141 na mkataba wake ulikuwa uishe tarehe 30 Mwezi Desemba, 2023. Mpaka inafika Mwezi wa Desemba bado hajakamilisha vijiji 40. Akaomba aongezewe muda, tumemwongezea muda mpaka Mwezi Machi, Mwezi Machi umefika bado vijiji vile 40 havijafanyiwa kazi. Sasa hivi tena kaomba aongezewe muda mpaka Mwezi Juni. Sasa haiwezekani, huyu mkandarasi *JV Pomy Engineering and Qwihaya Enterprises* wanatukwamisha sana Wanarukwa. Haiwezekani leo wananchi wanaambiwa umeme upo, umeme unatosha lakini kuna vijiji bado havijafikiwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma maoni ya Kamati ya tangu mwaka jana na mwaka huu wanapendekeza hawa wakandarasi ambao hawafanyi vizuri Serikali ione namna nzuri ya kushughulika nao. Sisi wananchi Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu wala hatujui chochote tunachotaka ni umeme. Hatujui wao hawajalipana, tunachotaka ni umeme. Sasa huyu Mkandarasi tangu mwaka jana hajamaliza,

ameongezewa muda hajamaliza. Wananchi mpaka leo hawana matumaini kama huo Mwezi Juni umeme utakuwepo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia unaweza kuhitimisha tafadhali.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu atakapokuja kutoa majibu ya hitimisho, sisi wananchi wa Rukwa tunataka kujua hatma ya hivi vijiji 40, ni lini hasa tutakuwa tumepata umeme wa uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sylvia Sigula. Namkaribisha Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, atafuatia Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuliongoza Taifa letu kubwa na la kimfano Afrika na dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wizara kwa kazi kubwa wanayoendelea nayo. Kuanzia kwa Waziri wake ambaye ni Naibu Waziri Mkuu, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Biteko. Nimpongeze Naibu wake na watendaji wote wa Wizara, kwa kweli Wizara ina watu makini na wasikivu, tunashauriana tunasikilizana na kazi zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa miradi mikubwa ambayo inaendelea kutekelezwa ya kuzalisha nishati. Kama wengine waliotangulia kusema hatuwezi kujenga uchumi bila nishati hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Muhongo amechangia asubuhi na wengine waliochangia wameonesha umuhimu wa kuwa na Wizara hii na kazi kubwa waliyonayo. Kagera hatujaungwa kwenye gridi ya Taifa kama dada yangu Mheshimiwa Mushashu alivyosema, bado tuna hitaji kubwa na kilio chetu kikubwa ni kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Umeme tulionao tunaupata kutoka nje, kama waswahili wasemavyo nguo ya kuazima haikustiri, kwa hiyo tunaiomba Wizara hii pamoja na Serikali yetu sikivu na pendwa, walituahidi Mradi wa Rusumo ukikamilika Kagera itaungwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye bajeti kwamba Rusumo sasa imekamilika na nawapongeza Wizara, nimeona kwenye bajeti ijayo kwamba mradi sasa umeanza kutekelezwa, tunawaomba sasa waukamilishe na Kagera hasa baadhi ya wilaya ziweze kuungwa kwenye gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama dada yangu Mheshimiwa Benardeta Mushashu alivyosema, nimeangalia takwimu tulizonazo Kagera vijiji ambavyo vimeungwa kwenye umeme ni 39% tu, tunaomba bado tuna kazi kubwa na safari bado ni ndefu kuhakikisha kwamba vitongoji vilivyobaki ambavyo havina umeme, sasa najua Wizara ina watu makini, naomba sasa hivi vijiji na vitongoji vyenyewe vikapatiwe nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kwenye hili kwamba tumekuwa tukisikia Waheshimiwa Wabunge wanapewa vitongoji 15, sijui vingapi tunapokuwa hapa, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, hii sera nadhani ni nzuri inatuheshimisha kama Waheshimiwa Wabunge, lakini nadhani tuangalie ni wapi ambapo kuna mahitaji makubwa zaidi baada ya kila Mheshimiwa Mbunge kumpa vitongoji 15. Nadhani tukae kama Taifa tuangalie ni wapi pana mahitaji makubwa. Ukiangalia takwimu tulizonazo kwa Mkoa wa Kagera bado tuko nyuma sana, nadhani Serikali inahitaji kutupa jicho kubwa zaidi kuliko pale ambako labda huduma imeshasambaa kwa ukubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye Wilaya yangu ya Muleba. Muleba tuna vijiji vingi lakini kwenye taarifa tuliyonayo leo ni vijiji 12 havijapata huduma ya umeme. Najua kuna kazi zinaendelea, kuna baadhi ya vijiji vina wakandarasi, lakini baadhi ya wakandarasi kama mtangulizi alivyomaliza kusema, wanafanya kazi, wamepewa kazi na Wizara lakini kazi inaenda kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasiliana na Watendaji wa Wizara, nilishalipeleka kwa Mheshimiwa Waziri, akatoa msukumo, Mheshimiwa Naibu Waziri amelipatia msukumo, kwenye maonesho yaliyopita, nashukuru tumeongea na watendaji wa *REA* na *TANESCO*, wamenihakikishia kwamba kabla ya mwezi Juni vijiji vyote vitakuwa vimepata umeme. Nina imani kwenye hilo kwa sababu nawaamini wana nguvu ya kufanya na wamekuwa wakifanya, nina hakika ifikapo mwezi Juni, Kijiji changu cha Kiholele ambacho kina mkandarasi, Kijiji cha Bihanga, Kijiji cha Burungura vitakuwa vimepata umeme na wenyewe waweze kufurahia matunda ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ya Muleba tuna Kata tano ambazo ziko visiwani, ziko *off grid*, naomba Waziri atusaidie tuweze kujua hawa wananchi ambao wako *off grid*, wako visiwani katika Wilaya yangu ya Muleba, naongelea Wilaya ya Muleba siongelei Jimbo, tunacho Kisiwa cha Ikuza, tuna Kisiwa cha Mazinga, tuna Kisiwa cha Bumbire, tuna Kisiwa cha Goziba, tuna Kisiwa cha Kerebe na hizi zote ni kata ambazo zinaunda kata tano kati ya kata 43 tulizonazo katika Wilaya ya Muleba. Kata hizi tunamwomba Waziri atupe mkakati wizara inafikiria kufanya nini ili na hawa wananchi wa hivi visiwa vyetu vitano, kata zetu tano waweze kupata hii nishati ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu pale Muleba tuna wakandarasi ambao walitoa huduma kipindi cha mwaka 2014/2015, lakini walipomaliza pale walimaliza kwa kutoelewana na Serikali na mkataba ulivunjwa lakini kuna *sub contracts* ambao walikuwa wametoa huduma kwenye hizi kampuni, kampuni yenyewe nadhani kama sijasahau ni Kampuni ya *UR*, wakaondoka lakini walituachia malalamiko na manung'uniko makubwa, watoa huduma waliokuwa wanawapatia huduma hiyo kampuni, waliondoka bila kuwalipa.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha bajeti yake hapa, atuambie, hawa wananchi tunawasaidiaje ili waweze kupata pesa yao kwa sababu najua hii kampuni bado ipo na inaendelea kufanya kazi sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mkataba ulikatishwa, lakini wananchi bado wanadai, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie tuweze kumaliza hayo manung'uniko ya hao *sub contracts* waliotoa hizo huduma, kazi ilifanyika lakini hawakupata malipo na wanadai hela nyingi sana kutoka kwa mkandarasi huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo suala la vitendea kazi katika wilaya yangu. Mheshimiwa Waziri anajua Wilaya ya Muleba ni kubwa na huku kwetu katika Mkoa wa Kagera inaitwa Kanda Maalum. Ni wilaya ambayo ina Kata 43, sasa ukiangalia wilaya yenye Kata 43 huwezi kuilinganisha na wilaya nyingine ambazo zina kata chache. Tunayo Majimbo mawili lakini tuna ofisi moja ya *TANESCO* na tunapogawa vitendea kazi tunaichukulia Kanda Maalum kama Wilaya ya kawaida lakini pale tuna Wilaya mbili. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye mgawanyo wa vitendea kazi, vijana wake wanafanya kazi kubwa na ni wasikivu, wanajituma kwelikweli, lakini wana tatizo la magari. Wana gari moja ambalo na lenyewe kusema kweli muda wake unaelekea ukingoni. Namwomba Waziri, hawa vijana wake ambao wanatufanyia kazi nzuri katika Wilaya ya Muleba, atusaidie wakapate vitendea kazi, awapatie magari ili waweze kuhudumia wilaya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya yetu pamoja na kuwa kubwa, lakini jiografia yake ni mbaya, kuna maeneo ambayo mvua zikinyesha huwezi kufika kwa mguu na huwezi kufika kwa magari ya kawaida, sasa hawa waangaliwe kwa jicho la namna ya pekee hasa kwa upande wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niongelee suala la gesi. Naishauri Serikali, wenzangu waliotangulia wamesemea suala la gesi, ni kweli tunahitaji gesi na bei yake ni nafuu. Napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake, atupatie elimu kidogo. Tuna mkakati gani kama Taifa kuhakikisha kwamba gesi ambayo Dar es

Salaam tumeanza, lakini hii miji mikubwa hasa Majiji kama Mwanza, Mbeya, Arusha, tunawapelekeaje hii huduma ili kupunguza gharama ya nishati katika haya majiji makubwa ambayo wana magari mengi na msongamano mkubwa wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam peke yake, tumefanya kazi kubwa na nzuri ya kimajaribio tuangalie tunakuja na mkakati gani kuhakikisha kwamba Jiji lote la Dar es Salaam, Wilaya zote za Jiji la Dar es Salaam na wenyewe wanapata hii huduma kubwa na nzuri ambayo inapunguza matumizi ya pesa yetu ya kigeni kuagiza mafuta kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru na nawatakia kazi njema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo. Atafuata sasa Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, baada ya Mheshimiwa Shally atakuja Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mungu kwa kunipa pumzi ya uhai na kuweza kusimama hapa leo kuleta hoja zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye ni Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Biteko, hakika hotuba yake imejaa na imesheheni kila jambo ambalo tungependa kulifahamu. Kipekee pia naomba kumpongeza sana Naibu Waziri wake Mheshimiwa Judith Kapinga, binti yetu ambaye hakika yuko makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza timu nzima ya Wizara ya Nishati akiwepo Katibu Mkuu, Ndugu yetu Felchesmi Jossen Mramba na Naibu wake ndugu yetu Mataragio, pia timu yote naa idara mbalimbali zilizo chini ya Wizara hii ya Nishati. Imenipendeza kufanya hivyo baada ya kuona mambo makubwa waliyofanya. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uteuzi huo na safu hiyo makini ambayo inatufanya leo tunasherehekea utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, kipindi kama hiki, wizara hii iliomba shilingi 3,048,632,319,000, lakini hadi ninaposimama hapa nikizungumza, wameshapewa shilingi 1,813,026,147,056. Ni sehemu ndogo sana waliyopewa na tumebakiza miezi michache bajeti iishe, lakini kazi zilizofanyika ni nyingi na kubwa, sisi ni mashahidi, tumeona karibu wanakamilisha lile Bwawa la Mwalimu Nyerere na pia mambo mengine yamefanyika. Ombi langu ni kwa Waziri wa Fedha, ile hela iliyobakia sasa ilipwe, atakapoziona hizo *certificates* tunaomba alipe kwa sababu sisi ni mashuhuda, tumeona kazi imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, natamka wazi naunga mkono hoja na nawaomba wenzangu, tuwaunge mkono waweze kupatiwa ombi la mwaka huu, kwa sababu bajeti yao ina uhalisia. Nimetamka, waliomba shilingi trilioni tatu, mambo yamefanyika, mwaka huu wanaomba shilingi 1,883,759,455,000. Unaweza ukaona jinsi ambavyo hii bajeti ina uhalisia, nilitaka kuliweka hilo wazi. Naomba tuwaunge mkono na wapewe, wala tusianze tena kutaka ufafanuzi wa kushika shilingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye maeneo mawili, naanza na moja la *TANESCO* kuhusu huduma kwa wateja, nasema wazi kwamba tumependa mabadiliko yaliyofanyika *TANESCO*, tumeona kazi inayofanyika lakini umeme bado unakatika. Sitaki kufika kule kwangu maana yake ile *lane* yangu ndiyo mbovu kabisa, huko ninakoishi, nitarejea huko baadaye, lakini wametuambia katika kitabu alichosoma Naibu Waziri Mkuu, kwamba *TANESCO* wameboresha elimu kwa wateja ikiweko *chat board* yaani unawaeleza tu shida yako bila kupiga simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna mfumo mwingine waliouleta *TANESCO* kuanzisha Mfumo wa Benki ya Taarifa na Elimu *(Desa System)*. Sasa, tunaomba basi, hiyo elimu itolewe kwetu na pia kwa watu wetu. Tunaenda ku-*desa* vipi, maana yake kama kuna kitu ambacho kina shida na kinatesa na kichefuchefu, ni jinsi ambavyo tunavyoripoti kukatika kwa umeme, unaambiwa nenda *lane* fulani, mara inakata, wenyewe pia wanakatiwa umeme hukohuko walipo kwenye mitambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo inakuwa kwa watu ambao wanakaa mbali kama vijijini, mtu analipa nauli anakwenda mpaka mjini kwenda kuripoti hatukuwa na umeme, labda ni hizi mvua zinazoendelea, ni transfoma ilikatika, lakini ni kitu chenye usumbufu. Wameeleza kama maeneo manne ambayo wanakwenda kurekebisha ili wateja tuweze kuwapata kwa unafuu zaidi. Naomba sana, hili jambo lifanyike na elimu itolewe tuweze kuwafikia *TANESCO*. Hata hapa, nadhani watu walio nje ya Dodoma wanadhani sisi ndiyo tunaopata umeme siku zote, hapana. Ile juzi wametueleza kwamba hii shida inakwenda kuisha, kwa hiyo tunatarajia hii shida iishe na mwakani tusisimame tena hapa kuzungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalokwenda kuzungumzia, nalo naanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kumletea mwanamke nishati safi na salama ya kupikia. Hili jambo ni jema na naipongeza sana hii Wizara ya Nishati kwa sababu kwenye ukurasa wa randama, ukurasa huu wa tano, kwenye *Project Code* 3001 – 3002, wametenga shilingi bilioni nane kwa ajili tu ya hii *clean cooking project* na hela hiyo inatoka kwenye hela za ndani, kwa hiyo naona hili jambo linakwenda kuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walianza vema sana, walituletea *REA*, *REA* wakafanya kazi nzuri sana, wametupa mafunzo hapa lakini haikuishia hapo, *REA* ikatoa tenda. Mitungi ya gesi ikamwagika kutoka kwenye makampuni mbalimbali ambayo ni ya wadau. Tuliona mitungi ya *Oryx* kwa wingi sana, tukaona mitungi ya *Taifa Gas*, tukaona mitungi ile ya *grey*, majina ni mengi lakini *Oryx* iko kichwani kwa sababu aisifuye mvua imemnyeshea. Tuliiona hiyo mitungi na ipo mitungi ya rangi zote kijani, *grey*, manjano, *Mihan* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, hii hela iliyotamkwa hapa, ikaendeleze hayo mambo mazuri ambayo yameanza. Tuliona Wizara ikifanya kongamano lililofana sana hapa Dodoma na tukamwona Mheshimiwa Naibu Waziri akilisimamia na sisi wenyewe tukaona na tukashiriki, wanawake wanaendelea kusubiri. Mitungi hii siyo rahisi itolewe bure kwa kufuatia kaya zilizoko nchini zilizooneshwa na *NBS,*

kwa sababu kaya zote zimeorodheshwa, vijiji, vitongoji, kata, wilaya na Serikali haiwezi kugawa zote, kwa hiyo lazima tunachangia, katika kuchangia huko, Waheshimiwa Wabunge tunachangia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sasa, kadri tunavyoendelea kuboresha elimu au wanavyotuboreshea elimu, Wabunge wao tuko tayari kwenda kushusha elimu hiyo chini mpaka kwenye *level* ya kata na kaya. Bado nasisitiza mitungi hiyo isigawiwe bila elimu. Leo ukatokea mlipuko, watasema aah! ni vile vitu vipya vilivyoletwa vya gesi, kumbe hapana! Wapate elimu, hairuhusiwi, haikubaliki gesi kuleta maafa katika familia. Kwa hiyo, tuko tayari sisi kuendelea kuwa walimu wa walimu kama Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa wote na pia tuko tayari kuendelea kugawa nishati hiyo kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alitamka na akasema ifikapo 2034, angetamani kuona taasisi ambazo zina watu zaidi ya 100 watumie gesi hii. Wanasema *her wish is a command*, ametaka hivyo, hiyo ni ameshatamka, mamlaka imesema! Namba moja ikisema, wote inatakiwa tutekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, kutumia nishati hiyo inatakiwa pia miundombinu iwe imetengenezwa, kwa hiyo tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, aweze kuendelea kuzungumza vizuri na hawa wadau ili yale maeneo yenye watu zaidi ya 100 zikiwemo shule, maeneo ya kuishi watu ambao wana shughuli mbalimbali, vyuo, magereza, kokote kule ambako kuna watu 100 na zaidi, waweze kujengewa hiyo miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikishajengwa miundombinu, akatokea hapo mmoja mwenye roho nzuri, anaweza pia kupeleka hiyo gesi kwa kuanzia halafu mwendelezo ukawa ni kazi kwao. Tunajua na tunakubali kwamba hata huko Ulaya walianza kwa moto wa kufikicha lakini inapofika mahali…

*(Hapa kengele ililia kuashira kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba hitimisha tafadhali.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nilishaunga mkono hoja, lakini naunga tena mkono hoja na nawaomba wote tuunge mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ahsante. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na mjadala wetu naomba tutambue wageni waliokuja Bungeni jioni hii, hawa ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo:-

Tunao wanafunzi 37 ambao pia ni Wanachama wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Tiba. Tunaomba msimame tuwatambue, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na uchangiaji, nilimtaja Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatia Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii Wizara ya Nishati. Awali ya yote ni pongezi, nampongeza sana Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi nzuri anayofanya, Naibu Waziri wa Nishati kwa kazi nzuri, Katibu wa Wizara na Naibu Katibu, Mkurugenzi wa *REA* na *TANESCO*, Wenyeviti wa *REA* na *TANESCO* wote wanafanya kazi nzuri, hongera sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwateua wote hao. Mheshimiwa Rais tunamwamini amefanya kazi nzuri na tunamwombea yeye aendelee kuwepo. Kuna vitu vingine vingi sana huwa najiuliza, unapomzungumza Mheshimiwa Rais labda kwa jambo fulani, jambo fulani, jambo fulani unashindwa kujua watu aliowaweka kwenye vitengo maalum ni watu thabiti. Kama leo tuna matatizo ya umeme nchini, tuhangaike na Mheshimiwa Dkt. Doto tu, kwa nini tunahangaika na Mheshimiwa Rais? Mheshimiwa Rais amemteua Mheshimiwa Dkt. Doto afanye hiyo kazi, tuhangaike naye humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama masuala ya kilimo tuhangaike na Mheshimiwa Bashe, kama ni suala la madini Mheshimiwa Mavunde yupo. Kwa hiyo sisi tunachosema ni kwamba Mheshimiwa Rais ametuteulia watu mahiri tuhangaike nao kama hawatendi kazi. Huo ndiyo ushauri wangu, nataka kuona kwamba unafanyika. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri mdogo kwa Wizara hii ya Nishati na hasa watu wa *TANESCO* na *REA*. Kumekuwepo na lugha ambazo hazifanani, hapa katikati tulikuwa tunasema Bwawa la Mtera mvua inanyesha maji hayajai, umeme haupo, tukapiga kelele tukazungumza mvua ikaja. Baada ya muda mfupi maji yakajaa umeme siku mbili umekatika hapa nchini, wanasema Bwawa la Mtera maji yamejaa, yanaharibu mifumo ya umeme, khaa! Sasa hayo maneno gani? Maji hayapo umeme hamna, maji yamejaa mifumo imeharibika. Kwa hiyo tuwe makini sana kwenye hili jambo la umeme na mimi niombe Mheshimiwa Waziri wa Nishati na bahati nzuri Mheshimiwa Rais amemteua amempa na madaraka mengine makubwa. Kwa hiyo haogopi mtu yeyote, wala hakuna anayemsogelea. waangalie watu wanaokaa kwenye vyanzo vikubwa vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Bwawa la Mtera, Bwawa la Nyerere na maeneo mengine yote ambayo yanaongelewa kwenye maji, wangalie watumishi wanaokaa maeneo hayo kama wana muda mrefu kwenye maeneo hayo wawaangalie kama wanatenda kazi, kama hawatendi kazi wawapunguze kwa kuwapeleka katika maeneo mengine. Nasema hivi kwa sababu ni lazima wawe na lugha moja ya kuzungumza, siyo maji yajae umeme eti shida, maji yapungue umeme ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni la ushauri, naomba ushauri wa Mheshimiwa Profesa Muhongo ufuatwe hasa umeme wa jua. Huko tunakoenda tumeshaona hivi vyanzo vya maji vina matatizo. Ni kweli tuna umeme *megawatt* 2,115 ya Bwawa la Nyerere, lakini huko nyuma tumeshaona mabwawa ya maji yanapungua na umeme unakosekana. Kwa hiyo niombe, tuone

kwamba hivi vyanzo vya umeme vingine tofauti na vyanzo vya maji, tuone kwamba unapatikanaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ninaoutoa muhimu sana kwenye *REA,* watuambie ni kweli 2025 vitongoji vyote vya Tanzania vitakuwa vimepata umeme? Je, ni mwaka 2025 au ni 2030? Lazima tuwe na lugha moja, siyo tunazungumza leo umeme 2025 vitongoji vyote vitakuwa na umeme, kumbe haiwezekani. Kama kuna mkakati wa kutosha wa kutengeneza vitongoji vyote vya Tanzania 2025 vitapata umeme tuambiwe ili twende kwa wananchi tuwaambie, siyo tunawaambia leo hiki kesho inakuwa tofauti. Kwa hiyo nilikuwa natoa ushauri huo ili tuweze kuuzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli watu walikuwa wanazungumza mara nyingi sana hapa. Ni kweli Mheshimiwa Naibu Waziri ametupa hotuba ya matumaini na Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba ni bora kutawala maskini mwenye matumaini kuliko kutawala maskini asiye na matumaini. Maskini mwenye matumaini ni yule ambaye ana kuku anakwambia nikope shilingi 1,000 nitauza kuku nikupe, nikope shilingi 2,000 nitauza mazao yangu nikupe. Maskini asiye na matumaini ni yule ambaye hana kitu chochote. Atakwambia nini umkopeshe alipe nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametuaminisha hapa kuna umeme wa Bwawa la Nyerere, kuna umeme wa Rusumo, kuna umeme wa gesi asilia, tumeona, wametupa vyanzo vingi vya umeme na kweli hapa katikati umeme umepungua kukatika. Watupe uhakika huko tunakokwenda, watu hawahitaji vyanzo vikubwa vya umeme, hatuambiwi kwamba umeme *megawatt* 5,000 wakati hata hakuna umeme, haiwezekani. Lazima watuambie umeme unapatikana na unawaka, si umeme huu tumezalisha mwingi na huku umeme unakatika kila siku. Hilo nalo tuliangalie kwamba wametupa matumaini, kwa hiyo tunahitaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamezungumza hapa vijiji, mimi huwa nafikiria jambo tofauti sana. Hivi unavyoniambia vijiji vyote 12 vina umeme ni sawa lakini vijiji ni nini? Vijiji ni vitongoji, kijiji kimoja kina vitongoji sita mpaka saba. Kwa hiyo kama kuna kijiji kimepata umeme

maana yake ni kitongoji cha *center* chenye umeme, vitongoji vingine vyote havina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatolee mfano mimi nina Jimbo lenye vitongoji vingi katika kijiji kimoja. Kuna Kijiji kinaitwa Mariwanda kina Vitongoji 16, hakuna Mbunge hata mmoja hapa ana vitongoji vya namna hiyo haipo kwenye kijiji kimoja. Vitongoji 16 kijiji kimoja, vilivyo na umeme ni vitatu. Kuna Kijiji kina vitongoji 14, vilivyo na umeme ni vitatu, vitongoji 11 vilivyo na umeme viwili. Ni kweli nimepewa umeme na watu wa *TANESCO* na *REA*, hasa *REA*. Namshukuru sana Mkurugenzi wa *REA* na mwenzake anaitwa Olotu wanafanya kazi vizuri, lakini tuna wingi wa vitongoji kwenye maeneo ya vijiji. Kwa hiyo lazima tuangalie kwamba tuhangaike na vitongoji ili watu wapate umeme kwa eneo kubwa kuliko kusema tumemaliza vijiji, lakini kumbe kijiji kimoja kina vitongoji 11, kitongoji chenye umeme ni kimoja. Sasa hilo nalo tuliangalie vizuri huko tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *REA*. Tusiende kufanya *survey*, twende tukafanye *survey* kabla ya kwenda kupima vijiji. Siku hizi *REA* walivyo wao maana yake wanakwambia bwana tumekuletea kilometa mbili kwenye Kijiji A. Ninachoshauri ni kwamba, waende kwanza wafanye *survey* kwenye eneo husika, wanaweza kukuta kuna shule inahitaji umeme kama umechukua nguzo nyingi, unaweza kukuta kuna kisima, unaweza kukuta kuna miundombinu mingine, inaweza kuwa idadi ya watu ni kubwa. Hiyo *survey* wanayoifanya ndiyo ikupe nafasi ya kutoa umeme kwenye kijiji kuliko ilivyo sasa, tunapeleka *survey* wakati tayari tunapeleka umeme kilometa tatu, *survey* haijafanyika na hilo limetokea kwenye maeneo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Nishati maombi maalum, Kijiji cha Nyabuzume na Kijiji cha Nyaburundu tumewapa umeme wa migodi. Pale kuna dhahabu nyingi sana zimetoka Nyabuzume na Nyaburundu, wanapeka kilometa 1.5. Wahitaji wa umeme huo ambao ni watu wa migodi wanahitaji kilometa tano *at least*. Kwa hiyo naomba Nyabuzume tuwape kilometa tatu na Nyaburundu tuwape kilometa tatu za kuanzia, tafadhali namwomba sana Mheshimiwa Waziri. Tunahitaji hela, watu ni maskini hata kama hiyo dhahabu imetokea nyingi

Nyabuzume, tunamwomba Waziri tafadhali awasaidie kwenye hiyo nafasi waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miradi ya umeme tunayokuwa tunaizunguza hapa tumekuwa nayo kwa muda mrefu na tuna mikakati. Wananchi unapozungumza habari ya kwamba miundombinu ni mibovu, kitu gani ni kibovu, hiki, hiki ni kibovu hawaelewi. Nimeona bajeti ya 2016 tumeweka bajeti na mikakati, 2017/2018, 2018/2019 mpaka leo ukisoma hiyo Hotuba yetu ya Nishati ina mikakati mingi sana. Tunaimarisha miundombinu, tunaimarisha hiki, tunaimarisha hiki. Ifike muda tuwaambie Watanzania hata kwa umeme walionao sasa, hata bila kuongeza mwingine basi inatosha kufanya hiyo kazi. Watu wanateseka, viwanda vinakuwa havina umeme, ukienda viwandani wanalia, watu wazima wanalia, mama ntilie wanalia na kila mtu analia, hapana ifike mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nawaza hivi, Naibu Waziri Mkuu anapatikanaje? Nilikuwa nawazawaza hilo. Nikaangalia nikaona 1985 Mheshimiwa Salim Ahmed Salim alipewa Unaibu Waziri Mkuu, sasa nikajiuliza alipewaje? Kumbe kipindi hicho nchi ilikuwa na matatizo mengi, kulikuwa na uchumi mgumu akateuliwa kusaidia nchi ikaenda ikasaidika kidogo. 1993 Mheshimiwa Mrema alipopewa kulikuwa na ujambazi wa kutupa kwenye nchi yetu akasaidia saidia mambo yakaisha yakaenda. Tamaa zake zikampeleka huko alikoenda lakini alisaidia nchi ikaenda ilikokuwa inaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imekuja mwaka huu amepewa Mheshimiwa Dkt. Doto, amepewa kwenye wakati ambao umeme ni shida kwenye nchi yetu. Umeme na Nishati ni shida kwenye nchi yetu, tumeona kwa kipindi kifupi walichonacho amepeleka *at least* mgao wa umeme umepungua. Kwa hiyo nafikiri kwamba kumbe Manaibu wanapewa kwa kazi maalum. Namwombea Mheshimiwa Dkt. Doto, afanye hiyo kazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, atafuatiwa na

Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ajiandae. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje tafadhali karibu.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Nishati na nimeshawahi kuwa Mjumbe kwenye Kamati hii na kwa kweli niwapongeze sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati lakini pia nimpongeze rafiki yangu ambaye alikuwa Mwenyekiti wetu wa Wabunge Vijana Bungeni Mheshimiwa Naibu Waziri Judith Kapinga, kwa kweli anatuheshimisha sana vijana wenzake kwenye Bunge hili. Pia, niwapongeze kwa kweli wote, Makatibu Wakuu, ndugu yangu James Mataragio, tulikuwa naye kule amekuwepo tangu kipindi hicho na tunaendelea kushirikiana naye vizuri, kwa kweli wanafanya kitu kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia zaidi sana katika eneo moja. Nitachangia *energy mix* (nishati mchanganyiko) kuelekea nishati jadidifu 100% *(Energy Mix in Transition to 100% Renewable Energy)* katika nchi. Kwa kweli kwanza nipongeze sana, nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimesoma na maoni ya Kamati na nimeona na wao wamezungumza kuhusiana na *energy mix*. Kwa kweli *energy mix* ndiyo suluhisho na kwa sababu jana tulijadili Bajeti ya Wizara ya Mazingira na kuna baadhi ya vitu ambavyo ndiyo maana tunakubaliana na suala la nishati mchanganyiko *(energy mix)* kwa sababu hakuna anayetabiri nini kitatokea baada ya muda fulani kwenye masuala ya mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa namna moja au nyingine athari za mabadilko ya tabiachi leo tulikuwa tunazungumza *Hydroelectric Power Plant* ya Mwalimu Nyerere ambayo ni *megawatt* 2,115, bado sisi hapa wote hatujui nini kitatokea miaka miwili, mitatu ijayo. Pengine panaweza pakakauka pale na hatuombei, lakini kwa sababu tunasema mambo yanabadilika kila siku hatujui. Kwa hiyo *energy mix* ndiyo *solution* kuelekea 100%. Kwa sababu nchi yetu imeridhia pamoja na nchi nyingine kwenye kuhakikisha tunapunguza

ongezeko la joto duniani na kuendelea ku-*maintain* 1.5 *Celsius* ongezeko la joto duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo miongoni mwa jitihada zote unazozifanya ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunahamia kwenye *renewable energy* nchi zote. Mimi hii naichukulia kama fursa kwenye nchi yetu kwa sababu na sisi mwaka jana pia tumesaini Mkataba wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa *IRENA* pamoja na kwamba tulichelewa lakini pia ni kitu kizuri kwamba nchi imeona ni wakati mwafaka wasaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesoma *document* kadhaa. Nimesoma *An Outlook of Tanzania's Energy Demand Supply and Costs by* 2030. Pia, nimesoma *Analytical Study on National Energy Policy and Regulation Frame Work in Tanzania, Technical Report* ya *Power Shift Africa* na hii pia nyingine ni ya *Power Shift Africa* lakini ni *African Development Bank Group* ambao wamefanya *Research* zao. Pia, nimesoma *Energy Development Plan to Re-carbonize the Economy* ya upande wa Tanzania peke yake ambayo pia imefanywa na *Power Shift Africa* na kwa kweli kwa kusoma hizi nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Profesa Muhongo asubuhi kuhusiana na wakati tunazungumza *energy mix* ni lazima tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu eneo moja la *hydroelectric power* ni eneo moja, lakini tukizungumza nishati jadidifu tunazungumza pamoja na umeme wa upepo, tunazungumza pamoja na umeme wa jua, lakini tunazungumza *geothermal.* Kwa sababu nafahamu kila Serikali inayokuwepo madarakani kwa namna moja au nyingine ni lazima Kiongozi wa nchi awe na mtazamo kuhusiana na jambo fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi nasema hivyo kwa sababu hata mimi ningekuwa kwenye nafasi fulani kwenye hizi kubwa za juu ambayo ina *impact* kwenye maamuzi ukiachana na nafasi zetu za Ubunge, ningetamani na mimi nibakishe kitu ambacho watu watanikumbuka nacho**.** Kwa hiyo nitoe wito kwa Washauri wa Mheshimiwa Rais, miongoni mwa vitu vya kufanyia kazi kwa kiwango kikubwa sana ni kuhakikisha tunapata umeme ambao ni *reliable*

kwenye nchi kama ambavyo tulianza na hatua ya kutengeneza Mradi Mkubwa wa Mwalimu Nyerere ambaye mtangulizi wake aliweka. Basi sehemu ya pili ya kutumia fedha zote ikiwezekana na fedha za mabadilko ya tabianchi ambazo tunazihitaji, basi Waziri atafute fedha na tuandike miradi tupate fedha kwa ajili ya ku-*fund* miradi ya umeme wa upepo na miradi ya umeme wa jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu kama nchi tuna baraka mimi naziita baraka. *Tanzania is a promising country* kwenye upande wa *solar*. Kwenye upande wa *solar* ambao Mheshimiwa Profesa Muhongo aliongea pia asubuhi kwa maana nchi nyingine ambazo ziko *industrialized* kama India na China wametumia hiki. Sasa Tanzania kijiografia kwa mwaka tuna uwezo wa kupata masaa 2,800 mpaka 3,500 ya miale ya jua. Sasa wakati tunajua mabadiliko ya tabianchi yanaweza yakakausha vyanzo za maji wakati huo huo kinyume chake ni kwamba kama kutakuwa na chochote kinachokausha vyanzo vya maji maana yake itakuwa ni upatikanaji wa jua la kutosha kwenye nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tusilie kwamba hapa Kanda ya Kati kuna ukame, tutumie ukame kutengeneza umeme wa jua kwa maana tuweke *resources* zetu kwa ajili ya ku-*fund* miradi ya umeme wa jua. Mheshimiwa Waziri wa Mipango yupo hapa na nafurahi sana kwa sababu yeye ndiye anayetupangia. Nilitamani sana kama mwanasiasa ambaye bado nina muda wa kufanya siasa kwenye nchi yangu, vijana washiriki katika mnyororo huu wa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunazungumza umeme wa jua na umeme wa upepo. Ili upate umeme wa jua na umeme wa upepo inabidi uwe na *wind turbines* (mitambo ya kutengeneza umeme wa upepo). Ili utengeneze umeme wa *solar* lazima uwe na *solar panels*. Kuna madini Tanzania yamegunduliwa ambayo yanaweza kutusadia kuweka viwanda. Kwa hiyo Waziri wa Mipango ni lazima awe anafikiri kwenye namna ya kushiriki kwenye mnyororo wa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tuna-*plan* kuweka 100% nishati jadidifu kwenye nchi halafu tunategemea kuagiza mitambo, tunategemea kuagiza *solar panels,* tunategemea kuagiza *wind*

*turbines* wakati kuna Wizara ya Mipango inaweza ikatusaidia tukatafuta *resources* tukajenga viwanda vya kutusaidia kuzalisha *solar panels* ili tukazalishe kwa sababu *critical minerals* zinazozalisha *solar panels* zipo nchini, tutazungumza kwenye madini. Kwa hiyo tusiwe tu tunagundua madini, tunasema tunahitaji 100% ya nishati, tunasema tunataka tupunguze kiwango cha joto duniani, tunataka tuhakikishe tunachimba madini yetu, tunanufaika, hivi vitu vyote ni *interconnected*. Natamani tuweke mipango kwa mtindo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kiasi hicho tutashiriki kwanza kuelekea 100% ya nishati. Pili, kuhakikisha vijana wanashiriki katika mnyororo wa thamani na Watanzania wanashiriki kwa sababu tutanufaika sisi ndani, vijana wetu wataajiriwa, vijana wetu watafanya biashara kwenye *solar panels* na *wind turbines*. Kwenye upande huo itoshe labda niseme kitu kimoja kwa sababu kwenye Kamati ukurasa wa 36, Kamati imezungumzia na Mheshimiwa Waziri pia kwenye Hotuba yake amezungumzia uwezo wa mitambo ya gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nisome takwimu; uwezo wa mitambo katika gridi ya Taifa Februari, 2024 kuzalisha umeme wa maji, mitambo ina uwezo wa kuzalisha umeme wa maji *megawatt* 836.61, lakini tunazalisha *megawatt* 755.56, hiyo upande mmoja. Kwenye gesi asilia mitambo ina uwezo wa kuzalisha *megawatts* 1,198.82 lakini tunazalisha *megawatts* 935.11, umeme wa mafuta uwezo ni *megawatts* 83.92, lakini tunazalisha *megawatts* 65.75. Sasa tungamotaka kwenye *megawatts* 10.5 tunazalisha *zero* na Kamati imeeleza kwamba mitambo haina uwezo, kuna masuala ya miundombinu mibovu. Sasa vitu kama hivyo vinaturudisha nyuma, wakati tunahesabu kwamba eti umeme *TANESCO* wanatangaza umeme umezidi tumezima mitambo, tunaonekana kama *jokers* samahani na kwa *due respect* vitu vingine tuviache tu vinatudhalilisha hata wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukijumlisha hizi *megawatts* zote *full power* ya *TANESCO* kwenye Gridi tutakuwa tuna umeme *megawatts* 4,000, tukijumlisha na Mwalimu Nyerere ikiwa *full power* zile 2,115 tutakuwa na umeme *megawatt* 4,241.85. Bado si kitu cha kujisifia, *capacity* yetu sisi ukiangalia *estimated* umeme ambao

tunahitaji, tunahitaji *by* sasa hivi tu tuna *megawatts* 5,000 na ili tukijumlisha zote *full power*, kwa sababu nimewaambia hapa uwezo ni huu na tunazalisha pungufu kwa sababu mitambo mibovu. Sasa sifikirii kama ni busara kufikiri kwa kurudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilifikiri kuna haja ya kufanyia kazi hoja ya Kamati, kwamba sasa Serikali ikafanye marekebisho ya mitambo badala ya kutoka kwenye miji na kujisifia kwamba tumezima mitambo kwa sababu umeme umezidi. Nafikiri tunaonekana tunakwenda kwa kurudi nyuma. Kwa hiyo, hili nilitaka niliseme na nakubaliana na Kamati na kwa kweli Kamati wamefanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda niende kwenye jimbo. Nashukuru sana kwa upande wa kwetu Singida, *REA* kwa Wilaya yangu ya Ikungi wamefanya vitu, niwapongeze sana. Kwenye Jimbo langu la Singida mashariki wame-*connect* vijiji vyote isipokuwa sehemu chache tu. Nimpongeze sana Meneja wetu wa *REA* pale, dada yetu anaitwa Leah, amefanya vizuri kwa sababu amefanyia kazi mambo ambayo tumemshauri na ame-*connect* vijiji vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *REA III,* Mzunguko wa Pili, vijiji 20 vimekuwa *connected* vyote upande wa Singida Mashariki. Niombe, bado hawaja-*connect* umeme katika Sekondari ya Ntuntu, Sekondari ya Lighwa pamoja na Kisima cha Maji cha Mungaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nyumba za ibada, Kanisa la KKKT Mbwanjiki, Kanisa la *Pentecostal* Mlumbi, Katoliki Dayosisi Singida Kinku, pia Kanisa la *FPCT* Mkunguakihendo. Hii yote ni mashariki, kwa kweli wanashukuru sana na wanaendelea pale kufanya shughuli zao na ni jambo kwa kweli ambalo ni zuri. Maeneo mengine ni Shule ya Msingi ya Kikio, Shule ya Msingi ya Nkundi, Shule ya Msingi Mnane, Lighwa, Ujaire, Sakaa, Taru, Ntuntu, Ntewa, kote wame-*connect* na ni jambo la kushukuru, ni vitu ambavyo kwa kweli tunaona ni *going forward.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na vitu vingine pia nitavipeleka kwa njia ya maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje. Anafuatia sasa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, baada ya Mheshimiwa Lupembe atakuja Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Nishati. Naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupatia uzima na uhai, anaendelea kututetea katika majukumu tuliyopewa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Rais, kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya. Tumeona Bwawa la Mwalimu Nyerere sasa hivi limekamilika kwa asilimia kubwa sana na mategemeo sasa hivi nchi yetu umeme utatulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Doto Biteko kwa kazi kubwa na kasi ambayo anaendelea kuifanya. Tumeona mabadiliko makubwa kwa muda mfupi. Tunaendelea kumwombea Mwenyezi Mungu aendelee kumpa hekima na kumsimamia katika majukumu aliyopewa ambayo ni mazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Kwa muda mfupi anafanya kazi kubwa na tunaiona jitihada yake. Tunaendelea kumwombea Mungu amsimamie katika haya majukumu aliyonayo. Naomba nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya katika majukumu aliyopewa kwenye Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Katavi wananchi wana hamu sana na gridi ya Taifa. Naomba niipongeze sana Serikali, tayari tumeona Kituo cha Kupoozea Umeme pale Ipole kimekwisha, tumeona kipozeo cha umeme pale Inyonga tayari kimekamilika na vilevile tumeona kipoza umeme katika Mji wa Mpanda tayari kimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona nguzo tayari zimewekwa, tukipita katika maeneo ya Barabara, lakini mpaka sasa hivi gridi ya Taifa ya Mkoa wa Katavi ina 56% tu mpaka muda huu ninapoongea hapa. Mwisho wa mkataba ambao na tulivyoahidiwa tutapata gridi ya Taifa, ni tarehe 30 mwezi Juni, 2024. Hapa naona takribani bado miezi miwili ili tuwashiwe gridi ya Taifa. Hata hivyo, kutokana na mazingira tunayoyaona si rahisi mwezi Juni kupata gridi ya Taifa kwa sababu nguzo zimewekwa tu. Naomba nipongeze wananchi wamelipwa fidia kote ambako nguzo zinapita. Tumeshawalipa fidia naomba nipongeze sana kwa hili, lakini tunaona kasi ya gridi ya Taifa kufika Mkoa wetu wa Katavi bado inasuasua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze kwa kasi ambayo tumeona, sasa hivi tumebadilisha kutoka kwenye nguzo za mbao tunakwenda kwenye nguzo za *cement*. Tumeona zipo katika maeneo yetu tukipita barabarani. Naomba sana kasi ya gridi ya Taifa Mkoa wa Katavi iongezeke, kwa sababu Mkoa wa Katavi ni mkoa wa kiuchumi, kuna viwanda, kuna mambo mengi na kuna wananchi wengi ambao wamekuja ili kuwekeza, lakini kutokana na kukosa gridi ya Taifa wameghairi na mpaka sasa hivi kuna miradi mingi na viwanda vingi vimesimama kutokana na kukosa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mkoa wa Katavi umeme tunaotumia ni wa ma-*generator*. Sasa hivi yale ma-*generator* yamechoka. Umeme Mkoa wa Katavi haujatulia, unazima kila wakati, biashara za wananchi wa Mkoa wa Katavi sasa hivi zimesuasua sana, umeme ni uchumi. Sisi tuna viwanda; kutokana na ukulima tuliokuwa nao ndani ya Mkoa wetu wa Katavi wananchi wanalima mpunga na kuna viwanda vya kuchakata mpunga. Sasa hivi vinasuasua kutokana na umeme kutotulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua 56% mpaka tuje kupata gridi ya Taifa siyo leo. Naomba basi tuongezewe hata ma-*generator* mawili, kwa sababu Mkoa wa Katavi kuna ma-*generator* matano tu. Tuongezewe ma-*generator* mawili ili kuongeza nguvu ili uchumi wa wananchi wa Katavi uweze kusonga mbele. Najua kuna mikakati na kwenye bajeti hii ametupangia bajeti kuhakikisha kwamba gridi ya Taifa inakamilika. Naomba sana, basi sisi Mkoa wa Katavi tunaomba

Naibu Waziri Mkuu, mwaka huu tuweze kupata gridi ya Taifa ili na sisi umeme wetu uweze kutulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *REA*. Naomba nimshukuru Mkurugenzi Mkuu wa *REA* kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Ndani ya jimbo langu nina vijiji 54, vijiji 53 vyote vimepata umeme kasoro Kijiji kimoja cha Kanoge mpaka sasa hivi hakijapatiwa umeme wa *REA*. Katika ramani Kijiji chetu cha Kanoge kilirukwa. Naomba kijiji hiki kiweze kupata umeme, kimebaki kijiji hiki peke yake ambacho hakina umeme wa *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunapeleka umeme katika vitongoji. Katika vijiji vyetu awamu ya kwanza na awamu ya pili tumeruka taasisi hususan shule za msingi, makanisa, hatujawafikishia umeme wa *REA*. Naomba kupitia hii awamu ya vitongoji, basi wapitishe umeme kwenye taasisi zetu, makanisa, shule za msingi, shule za sekondari ili watoto wetu waweze kusoma vizuri kwa sababu umeme ndiyo utawafanya waweze kusoma kila wakati, muda wote na vilevile kutumia *computer*. Sasa hivi Serikali imeelekeza kupeleka TEHAMA katika shule zetu; sasa, umeme haujawafikia. Naomba sana huu umeme unaoenda sasa hivi kwenye vitongoji vyetu, basi uende katika taasisi mbalimbali kama vile makanisa, misikiti, shule zetu za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii sisi kama Wabunge kwanza tunaomba tushukuru, tumepewa majiko ya gesi, tumepeleka katika maeneo yetu ya vijiji ili kwenda kuhamasisha ili kuhakikisha sasa hivi wananchi wanatumia majiko ya gesi kwa ajili ya kuepukana na kukata miti hovyo na wasitumie mkaa kwa sababu ya uharibifu na hali ya dunia jinsi inavyokwenda. Sisi wenyewe tumeshajionea mafuriko. Tumeona athari kubwa katika nchi yetu imetokea. Hata hivyo, majiko ya gesi ni gharama sana. Naomba Serikali kupitia kampuni mbalimbali ambazo wanauza majiko ya gesi, washushe bei kidogo ili wananchi waweze kununua, kwa sababu kutokana na gharama kubwa wanashindwa kumudu. Wapunguze gharama ili waweze kutumia majiko ya gesi na tuweze kutunza mazingira yetu vizuri katika maeneo yetu ya vijiji pamoja na vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru na naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Richard Lupembe. Sasa namwita Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mheshimiwa *Engineer* Samweli Xaday Hhayuma ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante mtani wangu kwa kunipa nafasi ya kujadili bajeti ya Wizara yetu ya Nishati jioni ya leo. Kwanza nitangulie kwa kutoa taarifa za kusikitisha, ambazo zilitokea juzi katika Jimbo letu la Kilwa Kaskazini, katika Mji Mdogo wa Somanga ambapo tulipoteza wananchi wetu (wapigakura wetu) 13 katika ajali mbaya iliyotokea katika Mji Mdogo wa Somanga. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia taarifa ya pili ningependa kuikumbusha Serikali. Wilaya yetu ya Kilwa imekuwa ikikumbwa na mafuriko kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa na hivyo kupelekea athari mbaya za vifo, nyumba zaidi ya 200 kuanguka, mashamba kusombwa na maji, lakini pia hifadhi za chakula kusombwa na maji. Tunaiomba Serikali iiangalie Wilaya yetu ya Kilwa kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya ya kuwekeza fedha nyingi akiwa na dhamira njema ya kuhakikisha kwamba anatatua tatizo la nishati katika nchi yetu ya Tanzania. Pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Mashaka Biteko kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya. Kwa muda mfupi tangu ameingia madarakani kwa nafasi hii kwa kweli amefanya kazi kubwa inayostahili pongezi kwa kushirikiana na msaidizi wake, Naibu Waziri dada yangu Judith Kapinga. Nawapongeza sana, pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Nishati na taasisi zote zilizo chini ya Wizara yao. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kuzungumzia Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kazi imefanyika kwa ufanisi mkubwa. Sasa hivi tuko katika hatua za mwisho za utekelezaji wa mradi ule ambao utatugharimu jumla ya shilingi trilioni 6.5 ambapo sasa umefikia asilimia 97.43. Ni hatua kubwa imepigwa. Kwa hiyo niiombe Serikali iendelee kuusimamia vizuri mradi ule. Pia ili kuepuka ulipaji wa riba naomba mkandarasi aendelee kulipwa kwa wakati ili tupate matokeo mazuri na tija ambayo itakuza uchumi na kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, napenda kuzungumzia mradi wa megawati 20 ambao umetekelezwa hivi karibuni na Kampuni ya kizalendo ya *Power Associate Limited* kule Mtwara. Kwa kweli mradi umekwenda kwa ufanisi mkubwa, umegharimu fedha kidogo jumla ya shilingi bilioni 3.6 na umekamilika kwa wakati. Hii inaonesha namna gani Wizara yake Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu haikufanya makosa kumpa mkandarasi mzalendo kazi hii. Niiombe Serikali iendelee kuwaamini wakandarasi wetu wazalendo, siyo tu kwa Wizara ya Nishati bali wizara zote pamoja na halmashauri zetu zote na taasisi zote za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa sasa umeme unapatikana kwa uhakika, baada ya kuwa tumekarabati ule mtambo wa uzalishaji wa umeme pale Somanga wa Megawati 2.5. Kazi iliyobaki ni kukarabati pia miundombinu na usambazaji wa umeme. Tunahitaji sana nguzo za zege, kwa sababu tumetoka kwenye kukatika umeme kwa zaidi ya mara 15 kwa siku. Jana naangalia ripoti ambazo huwa wanatutumia wataalam wetu wa *TANESCO*. Jana umeme umekatika mara nne Wilaya ya Kilwa. Mara moja walikuwa wanakata miti kwa hiyo wakalazimika kukata umeme, lakini shida mara tatu ulikatika kwa sababu ya miundombinu ambayo ni dhaifu. Kwa hiyo, naomba ile miundombinu iondolewe iwekwe ya zege ili umeme ufike kwa uhakika iwe mvua iwe jua, kukitokea hata ule moto kichaa, basi mambo yote yaweze kwenda vizuri. Nina hakika sasa kusini inakwenda kufunguka na uwekezaji utaongezeka, uchumi utakua pia hata wale wafanyabiashara wadogo wadogo ambao walikuwa wanategemea umeme, wataweza kutumia umeme na kuleta ufanisi katika shughuli zao za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia ule mradi unaotekelezwa kupeleka gridi ya Taifa kutokea Songea na Tunduru kupitia Masasi uweze kutekelezwa kwa haraka ili hii tija sasa iweze kuongezeka na tuwe na *alternatives* nyingi za kupata umeme wa uhakika katika Mikoa yetu ya Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa *REA,* napenda kuzungumzia kijiji changu kimoja, kinaitwa Kijiji cha Hanga. Tangu mwaka 2020, wakati vijiji vingine vilipokamilisha utekelezaji wa umeme wa *REA II* kile kijiji kimetelekezwa. Ningeiomba Wizara na Taasisi yake ya *REA,* iweze kukiangalia Kijiji cha Hanga. Wale wananchi wamekuwa wakilalamika tangu wakati wa kampeni, hadi uchaguzi unafanyika mpaka leo lakini kile kijiji hakijaweza kuunganishiwa umeme. Naomba *REA* na Wizara wakisimamie ili kipate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *CSR* naomba Bomba la Gesi limepita kutokea Mtwara katika kata zangu tatu. Kata mbili hizi zimekuwa angalau zinaonja manufaa ya kupita kwa gesi katika yale maeneo, Kata ya Tingi na Somanga, lakini Kata ya Miteja kwa kweli haijawahi kunufaika na chochote. Pamoja na juhudi zinazoendelea za kupeleka umeme wa mitaani katika Mji Mdogo wa Somanga, niiombe Serikali basi iangalie Kata ya Miteja ili angalau tujengewe hata kituo cha afya, kwa sababu wananchi wa kata ile wamekuwa wakihangaika kwenda katika maeneo ya mbali kufuata huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, naomba kuzungumzia *LNG*. Mpaka sasa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ufahamu haujatolewa wa kutosha kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya *LNG* katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Ningeomba ufahamu wa kutosha utolewe ili watu wa Mikoa yetu hii ya Lindi na Mtwara wajue kinagaubaga, kwamba watanufaika na nini na ule mradi. Pia hata sisi Wabunge katika maeneo mengi tumekuwa hatujui sana haya mambo. Kwa hiyo hata viongozi tunastahili pia kupewa elimu ya kutosha kuhusu utekelezaji wa miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane. Namwita sasa Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafuatia Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai na kuniwezesha kusimama jioni hii kwenye Bunge lako Tukufu na kutoa mchango wangu kwenye hotuba iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama iliyo ada kwanza niwashukuru Naibu Waziri Mkuu, Naibu Waziri wa Nishati na watendaji wote wa Wizara hii ya Nishati kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kuliangaza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu ya leo naomba niielekeze kwanza kwa upande wa *REA*, ama kwa hakika *REA* wanafanya vizuri. *REA* Liwale yenye vijiji 76 tumebakiza kijiji kimoja ili kifikiwe na umeme na vijiji vitatu nimeambiwa viko njiani bado vinasubiri ukaguzi, jambo hili ni la kusifiwa sana. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale ni wilaya ambayo sisi hatuna mitaa, sisi tuna vijiji, Wilaya yetu ya Liwale Mjini ina kata tatu. Kata hizi ni Kata za Likongowele, Nangando na Liwale Mjini, hatuna mtaa. Sasa, shida iliyopo ni kwenye malipo ya umeme. Hawa watu ambao wako kwenye hizi kata za Liwale Mjini, wanatakiwa walipe shilingi 350,000 jambo ambalo si sawa kwa sababu wana sifa zote za kuwa vijijini. Iko Kata ya Liwale B; hii kata iko kilometa mbili kutoka Liwale Mjini, vijiji vyake vyote vinalipa shilingi 27,000, na kwenye Kata hizi tatu za Liwale Mjini, viko vijiji zaidi ya kilometa mbili kutoka Liwale Mjini lakini vinatakiwa vilipe shilingi 350,000, jambo hili haliwezi kuwa sawa. Kuna Vijiji vya Kuchocholokana, Nangando, Nganyaga, Naluleo, Kilipwike na Hulia, hivi vyote ni vijiji na vina sifa zote za vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali wapelekewe umeme; hawa watu walipe shilingi 27,000 kwa sababu wana sifa zote za vijiji. Kama ni suala ya vipato, kukaribia mjini haina maana kwamba kipato chako ni cha juu. Wapo watu wanaishi vijijini, wana kipato kikubwa kuliko hata hawa ambao mnawaita wako mjini. Jambo hili naomba tulichukulie vizuri na tulielewe vizuri, naomba sana Mheshimiwa Waziri, hawa watu waendelee kulipa shilingi 27,000 ili waweze kufikiwa na umeme kama wanaopewa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la *CSR*; ninapozungumzia *CSR* nazungumzia *CSR* ya Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mwaka jana wakati nachangia hapa nilitoa hoja ya kuiomba Serikali itambue kwamba Liwale ni miongoni mwa wilaya inayochangia ardhi kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere na leo nimekuja na takwimu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Mwalimu Nyerere lina *square metre* 1,194,400,000, *contribution* kwa kila wilaya, Kilombero wana *square metre* 552,280,155, Liwale wana *square metre* 341,406,683, Morogoro wana *square metre* 176,660,786, Rufiji wana *square metre* 99,925,691, Ulanga wana *square metre* 24,126,686, huo ndiyo mchango wa ardhi kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakuja kwenye hiyo inayoitwa *CSR*, kwanza ninachofahamu, miradi yote inayotekelezwa na *CSR* kwa fedha za *CSR* huwa inakwenda sambamba na mradi husika, lakini leo Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere unakwenda kufika mwisho lakini hakuna mradi hata mmoja uliotekelezwa kwa fedha za *CSR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zisizo rasmi; mgao wa *CSR* Bwawa la Mwalimu Nyerere haukufuata sheria. Hapa mimi nashindwa kuelewa, Serikali waje na majibu, hivi shida ni Sheria ya *CSR* au *CSR* haifahamiki au watu wanafanya makusudi kukiuka *CSR*? Kama unaweza ukapeleka Mradi wa *CSR* shilingi milioni 80 Kigoma ikajenga Chuo cha TEHAMA, ukapeleka Mradi wa *CSR* Dodoma shilingi milioni 40 ukajenga Chuo cha Tiba, shilingi milioni 40 mnataka kuipeleka

Tanga ikajenge Chuo cha Tiba, ni sawa kwa jina kwamba huu mradi ni Mradi wa Kitaifa, nakubaliana na hilo, lakini iko miradi ya Kitaifa, kuna *SGR* ni Mradi wa Kitaifa, *CSR* yake itagawiwa kama ilivyogawiwa hizi? Kuna Bomba la Mafuta la Hoima, Chongoleani – Hoima Uganda, nalo *CSR* yake itagawiwa kama ilivyogawiwa hii? Kuna Mradi wa Daraja la Kigongo – Busisi nalo ni Mradi wa Kitaifa, *CSR* yake itafika lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna Mgodi wa Mererani, kuna Mgodi wa Bulyanhulu, kuna Mgodi wa *North Mara*, *CSR* yake itaenea kama ambavyo wanafikiria hili? Kwa nini jambo likiwa ni...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:**...habari za Kusini kunakuwa na songombingo songombingo? Naomba ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka kuna Taarifa. Taarifa tafadhali.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa, niko hapa naitwa Mheshimiwa Tabasam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasamu, tafadhali karibu.

## TAARIFA

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba nimemsikia mchangiaji anasema Miradi ya *CSR* namna inavyosambazwa pesa zake na akataja Daraja la Kigongo – Busisi. Sisi *CSR* ya Kigongo – Busisi hatujawahi kuiona. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sifikirii kuipokea taarifa yake, ngoja niipokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri mwenye dhamana anahitimisha hotuba yake mwaka jana kuhusiana na *CSR* alisema

hapa mbele kwamba, tunakwenda kujenga miradi ya Kitaifa lakini hata hivyo kwa ile sehemu ambayo imehusika moja kwa moja *direct* tuleteeni maandishi mahitaji yenu tuweze kutekeleza. Mimi ni miongoni mwa nilioongea na Mkurugenzi wangu tukaandika miradi tukapeleka, mpaka leo hatujui mwanzo wake ni nini wala inaishiaje. Jamani, watu wanasema ukitaka kula na kipofu usimshike mkono, kwa sababu wameamua kula na kipofu, basi angalau watudanganyedangaye. Hivi kweli mahali ambapo tunachangia zaidi ya mita 340 na pointi, tushindwe kupata hata zahanati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Liwale tuna stendi yetu pale ya kisasa, tunavurugana huu mwaka wa 10 hatujaweza kuijenga. Tuna uwanja wetu wa mpira ambao umejengwa na halmashauri, tunategemea tungepata hapa angalau hata shilingi bilioni moja, hata shilingi bilioni mbili, shilingi bilioni tatu, wanakula na vipofu tunaona hili jambo wanalolifanya haliko sawasawa. Haiwezekani Liwale ambayo inachangia kilometa nyingi namna hiyo tukose hata shilingi bilioni tano, nini kinafanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo takwimu hapa zisizo rasmi; wanasema hawa wenzetu wa Morogoro wana shilingi bilioni 10, Pwani wana shilingi bilioni 10, yaani Pwani yenyewe wamesema wanaenda Kisaki na hawa ndugu zetu wa Pwani wanasema itapelekwa Mloka, sisi Liwale wanatuweka wapi au hatuhusiki? Hapa sioni nia njema, sioni nia njema ya Serikali kwenye mradi huu, kwenye *CSR* hii na ndiyo maana mpaka leo hakuna mradi uliotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua unapokuwa na nia ambayo siyo njema hata Mwenyezi Mungu naye ana karama zake. Ndiyo maana unakuta huu mradi unayumba, mpaka leo hii hakuna hata mradi mmoja uliotekelezwa, lakini ni kwa sababu hawajanyooka, wangenyooka haya mambo yangeenda lakini kwa kuwa waliamua kuzungukazunguka, mara wapeleke Kigoma, mara wapeleke Tanga, mara wapeleke wapi, matokeo yake tumekwenda mahali tumekwama, hili jambo haliwezi kuwa sawa. Nawaomba sana, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, asiponieleza sababu ya kupeleka shilingi bilioni 80 Kigoma nitashika shilingi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka. Sasa namwita Mheshimiwa *Engineer* Samweli Xaday Hhayuma, atafuatia Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay na Mheshimiwa Athuman Almas Maige ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye Sekta ya Nishati na nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati, nampongeza Katibu Mkuu, Mhandisi Felchesmi Mramba na timu yote ya Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Sekta hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana timu yangu ya mkoa ikiongozwa na Meneja wa Mkoa na timu ya wilaya ikiongozwa na Meneja wa Wilaya, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ndani ya maeneo yao na Meneja wangu wa wilaya kwa ushirikiano mkubwa ambao ananipatia. Pia, naipongea sana ile timu ya Wizara kwa sababu kazi kubwa inayofanyika tunaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na changamoto kubwa ya mgao wa umeme; kazi kubwa imefanyika ambapo wakati mwingine wengine tunaweza tusione sasa hivi kilichofanyika kwa sababu tulisema wakati ule kwamba, changamoto ilikuwa ni maji kwenye maeneo ambayo tulikuwa tunategemea umeme kuzalishwa kwa maji na mvua zinanyesha. Niwahakikishie kwamba kazi kubwa imefanyika kuhakikisha kwamba tatizo la umeme limeondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuthibitisha hilo, umeme kwenye gridi ya Taifa umeongezeka kutoka megawati 1,872.1 Mei, 2023, mpaka megawati 2,138 Machi, 2024. Kazi hii ni kubwa na ukiangalia kwa sasa hata kama kuna malalamiko, lakini yamepungua sana. Kati ya sehemu ambayo tumefanikiwa sana ni kuingiza umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo tunatarajia litazalisha megawati 2,115

ambapo mpaka sasa tumeshaingiza megawati 235 kwenye gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani, mwaka jana wakati tunajadili Bajeti ya Nishati niliiomba Wizara hii iangalie maeneo ndani ya Wilaya ya Hanang ambayo yalipata umeme muda mrefu. Hivi ninavyoongea tumeidhinishiwa vitongoji 49 na wakati ule nilitaja eneo la Gitting kama mfano, eneo la Nangwa kama mfano, eneo la Gendabi kama mfano na eneo la Mogitu kama mfano wa maeneo ambayo yalipata umeme muda mrefu na nikasema wananchi wameongezeka sana na maeneo hayo yaangaliwe ili wale ambao wamejenga nyumba zao na wanaishi gizani wapate umeme. Mpaka sasa juhudi zinafanyika kuhakikisha kwamba umeme unaenda kwenye vitongoji vya maeneo hayo ambayo nimetaja. Naishukuru sana Serikali na wakati huo huo vitongoji 15 navyo vikiendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi kwenye eneo la utekelezaji wa miradi; tulipata mkandarasi anaitwa Daniel ili atekeleze mradi wa kupeleka umeme kwa wachimbaji wadogo, kwenye viwanda lakini pia kwenye visima vyetu vya maji. Maeneo ambayo tuliyaainisha wilayani, eneo la Getasam, eneo la Moram, eneo la Mara B, Gijega, Jorodom, eneo la Muungano, eneo la Quaredan na eneo ambalo tunatarajia kuwa na mgodi wa madini ya mwanga, utendaji wake siyo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara imwangalie mkandarasi huyu kwa umakini kuhakikisha kwamba kazi inafanyika, amefanya *survey* kipindi kirefu akapotea, tunavutana sana na kazi haiendi sawasawa. Naomba huyu aangaliwe ili kuhakikisha kwamba wananchi ile huduma wanayoitarajia waipate kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie eneo la uzalishaji wa umeme kupitia Sekta Binafsi, kwenye taarifa ya Wizara, Sekta Binafsi inazalisha megawati 31.8 pekee. Nchi yetu ina vyanzo mbalimbali vya umeme, tuna umeme chanzo cha makaa ya mawe, chanzo cha umeme jua, joto ardhi tuna upepo na vyanzo vingine. Kusema Sekta Binafsi mpaka sasa inachangia megawati 31.8 pekee, wakati huohuo tukitegemea kwamba Serikali iendelee kuwekeza

rasilimali kidogo ambayo tunahitaji kwenye Sekta ya Elimu, rasilimali hiyo hiyo tunahitaji kwenye Sekta ya Afya ili itoe huduma, unaona kabisa kwamba kuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 kuja 2012 tulikuwa na changamoto kubwa sana ya mgao wa umeme na ukiangalia hata bajeti ya Wizara kwa sasa kwenye upande wa maendeleo umeshuka karibu 36, maana yake keki tuliyonayo tunaigombania na haitoshi vizuri. Nashauri kwenye eneo hili, Wizara ione namna ya kuishirikisha Sekta Binafsi kwenye uzalishaji wa umeme. Tuzalishe mabilionea wa Tanzania kutoka kwenye Sekta ya Umeme na hii inawezekana. Tuwashirikishe, kama ni sera inasumbua tuangalie namna ya kuibadilisha ili tuone Sekta Binafsi inashiriki na hatimaye tunazalisha umeme wa kutosha, tukiwa na umeme wa kutosha maendeleo ya nchi yetu yataenda kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, wakati tukiwa na hali mbaya ya mgao wa umeme, Jimbo la Hanang tulikuwa na hali mbaya mara mbili. Changamoto kubwa ni kwamba sisi hatuna kituo cha kupooza umeme. Waya ukiguswa tu na ndege umeme umekatika wilaya nzima na hatuna umeme. Tukigawiwa megawati zile chache, maana yake ni wilaya nzima, tukikatiwa wilaya nzima iko gizani, nguzo ikianguka wilaya nzima iko gizani. Changamoto hii niliiwasilisha hapa Bungeni mwaka 2021 na Serikali ikanijibu, kwa ruhusa yako naomba ninukuu majibu ya Serikali; "Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme nchini *(TANESCO)* imeanza taratibu za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na kituo kidogo *(switchyard)* cha *kilovoti* 33 kutoka njia kuu ya kusafirisha umeme wa msongo wa *kilovoti* 400, inayoendelea kujengwa kutoka Singida hadi Namanga katika Kijiji cha Mogitu, Wilaya ya Hanang.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo hicho kitaboresha hali ya upatikanaji wa umeme kwenye maeneo ya Hanang na maeneo jirani na ujenzi wake utaanza Julai, 2022 na utakamilika Julai, 2023 na

gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 2.6. Fedha hizi zinategemewa kutolewa na Serikali kwa 100%." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ninavyoongea hakuna kilichofanyika, ombi langu tu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, wana-Hanang tuna changamoto kubwa na ukisikia tu kila baada ya muda unasikia taarifa ya kukosekana kwa huduma ya umeme na watakwambia sababu ni ukarabati wa hitilafu ambao watasema aidha imetokana na nguzo kuanguka au kitu kingine chochote, baada ya hapo tu itafuata taarifa ya kukosekana kwa huduma ya maji, changamoto ni kubwa, lakini pamoja na changamoto hizi, kwa kuwa nina imani na Mheshimiwa Naibu Waziri ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* naomba hitimisha.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka na utendaji kazi wake, sina shaka na umahiri wake na sina shaka na upendo wake kwa Wana-Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na bajeti yake, sina changamoto nayo, naamini hili atalishughulikia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Samweli Xaday Hhayuma. Sasa namwita Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, atafuata Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa Deus Clement Sangu ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Kwanza nianze kwa kuungana na wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu wa heri, aliyetujalia muda huu leo tukiwa tunajadili mustakabali wa Watanzania, kwa kweli tuna kila sababu ya kumshukuru kwa sababu ya rehema zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua pia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa inayofanyika nchini. Kwanza

kwa jitihada kubwa, hizi juzi tumeona treni ya mwendokasi ikifanya majaribio. Wakati tukiwa mwanzo wa mwaka huu niliuliza swali hapa Bungeni kutaka ziara au huduma ya safari ya treni mwendokasi itaanza lini? Walisema kabla ya mwezi Juni na Serikali imetekeleza kwa wakati, katika majaribio yale Watanzania wamefurahia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kwa kazi kubwa ya kukamilika kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kama mnavyojua, nchi yetu ilitoka kwenye mchakato mgumu wa kukatika kwa umeme na upungufu wa umeme nchini. Hii ni faraja kubwa kwa Watanzania na kwetu sote wawakilishi wa wananchi kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingine ni kwako wewe Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Biteko na Naibu Waziri pia na watendaji wote wa Wizara. Kwa kweli tunakupongeza kwa kuteuliwa kwako kuwa Naibu Waziri Mkuu lakini pia Wizara hii muhimu sana. Umetusaidia sana kufanya kazi kubwa ulipokuwa Wizara ya Madini wakati ule na ikampendeza Rais akupeleke mahali hapo. Pia, kwa kazi kubwa inayofanywa na watendaji wote wa Wizara pamoja na Kamati yetu na taarifa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mchango mdogo katika Hotuba ya Waziri pamoja na Taarifa ya Kamati, lakini kwa kuishauri Serikali. Kwanza natoa mchango huu kwa kuisemea kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, nadhani Watanzania wa sasa kwa sababu tayari bwawa limekamilika, kuna haja kubwa ya utakapokuja pale utoe kauli ya namna gani basi zile nyumba zote zilizo ndani ya mita 20 mpaka mita 30 katika Mradi ule wa *REA*, hazijapata kuunganishwa na mpango huu wa umeme wa *REA*, ziunganishwe zote nchini kwa sababu wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa. Kama tunavyojua Mradi wa *REA* una miaka karibu 10 au na zaidi kutoka utekelezaji wake wa kusambaza umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna majengo mengi sana yapo ndani ya mita 30, mita 20, pamoja na taasisi za Serikali zilizorukwa, lakini pia kwa sababu tayari bwawa limekamilika na uzalishaji wa umeme upo, ni imani yangu kwamba, hizi nyumba zitaunganishwa. Vilevile naamini

hatutakuwa na zoezi la kupunguza maji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini huduma iliyokusudiwa kwa Watanzania itapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza ujazilishi, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kweli hatuwezi kukamilisha zoezi hili. Kwa hiyo, pamoja na Wabunge wenzangu tunaomba sana, wale wananchi wote waliopo ndani ya hizo mita 30, mita 20, utafutwe mpango wa dharura wa kuhakikisha angalau wanaunganishiwa nishati hii. Wengine wamefanya *wiring*, wengine wanasubiri umeme na wanatarajia kwamba, watakapounganishiwa basi kwanza tutapata uzalishaji mkubwa wa umeme kutoka kwenye bwawa lililojengwa na pia tutajibu kiu na matarajio ya Watanzania ambao walikuwa wanasubiri umeme kwa hamu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo naona ni muhimu sana kufanyike mpango wa mapitio. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati sasa hivi tunapozungumza umeme kwenda kila kijiji ifikapo Juni 30, kuna maeneo kwa mfano Jimbo langu la Mbulu Mjini, nina vijiji kama 10, nguzo zimesimikwa ardhini zina karibu miezi nane, miezi sita na nyingine ni karibu mwaka, lakini hakuna umeme wala nyaya zilizounganishwa. Nguzo hizo zinaendelea kuoza ardhini, nadhani kuna haja kubwa ya kufanya tathmini ya namna ya kupeleka nguvu kubwa kwenye kuunganisha umeme kwenye maeneo yote nchini ili kuhakikisha kwamba, angalau maeneo yale ambayo wakandarasi wa kusimika nguzo wamewekwa basi waharakishe na fedha zitafutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa hapa ni kwamba, angalau Serikali ijitahidi katika mwaka huu wa fedha tunaouanza itoe fedha zote ambazo tunaomba kwa ajili ya Wizara hii ili iweze kutekeleza mahitaji ya wananchi kupata nishati ya umeme. Kwa sababu, hatua hii ya ujazilishi tusipofanya jitihada tunakosa tija na manufaa ya ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa sababu, kwa vyovyote vile umeme tutakaouzalisha ni mkubwa, lakini watumiaji watakuwa ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, Serikali iangalie mpango huu wa kutoa kazi za kikandarasi kwa wenzetu hawa kupitia *REA*.

Unakuta mkandarasi mkubwa anashika mikoa mitatu, anatafuta *subcontractors* wengine kwa hiyo, kunakuwa na mkanganyiko mkubwa, huyu analeta nguzo, unakuta hapa amesimika nguzo, mahali pengine hajapeleka waya, mahali pengine hata kuwasha umeme bado, waya zimeunganishwa. Kazi hii itakapokuwa inakwenda katika mazingira ya namna hii, wananchi wanasubiri umeme hawafikirii tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yetu mengi katika majimbo tuliyotoka, hasa Jimbo la Mbulu Mjini, maeneo mengi ni sura ya vijiji. Mimi, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, japokuwa ameniahidi atafanya ziara mwezi Juni katika jimbo langu, lakini Jimbo la Mbulu Mjini tuna kata 10 ambazo zipo vijijini, maeneo yake ni ya vijijini, kata saba za mjini pia eneo la mji kwenye kata tatu tu ndiyo katikati ya mji. Kata nyingine ni za pembeni, ukienda Kata ya Silaloda kwa mfano ni kilometa kama nane, lakini huko ni vijiji hakuna hata nyumba za miji au nyumba zilizokusanyika mahali pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nguzo nyingi zinahitajika na usambazaji wa umeme unahitajika. Kwa hiyo, mpango huu kuunganisha wananchi wetu kwa shilingi 27,000 ukizungumza maeneo ya mji hayapo kwenye huu mpango, siyo sahihi, ukija pale utuambie. Kwa kweli, bado Serikali itazame jambo hili na kuyaweka maeneo haya katika mpango ule wa shilingi 27,000 ili umeme uweze kusambaa vizuri na kuweza kupata huduma iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo ya shule, kwenye makanisa, migodi, visima vya maji, vijiwe vya biashara pamoja na maeneo mengine yenye uzalishaji mkubwa tuna mahitaji makubwa ya umeme kwenye majimbo na hasa Mbulu Mjini. Kuna mgodi wa *TAWA,* ambao umeanza nadhani miaka 10, watu wanatumia majenereta, umeme haujafika. Tunaishukuru Serikali imepeleka nguzo, maeneo kama yale yakifanyiwa tathmini yanaweza kuleta tija katika uunganishaji wa umeme, lakini pia kwa mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukatika kwa umeme. Mkoa wa Manyara nadhani ni mkoa unaoongoza sana kukatika kwa umeme katika Taifa letu katika kipindi kilichopita. Kwa kweli, tunapata kadhia

kubwa kwa wananchi, lakini janga lile lilikuwa kubwa. Hata hivyo, hata sasa bado kuna hali ya kukatika kwa umeme kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu. Nashauri, kama itawezekana tutafute mradi wa dharura wa miundombinu yote iliyochakaa nchi nzima kufanyiwa mapitio, ili walau tujue maeneo gani kwa mwaka huu yatafanyiwa ukarabati kuondoa tatizo hili la leo. Kunatokea tatizo la nguzo, kesho kunatokea tatizo la *transformer*, siku nyingine kunatokea tatizo la hitilafu kwenye njia ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanazalishwa kwa sababu, baadhi ya miundombinu yetu imechakaa na kwa kuwa, imechakaa kuna haja kubwa ya kufanya mapitio kinchi ili kuona tunazalishaje na kuondoa kadhia kubwa kwa wananchi wetu. Tunapata changamoto hiyo ya kukatika kwa umeme Mkoa wa Manyara, lakini pia tuna maeneo ya kijiografia ambayo ni ya vijiji, ambayo ni ya vitongoji. Kauli hii ya kusema umeme utawashwa Juni, 30 kwa kila kijiji, tunampenda sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, yeye ni mtendaji mzuri, je, inatekelezeka? Mbona hii inakuwa ni ajali kabisa ya kisiasa kwa wanasiasa kuanzia sisi Wabunge wote na hata Serikali kwa ujumla? Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, jambo hili litazamwe, Juni ni kesho kutwa, tumebakiza miezi miwili, katika vijiji vyangu 10 vya Mbulu Mjini kutawaka umeme? Japo tayari tumeweka nguzo zote katika kila kijiji, nyingine hazijasimikwa kama kule *TAWA*, nyingine zimesimikwa lakini hakuna waya na inawezekana hata wakandarasi wakatuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, jambo hili linahitaji maandalizi, mapitio yakifanyika nchi nzima tunaweza kuwa na kauli ya pamoja ya kwenda kuwaambia wananchi ili waiamini Serikali yao, lakini pia wajue utaratibu wetu umekaaje. Hawa wakandarasi wababaishaji ni hatari sana, hapa kila Mbunge ukimuuliza hawezi kujua mpango ambao upo kwa jimbo lake kwa kipindi hiki cha mwezi wa Januari kwenda Aprili na Mei kwenda Juni, yaani mipango yao ni ya mfukoni, mipango yao ni ya kutembea nayo, mipango yao haiko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ifike mahali kama ambavyo wanafanya baadhi ya Mawaziri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Hitimisha tafadhali, ahsante.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mengine nitaandika kwa maandishi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuipa Wizara hii fedha nyingi za miradi ambayo imeitekeleza. Nasema huyu ndiyo Rais mwenye upendo kwa Watanzania wote, mwenye utu na mlezi wa wananchi wake, tumpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa usimamizi wake mzuri wa Wizara hii mpaka imefanya mambo makubwa, miradi mikubwa imetekelezeka. Hii ni muhimu sana, hivyo kuleta mafanikio makubwa katika utendaji wa Wizara yote. Pia nawashukuru watendaji wengine akiwemo Naibu Waziri, mtani wangu Judith Kapinga na watumishi wote wa *TANESCO* na *REA* ambao katika Jimbo la Tabora Kaskazini wameweka alama kubwa ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye macho haambiwi tazama. Wizara hii imefanya kazi kubwa hasa katika kujenga miradi ya vyanzo vya umeme na usafirishaji wa umeme nchini kote, Miradi mikubwa kama wa Kinyerezi, Rusumo na ule baba lao wa Bwawa kubwa la Rufiji la Mwalimu Nyerere. Bwawa hili ndiyo mwarobaini wa upungufu wa umeme katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa *REA;* katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini umeme umefika kila kijiji na natumia neno umefika, siyo kuna umeme vijijini, lakini nasema hongera sana katika vijiji vyangu vyote 82 vya Jimbo la Tabora Kaskazini umeme umefika na sasa tunaendelea na ujazilizi wa vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la mambo mtambuka kwa Wizara hii ya Nishati na hasa vijijini kwetu na hata mijini pia, kwa kutumia mkaa na kuni kama nishati ya kupikia au kupata joto majumbani. Hapa ndipo Wizara ya Nishati inachukua majukumu mtambuka, Wizara hii ina jukumu la kuzuia kuenea kwa jangwa nchini kwa kuzuia kukatwa miti kwa kusimamia upatikanaji wa nishati mbadala ya kupikia kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimboni kwetu tunalima tumbaku, zao hili ni la muhimu sana. Hivi sasa tumbaku ndiyo inaongoza kuleta hela za kigeni, kwa mwaka tumbaku inaleta dola milioni 400 sawa na shilingi trilioni 1.2, inafuatiwa na korosho ambayo inaleta dola milioni 200 na ushee. Kilimo hiki cha tumbaku kina matokeo hasi katika miti, tunakata miti mara mbili, wengine wote wanakata miti kwa mkaa na kuni za kupikia. Sisi pamoja na hilo la pili, tunakata miti kwa ajili ya kukaushia tumbaku, lakini hatuwezi kuacha kulima tumbaku, kwetu sisi Wanauyui, Tabora Kaskazini na Tabora yote kwa ujumla. Tumbaku ni muhimu sana kwa kutuingizia dola milioni 400 kwa mwaka ambapo 60% ya tumbaku yote inalimwa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ione umuhimu wa kufanya lolote kuzuia au kuleta afua za kuzuia madhara ya tabia ya nchi. Hivi karibuni wametupatia majiko ya gesi kupeleka kwa wakulima vijijini, nikajiongeza nikaongeza mengine 200 yakawa 500, *impact* au matokeo yake yamekuwa ni makubwa sana. Tunaomba Serikali kwenye mpango wake huu wa kusaidia majiko, maeneo yanayolimwa tumbaku yabaki na matumizi ya kuni kwa tumbaku tu, lakini ile ya kupikia Serikali iweke ruzuku kwenye majiko ili kupunguza kabisa matumizi ya kuni. Hili ni la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la tumbaku hatuwezi kuliacha kwa sababu tunalihitaji sana kwa ajili ya kuleta uchumi wa hela za kigeni.

Kwa kweli, Serikali itoe kipaumbele katika ugawaji wa nishati safi na kama ilivyo ni ajenda ya Mheshimiwa Rais kumtua mama kuni kichwani. Nashauri Serikali itakapoanza kutoa ruzuku ifikirie sana maeneo ambayo miti mingi inakatwa kwa sababu ya kupikia na kukaushia tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuacha kulima tumbaku, narudia mara kwa mara kwa sababu, inatuletea faida sana. Naitaka Serikali kupitia Wizara hii ya Nishati, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na ndugu yangu Naibu Waziri wa Nishati, mlisimamie hilo. Wajaribu ku-*support* tumbaku kwa njia nyingine ili kuokoa miti. Naomba maeneo yote yanayolima tumbaku, siyo Tabora tu, lakini maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la kukatika umeme kila wakati katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini. Wilaya ya Uyui iko mbali, njia ya kwenda Nzega, lakini umeme unaotoka Tabora kwenda Nzega mpaka Isikizya ndiyo huo unakuja mpaka Karangasi na Manyoni. Tatizo lolote likitokea huku Chaya tunapopishana na ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge wa Chaya umeme unazimika mpaka Isikizya kule Uyui, kilometa 130 na hapo wanaanza kutembea na gari kwa saa kadhaa kutafuta *fault* iko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa nilipokuja kwenye maonesho pale kwamba, kumbe njia rahisi ni kujenga Kituo cha Kupoza Umeme pale Isikizya na wakati huu ambapo hawajajenga kituo ipo njia rahisi ya kuweka *load circuit breakers* njiani ili umeme ukikatika mahali fulani kule kwingine umeme uendelee kuwapo. Mazoezi yote mawili, moja ni la muda huu la kuweka *circuit breakers,* lakini la pili ni waweze kujenga Kituo kile pale cha Kupoza Umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui Iskizya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuipongeza sana Wizara hii inafanya kazi kubwa sana na tumeona matokeo yake kwa kumalizia Bwawa la Mwalimu Nyerere, mgao umepungua sana. Tuna imani kubwa, Mwezi Juni tuliwaomba Bunge wamalize mgao huu, Wizara hii itakuwa imefanya historia kubwa sana na Mheshimiwa Naibu Waziri

Mkuu atakuwa ameandika ramani mpya ya matendo mema katika utendaji wake wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deus Clement Sangu, atafuatia Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo na Mheshimiwa Ally Juma Makoa ajiandae.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Nishati. Kama wenzangu waliotangulia, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya hasa katika sekta hii muhimu ya Nishati ambayo hivi karibuni imekumbwa na misukosuko mingi, lakini Mheshimiwa Rais, amesimama imara kuinusuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ambaye pia ni Waziri wa Nishati. Kwa kweli, kwa muda mfupi ambao ameingia katika Wizara hii tumeona mabadiliko makubwa na mimi binafsi, achilia mbali katika ziara za Kamati, nimeona miradi mingi mizuri na usimamizi wenye tija. Nampongeza pia, Naibu Waziri kijana kabisa, dada yangu Mheshimiwa Judith, kwa kazi kubwa anayoifanya, amewaheshimisha vijana kwa kazi yake nzuri. Aendelee kuchapa kazi, Mwenyezi Mungu atambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitaongelea mambo mawili. Jambo la kwanza naanzia pale alipoishia Mheshimiwa Sylvia, hali ya utekelezaji wa Mradi wa *REA,* Mkoa wa Rukwa na la pili ni dhana ya *local content* katika Miradi ya Gesi na Mafuta.

Mwenyekiti, naanza moja kwa moja kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa jambo kubwa ambalo sasa wametufanyia Mkoa wa Rukwa. Mkandarasi ameanza kazi ya upelekaji wa gridi ya Taifa mwezi Novemba mwaka jana na tunaamini kwa kadri ya mkataba, tayari Mkoa wa Rukwa ifikapo mwakani Mwezi Oktoba tutakuwa tumeunganishwa na gridi ya Taifa. Naomba tu Wizara imsimamie

mkandarasi huyu ili itakapofika Oktoba, 2025, mradi huu uwe umekamilika tuondoke kwenye kudoea umeme kutoka nchi jirani na sisi Mkoa wa Rukwa tutegemee umeme kutoka kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema jambo hilo ambalo lina manufaa makubwa kwa mkoa wetu, nakuja kwenye suala alilosema Mheshimiwa Sylvia Sigula. Ni jambo ambalo linatukera sisi kama Mkoa wa Rukwa. Mkandarasi huyu alikabidhiwa kazi ya kupeleka umeme na alitakiwa kazi hii aikamilishe mwaka jana mwezi Oktoba, lakini cha ajabu akapewa *extension* tena ya miezi mitatu. Ilipofika Disemba tukategemea vijiji vyote kwenye ile kilometa moja, vijiji vyote vitawashwa, hakumaliza kazi hiyo akaongezewa tena mkataba wa miezi mitatu ili aweze kumalizia kazi iliyobaki kwa kilometa moja. Cha ajabu mwezi Machi umeisha ile kazi haijakamilika na bado nasikia amewaandikia tena *REA* waje huko tena wamwongezee miezi mingine, sijui mingapi mpaka kufika mwezi Juni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linatukwaza, kila Mwanarukwa linamkwaza. Jimbo la Kwela tu kuna vijiji 17 havijapata umeme hata ile kilometa moja ya kwanza hajaweza kukamilisha huo mradi. Nashangaa sana *REA* kwa nini walimwongezea kilometa mbili mkandarasi ambaye tunamlalamikia usiku na mchana, kila siku tunapiga kelele, lengo lilikuwa ni nini? Namwomba sana kwa heshima kubwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, jambo hili walichukulie kwa uzito mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa, Ndugu yangu *Engineer* Ruhavi, Mameneja wangu wa Wilaya na watendaji wote wanahangaika usiku na mchana, lakini mkandarasi huyu anawasumbua. Juzi nilikuwa ziara Kata ya Mnokola, Kijiji cha Kisalala, Mnokola na Mititi, ameenda kushusha nyaya pale, baadaye baada ya wiki moja anaenda kubeba zile nyaya. Nauliza mkandarasi kwa nini unahamisha? Yeye alinidanganya kwamba, tumeibiwa; sasa nikauliza, mwanakijiji gani anaweza kwenda na *crane* akabeba zile nyaya? Mwanakijiji anapeleka wapi zile nyaya? Kwa matumizi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumekuwa na ulaghai na nashangaa sana kama Menejimenti ya *REA* wamekaa naye huyu vikao vingi sana vya mashauriano, sasa kwa kazi hii ya umma yenye maslahi makubwa hivi, kwa nini tubembelezane? Kwa nini tusichukue hatua tumwondoe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata bahati ya kuzungukia miradi mingi kupitia Kamati ya Uwekezaji kwa mikoa mingi. Mikoa mingi niliyopita kama Mwenyekiti wa Kamati, nimekuta umeme 99%, mkandarasi amemaliza. Ukija kwangu ndio kwanza nusu ya vijiji tulivyotakiwa kumaliza mkandarasi hajakamilisha, Mkoa wa Rukwa vijijini 40. Leo hii ukifanya ziara Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ukifika Rukwa ukigonga tu Ofisi ya CCM ya Mkoa, salamu ya kwanza ambayo itamkatisha tamaa ni jinsi ambavyo Mkoa wa Rukwa tumeumizwa na uzembe wa mkandarasi huyu kufikisha umeme. Sijui na sasa hivi anafanya kazi kwa mkataba gani na kwa jinsi wanavyofanya *extension, extension* zitakuwa zina muda mrefu kuzidi *original contract*. Maana yake wanampa tu, akija anawandikia wana-*approve,* akija anawandikia wana-*approve*. Sijajua ana *specialty* gani? Mkandarasi huyu mpaka tuanze kumu-*entertain* anatuumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Bodi ya *REA* imepita kwenye Kijiji cha Chombe na Kianda Igonda, kulitokea hitilafu hajakabidhi ule mradi lakini vijiji hivi vimewaka. Wiki tatu hawaja-*resolve* lile tatizo na Bodi ya *REA* imeenda kumwagiza bwana tarahe 19, ahakikishe amewasha umeme kwenye Kijiji cha Chombe na Kianda Igonda. *Now,* Bodi ya *REA* kabisa wanaomwajiri wamedharaulika, sasa atamsikiliza nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu jambo hili ni jambo ambalo limetukwaza sana Rukwa, limetukwaza sana Jimbo la Kwela. Tunaomba kabisa afanye jambo la pekee kabisa, aunde timu ichunguze kuna shida gani kwa huyu Mkandarasi wa Mkoa wa Rukwa. Baada ya kusema hayo, nisiende sana huko nadhani ujumbe mmeupata vizuri jinsi tulivyokwazika na mkandarasi huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni suala la *local content* limeongelewa sana, mambo ya *CSR* na yameongolewa kwa namna mbalimbali humu ndani. Kuna jambo moja ambalo nataka niishauri Wizara hii ya Nishati, *EWURA* ndiyo tumewapa jukumu la kusimamia dhana yote ya *local content* kwenye Miradi yote ya *Oil and Gas*, lakini kuna hili suala linaloendelea la Bomba hili la Mafuta la kwenda Uganda *(EACOP)*, kuna mambo ambayo tuliyaona yanasikitisha. Tumekuta kwanza, *CSR* zinatolewa lakini katika utoaji wenyewe wa *CSR* ni *confidential.* Unafika halmashauri wanaomba waambiwe *contribution* waliyopewa ni kiasi gani? Wale wanaowasaidia wanasema sisi *policy* zetu zinatukataza ku-*disclose*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *interpretation* yake ni nini? Unapewa msaada, yeye hatujui ataenda ku-*declare* vipi kwenye vitabu vyake? Kwa maana hiyo, inaweza ikatumia *CSR* kama sehemu kufanya *tax evasion.* Anafika pale ametoa madawati ya milioni tano, kwenye vitabu vyake ataandika bilioni tano. Kwa hiyo, tukawaambia haiwezekani *CSR* ikawa *confidential* na kuna *CSR policy. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mikataba ile ya ujenzi ule wa bomba inatakiwa baadhi ya kazi zifanywe na kampuni za wazawa kwa maana ya Kampuni za Kitanzania. Kampuni za Kigeni zinatufanyia ujanja wanapewa ile zabuni wakishapewa zile *tender za sub-contract* wanaleta kampuni za kwao kule za kigeni. *Implication* yake ni nini? Tufanye *capital flight* hela ilitakiwa kubaki kujenga uchumi wa nchi yetu inaenda kule kwao. Sasa sisi tumeingia ubia, kwa mfano *EACOP* na Uganda, pesa zetu tumeziingiza pale badala yake Uganda watanufaika. Sisi kwa sababu dhana ya *local content* hatuisimamii vizuri tutapigwa. Niombe na tuliwaambia watu wa *EWURA* wafanye *investigation* watuletee ripoti ili tuisaidie nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, atafuatia Mheshimiwa Ally Juma Makoa na mchangiaji wa mwisho atakuja Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kusema mawili, matatu kwenye sekta hii muhimu sana ya nishati katika nchi yetu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa utendaji wake mzuri. Pia, niseme tu ukweli Mheshimiwa Dkt. Doto ni mchapa kazi, ni mtendaji na ni mtu ambaye ni msikivu kwa kusema kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa naongea naye akaniambia bwana hizi kazi wakati wowote (usiku wa manane) unasikia simu kuna jambo limetokea huko inabidi uachane na mambo yako yote ukaanze kushughulika na masuala ya dharura. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Doto tunakupongeza sana pamoja na timu yako yote akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri na Menejimenti yote kwa ujumla. Hata kule mkoani kwetu meneja wa mkoa yule anatupa ushirikiano wa pamoja na wilaya kwa ujumla, tunafanya nao kazi kwa kushirikiana. Kimsingi Wizara hii ipo karibu na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, pamoja na Wizara kwa ujumla kwa kukamilisha kwa kiwango kikubwa sana Bwawa la Mwalimu Nyerere, ambalo tunasema ndiyo inaenda kuwa ndiyo tiba ya tatizo la umeme hapa nchini. Tulikuwa na janga kubwa la mgao wa umeme, sasa ule mgao tuseme ni kwamba umeondoka imebaki tu sababu za kiufundi. Kwa hiyo, hii inatupa matumaini makubwa sisi Wabunge ambao tupo moja kwa moja kwa wananchi kule. Likitokea tatizo anayepigiwa simu ni Mheshimiwa Mbunge bwana mbona mnakatakata umeme, lakini sasa hivi hilo tatizo halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweka *connection* moja kwa moja Bwawa hili la Mwalimu Nyerere na nataka niseme hapa kwamba, Bwawa la Mwalimu Nyerere ni neema kubwa sana kwa Watanzania, kwa sababu linaenda kutuhakikishia uhakika wa uzalishaji wa umeme. Kwa hivyo, hata tunaposema tunakwenda kwenye Tanzania ya Viwanda, hata wawekezaji sasa watakuwa na uhakika wanapoleta *investment* zao hapa. Wanakuwa na uhakika wa upatikanaji wa umeme. Kwa hiyo, niendelee kusema kabisa kwamba kusitokee watu wanabeza beza hili Bwawa, ooh mara sijui kulitokea nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hapa hapa niunganishe na kutoa pole kwa Watanzania waliopatwa na majanga mbalimbali ya maji kutokana na mvua kubwa ikiwemo kule Hanang na yale maporomoko yaliyotokea kule Mbeya kwa Mheshimiwa Spika. Hata nadhani leo tumepata taarifa kule Mikocheni Njia ya *ITV* pale, maji yamefunga barabara yaani yamefurika imekuwa kama kabwawa hivi. Sasa kule nako kuna bwawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu kwamba hizi mvua zimekuwa *excessive* mwaka huu na ni masuala ya hali ya hewa. Kwa hiyo watu lazima waelewe, tusifike mahali tukaanza kubeza juhudi zinazofanywa na Serikali kwa ku-*connect* na mvua, mvua haiwezi kuzuilika. Hii mvua ni ya Mungu, hatuwezi ku-*connect* utendaji wa Serikali na mvua. Nitumie nafasi hii kuwashauri Watanzania wenzagu, pale tunapoona jambo zuri linafanyika tuliunge mkono na tulipongeze. Kama tunaona jambo halipo sawasawa tushauri kwa busara na kwa utulivu. Tusiwe tunaongeaongea vitu vingine ambavyo havina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu hapa kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Waziri anapaswa kujielekeza sasa hivi kwenye sekta hii ya umeme ni kuhakikisha tunajikita ama tunajielekeza kwenye miundombinu ya umeme. Haiwezekani ikafika mahali sijui kuna *transformer* imesababisha umeme umekatika mahali ikawa ni kelele nchi nzima, hapana. Hivi ni vitu vya kawaida ambavyo ni vya kitaalamu *(technical)* ambavyo inapaswa Wizara wawe navyo karibu. Nguzo imedondoka mahali au imekatika inaleta kelele ambazo hazina tija. Kwa hiyo, lazima tujikite kwenye vitu hivi vya kitaalamu *(technical)* ili kuhakikisha tunaondoa malalamiko yasiyokuwa na tija ambayo kuna watu wanaingia humo humo wanaanza kupandikiza chuki ambazo wala hazina msingi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye kuzungumzia mambo mahususi kwenye jimbo, ambayo hata wenzagu wamezungumzia kwenye maeneo yao. Kwanza, ni umeme kwenye taasisi za umma, umeme unafika mahali lakini unakuta taasisi fulani imeachwa jirani pale, shule, zahanati, msikiti ama kanisa. Ni vyema na

niombe sana Wizara wajikite kuangalia haya maeneo, ni muhimu sana wapatiwe umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kule kwenye jimbo langu kuna Shule ya Msingi Nkwae, Idang'adu, kuna Hospitali pale Misinko, kuna Ughandi kwenyewe, kuna Mfumbu, Mjura, Ikumese, Mpambaa, Shule ya Msingi Kafanabo, Chifu Gwao Shule Shikizi, Shule ya Sekondari Mikiwu na Zahanati ya Malolo. Haya maeneo yapatiwe umeme kwa sababu hayapo mbali, umeme haupo mbali, lakini unakuta ni nguzo moja wanaambiwa hamna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri *TANESCO* wanapoona *REA* wameishia mahali wao wafike. Wasiwaache *REA* pekee yao wawaunge mkono kwa nguzo moja ama ikiwezekana kuwe na programu mahususi ya kuhakikisha maeneo yale ambayo *REA* wameishia na *TANESCO* nao wasaidie. Hii inaleta malalamiko wakati mwingine hata wananchi tu wa kawaida, umeme upo pale nguzo moja inakuwa ni shida, umeme hamna. Wanaambiwa bwana hapa sisi tumeishia hapa, sasa hii inaleta shida na wananchi wetu hawamjui *REA,* hawajui nani, wao wanajua ni Serikali. Kwa hiyo, ni vyema kukawa na *coordination* ya kutosha ili kusiwe na malalamiko yasiyokuwa na msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ule umeme wa kwenye vitongoji, tulikuwa tumeahidiwa kupata vile vitongoji 15, huu Mradi bado haujatekelezwa. Kwa hiyo, niishauri sasa Serikali watuletee huu mradi lakini pia kwa sasa tusiishie kwenye hivyo vitongoji 15, wa-*extend* waongeze huo wigo ili wananchi wengi wapate umeme. Kule kwangu kuna vitongoji ambavyo vina *size* ya vijiji, ni vikubwa kama vijiji. Naomba sana, kitongoji kile, tunaita Kijiji kivuli cha Mukulu wapatiwe umeme. Pale Nkwae Kijiji cha Ikiwu wapatiwe umeme, Mlimani nao wapatiwe umeme, Mburi, Ng'ongoamwandu nao wapatiwe umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kumalizia, naona umewasha *mic*, kwenye suala la gharama, wale wananchi wetu ambao wapo tunasema *peri urban,* vijiji lakini ni kama aina fulani ya kamji. Sasa hivi wanaambiwa walipe shilingi 320,000…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hitimisha tafadhali.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi. Niombe ile shilingi 320,000 ifanyiwe *re-thinking* hata kama haitakuwa shilingi 27,000 basi ishuke itoke huko ije hata kwenye shilingi 50,000…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** … ili iwe *affordable* kwa wananchi wetu. Baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa ni Mheshimiwa Ally Juma Makoa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana ya Nishati. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema mbalimbali. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuwapa afya njema viongozi wetu wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wanamsaidia Mheshimiwa Rais na Watendaji wa Serikali wote ambao wapo kwa ajili ya kuhudumia wananchi hawa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nimesimama kuchangia nikiri kwamba, mambo mengi tayari tuliyazungumza na Wizara nikimshirikisha mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye ndiye Waziri wa Nishati na kwa kweli namshukuru sana aliweza kunipa ushirikiano mkubwa. Nikiri Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwamba, watu wake wamenihudumia vizuri sana na imekuwa ni kawaida, watu wake ni wakarimu sana. Kwa

kweli tumefika tumezungumza nao na wamenipokea vizuri na nikiri wamekubalina na yale ambayo tuliyaomba kwa ajili ya manufaa Wanakondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Naibu Waziri, dada yetu Mheshimiwa Judith amekuwa amei-*own* sana Wizara hii kana kwamba amekuwa hapo kwa muda mrefu. Naamini anamsaidia Waziri vizuri na anamsaidia Mheshimiwa Rais, vizuri. Aendelee kuchapa kazi kama *icon* ya vijana wa Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukurani kwa Wizara kwa niaba ya Wanakondoa kwa sababu ni mji ambao uliachwa nyuma sana. Ni mji wenye mitaa michache sana (36), lakini ni mji ambao una mitaa mingi ambayo haijafikiwa na umeme na pia ni mji lakini hauna umeme. Tumefanya mazungumzo ya muda mrefu sana na Wizara ya Nishati na ni watu wakarimu wamenielewa. Tumepewa hiyo mitaa 15, *REA* wameichukua. Namshukuru sana Mhandisi Hassan Said amekuwa mkarimu sana na alitupokea tukiwa na viongozi wangu na tukawa tumei-*mention* mitaa ile 15 na maeneo ambayo yanatakiwa yapewe umeme na *REA* na yamechukuliwa. Nashukuru sana hilo na nawashukuru kwa niaba ya Wanakondoa na naamini sasa Wanakondoa watapata na wenyewe huduma ya umeme kwa gharama ile ile ambayo wangepata Watanzania wengine kutokana na hali ngumu za wananchi wetu, tunafahamu ni mitaa lakini ni vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yamebaki tumezungumza na Menejimenti ya *REA*, wameyachukua na wameyaweka kwenye Mpango wa Bajeti hii ambayo tunaijadili. Kwa maana hiyo, sasa naunga mkono hoja ya Wizara hii. Naunga mkono sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu mambo mazuri yanakuja kwa ajili ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nina mambo machache sana. Namshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara maana ni mtu makini sana na ana vijana wake makini sana. *Engineer* Bakar Kalulu huyu ni Meneja wa *TANESCO* Kondoa, ni mchapakazi sana. Pia, namshukuru hata Meneja wetu wa Mkoa wa Dodoma ni mtu mahiri, ni

mtu msikivu na kwenye maeneo mengi ametusaidia sana katika kutatua changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kata moja, kata ya kwanza, naweza nikaizungumzia Kata ya Kingale, kuna Mitaa Tampori, kuna Mtaa wa Kwamtwara na Mtaa wa Chemchem, mitaa hii ni mikubwa, lakini haijawahi kufikiwa na umeme. Hata hivyo, Wizara imekwishaichukua na watu wa *REA* wameichukua hii na wataiingiza katika mpango. Kwa hiyo, kwa niaba ya wakazi wa mitaa hii mitatu, nawashukuru sana na naomba wachukulie hiyo *serious* ili watu hawa pia waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hiyo hiyo ya Kingale kuna maeneo ambayo hayakufikiwa na umeme kwenye vitongoji, pia, vimechukuliwa vimewekwa katika mpango. Kwa hiyo, Wanakondoa wasubirie kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inawapelekea umeme na watapata huduma. Kata ya Suruke tunashukuru tulikwenda tukazungumza na Menejimenti ya *REA* wakatupatia mitaa ile mitatu ya kata, kata ilikuwa haina umeme, lakini wakawa wametupelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwamba wamewasha umeme kwenye mitaa na kwa mara ya kwanza kwenye kata hiyo wamewasha umeme na umebaki Mtaa mmoja wa Tungufu ambao kidogo kuna changamoto ambazo zipo ndani ya uwezo wa Menejimenti ya Wilaya. Wakifanyia kazi najua Tungufu pia watapata umeme. Kwenye kata hii ndipo kwenye ile changamoto sasa ya maeneo ya Guluma ambayo hayakufikiwa na umeme. Mradi umepita ukaruka haya maeneo, ni wakazi wengi wanafika 2,000, lakini mradi huu uliwaruka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo nilipokwenda kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na pia nilifika kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, lakini vilevile tumezungumza na Menejimenti ya *REA* kuona ni namna gani wanaweza kumalizia ile mitaa, wananchi wanalalamika sana. Kwa maana hiyo, kwenye Kata hii ya Suruke kuna mambo mawili, naomba wanisaidie kwa uharaka wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ni hilo la kuhakikisha ule Mtaa wa Guluma Churumai ambao umebaki umaliziwe kwa mkandarasi Huyu huyu kabla hajakabidhi mradi, kwa sababu ni kitendo cha kumwongezea tu *scope* ili aweze kumaliza ile Mitaa ya Churumai na Guluma iweze kupata umeme. Uzuri nguzo zipo, bado zimejaa tele katika mtaa huo huo na ndipo nilipomwambia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwamba kulikuwa na wazo la kutoa zile nguzo na kuzihamisha jimboni. Ni jambo ambalo lingetufedhehesha sana hasa mimi Mheshimiwa Mbunge, Diwani na Wenyeviti, lakini pia tusingemsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ana njaa hapo unanyanyua chakula unapeleka sehemu nyingine kabla hujakamilisha. Sasa nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuzuia jambo hilo na naomba sasa mkandarasi huyu huyu kwa sababu bado yupo *site,* amalizie zile kaya ambazo zimebaki. Kata ya Serya, Mongoroma, Chandimo, Dumi na Hurumbi, pia ni maeneo ambayo hayana kabisa umeme. Basi naomba wakandarasi hawa wapatikane mapema ili wapeleke umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengi katika mitaa yangu ambayo hayana umeme, Kata ya Kilimani, kuna maeneo ya Damai. Jambo kubwa ambalo naomba Damai, Chavai na Kirere nilichokuwa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, yapo maeneo *TANESCO* wameyahudumia. Wamepeleka miundombinu ya umeme lakini wamepeleka kwa bei ya shilingi 320,000 mpaka 600,000 na 900,000, wananchi wa mitaa ile hawana uwezo wa kuingiza umeme kwa gharama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba kwamba *TANESCO* waweze kuona, Katibu Mkuu asaidie hapa aweze kuona, kwa sababu kuna mahali jirani walifungiwa kwa shilingi 25,000. Wao wanapelekewa kwa shilingi 320,000 jambo ambalo linawafanya wananchi wengine wanakuwa wanyonge wakati Serikali yetu ni hii na uwezo wao ni mdogo kama wale waliofungiwa kwa shilingi 27,000. Kwa hiyo yale maeneo yote ambayo *TANESCO* wamepeleka umeme, nguzo zimesimama, nyaya zipo tayari wamefunga *transformer,* lakini hakuna mtu hata mmoja aliyeunganishiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo Mtaa mmoja wa Damai wameunganisha wafanyabiashara wawili tu wa mashine za kusaga, wananchi wengine wote wanasubiria ile *fair* ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufunga umeme kwa gharama ile ya Watanzania maskini wengine. Kwa maana hiyo tunaomba yale maeneo yote yaliyofikiwa na umeme wa *TANESCO* hebu walione hilo. Kwa upande wa Kata hii ya Suruke tumekwishaandika barua tumeipeleka kwa Meneja wa Mkoa ili kuomba *TANESCO* waone hali duni ya Watanzania ambao wanaishi kwenye mitaa ambayo inafanana na vijiji, waweze kuwekewa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote kwa yote naunga mkono hoja na naishukuru sana Wizara kwa kukubali mitaa yangu ile kuchukuliwa na *REA* na kukubali mitaa iliyobaki tuiingize kwenye mpango huu. Nawatakia kila la heri Mungu awabariki sana, wachape kazi kwa ajili ya Watanzania. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga aweze kutoa mchango wake. Karibu.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niwe mchangiaji wa mwisho katika siku hii ya leo. Jambo la kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kutekeleza miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kuisimamia Wizara hii ya Nishati, nawapongeza viongozi wa taasisi zote na mashirika yote yaliyopo chini ya Wizara hii, kwa kweli kwa pamoja wanafanya kazi nzuri sana, hongereni sana. Nawapongeza pia kwa kuja na bajeti nzuri, bajeti ambayo inatupa mwelekeo mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa umeme kwenye maendeleo ya nchi yoyote unajulikana na unaeleweka vizuri, nchi yoyote inapotaka kujinasua katika ujenzi wa viwanda inahitaji umeme

wa uhakika. Tunahitaji umeme kwa ajili ya kujenga viwanda mama, viwanda vidogo vidogo, viwanda vya kuongeza thamani ya mazao, tunahitaji umeme kwa ajili ya kuweka maisha yetu yawe mazuri ili wananchi waweze kula maisha safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, tunahitaji nishati nzuri kwa ajili ya kupikia. Tunahitaji umeme ili wananchi waweze kupikia pia tunahitaji gesi kwa ajili ya kupikia na tunahitaji kwa ajili ya kusafirishia mazao na kufanya kazi nyingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hizi za umeme, kazi za nishati zikifanyika vizuri tutapunguza umaskini wa nchi yetu, tutapunguza tatizo la ajira kwa wananchi wetu kwa sababu wananchi walio wengi kule vijijini umeme ukifika wanaanzisha viwanda vidogo vidogo mwingine anakuwa na friji anaanza kutengeneza *ice cream*, mwingine anaanza kufanya kitu kingine chochote, mwingine anakuwa na soda na kadhalika, hii inachangia kutoa ajira na kupunguza tatizo la ajira lakini pia inachangia kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Songwe pamoja na kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara hii lakini kumekuwa na shida kubwa sana ya kukatika umeme katika Mkoa wa Songwe. Umekuwa unakatika mara nyingi sana, hii inatokana na miundombinu ya umeme kuwa midogo na bado haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunasubiri sana ule mradi wa *backbone* wa *grid* kubwa ambao walisema kwamba itatoka Iringa, itakuja Mbeya, itakuja Vwawa, itakwenda Tunduma itaenda mpaka Rukwa ili kusudi umeme sasa uweze kusambaa na uweze kupatikana. Sasa hivi umeme unaopatikana kule ni mdogo pamoja na kwamba sasa hivi uzalishaji umeweza kunasua, Bwawa kubwa lile wameweza kuzalisha umeme wa kutosha na ziada, lakini miundombinu ya kusafirisha ule umeme kutufikia bado ni hafifu na hivyo kusababisha ukatikaji mkubwa sana wa umeme katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwetu tulikuwa tuna-*experience* karibu ukatikaji wa umeme mara 15, mara ngapi kwa siku,

sasa hivi waliposema umeme umekuwa mwingi nikategemea sasa kukatika kutakuwa kumekwisha, lakini mara utasikia kuwa nguzo imedondoka, mara sehemu fulani kumetokea hii, bado tatizo lipo! Kwa hiyo tunaomba ule mradi *backbone* kwa kweli wauharakishe, ambao utaenda kuunga na *switch* ile ya kwenda Zambia ambapo sasa kama kuna tatizo la upungufu wa umeme hapa nchini tunaweza kutumia umeme wa Zambia, tunaweza tukatumia umeme wa Kenya, tunaweza tukatumia umeme wa Ethiopia na maeneo mengine. Kwa hiyo, katika utaratibu huu kwa kweli ni vizuri sana wakahakikisha kwamba ule mradi unakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu vijiji. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na nawashukuru sana *REA* pamoja na *TANESCO*, wamefanya kazi nzuri. Vijiji vyangu vyote ambavyo vilikuwa havina umeme sasa hivi umeme umefika, lakini haujawashwa kwa wananchi, umewashwa kwenye transfoma. Sasa wananchi siyo kwamba wanataka wauone kwenye transfoma, wanataka wauone ule umeme wanautumia kule majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu karibu zaidi ya miezi mitatu sasa hivi hawajasambaziwa na tatizo limekuwa kwamba kuna upungufu wa mita. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu umeme umeshafika, tunaomba walishughulikie haraka suala la mita ili vile vijiji vyangu karibu 15 ambavyo umeme umefika, umewaka kwenye transfoma uweze kuwaka katika maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kwa sababu wananchi kama wale wa Kijiji cha Ilomba, Idunda, Ipyana, Nyimbili, Hantesya na maeneo mengine wamekuwa wakilalamika sana wanahitaji umeme, kule Namwangwa wanahitaji umeme kwa kweli, kwa hiyo naomba waharakishe suala la kupeleka hizo mita ili wananchi waweze kufungiwa na waweze kupata umeme na waanze sasa kula maisha vizuri. Tunamshukuru sana kwa upande wa vitongoji, kuna vitongoji ambavyo bado havina umeme. Mradi umekuja na vitongoji vichache lakini vipo vitongoji vingi ambavyo bado havina umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wilaya yetu ya Mbozi nina vitongoji karibu 600 na zaidi, vitongoji 300 vina umeme, nusu bado havina umeme. Sasa tunaomba mkakati uongezeke ili kuhakikisha vitongoji vile ambavyo havina umeme vinakuwa na umeme. Maeneo kama Izyika kule, maeneo ya Hasanga, maeneo ya Josho kule bado vile vitongoji hawana umeme na umeme unahitajika sana. Maeneo kama ya Nsenya, Msia Kati, Igunda na maeneo mengine yote yanahitaji umeme. Tunaomba kweli huu mradi wa vitongoji kwa kweli waongeze kasi ili kusudi wananchi waweze kunufaika na suala hilo la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri ningependa kushauri mambo mawili. Jambo la kwanza, sasa hivi tatizo la *climate change,* tatizo la mabadiliko haya ya tabianchi yataendelea kutusumbua na yanatuathiri sana. Tunahitaji kuwa na mkakati wa kutosha kuhakikisha kuwa tunakabiliana nayo. Angalia kuna wakati unakuta kwamba kuna upungufu wa maji umeme utapungua, sasa maji yamezidi umeme utapungua. Kwa hiyo tatizo linakuwa bado ni kubwa. Mafuriko yakitokea tuna tatizo, tukiwa na ukame tuna tatizo. Kwa hiyo, tunahitaji mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba kwa kweli tunakabiliana na hili suala vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, sasa hivi ukataji wa miti, watu wanakata miti sana. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wametupa majiko ya gesi machache kwa ajili ya kuwapa wananchi ili waweze kutumia majiko ya gesi, lakini bado safari ni ndefu, kwa sababu wananchi walio wengi wa Tanzania kwa zaidi ya 98% wanatumia kuni na bado tunaendelea kukata miti na wanakata ovyo ovyo. Matatizo yote haya kama hatutakuwa na *program* ya kuhakikisha kwamba tunarudishia au tunapanda mti, bado tatizo la tabianchi litaendelea kutuathiri sana. Kwa sababu ukame unaweza ukatukuta, miti itaendelea kukatwa na tutakuwa na upungufu wa maji na hivyo kusababisha kusiwe na umeme wa kutosha. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kulishughulikia suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja kama unaweza kuniruhusu, kwa sababu ya muda niombe tu, kuwapongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini wachukue hatua katika kukabiliana na

haya masuala, zaidi ya hapo naomba niseme kwamba tunahitaji umeme na tunayo imani kazi wanayoifanya ni nzuri, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge na kipekee Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia leo, tumemaliza orodha ya wachangiaji ambao tulikuwa nao leo na sasa naomba niahirishe Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.47 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 25 Aprili, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*